
**Mwongozo wa Nne**

# Mafunzo Ya Omega

## *Mafunzo ya Vitendo Kwa wapanda Kanisa*



*Na Muungano wa Kueneza Upandaji kanisa Wakishirikiana na Huduma ya Peter Dayneka wa Urusi*

**Kozi ya Omega:**
**Mafunzo ya Vitendo Kwa Wapanda kanisa**
**Mwongozo wa Nne**

Tafsiri ya asili ilichapishwa na
The Bible League, P.O. Box 28000, Chicago, IL 60625 USA
Tel: (800) 334-7017 E-mail: info@BibleLeague.org www.bibleleague.org

Copyright © 2000,2006 United World Mission.
Machapishwo haya kwa asili yalinukuliwa na *The Alliance for saturation Church Planting* na yaliandaliwa na ushirika huo kwa kushirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250.

Unaruhusiwa na Unashauriwa kuzalisha na kusambaza zana hii katika mfumo wowote endapo kama: (1) Unampa sifa mwandishi, (2) unaonyesha kama marekebisho yamefanyika, (3) Hulipishi zaidi ya gharama ya kuzalishia tena, na (4) hutengenezi kopi zaidi ya 1000.
Kama utapenda kuweka nakala za nyenzo hii kwenye internet au kama matarajio yako ya matumizi ni tofauti na vichwa vya habari hapo juu tafadhali wasiliana na
United World Mission: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pines Blvd.
Charlotte, NC 28273-5596, or omega_course@alliancescp.org

Kutafsiri na kurithi katika lugha yako pia kunashauriwa. Tena, tafadhali wasiliana na omega_course@alliancescp.org ili kwamba tuweze kutia moyo na kuwajulisha wengine wanaoweza pia kuwa wamevutiwa katika lugha yako au matumizi yaliyokusudiwa.

Kwa taarifa zaidi juu ya huduma zao za kuheshimika, tafadhali wasiliana na :

THE ALLIANCE
FOR SATURATION CHURCH PLANTING

(tovoti/rasilimali zinapatikana ila kwa sasa ushirikiano huo haupo tena)
http://www.alliancescp.org/resources/interchanges/2005_aug.html

Peter Deyneka
Russian Ministries

P.O. Box 496
Wheaton, IL , USA 60189
Tel: (630) 462-1739 Fax: (630) 690-2976
info@russian-ministries.org
www.russian-ministries.org

Kwa asili yalipigwa chapa au yalichapishwa katika nchi ya Marekani (USA).

# SHUKURANI

Tunatoa shukurani zetu kwa moyo wa dhati na za pekee kwa wote waliochangia katika matayarisho ya miongozo hii ya mafunzo. Wafuatao ni watu waliojitoa sana kwa kiwango kikubwa kwenye hatua ya kuandika na kutengeneza miongozo hii. Bwana, panda kanisa lako…mpaka miisho ya dunia.

Jay Weaver, Mtengenezaji, Timu ya Ulimwengu

| | |
|---|---|
| Richard Beckham | *Greater Europe Mission* |
| David & Lisa Bromlow | *Christ For Russia* |
| Ron Brunson | *World Witness and United World Mission* |
| Don Crane | *Greater Europe Mission* |
| Bea Crane | *Greater Europe Mission* |
| Hunter Dockery | *World Harvest Mission* |
| Mike Elwood | *Greater Europe Mission* |
| Jeff Geske | *United World Mission* |
| Dave Henderson | *C B International* <br> *—Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |
| Bob Mackey | *United World Mission* |
| Bob Martin | *United World Mission* |
| Paul Michaels | *Grace Brethren Intl. Mission* |
| Norie Roeder | *United World Mission* |
| Ki Sanders | *World Team* |
| Larry Sallee | *UFM International* <br> *—Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |
| Eric Villanueva | *United World Mission* |
| David Westrum | *Interlink Ministries* <br> *—Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |

**SHUKRANI ZA PEKEE KWA AJILI YA MSAADA WAO WA KIUONGOZI NA UTALAAM**

| | |
|---|---|
| Edith Bond | *The Alliance Regional Resource Team* |
| David Gál | *The Alliance Regional Resource Team* |
| Nell Harden | *Retired English Professor* |

# MWONGOZO WA NNE

## Yaliyomo

**DIBAJI** ........ **8**

**KUHUSU MUUNGANO** ........ **10**

**MZUNGUKO WA UPANDAJI KANISA** ........ **11**

**MTAALA** ........ **12**

**MTAZAMO WA UTARATIBU** ........ **14**

**MAONO YA KUM** ........ **19**

**SOMO 10: Vipengele vya Mkakati kwa Harakati za Upandaji Kanisa** ........ **20**

I. Kujenga Imani katika Maono ........ 20
II. Weka Malengo Kulingana na Imani ........ 22
III. Fanya majaribio ya Kuzidisha Badala ya Kuongeza ........ 22
IV. Fanya Kazi Kimkakati Kutokea kwenye Kitovu Kuliko tu Kwa Mbali ........ 23
V. Anzisha Timu za Kuwezesha zinazokwenda Huku na Huko ........ 23
VI. Wezesha Watu ........ 24
VII. Anzisha Mitandao ........ 24
VIII. Tafuta Uongozi wa Mungu na Mda Muafaka ........ 25

***Ziada: Imani na Utii Dhidi ya Kutokuamini na Hofu* ........ *27***

***Ziada: Vitu ambavyo Vinachochea Kukua kwa Asili* ........ *28***

**SOMO LA 11: Dalili za Harakati** ........ **29**

I. Dalili ya 1: Mda Maalumu ........ 30
II. Dalili ya 2: Uongozi Unaoibuka ........ 31
III. Dalili ya 3: Watu Kuweza Kuhusika ........ 32
IV. Dalili ya 4: Mifumo Mipya ........ 33
V. Dalili ya 5: Harakati ni Kitu cha Hiari ........ 34
VI. Dalili ya 6: Harakati Zinahamasisha Watu na Miundo ........ 35

**SOMO LA 12: Uangalizi Katikati ya Harakati** ........ **37**

I. Uongozi katika Makanisa Machanga Yaliyopandwa ........ 37
II. Kufanya Mawasiliano na Makanisa Mapya ........ 38
II. Kulinda Dhidi ya Mafundisho ya Kinyume ........ 40
IV. Kuweka Rasilimali ........ 41
V. Harakati za Kiinjilisti na Upandaji Kanisa ........ 442

**KANISA ....45**

**SOMO LA 12: Nguvu ya Kanisa Linaloibuka .... 46**

I. Ni Wakati Gani Kanisa ni kanisa? .... 46
II. Kupangilia Kama Kanisa .... 49

**SOMO LA 13: Tabia za Makanisa Yanayokua .... 52**

I. Ni nini Kanisa Linalokua? .... 52
II. Jinsi Gani Ukuaji wa Kanisa Unatokea .... 53
III. Tabia Kumi na Mbili za Makanisa Yanayokua .... 54
IV. Kutathimini na Kusimamia Ukuaji wa Kanisa .... 58

**SOMO LA 14: Serikali ya Kanisa na Ofisi za Kanisa .... 60**

I. Kanisa ni Nini? .... 60
II. Aina za Serikali ya Kanisa .... 60
III. Ofisi katika Kanisa .... 62
IV. Majukumu na Milango Wazi ya Viongozi wa Kanisa .... 63

**TABIA YA KIROHO ....67**

**SOMO LA 11: Upendo Kama Msingi wa Huduma .... 68**

I. Injili Kama Kielelezo cha Mahusiano .... 68
II. Upendo wa Mungu wa Kujitoa, Usio na Masharti .... 69
III. Upendo wa Mungu Ukitumika Kwenye Mahusiano .... 70
IV. Upendo kama Chimbuko la Huduma .... 71

**SOMO LA 12: Kuuelewa Moyo wa Baba .... 73**

I. Mifano Mitatu Kuhusu Vitu Vilivyopotea -Luka 15 .... 73
II. Mfano wa Mwana Mpotevu .... 74
III. Matumizi—Tunapenda Kama Baba Anavyopenda? .... 75

**SOMO LA 13: Neema ni Kwa Wanyenyekevu .... 77**

I. Utu—Ni Nini Maana Yake? .... 77
II. Mifano ya Utu .... 78
III. Maombi Yanaonyesha Utu kuelekea kwa Mungu .... 79
IV. Maisha ya Kikristo Yana Tabia ya Utu .... 79

**MAOMBI ....81**

**SOMO 8,9: Kongamano la Maombi .... 82**

I. Injili kwa Watu Wote .... 82
II. Kuuombea Ulimwengu .... 83
III. Kongamano la Maombi – Kuuombea Ulimwengu Wote .... 84

**UONGOZI ....................................................87**

**SOMO LA 6: Uongozi wa Kitumishi ........................................ 88**

I. Uongozi wa Kidunia ........................................ 88
II. Uongozi wa Kitumishi ........................................ 89
III. Mafundisho ya Agano Jipya Juu ya Uongozi wa Kitumishi ........................................ 90
IV. Matumizi ........................................ 91
***Ziada: Orodha ya Mambo ya Kiongozi........................................ 93***

**SOMO LA 7: Nguvu za Uongozi ........................................ 94**

I. Tabia ya Kiongozi ........................................ 94
II. Tabia za Kikundi ........................................ 97
III. Asili ya Kazi ........................................ 99

**SOMO LA 8: Mitindo ya Mwingiliano ........................................ 101**

I. Gundua Mtindo Wako wa Kuingiliana ........................................ 101
II. Mitindo Minne ya Mwingiliano ........................................ 103

**SOMO LA 9: Hitaji la Uongozi ........................................ 107**

I. Ni Aina Gani ya Viongozi Kanisa Linahitaji? ........................................ 107
II. Ni Viongozi wangapi Kanisa Linahitaji? ........................................ 109
III. Ni Wapi Tunawapata Viongozi Hawa? ........................................ 111

**SOMO LA 10: Kuwafundisha Viongozi wapya ........................................ 112**

I. Mifano ya Kibiblia ya Kuzidisha Uongozi ........................................ 112
II. Malengo ya Kufundisha ........................................ 114
III. Utaratibu wa Hatua Tano za Kufundisha Viongozi Wapya ........................................ 116
***Ziada: Hadhi za Kutia Moyo katika Uongozi Mpya........................................ 119***

**VIKUNDI KIINI ....................................................121**

**SOMO LA 10: Maswali ya Majadiliano ya Kikundi Kiini na Matatizo ........................................ 122**

I. Uhalisi wa Huduma ya Kikundi Kiini ........................................ 122
II. Maswali na Matatizo ........................................ 123
III. Suluhu ........................................ 123

**SOMO LA 11: Kuzidisha kwa Kikundi Kiini ........................................ 124**

I. Lengo la Kuzidisha ........................................ 124
II. Utaratibu wa Kuzidisha kwa "Asili" ........................................ 125
III. Vizuizi vya Kuzidisha ........................................ 129

**KUFUASA ....................................................133**

**SOMO LA 6: Warsha ya Kufuasa ........................................ 134**

I. Majadiliano ya Kikundi Kidogo (1/2 saa) ........................................ 134
II. Warsha ya Kufuasa (Dakika 20) ........................................ 135
III. Suluhu (Dakika 3 ) ........................................ 135

**UWAKILI ....................................................137**

**SOMO LA 1: Utangulizi kwenye Uwakili ........................ 138**

I. Uwakili ni Nini? ........................ 138
II. Kwa Nini Kuzungumzia Uwakili? Maswala Mawili ........................ 138
III. Kanuni za Uwakili katika Biblia ........................ 139
IV. Uwakili Wetu ........................ 141
V. Uwakili na Mpanda Kanisa ........................ 143

**SOMO L:A 2: Uwakili Katika Fedha ........................ 144**

I. Kuichunguza Biblia Yote ........................ 144
II. Utoaji wa Mtu Pekee ........................ 146
III. Fedha za Kanisa la Mtaa ........................ 147
IV. Ufadhili na Harakati za Upandaji Kanisa ........................ 149

**SOMO LA 3: Usimamizi wa Mda ........................ 152**

I. Kuweka Vipao Mbele—Kujifunza Jinsi ya Kutunza Mda ........................ 153
II. Uwekaji Vitendea kazi kwa Vitendo ........................ 153

**SOMO LA 4: Utaratibu wa Upangaji Kimkakati ........................ 159**

I. Nini Maama ya Upangaji Kimkakati? ........................ 159
II. Utaratibu wa Kupanga Kimkakati ........................ 160

**SOMO LA 5: Warsha ya Utaratibu wa Upangaji Kimkakati ........................ 165**

**FAMILIA ....................................................167**

**SOMO LA 1: Wajibu wa Kiblia katika Familia ........................ 168**

I. Wenzi Waliooana ........................ 169
II. Wajibu wa Mme ........................ 169
III. Wajibu wa Mke ........................ 171
IV. Wajibu wa watoto ........................ 172

**SOMO LA 2: Uleaji ........................ 174**

I. Baadhi ya Uchunguzi wa Mwanzoni ........................ 174
II. Baadhi ya Kanuni za Kibiblia ........................ 175

# DIBAJI

## KUSUDI LA NYENZO HII

Wapanda kanisa mara nyingi wanafunzwa na kupelekwa nje wakiwa na mafunzo kidogo au bila mafunzo kwa ajili ya kazi iliyo mbele yao. Viongozi wa kanisa ambao wamezidiwa na matatizo ya huduma mara nyingi wanakosa maono wazi ya kile Mungu anachotaka kukamilisha kupitia wao. Wote wapanda kanisa na viongozi wa kanisa wanahitaji mafunzo na maono, lakini shule za Biblia na seminari siyo uchaguzi unaofahamika kwa wengi.

Nyenzo hii imeandaliwa siyo kutoa maono tu kwa wapanda kanisa na viongozi wa kanisa, lakini pia msingi wa kibiblia na ujuzi wa vitendo wa huduma ili kuona maono hayo yanakuwa kitu halisi. Siyo kielimisho cha “maazimio.” Badala yake, inatoa misingi muhimu ya kibiblia na kielimu, vilevile na ujuzi wa vitendo wa huduma, unaohitajika kwa upandaji kanisa. Ingawa kozi ya Omega iliandaliwa kwa ajili ya Ulaya ya mashariki na Kati na Muungano wa Urusi ya zamani, tumetiwa moyo na taarifa ambazo zimeshapatikana kuwa za msaada zinaporithiwa katika mandhali zingine.

Kozi yote hii imeandaliwa kukamilisha malengo mawili:

1. Kutoa mafunzo muhimu kwa makanisa kuweza kupandwa.
2. Kutia moyo uhamasishaji katika mwili mzima wa Kristo kuelekea harakati za upandaji kanisa.

Leo tunaona harakati za upandaji kanisa zikitokea katika nchi nyingi ulimwenguni kote, ikiwemo, Brazil, Roma, Ufilipino, Nigeria, na kwingine. Tunaamini kwamba kanisa la mtaa ni chombo cha msingi cha kuinjilisha ulimwengu, na kwamba upandaji wa kanisa unaotokana na kanuni ya kuongezeka mara dufu ni njia yenye mafanikio zaidi ya kutumia kuelekea kwenye kukamilisha utume mkuu. Makanisa mapya lazima yapandwe kwa maono ya kuongezeka mara dufu na uwezo wa kupanda makanisa mengine mapya. Hili linapotokea, kuna uwezekano wa harakati za makanisa zinazoweza kupangusa kuzunguka taifa na kubadilisha maisha ya watu katika nchi yote.

Harakati za upandaji kanisa zinahitaji watu waliohusika katika ngazi zote za kazi ya upandaji kanisa, kutokea kwa waumini wachanga walio na shauku ya imani yao mpya, hadi kwa viongozi wa madhehebu. Wapanda kanisa peke yao hawawezi kuwa kiungo cha harakati za upandaji kanisa. Nyenzo hii inafaa na ina manufaa makubwa katika ngazi zote za wafanya kazi wa kanisa na viongozi wa kanisa ambao wanaweza kuunga mkono juhudi za wapanda kanisa moja kwa moja au kwa namna nyingine wanapokuwa wanajitahidi kutimiza huduma aliyowaitia Bwana.

## MTAZAMO WA TARATIBU

Mwomngozo huu ni moja ya miongozo mitano, ambayo kila mmoja una wastani wa masomo 26 ya saa moja. Ili kukamilisha malengo yaliyoelezewa hapo juu, kozi yote inatosheleza mapana mbalimbali ya masomo ambayo ni muhimu kwa kazi ya upandaji kanisa. Haya ni pamoja na maono ya KUM, huduma ya kikundi kiini, ufuasishaji, kanisa, uinjilisti, mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, uongozi, maombi, tabia ya kiroho na mengine mengi.

Taratibu ziligawanywa katika miongozo mitano ili kutoa njia inayozidi kupanuka kwenye kozi ya mafunzo. Wakati kila mshiriki anapomaliza mwongozo, anatumia mda kabla ya mwongozo unaofuata akiziweka katika matendo kanuni alizojifunza. Kwa hiyo vipindi vingi vya baadaye vinajengwa juu ya kanuni na ujuzi uliojifunzwa na kufanyiwa mazoezi katika masomo ya mwanzoni.

Kwa maneno mengine, taratibu zimeandaliwa kujifunzwa na kutumiwa sambamba na upandaji halisi wa makanisa. Washiriki wanapofanya kazi kwa juhudi kwa ajili ya kuanzisha kanisa jipya, watahitaji kiwango fulani cha ujuzi na ufahamu, na watakutana na matatizo mbalimbali wanapoendelea. Ujuzi na ufahamu unaohitajika mwanzoni mwa upandji kanisa unatolewa katika mwongozo wa kwanza, wakati shughuli na kanuni zinazohitajika baadaye katika upandaji kanisa zinatolewa katika miongozo ya mbeleni. Kila mwongozo umeandaliwa kutoa ujuzi, kujibu maswali, na kujadili matatizo nyeti ambayao yanahusiana na hatua sambamba ya upandaji kanisa ambapo washiriki wanafanya kwa juhudi. Baada ya dibaji hii utaona orodha ya shughuli muhimu za maendeleo au “mapito**”** ambayo wafunzwa wameandaliwa na kutarajiwa kuutumia wakati wa mafunzo ya semina.

Masomo yamegawanywa kwa mada, na kila moja ya miongozo mitano ina masomo kutoka baadhi ya mada. Baadhi ya visa, kama vile “maono” na “kanisa” yote yamo katika miongozo yote mitano. Mengine, kama vile “kufuasa” kunatokea baadaye kwenye kozi, wakati mshiriki anapokuwa kwenye

hatua katika huduma yake ambapo visa hivi ni muhimu. Mtazamo wa kozi yote ulio na orodha ya mada ya somo kwa kila moja ya miongozo mitano imehusishwa baadaye katika hatua hii.

**UTUMIAJI WA NYENZO**

**Ushauri Kwa Washiriki**

Mda wa kutosha, maombi na juhudi yamewezesha utayarishaji wa miongozo yote hii mitano katika kozi yote. Kila mwongozo umeandaliwa kugusia ujuzi maalumu wa huduma na ufahamu unaohitajika wakati wa utaratibu wa kuanzisha kanisa jipya. Kwa hiyo inashauriwa kabisa kwamba unaanza na mwongozo wa kwanza, siyo mwongozo mmojawapo wa baadaye. Kwa heshima hiyohiyo, kila somo limechaguliwa kwa uangalifu na kufanyiwa ufundi ili lifae, kutumika na la lazima katika kazi ya upandaji kanisa. Ni kwa manufaa yako pia kutovuka somo.

Tambua kuwa kusoma halisi kunatokea unapoyatumia mawazo yaliyotolewa katika masaomo haya katika maisha yako binafsi na katika huduma yako. Masomo mengi yana utekelezaji wa azimio mwishoni. Utekelezaji huu wa azimio umeandaliwa kukusaidia wewe kutumia mawazo katika somo na unatakiwa umalizike kabla hujaanza kufanyia kazi mwongozo unaofata. Inaweza kuwa msaada wa hali ya juu kuwa na mshauri wa kukutia moyo na kukushauri unapofanya mwenyewe upandaji kanisa. Mshauri pia anaweza kusaidia hitaji lako la uwajibikaji unapokuwa unayatumia mawzo yaliyojifunzwa katika maisha yako na huduma. Kuwa na mtu anayekuwa nawe bega kwa bega siyo tu maandalizi ua ufanisi, lakini wapanda kanisa wengi wanashuhudia msaada ambao hili linatoa katika maisha yao na katika huduma yao. Kwa hiyo, tunakutia moyo kabisa kwa maombi kutafuta aina fulani ya ushauri kuwezesha na kudumisha huduma yako ya upandaji kanisa.

**Ushauri kwa Wakufunzi**

Nyenzo hii inaweza kutumika kwa aina mbalimbali ya maandalizi kama vile shule ya Biblia, semimari au semina ya kikanisa. Kwa jinsi hiyo hii siyo tu kama nyenzo ya kuanzia ya kuelimishia. Ni nyenzo ya kufundishia. Elimu inayokazia katika ufahamu na habari.Kusudi la nyenzo siyo tu kukuwezesha kupata ujuzi, lakini pia ni kuchochea kuelekea kufikia kuweka huduma inayofanana na ya kibiblia. Mwongozo huu ni kwa ajili ya 'watendaji'.

Ingawa njia unayochagua kufundishia masomo kwa kila mwongozo itategemeana na mandhali yako, kila mwongozo unaweza kufundishwa katika semina ya wiki nzima. Kutokana na maelekezo haya, vituo mbalimbali vya mafunzo vimefanikiwa kwa kutumia mpangilio tofauti unaoendana na mtiririko wa maisha na huduma zilizopo. Wakati mwingine wamechagua siku mbili mfululizo za mapumziko ama vipindi vya kila wiki. Inashauriwa kwamba utekelezaji wa azimio mwishoni mwa kila somo usisitizwe ili kwamba uwe umemalizika kabula ya semina nyingine. Kipindi cha kati ya miezi minne hadi sita ni kipindi kinachofaa kujatarajia kati ya semina na semina. Faida ya njia hii ya ufundishaji ni kwamba inaunganisha kanunu ulizojifunza kwenye semina na ushiriki kwenye semina.

Wakati wa semina siyo lazima kufundisha kila kiini kilichopo kwenye mwongozo kwa sababu washiriki wanaweza kusoma nyenzo wenyewe. Wakati mwingine kufanya wafunzwa kusoma soma na kujadiliana jinsi linavyogusa uzoefu wao ni njia nzuri. Na wakati mwingine, maelezo kutoka kwa mtu ambaye ana uzoefu wa somo lililomalizika inaweza kuwa njia nzuri ya kujenge mawazo. LAKINI USIKALIE NJIA YA MAELEZO. Uwe mbunifu wakati ukijaribu njia mablimbali kujenga kanuni na ujuzi uliomo kwenye masomo. Wakufunzi wengine wamepata mchanganyiko kama vile kujadiliana kwenye makundi, karakana, na inaonekana kufanya kazi na kuwafurahisha.

Umetengwa kwa kutumainiwa, Mungu wa makanisa anahitaji mataifa yafuasishwe, na viongozi wanahitajika.

Una uwezo wa ajabu kusaidia kuandaa wengi watakaoendeleza harakati za upandaji kanisa na kuwezesha wengine katika huduma za kuzaliana kwa kanisa

**Msaada Zaidi**

Usisite kuwasiliana nasi kama tunaweza kuwa msaada zaidi kwako katika kueneza maono ya kueneza upandaji kanisa au kwa vitendo kuandaa wapanda kanisa.

Jay Weaver, General Editor
Budapest, Hungary, January 2000
JayWeaver@compuserve.com

# KUHUSU MUUNGANO

Taratibu hii imetayarishwa na *Muungano wa Kueneza Upandaji Kanisa* wakishirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250. *Muungano* ni ushirikiano wa makanisa na mawakala wa umishenari waliojitoa kuwahamasisha waumini kuenea katka kila nchi zilizopo kati na mashariki ya Ulaya na ushirika wa makanisa ya kiinjili ya Urusi ya zamani. Kueneza upandaji kanisa ni mbinu ambayo inakusudia kuanzisha makanisa katika kila mji, vijiji, na maeneo unayopakana nayo ili kwamba kila atakayemwamini Yesu apate kuwa na kanisa jirani atakaloweza kushiriki na kukua ndani ya Yesu na kujengwa au kuandaliwa kwa huduma. *Muungano* umejengwa juu ya msingi ambao kuunganisha nguvu kutaongeza ufanisi, kupunguza marudio na kuonyesha umoja kati kati ya mwili wa Kristo.

## TUNACHOAMINI

- Kanisa la mtaa ni zana ya msingi ya Mungu anayoitumia kueneza injili na ufuasishaji
- Ushirikiano na makanisa pamoja na mashirika ya kimishenari ni madhubuti kwa ongezeko la makanisa ya mtaa na maendeleo ya harakati za kueneza upandaji kanisa.
- Kuelimisha viongozi ni mhimu kwa upandaji kanisa na ukuuaji wa kanisa.
- Maagano ya Lausanne ni maelezo ya imani ya Muungano (Alliance)

## TUNACHOFANYA

### Kuelimisha na Kushauri Wapanda Kanisa

*Muungano* unatoa ujuzi unaotokana na mafundisho katika mtindo wa semina pamoja na mazoezi ya huduma yanayolenga kwenye kuanzisha makanisa yanayozaliana.

### Ukusanyaji Bayana wa Taarifa.

Taarifa makini zinapelekea uamuzi mzuri katika kazi za upandaji kanisa. *Muungano* unaweza kuhusika katika kufundisha na kushauri katika hitaji la kukusanya taarifa zinazohitajika katika eneo la upandaji kanisa na kukua kwa kanisa.

### Harakati za Kuhusisha Maombi

Harakati za upandaji kanisa zinaanza na maono, ambayo yanagunduliwa na kuandaliwa kwa kutafuta moyo wa Mungu kwa maombi. *Muungano* unaweza kukusaidia kuelewa zaidi nafasi ya harakati za maombi katika kazi ya upandaji kanisa, na namna unavyoweza kuwezesha harakati za maombi katika eneo au sehemu yako.


### Utupaji Maono

Ni kitu gani Mungu anataka kwa nchi yako? Anataka makanisa kila mahali! *Muungano* unaweza kusaidia kuendeleza maono ya makanisa mapya kwa zana ya semina katika kanuni ya kuendeleza upandaji kanisa.

## KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:

*The Alliance For Saturation Church Planning* (*Muungano wa Kueneza Upandaji wa Kanis*a)
Regional Resource Team
H-1111 Budapest
Budafoki ut 34/B III/2, Hungary
Tel: + (36-1) 466-5978 or 385-8199
Fax: (36-1) 365-4606
E-mail: KUMAAlliance@compuserve.com

# MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA




Kupanda kanisa siyo mfuatano wa matukio na shughulu zilizounganishwa bila utaratibu; Ni utaratibu wenye msukumo wa lengo. Utaratibu huu unahitaji ulinganifu wa shughuli, mchanganyiko wa ujuzi, falsafa ya kawaida na ujasili katika uongozi. Maendeleo katika maeneo haya nyeti ndilo lengo la kufundisha wapanda kanisa. "mzunguko wa kupanda kanisa" ni mchoro wa utaratibu wa kupanda kanisa ambao kwa macho unaonyesha, kutoka katika wazo fulani la mtazamo, mwingiliano wa kanuni za ufunguo na kufanya mazoezi ya kazi katika utaratibu huo. Hii inawakilisha 'ramani ya barabara' kwa mpanda kanisa, kuruhusu watu kuonyesha ni wapi wametoka na wapi wanaelekea.

# MITAALA

### Ya Utaratibu wa Upandaji Kanisa kwa Kozi ya Omega

**Mitaala** (vianzio) ni msingi mugumu wa shughuli za huduma ambazo zimeshirikishwa katika utaratibu huu. Kila mtaala unaweza kufikiriwa kama jiwe la kuvukia la mtu binafsi katikati ya utaratibu mkubwa wa kuanzisha kusanyiko jipya. Mitaala inatoa hatua ya utekelezaji imara ambao unaweza kusaidia wafunzwa kuweza kwa vitendo kutumia mawazo yaliyomo kwenye Kozi ya Omega. Zote ni mawe ya mbali ambato yanaonyesha maendeleo, vile vile ubao wa alama ambao unasaidia kutoa mwelekeo zaidi. Zifuatazo ni orodha za mitaala na msisitizo katika Kozi ya Omega

| MWONGOZO WA KWANZA: | Msisitizo juu ya Maono ya KUM, Kusudi la Kanisa, Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno na Utafiti |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuchunguza kusudi la Kanisa katika mwanga wa Utume Mkuu
- Kuanzisha mkakati wa jumla wa huduma ukizingatia maono ya "Z-kufikiri"
- Kuchunguza "mfumo na kazi" katika Kanisa la kwanza na Kanisa la sasa
- Kujifunza na kufanya majaribio ya Kujifunza Biblia kwa kufata neno
- Kuandika na kushirikisha ushuhuda binafsi
- Kuanzisha vikundi vya kusaidia maombi kwenye uinjilisti na upandaji kanisa
- Kukamilisha mradi wenye mambo mengi wa utafiti katika eneo linalolengwa

| MWONGOZO WA PIL: | Msisitizo Juu ya Uinjilisti na Vikundi Kiini |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kushirikishana yaliyopatikana katika mradi wa utafiti na wengine katika eneo linalolengwa
- Kuandika maelezo ya kusudi la kanisa
- Kuanzisha falsafa ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuanzisha mkakati wa binafsi wa uinjilisti, ikiwemo uinjilisti wa mmoja kwa mmoja
- Kuanzisha vikundi kiini kwa msisitiza juu ya uinjilisti
- Kutumia njia ya kujifunza neno kwa kulifuata binafisi na kwenye vikundi kiini

| MWONGOZO WA TATU: | Msisitizo juu ya Ufuasishaji, Vita Vya kiroho, Vikundi na Kufanya Kazi Kwa Timu |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuwatambua na kuwaelimisha viongozi nyeti wa vikundi kiini
- Kutumia muda katika maombi na kufunga
- Kutathimini mtazamo wa dunia wa wapanda kanisa ukilinganishwa na mtazamo wa dunia kibiblia
- Kutumia ukweli wa maandiko kupinga vipingamizi vya kiroho katika maisha na katika huduma ya wapanda kanisa
- Kuunda mpango binafsi wa kufanya ufuasishaji kwa watu wanaojihusisha katka huduma ya upandaji kanisa
- Kufanya maendeleo ya timu na shughuli za kutathimini
- Kuchanganua vipawa vya kiroho vya wapanda kanisa na vya timu ya upandaji kanisa

## MONGOZO WA NNE: Msisitizo Juu ya Uongozi na Uwakili Mwema

**Vitu Maalumuu vya Kutekeleza**

- Kutathimini uwezo na udhaifu wa mtindo wa uongozi wa huduma ya mpanda kanisa, kwa msisitizo juu ya njia za mwingiliano wa mtu binafisi na wengine
- Kushirikisha kanuni za kiongozi mtumishi kwenye maisha na huduma ya mpanda kanisa
- Kufuatilia matumizi ya muda katika maisha na huduma ya mpanda kanisa, kuweka vipao mbele, na kutengeneza ratiba
- Kutathimini utoaji fedha wa mpanda kanisa, vilevile na wa kanisa lenyewe lililopandwa
- Kutazama kwa upya nafasi ya mke na mme kibiblia na wajibu ambao wapanda kanisa wanao kwenye famila zao
- Kuongoza vikundi kiini vilivyopo katika utaratibu wa kuongezeka mara dufu
- Kuandaa mpango wenye mkakati utakaoelekeza kwenye huduma ya kueneza upandaji kanisa

## MWONGOZO WA TANO: Msisitizo Juu ya Kuongezeka Mara Dufu, Kuhamasisha Wengine, na Kuchochea Harakati za KUM

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuanzisha Ushirikiano wa huduma na vikundi vingine vya kiinjili katika eneo linalolengwa
- Kupanga na kuweka muundo wa usimamizi kwa vikundi kiini ambao utachochea kukua kunakoendelea na kuongezeka mara dufu
- Kuwafundisha watu kuomba kwa ajili ya Ongezeko la upandaji kanisa; kuhamasisha maombi katika mji, mkoa na hata katika ngazi ya Taifa
- Kuanzisha na kuweka mpango kwa mkufundisha na kushauri wapanda kanisa wapya
- Kuwezesha na kutoa viongozi wapya kwa ajili ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuchochea maono katika makanisa mapya kwa wamisionari kujihusisha siyo tu katka eneo lao wanalolenga, bali pia mpaka “miisho ya dunia”

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya MISINGI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA KWANZA

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Njia za Kujifunza Biblia (NKB) | Uinjilisti (UI) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 1:**<br>"Z" Kufikiri<br><br>**Somo la 2:**<br>Utume Mkuu na Upandji Kanisa<br><br>**Somo la 3(3A):**<br>Mzunguko wa Upandaji Kanisa 3A: *Vielezo vya Upandaji Kanisa*<br><br>**Somo la 4 (4A, 4B)**<br>Kanuni za Utafiti 4A: *Kulifahamu Eneo unalolenga*<br>*4B: Mifano ya Maswali ya Utafiti* | **Somo la 1:**<br>Misingi ya Kibiblia kwa Ajili ya Kanisa<br><br>**Somo la 2 (2A):**<br>Kusudi la Kanisa<br>2A: *Karatasi ya Mazoezi Kwa Utume Mkuu*<br><br>**Somo la 3 (3A):**Mfumo na Kazi<br>3A: *Mfumo na Kazi Iliyotumika*<br><br>**Somo la 4:** Kutafsiri Maana ya Kanisa la Mtaa | **Somo la 1 (1A)**<br>Kuhesabiwa Haki Kwa Imani<br><br>**Somo la 2:** Kuishi Kufuatana na Injili<br><br>**Somo la 3:**<br>Ukuaji wa Mkristo<br><br>**Somo la 4:**<br>Nguvu ya Injili Inayobadilisha<br><br>**Somo la 5:**<br>Kutunza Kumbukumbu za Maisha ya Kiroho | **Somo la 1, 2:**<br>Kongamano la Maombi:<br>Kuombea Uamsho<br><br>**Somo la 3 (3A):**<br>Jinsi ya Kuwezesha Maombi<br>3A: *Maombi ya Utatu* | **Somo la 1 (1A):**<br>Utangulizi wa Njia za Kujifunza Biblia Kwa Kufata Neno<br>1A: *Jinsi Tulivyopata Biblia*<br><br>**Somo la 2 (2A):**<br>Kulichunguza Neno la Mungu<br>2A: *Lugha ya Biblia*<br><br>**Somo la 3:**<br>Warsha ya Uchunguzi<br><br>**Somo la 4 (4A):**<br>Kufafanua Neno la Mungu<br>4A: *Majedwali ya Biblia*<br><br>**Somo la 5:**<br>Warsha ya Ufafanuzi<br><br>**Somo la 6:**<br>Kulitumia Neno la Mungu<br><br>**Somo la 7 (7A):**<br>Warsha ya Kulitumia Neno la Mungu<br>7A Waefeso-an 1.B.S. | **Somo la 1:**<br>Utangulizi Juu ya Uinjilisti<br><br>**Somo la 2,3:** Kutayarisha Ushuhuda Binafsi |
| **4** | **4** | **5** | **3** | **7** | **3** |

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KULETA** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA PILI

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Njia za Kujifunza Biblia (NKB) | Uinjilisti (UI) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 5:** Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 6:** Warsha ya Utafiti<br><br>**Somo la 7:** Kuhamasisha Rasilimali Kupitia Utafiti | **Somo la 5:** Asili ya Kanisa<br><br>**Somo la 6 (6A):** Kazi za Umoja za kanisa<br>*6A: Ubatizo Katika Agano Jpya*<br><br>**Somo la 7:** Kuandaa Maelezo ya Kusudi la Kanisa<br><br>**Somo la 8 (8A):** Falsafa ya Huduma ya Upandji Kanisa<br>*8A: Kuanzisha Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa* | **Somo la 6:** Kuishi Kama Wana Badala ya Mayatima<br><br>**Somo la 7 (7A):** Kujifunza Kuwa Wana<br>7A: *Yatima Dhidi ya Wana* | **Somo la 4:** Kongamano la Maombi: Kuabudu na Kuritafakari neno | **Somo la 1 (1A):** Misingi ya Kibiblia ya Uongozi *1A: Mchanganuo wa Uongozi*<br><br>**Somo la 2 (2A):** Sura ya kiongozi<br>2A: *Hadhi ya Kiongozi* | **Somo la 1:** Kazi na Faida za Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 2 (2A, B):** Kanuni za Uongozi wa vikundi Kiini<br>*2A: Vikundi Kiini Vivunja Barafu*<br><br>2B: *Mifano ya Shughuli*<br><br>**Somo la 3 (3A):** Kuanzisha Vikundi Kiini<br>3A: *Karatasi ya Upangaji*<br><br>**Somo la 4 (4A):** Uinjilisti wa Vikundi Kiini<br>4A: *Kuhusu "Oikos"*<br>**Somo la 5:** Kuonyesha Mfano wa Kikundi Kiini<br><br>**Somo la 6**:<br>Falsafa ya Huduma ya Vkundi Kiini | **Somo la 8 (8A):** Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Njia ya Kujifunza Biblia Kwa Kulifata Neno<br><br>**Somo la 9 (9A,9B)** Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kulifuata Neno<br>9A: Mafunzo ya Mathayo 20:17-28<br>9B: Kujifunza Juu ya LK 15:1-7<br><br>**Somo la 10, 11 (10A):** Warsha ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno<br>*10A: Vfungu Kwa Ajili ya IBS* | **Somo la 4 (4A):** Uinjilisti na Upandaji wa Kanisa<br>*4A:Kutathimini Mikakati ya Uinjilisti*<br>**Somo la 5 (5A.5B):** Vizuizi dhidi ya Mafanikio ya Injili<br>*5A: "Kanisa kwa Watu Wote"*<br>*5B: Kujibu Juu ya Kupinga kwa Kawaida*<br>**Somo la 6;7 (6A,6B,6C**) Utaratibu wa kukata Shauri<br>*6A: Sura ya Mtu katika Kuinjilisha*<br>*6B:Kanuni Tatu*<br>*6C: Kuchunguza Njia Aliyotumia Yesu* |
| **3** | **4** | **2** | **1** | **2** | **6** | **4** | **4** |

Namba katika mabano (27) zina maanisha mwishoni

## Kimsingi inagusia **Awamu ya UANZILISHI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

### MTAZAMO WA MEONGOZO WA TATU

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Uinjilisti (UI) | Kufuasa (KS) | Vita Vya Kiroho (VK) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 8:** Kusonga Mbele kwa Kwanza<br><br>**Somo la 9:** Asili ya Harakati za Upandaji kanisa | **Somo la 9,10:** Kanisa na Vipawa Vya Kiroho<br><br>**Somo la 11:** Nguvu Za Kijamii za Kanisani | **Somo la 8,9:** Sheria na Injili<br><br>**Somo la 10 (10A):** Toba Kama Njia ya Maisha<br>*10A: Sehemu ya Wenye Dhambi* | **Somo la 5:** Maombi na Kufunga<br><br>**Somo la 6,7:** Kongamano la Maombi: Kuombea Kuenea kwa injli | **Somo la 3:** Mzunguko wa Uongozi<br><br>**Somo la 4:** Utangulizi kwa Kazi ya Timu<br><br>**Somo la 5:** Maendeleo ya Timu | **Somo la 7 (7A)** Nguvu ya Majadiliano ya Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 8:** Kutunza Watu Walio Kwenye Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 9:** Kufundisha Viongozi Wapya wa Vikundi Kiini | **Somo la 8:** Injili ya Mahusiano | **Somo la 1:** Utangulizi katika kufuasa<br>**Somo la 2 (2A):** Jukumu lako Katika Kufanya Wanafunzi<br>*2A:Tabia ya Upendo wa Kikiristo*<br><br>**Somo la 3 (3A):** Fahamu Lengo Lako, Fahamu Watu Wako<br>*3A:Imani, Tumaini na Upendo*<br><br>**Somo la 4 (4A)**:Kuwasaidia Wanafunzi Kukua Kiroho<br>*4A:Kukua Kiroho Kunahitaji Tathimini*<br><br>**Somo la 5(5A):** Mifumo ya Kufuasa<br>*5A:*<br>*Kufanya Mpango wa Kufuasa* | **Somo la 1:** Kuelewa Mtazamo wa Kidunia<br><br>**Somo la 2:** Nguvu za Vita vya Kiroho<br>*2A: Mafunzo ya Waefeso 4:17-5:21*<br><br>**Somo la 3: (3A,3B):** Mashambulizi ya Kiroho<br>*3A: Kujifunza Biblia*<br>*3B: Mchanganuo Kutoka Ulimwenguni Kote* |
| **2** | **3** | **3** | **3** | **3** | **3** | **1** | **5** | **3** |

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KUFUNDISHA** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTZAMO WA MWNGOZO WA NNE

| **Maono ya KUM (MO)** | **Kanisa (KA)** | **Tabia ya Kiroho (TK)** | **Maombi (MB)** | **Uongozi (UO)** | **Vikundi Kiini (VK)** | **Kufuasa (KS)** | **Uwakili Mwema (UM)** | **Familia (FA)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 10 (10A, 10B):** Vipengele vya Mkakati kwa Harakati za Upandaji Kanisa<br>*10A: Imani na Utii dhidi ya Hofu na Kutokuamini*<br>*10B: Vitu Vinavyoamsha Ukuaji wa Asili*<br><br>**Somo la 11:** Dalili za Harakati<br><br>**Somo la 12:** Uangalizi Kati Kati ya Harakati | **Somo la 12:** Nguvu ya Makanisa yanayoibuka<br><br>**Somo la 13:** Tabia ya Makanisa Yanayokua<br><br>**Somo la 14:** Serikali ya Kanisa na Ofisi za Kanisa: | **Somo la 11:** **U**pendo Kama Msingi kwa Huduma<br><br>**Somo la 12:** **K**uuelewa Moyo wa Baba<br><br>**Somo la 13:** Neema ni Kwa Wanyenye kevu | **Somo la 8, 9:** Kongamano la Maombi Kuomba Kibiblia | **Somo la 6 (6A):** Uongozi wa Kitumishi<br>*6A: Orodha ya Viongozi*<br><br>**Somo la 7:** Nguvu za Uongozi<br>**Somo la 8:** Mitindo ya Mwingiliano<br><br>**Somo la 9:** Mahitaji ya Uongozi<br><br>**Somo la 10 (10A):** Kufunza Viongozi Wapya<br>*10A:Hadhi za Kutia katika Uongozi Mpya* | **Somo la 10:** Majadi-liano ya Maswali na Matatizo ya Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 11:** Kuzidisha Kwa Kikundi Kiini | **Somo la 1:** Warsha ya Kufuasa | **Somo la 6:** Utangulizi juu ya Uwakili Mwema<br><br>**Somola 2:** Uwakili mwema Kwenye Fedha<br><br>**Somo la 3:** Matumizi ya Muda<br><br>**Somo la 4:** Utaratibu wa Upangaji Kimikakati<br><br>**Somo la 5:** Warsha juu ya Utaratibu wa Upangaji Kimikakati | **Somo la 1:** Majukumu ya Kibiblia Katika Familia<br><br>**Somo la 2:** Kulea |
| **3** | **3** | **3** | **2** | **5** | **2** | **1** | | |

Namba katika mabano (25) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KUZIDISHA NA HARAKATI** Katika Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA TANO

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Kuhubiri (KR) | Familia (FA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 13:** Maono na Kupiga Darubini<br><br>**Somo la 14:** Kuhamasisha<br><br>**Somo la 15:** Hatua Inayofuata<br><br>**Somo la 16:** Mafunzo Kama Sehemu ya Harakati za Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 17:** Kuhamasisha Viongozi Kupitia Uanzilishi wa Kitaifa | **Somo la 15:** Malezi ya Kanisa<br><br>**Somo la 16:** Ibada ya Umoja katika Kanisa la Mtaa<br><br>**Somo la 17:** Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja Katika Kanisa la Mtaa<br><br>**Somo la 18:** Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo<br><br>**Somo la 19:** Mguso wa Kihistoria wa Kanisa __ (Historia ya Kanisa Katika Mandhali ya Nchi) | **Somo la 15:** Huduma ya Upatanishi<br><br>**Somo la 16:** Unyoofu wa Maadili Kwa Wapanda Kanisa | **Somo la 10:** Maombi ya Kuwezesha kwa Harakati za Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 11,12:** Kongamano la Maombi: Kumshukuru Mungu Kwa Ajili ya Uaminifu wake | **Somo la 11:** Kutoa Viongozi<br><br>**Somo la 12:** Uongozi wa Harakati<br>*12A: Viongozi wa Harakati* | **Somo la 12:** Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa<br><br>**Somo la 13 (13A):** Kusimamia vikundi Kiini<br>*12A: Hatua ya Mwisho* | **Somo la 1:** Mahubiri ya Kibiblia 1: Kuelewa Ujumbe<br><br>**Somo la 2:** Mahubiri ya kibiblia 11: Kuelewa Wasikilizaji<br><br>**Somo la 3:** Mahubiri ya kibiblia 111: Kujielewa Mwenyewe | **Somo la 3:** Huduma Kwa Famila |
| **5** | **5** | **5** | **3** | **2** | **2** | **3** | **1** |

Namba katika mabano (23) zina maanisha mwishoni

**JUMLA YA MASAA YA KOZI YOTE: 127**

# MAONO YA KUM

MAONO YA KUM

SOMO LA 10

# Vipengele vya Mkakati kwa Harakati za Upandaji Kanisa

☞ **Kusudio la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha jinsi ya kufanya kazi kimkakati kuelekea harakati za upandaji wa kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Mkakati kwa kifupi ni njia ya ufanisi kwa ajili ya kukamilisha kazi.
- Mikakati ya aina fulani ya huduma inasisimua harakati za upandaji kanisa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa jinsi ya kufanya kazi kimakakati kuelekea upandaji kanisa.
- Kuelewa ni mabadiliko gani yanatakiwa yafanyike katika eneo lake ili kuona harakati zinatokea.

☞ **Ziada**

10A Imani na Utii dhidi ya Hofu na Kutoamini

10B Vitu vinavyosisimua Ukuaji

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Mikakati hii, ingawa ni ya kibiblia, siyo amri za lazima. Badala yake, ni mikakati inayotumika na mifano ya walichofanya mitume katika hali zinazofanana na hiyo ambayo wapanda kanisa wanaweza kukutana nayo.

## UTANGULIZI

Mkakati ni njia ya ufanisi kwa ajili ya kukamilisha kazi. Inasemekana kuwa ujasiri na ushujaa umeshinda vita vingi, lakini mkakati huo umeshinda zaidi. Hili linaelezewa kwetu katika kitabu cha Yoshua. Ushindi wa ardhi ya Kanaani chini ya amri ya mtumishi wa Mungu Yoshua hakika ulikuwa wa kimkakati. Kwa kampeni tatu za ghafla, moja kupitia ndani, nyingine kusini na nyingine dhidi ya jeshi lililoungana la kaskazini, Waisraeli walipata kutawala ardhi pamoja na kwamba adui alibakia. Jeshi la Yoshua halikuwa limeandaliwa sawasawa, imara au kuhesabika zaidi kuliko wakanaani. Lakini kwa msaada wa Mungu kimkakati waliweza kumshinda adui. Mkakati una nafasi halali na muhimu siyo tu katika mashambulizi ya asili, lakini pia katika nyara (mateka) za kiroho za ulimwengu (Berkhof, p. 25). Katika somo hili tutachunguza mikakati kadhaa ambayo inaweza kutumika kuelekea harakati za Kueneza Upandaji Kanisa.

## I. KUJENGA IMANI KATIKA MAONO

Tabia muhimu zaidi kwa harakati za kueneza upandaji kanisa ni maono. Siyo kila mmoja atayakubali maono mara moja kuona makanisa yamepandwa kwenye eneo analoweza kufika kila mmoja. Baadhi watayapinga na wengine watakuwa kinyume nayo kama wanajua kuwa ni kweli lakini hawataungana nayo kwa moyo na roho. Lakini bado kutakuwa na wengine ambao mioyo yao imekuwa na shauku ya kusikia Mungu anachotaka kufanya kupitia kanisa lake na watayaunga mkono.

## A. Hamasisha kwa Ajili ya Maombi

Kama unataka kushinda upinzani na kuona harakati za kueneza upandaji kanisa katika eneo lako, unatakiwa kutafuta haja ya Mungu kwenye eneo. Hili linafanyika vizuri zaidi kwa maombi. Maombi ya mashambulizi kwa namna ya hekima kuhusu Mungu anachotaka kwa ajili ya eneo ni njia ya ufanisi ya kuunganisha watu na kupenyeza maono kuhusu utimizaji wa Utume Mkuu. Watu wanaoomba mara chache wana matatizo ya kukubali maono ya Mungu ya kueneza upandaji kanisa. Maombi yanawaleta pamoja hao ambao wamekuwa na shauku ya harakati kuu za Mungu kugusa taifa lao, watu wao na eneo lao.

Harakati za upandaji kanisa zinaweza kuendelea tu kama zikichochewa kwa maombi. Tokea mwanzoni, kanisa la kwanza lilijitoa kwenye maombi lenyewe (Mdo 2:42), na hata mateso yalipozidi, waumini walifanya mkutano wa maombi (Mdo 4:23-31). Mbele ya upinzani mkuu, waliomba kwa ajili ya ushupavu wa kutangaza imani zao bila hofu na aibu.

Paulo alielezea hitaji la maombi ya hali ya juu ya mpanda kanisa katika Waefeso 6:19-20. Aliomba mara mbili kwa ajili ya ujasiri wa kutangaza injili. Paulo pia aliomba kwamba waombe kwa ajili ya maneno sahihi, kutolewa kwake, maneno ambayo yanayopelekea mioyo ya watu kuamua kumpokea Kristo, na kwamba asiwe na hofu.

Hao wanaoomba wanachangia kwenye mafanikio ya hao wanaopanda makanisa. Kama unataka kuona harakati za upandaji kanisa katika eneo lako, moja zaidi ya vitu vya kimkakati unavyoweza kufanya ni kutia moyo maombi ya ushupavu.

## B. Uliza "Ni Nini Mungu Anataka?"

Njia nyingine ya kujenga ushawishi na maono ni kuuliza kila mara swali la "Z" –"Ni nini Mungu anataka?" Hiki kinatakiwa kiwe kichwa cha maombi, Mafunzo ya Biblia. Mahubiri, ma upangaji wa huduma.

Katika kujibu swali, tunajifunza kwamba Biblia inaweka wazi kwamba Mungu anafanya mpango wake kuukomboa ulimwengu kupitia watu wake. Hili linaonekana wazi katika maisha ya Ibrahimu baba wa imani. Ibrahimu alibarikiwa ili kwamba aweze kuwabariki wengine (Mwa 12:1-3). Hili lilikuwa kusudi la Israeli. Kusudi la kanisa ni sawa na hilo. Yesu alisema tulichaguliwa "... kuzaa matunda" (Yohana 15:16). Tunatakiwa kushuhudia katika namna kwamba ulimwengu usioamini uguswe.

Kwa kujifunza historia ya watu wa Mungu kunadhihirisha mambo mawili dhahiri na mwitikio tofauti hasa kwenye mapenzi ya Mungu. Jibu la kwanza ni lile la mashaka na kutokutii; la pili linatokana na imani inayopelekea utii.

### 1. *Mwitikio wa Mashaka na Kutotii*

Hatima ya haja ya Mungu iko wazi. Lakini wengi wataitikia kwa kukwepa kuhusu uhalisi wa matokeo yake. Mfano mzuri zaidi wa kibiblia wa hili unapatikana katika Hesabu 13:26-33 wakati wapelelezi 12 waliporudi kutoka ardhi ya Kanaani Mungu aliyowaahidi. Wapelelezi kumi, wakiwa wameona ugumu wa kazi, walifikia uamzi "Hatuwezi kuwashambulia watu hao kwa kuwa wana nguvu kuliko tulivyo" (Hes 26:13:31). Kutokuamini kwao kulizaa kutotii, ambako kulipelekea Waisraeli kuadhibiwa.

### 2. *Mwitikio wa Imani na Utii*

Kalebu, pia miongoni mwa wapelelezi 12, aliona changamoto zote zinazohusiana na utekaji wa ardhi. Lakini Kalebu mtu wa imani alisema, "Tunatakiwa twendelee juu na kuimiliki ardhi, kwa kuwa hakika tunaweza kufanya hivyo" (Hes 13:30). Imani ya Kalebu ilipelekea haja ya kumtii Mungu.

Kama mwandishi wa Waebrania anavyosema, "Bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu" (Ebr 11:6). Katika sura hiyo hiyo tunasoma mashujaa wakuu wa Agano la kale— Hao "ambao **kupitia imani waliteka falme**, wakaendesha haki na **kupokea kilichokuwa kimeahidiwa"** (Ebr 11:33). Imani ni muhimu kuona kile Mungu anachotaka. Ili harakati za upandaji kanisa katika eneo lako kuwa halisi, ni lazima ujenge imani katika maono. Mwitikio kwa imani utabarikiwa na Mungu! (Tazama Ziada 10A).

## II. WEKA MALENGO KUFUATANA NA IMANI

Wakati watu wa Mungu wanapoweka malengo, yatakuwa vielelezo dhahiri vya maono. Kumbuka, unapokuwa unaweka malengo kuna vitu ambavyo unaweza kupanga kufanya na kuna vitu unavyoweza kutumaini kuona vinatokea. Kwa mfano, mpanda kanisa anaweza kuwa na lengo la kuwaleta watu 10 kwa Kristo katika eneo maalumu linalolengwa kwa mwaka. Hili ni lengo ambalo mpanda kanisa anatumaini kuona likiwa limeonekana. Kwa kuwa kukata shauri kunahusisha utayari wa watu wengine kushiriki, mpanda kanisa ana kiasi fulani tu cha kuweza juu ya matokeo.

Kwa kuungwa na lengo hapo juu, mpanda kanisa anaweza kuwa na lengo la kushirikisha Kristo kwa watu 100 kwenye eneo linalolengwa mwaka huu. Lengo hili zaidi linahusika na shughuli na kuziendesha kuliko matokeo, na mpanda kanisa anaweza kufaulu hilo. Inaweza kuwa inachanganya sana kwa watu kuweka lengo kama la kwanza. Lakini wasiwe na mpango wa kuona limefaulu, kama lengo la pili linavyojieleza.

**MFANO**


Kanisa la Muria huko Indonesia lina mipango bora ya ukuaji. Kati kati ya miaka ya 1980 walikuwa na karibu ya makusanyiko sita yenye waumini kwa pamoja zaidi ya 500. Viongozi waliweka malengo ya kuwa na waumini 10,000 kufikia mwaka 2,000. Lengo hili linaweza kuwa lilionekana lisilowezekana kabisa, hata hivyo leo wako zaidi ya ratiba. Wanalifikia lengo kwa kulivunja vunja katika malengo madogo madogo. Kila mtu kumuuongoza mtu kwa Kristo kila baada ya miaka mitatu, wakati kila kusanyiko kazi yake ni kupanda kusanyiko jingine kila baada ya miaka mitatu. Kukua kutoka 500 mpaka 10,000 katika miaka 15 hakutokei kwa kuwa tu lengo hilo limewekwa (Shenk, p. 66-67).

## III. FANYIA MAZOEZI KUZIDISHA BADALA YA KUONGEZA

Kuongeza ni njia ya kawaida kwenye huduma. Tunafikiria kuongeza kanisa moja jipya, kuanzisha kikundi kimoja zaidi kidogo, kumuuongoza mtu mmoja zaidi kwa Kristo. Hii ni mikazo mizuri. Lakini namna ya Mungu siyo ya kuongeza—ni kuzidisha (2Tim 2:2).

Kanauni ya kuzidisha inahusika na uinjilisti, ufuasishaji, vikundi kiini, upandaji wa kanisa, maendeleo ya uongozi na mengineyo. Waliokata shauri wapya wanatakiwa wafundishwe kutafuta wakata shauri wengine, vikundi kiini vinatakiwa vizidi kila mara, makanisa yanatakiwa yazaliane na kupanda makanisa binti. Viongozi wanatakiwa wafundishe viongozi wengine wa kuendelea kufundisha viongozi wajao. Yote haya ni kuzidisha. Kwa vitendo, kanuni ya kuzidisha ina maanisha tunatakiwa tuweke njia za huduma na mitindo ambayo inazalisha kwenye utamaduni. Mitindo ya upandaji kanisa ambayo inategemea zaidi msaada kutoka nje au watalaamu inaweza isiwe ya kuzalisha. Vipindi vya mafunzo vinavyohitaji mda mrefu wa kukaa kujifunza pia ni vigumu kuzalisha.

**Kielelezo 10.1. Kuzidisha Dhidi ya Kuongeza**



## IV. FANYA KAZI KIMKAKATI KUTOKEA KWENYE KITOVU KULIKO TU KWA MBALI

Kila mpanda kanisa ana mahali pa kuanzia. Tumeshaona jinsi Paulo alivyochagua kimkakati mahali pa kuanzia ambapo atapanda makanisa ili kwamba yaongezeke ili kueneza eneo linalozunguka (Mwongozo wa Tatu Somo la Maono ya KUM 8). Miji ya biashara na vitovu vya usafirishaji vinaweza kutumika kuchochea injili.

Kuchagua vitovu vya kimikakati ni utaratibu unaoendelea. Mwanzoni mwa kanisa la Agano Jipya, Yerusalemui ulikuwa ni chimbuko ambapo kanisa liliendelea kwenda nje. Kitovu kinachofata cha kimkakati lilikuwa ni kanisa la Antiokia. Tokea pale, kadiri viongozi wa Antiokia walivyomwabudu na kumtangaza Mungu, Roho Mtakatifu alimtuma Barnabas na Sauli kupeleka injili mpaka kwa mataifa (Mdo 13:1-3).  Sehemu inayofata ya kimkakati ilikuwa Efeso, njia panda kwenda Asia na katikati mpaka kwenye majimbo manne (Galatia, Asia, Masedonia na Akia) ambapo Paulo aliweka zaidi huduma yake ya upandaji kanisa. Hatimaye Urumi, mji mkuu wa falme uligeuka kuwa kitovu cha kimkakati kwa ajili ya injili kusonga mbele.

Kufanya kazi kutokea kwenye kitovu cha kimkakati kunahusu uinjilisti vile vile na ufundishaji. Mafunzo ya mkazo katika maeneo ya kimkakati yanawaruhusu wapanda kanisa kumeza kikamilifu ujuzi wa huduma na mitindo ili kwamba waweze kwa ufanisi kuzalisha ujuzi na mifumo hiyo kwenye maisha ya idadi iliyozidi ya waufuasi kutoka kwenye eneo kubwa linalolengwa.

Kuanzisha mkakati wa kihali ya eneo kwa ajili ya kufundisha unaweza kupelekea watu wengi kuandaliwa. Tafuta maeneo ya kimkakati katika nchi ambapo kuna kukubaliwa kwa mafunzo ya wapanda kanisa. Viongozi wa mtaa wanaoshughulika na upandaji kanisa na wanaotaka kuhamasisha wengine katika maeneo yao wanaweza kufanya ufundishaji wa kupanda kanisa kwa msaada wako. Hii itasaidia mafunzo kuzidi na hatua ya hakika kuelekea harakati.

**MFANO**

Mradi 250, na ofisi zake kuu huko Moscow,ni huduma inayotafuta kutimiza Utume Mkuu katika Muungano wa Urusi wa zamani kupitia upandaji kanisa. Mkakati ni kufunza na kuhamasisha wapanda kanisa 250 katika vitovu vya maeneo 250 ya kimkakati katika Muungano wa Urusi ya zamani utakaopelekea makanisa mapya 62,500 kufikia mwaka 2020. Mkakati huu usio wa katikati unakuza kuhusika kwa ndani na umilikaji.

## V. ANZISHA TIMU ZA KUWEZESHA ZINAZOKWENDA HUKU NA HUKO

Agano Jipya linadhihirisha dharura ya jamii ya timu za wamishenari zinazokwenda huku na huko akiwemo Barnabas, Paulo, Yohana Marko, Sila Timotheo, Epafra, Prisila,  Akwila, Apolo, Luka, Dema, Tito, Ephaphrodito na wengine. Watenda kazi hawa walipanda, waliimarisha, na kuongoza makanisa mapya kutoka Galatia mpaka Urumi. Swali ni kwamba, kwa nini wawezeshaji hawa wa kuhamahama walikuwa wa lazima? Mitume kumi na moja walijitoa wenyewe kwenye maombi, usimamizi na kufundisha, ambako kulipunguza uwezo wao wa kupanda kanisa. Walikuwa wakiendelea kwa undani katika maarifa ya Mungu kutangua uzushi na mabishano ya siku hiyo. Kwa upande mwingine, makanisa mapya yalikuwa yana watu wa ndani kutokea kwenye jamii zao. Mara nyingi watu hawa wa ndani walipungukiwa kwa kutokuhamia mahali ambapo makanisa mapya yalihitajika kupandwa. Kwa hiyo, uhamaji, viongozi waliofunzwa walifanya kazi kama wapanda kanisa, walimu, viongozi, watia moyo, watatuzi wa matatizo na wajumbe wa kusanyiko jipya.

Viongozi wa mtaa waliojiimarisha wanaweza kuwa wamesongwa sana na usimamizi na kazi za kichungaji ili kuweza kuhusika kupanda makanisa mapya. Harakati za upandaji kanisa zinahitaji kwamba jumuia ya wamishenari ya viongozi wanaohama kuhamasishwa, kufundishwa, na kutumwa nje. Viongozi hawa kisha wanatenda kama daraja kati ya viongozi wa taifa na makanisa ya mitaa kupanua haraka zaidi za injili kwa kupanda makanisa mapya.

Maendeleo ya timu kama hiyo katika nchi yako inaweza kuwa mkakati muhimu wa kuendeleza injili katika eneo lako lote. Wajumbe wa timu ya kuwezesha wanatakiwa kuwa wafanyakazi wanaoheshimiwa walio na maono ya KUM na wanaweoza kufundisha, kuandaa na kuhamasisha wengine. Kama timu, wanaweza kusaidia wapanda kanisa na kutia changamoto wengine kuhusika katika upandaji kanisa. Wanaweza kufanya mambo haya vizuri zaidi wanapokuwa hawakufungwa na kanisa maalumu la mtaa kwa kipindi cha mda mrefu. Hili linawapa uhuru wa kusafiri na kupata kuona kile Mungu anachofanya katika eneo wakati huo huo pia ikiwaruhusu kuwa chombo cha sauti ya kwa waumini.

## VI. KUWEZESHA WATU

Harakati za kueneza upandaji kanisa zinahitaji watu waliojawa na mvuto kamili wa kuendeleza injili kwa kuanzisha makanisa mapya kila mahali. Watu hawa wanapotokea, harakati itafanyika zaidi kwa kuwaendeleza katika maeneo ya vipawa vyao. Kuwajenga wengine na maono na kuwatia moyo kutimiza huduma yao kutafanya injili bora zaidi kuliko kuwalazimisha wengine kutimiza kipindi.

**MFANO**

George Whitefield na Yohana Wesley wote walikuwa viongozi wa uamsho wa kiroho wa Uingereza katika karne ya 18. Whitefield alihubiri mbele ya umati kati ya watu elfu sitini na themanini kwa wakati huo na alichukuliwa kama muhubiri mashuhuri kuliko Wesley. Hata hivyo asili ya kimkakati ambayo Wesley alitumia ilipelekea mguso mkubwa. Wesley aliamini kuwa wale wote wasiokuwa viongozi walikuwa ndio ufunguo wa kuenea kwa injili. Alielewa nguvu ya miungano midogo na alijua jinsi ya kuendesha nguvu kazi. Kihekima aliwakusanya wakata shauri wake katika 'madarasa' ambayo leo tungeyaita 'vikundi kiini.' Kisha baadhi ya madarasa katika eneo waliunda 'jamii.' Baadhi ya watu 100,000 walikusanyika katika madarasa 10,000 kwenye kilele cha harakati. Nafasi ya Wesley kama kiongozi katika harakati ilikuwa ni kama msafiri mwezeshaji aliyehubiri, lakini zaidi ya yote kuwajenga viongozi wa jamii (Miller, "John Wesley" na Comiskey, "Mulipuko wa vikundi Kiini Nyumbani").

Ni wangapi tunaoweza kuwajenga? Kuwajenga watu kuelekea harakati za upandaji kanisa kunahitaji:

- Kuwashauri watu zaidi kuliko kuwaongoza.
- Kuwaandaa watu zaidi kuliko kuwaatawala.
- Kuwekeza katika watu zaidi kuliko kuhitaji kutoka kwa watu.
- Kuwatia watu changamoto zaidi kuliko kuwasukuma.
- Kuwatia moyo watu zaidi kuliko kuwahukumu.
- Kuwashawishi watu zaidi kuliko kuwalazimisha.
- Kuwafundisha watu zaidi kuliko kuwapa maelezo.

## VII. ANZISHA MITANDAO

Kama kitu hasa chenye lengo lile lile la upandaji kanisa (na hasa kueneza upandaji kanisa) vinakubaliana kufanya kazi pamoja, harakati itateleza kwa haraka kama shirika vilevile na mtu binafsi watahamasishwa kwa ajili ya kazi. Wakati mwingine miongoni mwa mawakala wa ushirika au maendeleo ya shirika jipya yanaruhusu makundi kufanya kazi pamoja kwa ulaini zaidi.

**MFANO**

Muungano wa Kueneza Upandaji Kanisa umejitoa kwenye kuwezesha wapanda kanisa katika nchi 27 za ulimwengu wa ukomunisti wa zamani katika Mashariki ya mbali ya Ulaya na Asia ya Kati. Watalamu wa Muungano hawawajibiki na kupanda makanisa, lakini kupitia juhudi za Muungano kuwezesha mataifa kupanda makanisa mapya zaidi ya makanisa 2000 yameshaanzishwa. Badala tu ya kutoa samaki (yaani wamishenari kufanya kazi ya upandaji kanisa), Muungano unapendelea kufundisha watu jinsi ya kukamata samaki wao wenyewe. Hii inahitaji kuwasaidia viongozi kukamata maono kwa ajili ya KUM, Kutia moyo maombi kwa ajili ya KUM, kuwafundisha wapanda kanisa, kusaidia kuanzisha utafiti na kufadhili mikutano juu ya maswala yanayohusu KUM.

### A. Kujenga Mawasiliano

Kama zilivyo harakati zote, harakati za upandaji kanisa zinategemea mawasiliano miongoni mwa walio katika harakati kwenda upande mmoja, kuweka wazi na kuendeleza tendo, na kuhalalisha. Mawasiliano mazuri pia yanasaidia kujenga na kuimarisha mahusiano muhimu kati ya watu katika harakati.

Uzalishaji wa maandisha na chombo cha mawasiliano kama vile magazeti, na katika hali zingine kurasa za interneti zinaweza kupeleka karaka na kuhalalisha harakati. Maandishi na uzalishaji wa matangazo vinatakiwa viwe vyenye hadhi ya kuridhisha ambayo watu watapokea na kufanyika vizuri kulingana na mandhali yao.Yanatakiwa yapatikane kwa yote bei na uwezo wa kuyapata. Yanatakiwa yawe ya kiwango cha kumaanisha ambacho kinaletea heshima uwezo wa viongozi kwenye harakati lakini yanayofaa na rahisi kwa wote kuyaelewa.

**B. Kufadhili Mikutano**

Katika harakati, viongozi wanatakiwa kuonana uso kwa uso. Kuwaweka watu pamoja kwa njia ya mikutano, baraza kuu na mashauri ni muhimu pia kwa harakati kutunza nguvu ya kuendelea. Hakuna kinachoweza kuchochea uwezekano kama chumba kilichojaa viongozi wenye hisia sawa. Mikusanyiko mikubwa kama baraza kuu inavuta na kushawishi watu. Matukio madogo kama ushauri yanawaruhusu viongozi kutatua maswala magumu na kuainisha mwelekeo ambao wanatakiwa wachukue katikati ya harakati.

> **MFANO**
>
> BK=2000 na zaidi ni harakati ambazo zinawafanya viongozi wakristo ulimwenguni kote kuwa katika mawasiliano mmoja kwa mwingine. Wanashirikishana malengo yanayofanana, matarajio, na mipango ya kuendeleza injili. Ingawa matukio kama baraza kuu na kutoa ushauri, vinaendelea kuwa katika mawasiliano. Kupitia harakati hizi na vitu vingine Mungu anavyofanya leo, huduma zinashiriki pamoja kuufikia ulimwengu kwa ajili ya Yesu kuliko ambavyo imewahi kutokea.

## VIII.TAFUTA UONGOZI WA MUNGU NA MUDA MUAFAKA

Harakati za upandaji kanisa zinategemea mda muafaka wa ukuu wa Mungu kuliko kipengele chochote cha kimkakati. Kwa sababu hii haiwezekani **kufanya** harakati kutokea. Kwa jinsi hiyo, inawezekana kuunda hali ambayo harakati **zinaweza** kutokea. Tunaona kanuni hii imeelezewa katika maelezo ya Paulo ya kupanda kanisa la Wakorintho. *"I (Paulo) alipanda mbegu, Apolo akamwagilia, lakini Mungu akaikuza "* (1Koro 3:6). Paulo and Apolo (na tunaweza kubunia wenginea) kupitia utii wao walifanya sehemu yao katika kuunda hali ili kwamba Mungu aweze kutukuzwa kupitia kanisa lake linalokua.

Kama vile ambavyo hakuna anayeweza kumfanya Mungu kufanya kwa njia iwayo yote, hakuna anayeweza kumzuia Mungu kama kiukuu anachagua kufanya katika tabia ambayo si ya kawaida. Ngoja tujiangalie na theologia zetu. Tunajaribu wakati mwingine kumlazimisha Mungu kufanya vitu? Katika hali kama hii, inaonekana kana kwamba itakuwa bora kutafuta ni nini Mungu anachotaka kufanya na kuungana nacho. Kisha tunaweza kufurahi kwa vyovyote anavyochagua kujionyesha mwenyewe kwa watu aliotupatia kuwafikia. Ataonyesha nguvu zake kwa njia ambazo mwenyewe amechagua anapofanya kazi kuyafikia mataifa.

## SULUHU

Mikakati tuliyojifunza ni aina ya njia zinazotumika katika sehemu za ulimwengu mahali ambapo harakati za upandaji kanisa zinashamili. "Huduma kama kawaida", ambayo inakazia katika kuongoza na kutawala, haipelekei kwenye kutoa nguvu za Mungu kufanya kazi kupitia watu wake. Kuna mkakati wa aina yoyote ambao ni wa msaada katika eneo lako?

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini maana ya mkakati?
- Kwa nini maono ni muhimu sana katika harakati za upandaji kanisa?
- Kwa nini kuzidisha ni muhimu sana katika harakati za upandaji kanisa?
- Mikakati iliyozungumziwa katika somo hili, ni upi unaofaa kwa hali yako ya sasa? Jinsi gani inaweza kukusaidia kuendelea na juhudi zako za upandaji kanisa?
- Jinsi gani wazo la timu zinazowezesha zinavyofanya kazi katika mandhali yako ya upandaji kanisa? Wapi timu hii inaweza kwenda na jinsi gain zinaweza kutumika.?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Chagua na tumia moja ya mikakati ya upandaji kanisa iliyozungumziwa katika somo hili na shirikisha matokeo kwa mkufunzi wako au mshauri.
- Tazama Ziada 10A. Linganisha orodha kwenye hali ya huduma yako.

## VYANZO


- Comiskey, Joel. *Home Cell Group Explosion*. Houston, TX: Touch Ministries, 1998.
- Correll, Richard C, *The Glory of God Among the Nations*. Grand Rapids: Church Planter Training International, 1998.
- Miller, Basil, *John Wesley*. Minneapolis: Dimension Books, 1943.
- Shenk, David W., and Ervin R. Stutzman, *Creating Communities of the Kingdom, New Testament Models of Church Planting*. Scottsdale, PA: Herald Press, 1988.

MAONO YA KUM *ZIADA*

10A

# Imani na Utii Dhidi ya Kutokuamini na Hofu

Hofu zifuatazo ni vipingamizi vya kawaida kwenye upandaji wa kanisa. Hofu hizi hazina msingi kwa ukweli. Kwa hakika, kifupi ni uongo wa Shetani.

| **"Uongo"**<br>**Kuamini ungo kunapelekea hofu** | **"Ukweli "**<br>**Imani katika ukweli inapelekekea utii** |
|---|---|
| Tunatakiwa kushughulikia kanisa la nyumbani kwanza | Kama vile Ibrahimu alivyokuwa amebarikiwa kuwabariki wengine, kwa hiyo kusudi la kanisa wakati wote linakuwepo nje ya lenyewe. Ukweli ni kwamba katika uchumi wa Mungu, kuna vya kutosha kuangalia makanisa yaliyopo kama tutakuwa waaminifu kwenye misheni ya Mungu. |
| Hatuna viongozi wa kutosha waliofundishwa. | Mara zote hatuna viongozi wa kutosha kwa sababu tunaweka mipaka ya elimu na mda wa maisha ya watu. Ni mfumo wa kukandamiza unaotokana na kumkatisha Roho Mtakatifu kuongoza na kufundisha wengine. |
| Hatuna fedha za kutosha. | Mungu anatoa fedha za kutosha kuona mapenzi yake yanatimia. Luka 6:38 inaonyesha wazi kwamba kama tukitoa, tunaweza kuwa na zaidi kuliko tunavyotumaini. Katika historia yote ya kanisa, watu wa imani wamekuwa wakipewa na baba. |
| Kanisa moja linatosha kwa mji huu. | Kueneza kunamaanisha kushuhudia kunakoendana kiutamaduni kwa kila mtu anayefikiwa. Kama Mungu anatarajia Utume Mkuu kutimizwa kupitia kanisa, hili ndilo Mungu analotaka. |
| Tutaligawa kanisa. | Kuzidishwa kwa mwili wa Kristo ni njia ya asili ya Mungu kuijaza dunia kwa utukufu wake. Roho Mtakatifu ni mmoja na hawezi kugawanywa. |
| Tutapoteza kiwango cha maadili yetu. | Usiogope, kwa kuwa Roho Mtakatifu atakuongoza katika kweli na haki. Atasafisha bibi arusi wa Kristo. |
| Hatuwezi kufanya hili bila msaada wa nje. | Hakuna watu katika uso wa dunia ambao hawana rasilimali kwa ajili ya kazi yao ya kiroho. Tabia hii imezalisha tabia isiyo nzuri ya utegemezi na kuleta mitindo migumu ya kanisa ambayo haiwezi kuzaa wala kizidishwa. |
| Tusingefanya nao kazi.' | Mafarakano na hasira kati kati ya mwili wa Kristo ni silaha kuu ya Shetani kulizuia kanisa kutotimiza misheni ya Mungu.<br>Waefeso 4:26,27 |

Imerithiwa kutoka kwa: Correll, Richard C. *The Glory of God among the Nations*. Grand Rapids: Church Planters' Training International.

**MAONO YA KUM *ZIADA***

**10B**

# Vitu Vinavyosisimua Ukuaji wa Asili

| Vitu Vinavyosisimua Kuenea kwa Injili kwa Asili | Vitu Vinavyoweza Kutosisimua Kuenea kwa Injili kwa Asili |
|---|---|
| Kuanzishwa kwa makanisa | Kuanzishwa kwa umishenari |
| Makanisa yanayojitawala | Kutawala kwa nje kwa makanisa |
| Makanisa yanayojizalisha yenyewe | Makanisa yanayodumaa |
| Makanisa yanayojisaidia yenyewe | Kutegemea nje |
| Kuzidishwa kwa viongozi | Kuongezeka kwa viongozi |
| Kufundisha ukiwa bado kwenye huduma | Kufundisha kabla ya huduma |
| Kuondoka mapema | Kukaa humo milele |
| Kumilikiwa na taifa | Kutegemea viongozi kutoka nje |
| “Z” kufikiri | Kutegemea kuelekezwa |
| Ushirikiano/ulinganifu/Umoja | Mugawanyiko |
| Uanzilisha wa mtaa na umilikaji | Utawala wa mabwana |
| Mafundisho yanayotokana na kanisa | Mafundsho yanayotokana vyama |

Umerithiwa kutoka kwa: Correll, Richard C. *The Glory of God among the Nations*. Grand Rapids: Church Planters' Training International.

MAONO YA KUM

SOMO LA 11

# Dalili za Harakati

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha kwamba upandaji kanisa unaweza kugeuka kuwa harakati

☞ **Wazo Kuu**

- Harakati ni tukio la kijamii ambalo kile kilichokuwa kichache kinakuwa cha kawaida.
- Kuna dalili fulani za harakati ambazo zinaweza kusaidia mpanda kanisa kutambua Mungu anachofanya katika eneo.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapokuwa yameeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa jinsi ya kugundua dalili za harakati.
- Kujua kanuni za huduma zinazopelekea kwenye harakati.
- Kushiriki siyo tu katika kupanda makanisa, lakini kufanya kuelekea harakati za upandaji kanisa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kutambulisha somo hili, kufanya wafunzwa kujadili harakati kutoka kwenye historia zao, za kiserikali na kiroho. Kuzungumzia kanuni za harakati kutoka kwenye mifano hii.

Somo hili linajadili "dalili" sita, za kutambua harakati. Chagua angalau mfano mmoja kutoka kwa kila moja ya maeneo sita na ujadili pamoja na wafunzwa darasani. Kama una mda wa ziada, unaweza kuchagua mengine kadhaa na kufanyia kazi pamoja na wafunzwa. Unapochagua mifano, weka akilini utamaduni maalumu na mandhali ya wafunzwa. Kazia kanuni zilizotumika katika kila mfano, ambao umechangia kwenye kuwezesha upandaji kanisa wa kibiblia na wa afya pamoja na mafundisho kamili na matendo

## UTANGULIZI

Harakati ni tukio la kijamii. Njia moja ya kuelezea harakati za kijamii ni kusema kwamba, " Kile ambacho mara kilichokuwa kichache kinakuwa cha kawaida zaidi." Inahusisha idadi ya watu inayoongezeka ambao wameshawishika juu ya kuhusu sababu ya kawaida, muda unaofaa, na viongozi wanaotamani kufanya mabadiliko ya awali kwenye ***hali iliyopo***. Viongozi maalumu wanaibuka kutia moyo, changamoto na kuongoza makundi yao yanayotarajiwa kuelekea kwenye chanzo. Harakati zinaamusha matukio na shughuli mpya. Kwa kifupi weka, ina maanisha kwamba kitu fulani ambacho walifanya mara chache, na sasa wanakifanya kwa pamoja. Kuna mguso wa kutosha kwenye kundi la watu ambao hata unabadilisha kufikiri kwao, lakini si bila mifarakano kwenye utaratibu.

Harakati za kidemokrasia katika Mashariki ya Mbali ya Ulaya zilizoanza 1989 ni mfano wa harakati za kiserikali. Kama maono ya mabadiliko ya siasa yaliyojaa kwenye mioyo ya watu wa kawaida, mapinduzi yalikuja kwa ghafla, yenyewe, na njia kama mchezo ambayo watu wachache waliweza kutarajia. Kuenea kwa injili katika Agano Jipya, mapinduzi ya waprostanti, uamsho wa Wesley na harakati za upandaji kanisa wa wakati ule yote ni mifano ya harakati za kiroho.

Lengo wazi mafunzo haya ya mpanda kanisa ni kusaidia harakati za upandaji kanisa kutokea katika eneo lako. Kunapokuwa na harakati za Mungu katika taifa, waumini watakuwa na kiu iliyorejezwa kwa ajili ya injili ambayo itawapelekea katika kueneza injili kote kwa upandaji wa kanisa wa haraka na vikindi kiini.

## I. DALILI YA 1: MDA MAALUMU

Mda unapokuwa sahihi, Mungu anapita na kuharakisha kile anachofanya kwenye taifa! Mungu kamwe hawahi wala hachelewi—wakati wote anafanya kile ambacho ni lazima kifanyike kwa mda ulio sahihi.

Kwa harakati kutokea, kunakuwa na hisia laini za uangalifu kuwahi mda. Kati kati ya taifa au kikundi cha kabila, matukio, hali na matarajio yanakuja kwa pamoja katika wakati fulani wa historia kuunda mali mchanganyiko wa mlipuko wa harakati. Katika Biblia, kuwahi mda ni muhimu sana kwamba Mungu mwenyewe aliagiza mda wa harakati. Katika kitabu cha Kutoka, ilichukua miaka mia nne kwa watu wa Israeli kuwa tayari kutoka nje ya Misri, Ilikuwa ni harakati gani! Watu milioni mbili waliondoka Misri iliyokuwa imekumbwa kadiri wingu lilivyowaongoza mchana na moto usiku. Danieli aligundua kuwa mda wa mungu wa miaka sabini umefika alipokuwa akiwaombea Waisraeli kurudi kwenye nchi ya ahadi kutoka kwenye mateka ya falme ya Uajemi (Dan 9:2). Mungu alipomsikia Danieli mawimbi ya Wayahudi yalirudi Yerusalemu. Walilijenga upya hekalu na kuta za mji uliokuwa ukiwa ukawa hai kwa mara nyingine.

wagalatia 4:4 inasema kwamba, “Kwa mda unaofaa Mungu alituma Mwanae..."

Katika Agano Jipya, kuwahi mda pia ni kigezo katika kuanzisha na kuhamasisha kanisa. Wanafunzi wa Yesu waliambiwa kusubiri mpaka watakapopokea Roho Mtakatifu. Walisubiri mpaka Pentekosti (Mdo 1:4; 2:1). Kanisa lilianza siku hiyo, na harakati kuu Yerusalemu zikafuatia. Kukutana katika miji kulienea kuzunguka mji, wakifundisha neno la Mungu. Waumini pia walikutana hadharani. Kwenye nyongeza ya mafundisho, kulikuwa na ushirika, kula pamoja, watu kuomba na wengine. (Mdo 2:42-47).

Harakati nyingine kuu za kanisa zilizoandikwa katika Agano Jipya ni kuendelea kwa hali ya juu kwa injili katika Asia ndogo. Matendo 19:10 inaeleza kwamba, “kila mmoja katika Asia ndogo alilisikia neon la Bwana, wote Wayahudi na Wagiriki." Mda wa Mungu ulikuwa nyeti sana katika harakati kwamba Mungu hata hakuweza kumruhusu Paulo kuingia kwenye mji miaka michache kabla! Matendo 16:6 inamwelezea Paulo na wenzake kama “walikuwa wamezuiliwa na Roho Mtakatifu kutohubiri neno katika jimbo la Asia."

Inaonekana kwamba kuwahi mda ni muhimu sana. Mungu anawaleta watu katika hatua ya kukubali upokeaji wa injili, ujumbe wa harakati za upandaji kanisa, na kuhamasisha kanisa kuhubiri injili ile ile na kupanda makanisa zaidi. Wakazi wanaopokea na kanisa lililohamasishwa linaungana kuunda mwendelezo mkubwa wa injili. Harakati hizi pia zitaacha alama yao katika historia. Kama siyo mda wa Mungu wa mlipuko wa harakati, usikatishwe tamaa—unaweza ukaendelea kujiunga pale Mungu anapotenda hata kwa njia ndogo. Kama mfano wa mbegu ya haradali unavyoeleza, Mungu anaanza vitu vikubwa kutoka kwenye mwanzo mdogo sana. Ni udhihirisho gani unaona kutoka kwenye eneo lako unalolenga kwamba Mungu yuko anatenda? Jinsi gani unaweza kujiunga hapo ukiwa na maono ya harakati za upandaji kanisa—*hata kama ni kidogo sana, muonekano wa mbegu kwenye darubini unaanza? Angalia anachofanya Mungu na wapi anafanya kazi katika eneo lako na jiunge ufanye kazi pale kuelekea harakati za upandaji kanisa.*

**MFANO**

Argentina imejulikana wakati wote kwa ajili ya kiburi cha watu wake. Baada ya kushindwa katika vita kwa Waingereza mwaka 1982, taifa lilinyenyekezwa. Hili lilileta mda maalumu kwa injili kuenea kwa sababu watu wengi walitambua hitaji lao la Mungu walipokutana na janga kama hili la taifa. Kati kati ya miaka mitano maono ya mbeleni ya harakati za upandaji kanisa wa vikundi kiini yaliongezeka kuwa watu 10,000.

## II. DALILI YA 2: UONGOZI UNAOIBUKA

Mara nyingi katika historia ilipoonekana kwamba ufalme wa giza unaelekea kushinda nguvu za haki, Mungu anawaita viongozi ambao,"wanazifahamu nyakati" na kujua nini watu wa Mungu "wanatakiwa kufanya." Katika mda muafaka, siyo mbali sana na si karibu sana, Mungu anaachilia mpasuko kwa kupitia viongozi hawa unaoleta ufalme wa giza kwenye magoti yake. Ndivyo ilivyokuwa kwa Musa, Daudi, Nehemia, Yohana mbatizaji, mtume Paulo, Martin Luther, Yohana Wesley na wengine.

> **MFANO**
>
> Muhubiri wa karne ya 18, Yohana Wesley, alikuwa kiongozi wa namna hiyo. Walimuita "Mtakatifu anayetumika katika falme ya Uingereza" (Miller p. 63). Uamusho ulioendeshwa na George Whitefield huko Uingereza ulianza katika ngazi ya chini ya kiroho wakati makanisa yalipoonekana kutokuwa na nguvu kuigusa jamii kwa ajili ya Kristo. Huduma ya Wesley ilipelekea kukata shauri kwa mamia ya maelfu na kuwa na mguso wa kijamii ambao ulisaidia kuamsha mageuzi kama yale ya Ufaransa. Uamsho wa wesley uliotapakaa kote Marekani, na uliongozwa na Jonathani Edwards na Fransisi Asbury, ulipelekea kueneza upandaji makanisa ya kuabudu ya kimethodisti.

Harakati zote zinahusu uongozi. Ili harakati za kueneza upandaji kanisa kutokea, viongozi lazima waibuke. Lazima wachochee maono, kuendeleza viongozi wapya, na kuwashawishi viongozi waliopo kusaidia na kujiunga na harakati. Kadiri harakati zinavyopamba moto, viongozi wapya wanaanza kuibuka kuziendeleza mbele.

Kama safu ya boti inayoelekea kukata maji kwenye mawimbi mazito, viongozi hawa kila mara watakutana na baadhi ya vipingamizi. Kila mara, Unapokuwa unaongoza mabadiliko kwenye ***hali iliyopo***, hao wanaoongoza harakati tokea mwanzo ni wana mageuzi zaidi. Asili hii ya mageuzi inaweza kuwa kama farasi asiyehasiwa kwenye kundi la farasi, akitia changamoto hao wote ambao wamekuwa kwenye kundi kwa mda—wanaosababisha msuguano. Bundi wanaweza kuruka kama viongozi wanatikisa na kupamba moto! Watu watapamba moto kwa kile viongozi wanachosimaia kwenye harakati—baadhi kuchangia na wengine kupinga

Harakati kawaida zinaweza kupamba moto kutokea kwenye kupingwa kwa kuwa upinzani unawalazimisha viongozi kurekebisha, kuimarisha, na kuendeleza hisia zao za mwelekeo na mvuto. Pengine, kama viongozi wa harakati za wakristo wanashikiria mawazo ya mara moja ambayo siyo ya kibiblia, watarekebisha mwelekeo wao na mvuto kuelekea kwenye nafasi ya kibiblia.

Baadhi ya viongozi wanatupa maono na mawazo (kama vile mitume, kutoka kwa Isaya mpaka kwa Yohana mbatizaji). Wanahitaji mabadiliko, lakini kuyahamasisha kwa kuingia kwa ndani kwenye matamanio ya mioyo ya watu kwa ajili ya Mungu kufanya kazi miongoni mwao. Wanapokuwa wanatangaza kusudi la Mungu kwa ajili ya watu wake, wanafanya kazi kuwashawishi kuondoka kutoka kwenye *hali halisi* na kufata mpango wa Mungu. *Harakati za upandaji kanisa zinahitaji viongozi watakaosihi sababu za kueneza upandaji kanisa kwa viongozi wengine wanaoweza kuwa wakatazi wa kupokea maono haya.*

Mtume Petro alilifanya hili vizuri zaidi katika mahubiri ya hadharani alipokazia kwenye matumaini na ndoto za mioyo ya Wayahudi. Alinukuru maandiko yake na yao kutoka kwa nabii Yoeli. Ujumbe wake uliamsha matamanio yao kwa Mungu kumtuma Roho wake kwa mara nyingine kuleta neno la kinabii. Lakini badala ya kuongelea juu ya Roho kuja kutokea umbali fulani, ilimutukuza nabii, alishangaza matarajio yao kwa kumunukuru Yoeli na kusema kwamba wanao wenywe wangeweza kutabili! Ambacho kingeweza kuelezewa kama harakati za kiroho zilizofuatia (Mdo 2). Lakini pia upinzani ulifuatia ujumbe wake. *Harakati za kupanda kanisa zinahitaji viongozi wanaovuta nje matamanio ya mioyo ya watu kwa ajili ya Mungu kutenda kupitia wao, kuendeleza injili yake kwa kuzidisha makanisa katika ardhi.*

Paulo alikuwa kiongozi anayetekeleza. Kama Kristo angekuwa hakuhubiriwa mahali fulani, angeweza kwenda pale na kufanya hilo (Rum 15:20-21). Aliweka mfano kwa wengine katika huduma. Bila kujali ugumu, mateso, na hata ufukara, (2Kor 11:23-27) alipanda makanisa! Wengine walimfuatia katika mfano huu (2Tim 2:3). Hili ni wazi, lakini lazima lisemwe: *Harakati za upandaji kanisa zinahitaji viongozi watakaoongoza timu za kupanda makanisa.*

Barnabas alikuwa kiongozi aliyewaendeleza viongozi wengine hata wakati walipodhaniwa hatari kwa sababu ya injili. Alisimama pembeni ya Paulo kulipokuwa na mashaka makuu kama shauri lake lilikuwa la moyo mweupe na la kweli (Mdo 9:26-27). Wakati Paulo alipokuwa peke yake Tasisi, Barnabas alimuita kwenda Antiokia na kumwachilia kwenye huduma yake ya kufundisha (Mdo 11:25-26). Ilikuwa kutokana na huduma yake Antiokia kwamba Paulo aliendelea kuwa mtume anayejulikana na mpanda kanisa.

Barnabas pia alikutana na upinzani Paulo alipokataa kumchukua Marko mchanga pamoja nao tena baada ya kushindwa katika safari ya kwanza. Barnabas alijitenga na Paulo kumrejeza marko kutumika kwenye huduma (Mdo 15:36-39). Baada ya mda, siyo tu kwamba Paulo mwenyewe alisema kuwa Marko amegeuka kuwa wa kutumika, lakini kuwa kama mwana kwa Petro na hata kuandika injili! Angalia kwa ajili yako mwenyewe katika 2Timotheo 4:11, Wakolosai 4:10, na 1Petro 5:13 na uzisome kwa sauti.

**MFANO**

Huduma kubwa zaidi ya J. Christy Wilson inaweza isiwe kwamba alikuwa mtu wa kwanza katika miaka 1500 kupanda kanisa la kiinjili huko Afuganistani, lakini kwamba ametia changamoto viongozi wengine wengi wa kikristo kwenye umishenari, yote umishenari wa kufanyia nje na katika huduma ya uchungaji. Yeye mwenyewe haongozi chama chochote. Bill Bright, kiongozi mmoja wa misheni kubwa na chama cha uinjilisti ulimwenguni anasema kwamba Dr. Wilson amemgusa kwa undani sana kama mtu wa kiroho ambaye amewahi kukutana naye. Dr. Wilson anaomba kwa ajili ya watu wengi kila wiki –kwamba Mungu aweze kuwatumia. Anawatia moyo watu, anaamini katika vipawa vyao vya kiroho na anatumia mguso wake mzito na kuzoeana kwa hali ya juu kuwapa kila nafasi ya kuwatumia. Kama mchungaji, mwaalimu wa juu, mmishenari, rafiki na mshauri, anawasaidia wengine kuona jinsi Mungu atakavyowatumia na kuwatia moyo kumtumikia Bwana kabla ya wengine kuwagundua. Mara nyingi, Atakuwa tayari na atazungumza hadharani vizuri juu ya mtu, ambaye ingawa mkanushaji, lakini anamtumikia Bwana na kutumiwa naye.

Mmoja anaweza kupitisha moto wa kurunzi kwa nyingine ambayo haiwaki bila kufifiza mwanga wa nyingine. Kuwasha kurunzi za viongozi wapya ili kwamba nao waweze kuongoza inasaidia mshitusho mdogo inapokuwa usiku kuelekea kwenye muwako unaoweza kuonekana kwa mbali. Katika njia sawa, kuandaa, au kuwezesha' wengine katika uongozi kunazifanya harakati kukua. Matendo 19:1-10 jinsi katika huduma ya mwisho ya Paulo kabla ya kufungwa, alivyoendeleza viongozi wengine kwa kuanza na kumi na wawili huko Efeso. Paulo mwenyewe alikaa kwenye mji, lakini hao aliowafundisha waliifikia Asia ndogo yote kwa neno la Bwana! Alielezea jinsi alivyofanya nao kazi katika kipindi hicho katika Matendo 20:17-38. Paulo aliwasha kurunzi zao! *Harakati za upandaji kanisa zinahitaji viongozi ambao wataambukiza na kuendeleza viongozi wengine ambao watafanya harakati kuendelea kupanuka*

Viongozi katika harakati wanawajibisha watu kwenye ukweli unapofunikwa na mapokeo. Petro, Barnabas na Paulo walilalama kwenye elimu ya maadili na dhamiri ya viongozi wengine kuwashawishi juu ya sheria za Mataifa na Wayahudi. Waliwaambia mitume na wazee jinsi ambavyo Mungu amewatumia kuwaleta Mataifa wasiotahiliwa kwa kristo. Kutoka kwenye mabishano haya, waliwashawishi mitume na wazee kuandika barua ya kuwafungua Mataifa wanaoamini kutoka kwenye lazima kwenda kwenye sheria za Agano la kale za kufata kawaida. (Mdo 15:6-7,23-29).

## III. DALILI YA 3: WATU KUWEZA KUSHIRIKI

Harakati zinapokuwa njiani, watu wanaendelea kushiriki kwenye maswala ya harakati katika kukuza idadi na kukuza kiwango cha majukumu kwenye sababu. Kwenye harakati za upandaji kanisa, *sababu ya kawaida ni* kujaza *ardhi kwa makanisa yanayoihubiri injili!* Hii inamaanisha kwamba watu wengi watahitajiwa kushiriki katika vipengele vyote vya kuanzisha makanisa mapya. Watu wengi watawajibika kikamilifu kuwa wapanda kanisa. Watu wengi watasaidia kwa vipawa maalumu kama vya mziki, uinjilisti, utafiti, na kwa njia nyingine yeyote ambayo itakuwa msaada wa kupanda makanisa. Watu wengi watakuwa sehemu ya utumaji kwa kuomba mara kwa mara kwa ajili ya wapanda kanisa na huduma yao.

**MFANO**

Huko Urumi, dalili ya mwanzo ya harakati za maombi ni dhahiri. Kutoka Alba Iulia, Urumi kundi la wanawake watatu walianza kuombeana na kuombea waume zao. Waliendelea kuombea makanisa yao, maeneo yao, kwa ajili ya taifa na makanisa mapya kuweza kupandwa. Ushirika ulikua zaidi ya makundi 30 na kadirio la wanawake 150 walioshiriki kwenye maombi. Ilienea kwenda Bucharest mahali ambapo kitabu kidogo cha maombi kwa ajili ya Urumi kilianzishwa na kutumika katika taifa lote na nje ya nchi. Huko Sibiu, makanisa mawili yasiyo ya dhehebu moja yaliomba pamoja. Huko Cluj, kuna maombi ya kila mwezi kuna kusanyiko la maombi ya wanawake yanayokaribisha kila kanisa. Mara kwa mara, wanawake wasiokata shauri wanahudhuria, hata baadhi wanakuwa waumini kupitia ushirika huu.

Uhusiano usioonekana tulionao na Mungu, uhusiano unaowezesha tulionao na Mungu katika maombi ni kiunganishi cha undani kabisa pamoja naye anayekizalisha na kuendesha harakati. Muonyesho huo wa harakati za Roho wake unaonyeshwa kadiri makundi ya waumini yanayozidi wanapokuja pamoja ili kukutana naye kwa njia ya maombi. Kwanza wachache, kisha zaidi na zaidi wanaokutana kwa ajili ya maombi, mpaka harakati za Roho wake zinapofagia kuzunguka taifa.

Kinachoonyesha harakati ni sababu *kwa nini* inavutia watu wengi. Watu wanashawishika na kujitoa kwenye sababu kuu, na kuambukiza mvuto wao na wajibu kwa wengine. Watu wamejitoa kwenye harakati za upandaji kanisa kwa sababu wameshawishika kuwa huyu ni Mungu yuko kazini.

**MFANO**

Harakati za maisha ya undani huko Nigeria zilikua kutokana na mafunzo ya Biblia nyumbani kwa William Kmuye, kisha kwa mwalimu wa chuo kikuu. Imekua hadi kufikia zaidi ya kusanyiko elfu tatu kutoka kwenye mafunzo hayo ya Biblia. Watu walihisi kuwa uwepo wa Mungu ulikuwa miongoni mwao kupitia kujifunza neno lake bila mchezo. Inagawa zinakua kwa haraka, harakati za maisha ya undani wamejitoa kwenye kutenda kibiblia, mafundisho madhubuti na kufundisha uongozi bora kupitia huduma ya kikundi kiini.

Ni aina gani ya huduma inakimbiliwa na umati wa watu kushiriki katika eneo lako?

## IV. DALILI YA 4: MIFUMO MIPYA

Harakati zinapokuwa njiani, siyo tu wenye ujuzi na viongozi waliowekewa mikono wanaohudumu katika huduma, lakini waumini wa kawaida wanagundua kuwa Mungu anataka kuwatumia pia. Harakati zinafanya watu kushiriki katika kila ngazi. Viongozi wanaibika wakiwa na shauku kwa ajili ya huduma. Watu wanakuwa hodari katika kumtumikia Mungu kwa njia zote mbalimbali ambazo wanaweza kuwa wamewahi kuzifikilia kuwa za kiujuzi tu au wakristo waliojiimarisha ambavyo wangeweza kufanya. Kwa mfano, siyo tu viongozi waliofunzwa katika seminari wanaoweza kufundisha na kuhubiri, lakini pia waumini kanisani ambao Mungu amewapa vipawa kwa ajili ya huduma hii.

**MFANO**

Mtu fulani alimuuliza mchungaji mpandaji kanisa wa kanisa la Assembly of God Brazili mahali alipohudhuria seminari. Kwa kuwa viongozi wachache sana wa Assembly of God wamewahi kuhudhuria elimu yoyote ya awali ya kitheolojia alimwangalia mtu aliyemuuliza kwa mshangao kwamba hata angeweza kuuliza. Jibu lake lilikuwa "kwa nini, seminari ya mtaani!" harakati kuu kama hizo zinahitaji viongozi na viongozi wake wamefunzwa kupitia uzoefu wa huduma ya vitendo.

Nini kinachofatia? Watu wengi wanapoanza kufanya kwenye huduma ya injili watagundua mafanikio zaidi, ya kufurahisha, au mitindo isiyo ya kawaida ya huduma ambayo inawasaidia wengine kushiriki vilevile. Kwa mfano, katika harakati za upandaji kanisa wimbo fulani unaweza kufahamika kwa sababu ya jinsi unavyogusa mioyo ya hao wanaosikia na kuuimba, au kwa sababu ya jinsi unavyowarudisha watu kwa Bwana. Mwelekeo mwingine unaoweza kuonekana kwenye harakati za upandaji kanisa ikiwemo njia za uinjilisti zenye ufanisi, mikutano ya kikundi kiini, na hata mitindo ya kuhubiri.

**MFANO**

Jeshi la Mungu, harakati za kikundi kiini kilichohubiri injili kutoka kanisa la Othodox waliona wenyewe ukuaji mkuu kutoka miaka ya 1930 mpaka kwenye 1950. Wakati miziki mingi katika makanisa ya kiinjili ilipoletwa kutoka nje na kutafasiliwa (mara nyingi vibaya), Harakati za jeshi la Bwana zilizalisha nyimbo za sifa kwa Mungu katika mziki ulizaliwa kwenye udongo wa Warumi kutoka kwenye mioyo ya Warumi. Waumini wa kiinjili Urumi kutoka makanisa mengine wanatumia mziki huu kumtukuza Mungu leo.

"Washangiliaji" Kutoka chepo ya kalivari walianza kutengeneza muziki, na kuanzisha mziki wa Maranatha na kuzalisha nyimbo ambazo zimetafasiliwa ulimwenguni kote. Mbili ya nyimbo hizi ni Mtafute yeye kwanza na Kama Ngedele.

Harakati za kushitusha za kikundi kiini za upandaji kanisa Uingereza zimefanya maandamano kwa ajili ya Yesu kuwa tukio la ulimwengu. Wimbo wa Yesu ng'aa Yesu ng'aa unatokana na harakati hizi pia.

## V. DALILI 5: HARAKATI NI KITU CHA HIARI

Wakati mlipuko wa harakati unapokuwa njiani, hakuna mtu mmoja au chama kinachoweza kuzizuia. Kwa kifupi kinakuwa kitu kikubwa kwa yeyote mmoja kuweza kukiandaa. Kwa jinsi hiyo, viongozi kwenye harakati wanaweza kukutana na kuelekeza mwelekeo wa harakati. Ni njonzi kabisa kufikiri kuwa madhehebu tofauti na makanisa yanayojitegemea yataungana pamoja na kuwa dhehebu moja kwa ajili ya harakati za upandaji kanisa. Tofauti ni dhahiri kabisa kwa wao kuwa ngome moja. Lakini wanaweza kuungana pamoja kama vyama tofauti kuelekea kwenye sababu ya pamoja ya kuendeleza injili kupitia upandaji kanisa! Hilo linatokea katika harakati za kueneza upandaji kanisa.

Inawezekana kabisa kwa viongozi kutoka madhehebu tofauti kuungana pamoja na kupanga kujaza taifa lao kwa makanisa yanayohubiri Biblia, hata kama ni Pentekosti au Babutisti (na mengineyo pia)! Kwa hiyo, harakati kiasili haziwezi kupangwa, lakini watu na miundo kwenye harakati wanaweza kuelekezwa kuelekea kwenye sababu ya upandaji kanisa.

**MFANO**

Katika mkutano ambao umewakutanisha viongozi wakuu wa madhehebu pamoja kujadili kuendeleza injili Brazil, Raisi wa kanisa la Assemblies of God, Jose Willngton anasoma zaburi 133, "Tazama jinsi ilivyo vema na kupendeza ndugu wakae pamoja kwa umoja!" Mkutano huu ulianzisha utaratibu ambao ulipelekea kwenye hisani ya BD 2000 ya kuwakirisha na mwingiliano wa madhehebu.

Harakati za kiroho mara zote hazitabiriki. Ni ile asili ya elimu ya nguvu inayorithiwa katika harakati. Hata hivyo kuhusika kwa namna hiyo katika harakati za Mungu mara nyingi hakujulikani. Sisi mara nyingi tunaendesha na kuendeleza katikati ya ghasia, kwa kifupi tukijaribu kusimamia kile tunachoweza na kuacha mengine kwenye ulinzi mtukufu wa Mungu. Bila kujua kama kutakuwa na fedha za kutosha, kamwe bila kuwa na hakika kama Mungu atafungua milango ya tunayowazia au kumtarajia kufungua, bila kuwa na hakika kama kutakuwa na watu wengine watakaoungana nasi, kamwe bila kuwa na hakika kama mikakati yetu ni asilimia 100 imeshirikishwa katika harakati zake, tunaendelea katika imani na ujasiri katika wema wa upendo wake.

Mtihani mzuri wa kuona kinachotokea kama ni harakati za Mungu au vipindi vya mwanadamu ni kuuliza, "mwanadamu anaweza kutawala hili?" Mwanadamu ana vizuizi vingi. Harakazi za Mungu lazima zizidi na kupita uwezo wa mwanadamu na matarajio. Mwanadamu anaweza kuufanya moyo wa mwingine kuwa wa kupokea? Mtu anaweza kumthibitishia mwingine dhambizi? Hivi ni vitu anavyofanya Roho wa Mungu. Haina maana kabisa kwamba kile akili ya mwanadamu inachopanga na kutawala ni harakati za Mungu. Husika katika huduma ambayo itafanikiwa tu kama Mungu yuko ndani yake. Epuka kitakachofanikiwa kwa kuwa unafanya mambo yaliyo sahihi.

## VI. DALILI YA 6: HARAKATI ZINAHAMASISHA WATU NA MUUNDO

Kukua kwa haraka kunahitaji miundo, viongozi zaidi na njia mpya za kuwasiliana. Kadiri harakati za upandaji kanisa zinavyopamba moto na mifumo mipya ya huduma kutokea, wakristo pia wataanza kuhamasika katika ngazi zote kuhusika katika upandaji makanisa. Miundo iliyopo kama makanisa ya mtaa, uongozi wa madhehebu, vyama vya kikristo, hata shule zitaanza kutafuta njia za kushiriki na kusaidia kazi ya upandaji kanisa. Wakati mwingine miundo mipya inaundwa kwa kusaidia ile iliyopo kushirikiana kuelekea kwenye harakati za upandaji kanisa. Maandishi ya vyombo vya mawasiliano yanahitajika kutokea kupeleka harakati mbali. Vitu vifuatavyo vinaweza kutokea wakati watu na miundo vinapohamasisha:

Wakati viongozi waliopo kama vile wachungaji, ofisi za kimadhehebu na wakristo wengine nyeti kuona kwamba harakati za upandaji kanisa wazi wazi ni mapenzi ya Mungu, watatia moyo miundo wanayoongoza kusaidia.

**MFANO**

Huduma (DAWM) ya kufuasa taifa lote iliwaleta pamoja viongozi wa kanisa huko Ufilipi katika mwaka 1973 kwa ajili ya kuomba na kupanga. Madhehebu kila moja liliweka malengo yao ya upandaji kanisa na kuweka shabaha ya kupanda makanisa mapya 50,000 kufikia 2003. leo wako kwenye shabaha kwa kuwa Mungu ameheshimu imani yao na umoja!

Wakati mwanzoni wakristo wasio hai wanapoona kwamba harakati za upandaji kanisa ni za Mungu, mara nyingi watajiunga kwa kuomba, utoaji wa fedha, na hata kwenda na kufanya kazi! Ufundishaji utafanyika kusaidia watu kushiriki katika namna inayoonekana, na baadhi ya mafundisho hayo yanaweza kupata njia yake kwenye shule za Biblia na seminari pia.

**MFANO**

Muungano wa Kueneza Upandaji Kanisa unaungana na makanisa ya mtaa na mawakala wa misheni kuhudumu kama muungano ulioungana katika nchi za zamani za kikomunisti. Muungano umesaidia kuwafundisha wapanda kanisa. Kwa kuendeleza timu za uwezeshaji katika nchi za zamani za kikoministiza Ulaya ya Mashariki ya Mbali, wamefikia nje kwenye makanisa ya kitaifa na kuwasaidia kufundisha wapanda kanisa wao. Muungano pia umezalisha vifaa vya kufundishia ikiwemo mwongozo huu.

Maandishi na vyombo vingine vya mawasiliano vitajulisha, kuongoza, na kutia moyo watu kuhusu wazo kuu na visa vya harakati. Hiki ni kipengele muhimu kusaidia makundi mbalimbali katika harakati kukua pamoaja katika mwelekeo sawa. Vyombo vya habari, hasa mandishi, vilevile yanahalarisha. Maandishi na vyombo vya habari vinaweza kuwasaidia watu kuzichukua harakati wanazozalisha bila mchezo. Vinasaidia pia harakati kuenea kupita tunavyodhania. Maandishi pia na vyombo vya habari vinafikia kimazingira mahali ambapo viongozi na washiriki kwenye harakati wasingeweza kamwe. Nyaraka za Agano Jipya ni mfano bora wa maandishi ambayo yalikua kutokana na harakati za upandaji kanisa. Bado yanaendelea kujulisha, kuongoza na kutia moyo harakati za upandaji kanisa leo! Unadhani wakristo wa karne ya kwanza walidhania barua za Paulo zitaongoza na kutia moyo waumini wa America ya Kusini miaka elfu mbili ijayo?

### SULUHU

Jinsi gani unajua kuwa Yesu anafanya kazi kwa juhudi? Wakati wote atapatikana akiwa ndani ya watu. Sehemu ya kwanza kuangalia kuona jinsi Mungu alivyo kazini ni kuangalia unapoishi! Jinsi gani Mungu anafanya kazi katika eneo lako? Baadhi ya Dalili za harakati zinaweza kuwa dhahiri katika eneo lako.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni aina gani ya maandishi yanahitajika kupeleka haraka harakati za upandaji kanisa?
- Inawezaje kuwa rahisi kuwa na kushauriana na baraza kuu kuelekea harakati za upandaji kanisa katika eneo lako au nchi?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Kutafuta njia ya kueneza maono ya kueneza upandaji kanisa. Ama kwa kuyahubiri, kuyaandika, au kumwambia mtu mwingine juu yake—lakini fanya kitu cha kuonekana kupitisha maono haya kwa watu kwa namna fulani.
- Jiunge kwenye kufanya ushirika na wengine walio na maono sawa. Tafuta na kutana mara kwa mara na kundi la watu waliojitoa kueneza upandaji kanisa.
- Anzisha baadhi ya mfumo wa mawasiliano kueneza maono zaidi ya mawasiliano yako. Jaribu kutengeneza gazeti, kitabu, video, kipindi cha redio au kingine kitakachowasilisha maono unapokuwa haupo
- Tafuta makundi mengine au vyama ambavyo vitakuwa vishiriki nawe kuelekea harakati za kueneza upandaji kanisa.

## VYANZO

Miller, Basil. *John Wesley*. Minneapolis: Dimension Books,1943.

MAONO YA KUM

SOMO LA 12

# Uangalizi Kati Kati ya Harakati

## MASWALA YA HARAKA

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutoa baadhi ya maarifa kwenye kazi ya uangalizi wa makanisa mapya kwenye mandhali ya harakati za upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Harakati za upandaji kanisa kawaida zinafatana na changamoto kadhaa.
- Biblia inatoa mchanganuo ambamo tunaweza kupata majibu ya changamoto ambazo mara nyingi zinakabili katika harakati za upandaji kanisa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua maswala yanayoibuka wakati kanisa linapoenea kwa haraka.
- Kuelewa jinsi viongozi wa kwanza walivyoitikia kwenye maswala haya.
- Kuandaliwa kukabili changamoto ambazo ni za kawaida kwenye harakati za upandaji kanisa.

☞ **Ushauri kwa wakufunzi**

Inaweza kusaidia kuwa na ramani ya ulimwengu wa Mediteraniani wakati wa nyakati za Agano Jipya unapokuwa unafundisha somo. Vilevile, uchunguzi wa uangalifu wa marudio ya Maono ya KUMP somo la 8 “Kujongeza kwa Kwanza” (Mwongozo wa Tatu) utakusaidia kujiandaa vizuri kufundisha somo hili.

### UTANGULIZI

Ulimwenguni kote mahali harakati za upandaji kanisa zinapoendelea, harakati hizi zinakutana na changamoto kuhusu uongozi, mafundisho, fedha, uinjilisti unaoendelea. Wapi tunapata majibu ya ugumu huu? Kimapokeo tunaweza tusifikilie Biblia kama kitabu cha upandaji kanisa, lakini kwa kuwa kinafundisha ukweli wa kimungu na kwa kuwa mengi yake yaliandikwa kwa kuitikia kanisa linalopanuka, ni mahali pazuri ulimwenguni pa kujifunza juu ya harakati za upandaji kanisa.

### I. UONGOZI KATIKA MAKANISA MAPYA YALIYOPANDWA

Moja ya maswala ya kawaida katika harakati za upandaji kanisa ni uongozi. Injili inapokuwa inaendelea kwa nguvu na makanisa kupandwa kwa haraka, mara nyingi kuna kipindi cha mda wakati uongozi wa kutosha inakuwa vigumu kuupata. Muda unapokuwa unaendelea, Paulo na wafanya kazi wenzake walirudi kwenye makanisa mapya yaliyopandwa kuwatia moyo (Mdo 14:21-22; 20:2), kuchunguza maendeleo yao (Mdo 15:36), kuteua viongozi (Mdo 14:23) na kuwaimarisha (Mdo 16:5). Maombi na kufunga ilikuwa sehemu ya utaratibu wa kuchagua uongozi.

Wakati makanisa yanapokuwa yanaendelea, yanahitaji uongozi wenye uzoefu. Uongozi wa wenyeji waliokomaa ni mpangilio mzuri, na juhudi zote za timu ya upandaji kanisa lazima waende kuelekea maendeleo ya uongozi huu wa wenyeji. Kwa jinsi hiyo, badala ya kuwalazimisha watu kwenye uongozi kabla hawajakomaa, mitume waliruhusu makanisa kuwepo bila kuwa na wazee mpaka walipowateua kwenye safari ya pili. Wakati mwingine uongozi ulitokea nje kwa mda. Paulo aliwatuma Sila na Timitheo kuongoza huduma huko Moria (Mdo 17:14). Alimwacha Prisila na Akwila huko Efeso/Corintho (Mdo 18:19). Kuelekea mwishoni mwa maisha yake, Paulo

inavyoelekea alimwacha Timotheo kuangalia Efeso na Tito kuwajibika kwa ajili ya Krete (Tit 1:5). Lengo la msaada wa nje ni kufundisha na kutoa uongozi mpya.

## II. KUWASILIANA NA MAKANISA MAPYA

Huduma ya Paulo ya umishenari ilipelekea vishada vya makanisa katika majimbo manne maalumu—Galatia, Asia, Masedonia, na Akia (Tazama Maono ya KUM somo la nane “Kusonga kwa kwanza” katika Mwongozo wa Tatu). Kutoka kwenye nyaraka zilizoandikiwa makanisa na viongozi katika majimbo haya, tunaweza kugundua jinsi ya kutumia kanuni za kibiblia kwenye matatizo yanayokabili makanisa mapya. . Barua hizi ziliandikwa kubainisha theolojia, kuwatia moyo waumini, kuelekeza kuhusu matatizo ya kanisa na kufundisha viongozi.

### A. Maelekezo kwa Wagalatia

Paulo aliandika kitabu cha Wagalatia kwa baadhi ya makanisa ya kwanza kabisa aliyopanda (Antiokia huko Pisidiaia, Lystra, Ikonia, na Derbe) ili kutoa nje mafundisho ya uongo ya Kiyahudi waliyofundisha kwamba utii kwa sheria za sanamu yalikuwa sehemu muhimu ya wokovu. Mafundisho ya uongo ni silaha ya kawaida ya adui, na makanisa mapya yanaweza kuwa mepesi kwa hilo. Paulo aliyahesabu mafundisho hayo kwa kuelezea tena nafasi ya imani kwenye injili.

### B. Maelekezo kwa Maknisa ya Masedonia

*1. Maelekezo kwa Wafilipi waumini*

Paulo aliwaandikia Wafilipi kutoka gerezani huko Urumi. Wafilipi inahusu hasa furaha. Ni ushuhuda wa namna gani kwamba Paulo alikuwa mwenye furaha hata gerezani! Siyo cha kushangaza kwamba Paulo ni mwenye furaha kama anavyodhihirisha kuelewa kwa hali ya juu kwenye tabia ya Kristo katika moja ya vifungu vya ukristo katika Biblia (2:5-11). Hakika kwa Paulo, “kuishi ni Kristo, na kufa ni faida”

*2. Maelekezo kwenye Kanisa la Wathethalonike*

Paulo aliandika barua mbili kwa waumini wa Thethalonike. Kulingana na 1Wathethalonike 1:8-10, waumini hawa walikuwa na mguso kwenye majimbo yao (Masedonia), eneo linalopakana (Akia) na ulimwengu. Kisa kinachotawala cha maandishi ya Paulo kinahusu kuja mara ya pili kwa Kristo.

### C. Maelekezo kwa Wakorintho huko Akia

Kanisa la Wakorintho hakika lilikuwa dhaifu na lenye hitaji la kiroho. Tunajifunza katika nyaraka za Paulo kwao kwamba kanisa lilikuwa limepatwa na balaa la mgawanyo, wivu, kutumia vibaya vipawa vya kiroho na meza ya Bwana na kwamba hawakujua jinsi ya kuitikia kwenye kutokuwa na maadili. Paulo hakukatia tamaa kanisa hili lililokuwa na shida kama wapanda makanisa wengi ambavyo wangeshawishika kufanya. Hata anawaambia kwamba majibu kwenye matatizo yao yako katikati yao (1Kor 1:4-9).

### D. Maelekezo kwenye Makanisa ya Jimbo la Asia

*1. Maelekezo kwenye kanisa la Efeso*

Efeso ilikuwa ni mji unaotawala katika jimbo la Asia, mahali ambapo Paulo alikaa na kufanya kazi kwa miaka mitatu. Wanatheolojia wengi wanaamini kwamba barua kwa Waefeso ilikuwa haikudhamiria kwa Waefeso tu lakini pia kwa makanisa binti ambayo yalitokana na kusonga mbele kwa injili katika jimbo la Asia (Matendo 19:9-10). Mafundisho katika barua hii yanahusika zaidi na harakati za upandaji kanisa. Maelezo kuhusu kusudi la kanisa (kurasa za 2 – 3) yanaweka wazi kuwa Mungu anakusudia mataifa (mataifa) kuielewa injili kupitia kuwepo kwa kanisa.

*2. Maelekezo kwa kanisa la Kolosai*

Barua ya Paulo kwa Wakolosai inaelekezwa kwenye kanisa ambalo hakupanda, katika mji ambao hajawahi kutembelea. Kanisa huko Kolosai lilikuwa sehemu ya harakati ambazo zilianzia Efeso na kuenea kote kwenye jimbo la Asia (Mdo 19:9-10). Kanisa la Kolosai lilipandwa na Epafura (Kol 1:7), aliyekuwa amefunzwa na Paulo na alikuwa ametumwa nje kutoka pale kuwa na Paulo katika kazi ya kimishenari kwenye sehemu zingine (Kol 4:11-13; mstari wa 23).

3. *Maelekezo kwa Timotheo*

Baada ya Paulo kuondoka Efeso, Timotheo aligeuka kuwa mjumbe wa Paulo na kiongozi kwenye kanisa la Waefeso. Akiwa amemwambia Timotheo “kukaa Efeso” (1Tim 1:3), Paulo aliandika barua mbili kwa “mwanae katika imani” wakati Timotheo akisimamia makanisa Asia kutoka Efeso. Katika barua yake ya kwanza kwa Timotheo, Paulo alifundisha matendo na tahadhari kuwa muhimu kutunza harakati za upandaji kanisa imara. Haya ni pamoja na kuangalia mafundisho (1Tim 1:3-5), ibada za hadharani na maombi, sifa za kiongozi kwa uongozi, maonyo juu ya kujipatia fedha, kutunza uaminifu wa kiroho, na ushauri wa kimatendo juu ya jinsi ya kushughulika na watu na maamzi yanayohusu siasa.

Kutoka kifungoni mwake, akiwa anakabili siku zake za mwisho duniani, Paulo aliandika barua ya pili kwa Timotheo. Hapa Paulo anatumia familia kama mfano wa mahusiano kati ya kiongozi kwenye kupanga kueneza upandauji kanisa. Mengi ya makalipio ni ya binafsi, kama baba kwa mwana anayempenda sana (2Tim 1:2; 2:1). Paulo alimwambia Timotheo kuweka mfano wa jinsi ya kuwatenda waumini wengine kanisani (1Tim 5:1-2). Kwa kifupi alisema kumtendea kila mmoja kama familia! wanawake ni madada au wamama na wanaume ni baba au makaka. Anga la familia linathibitisha kuwa watu wanapendwa na kukubalika. Kila mmoja anaweza kujisikia kama sehemu.

4. *Maelekezo kwa Filemoni*

Paulo aliandika barua yenye hisia kwa rafiki yake Filemoni, mjumbe wa kanisa la Kolosai. Maswala magumu ya kisiasa, hayo ya utumwa, Onesmo, aligeuka kuwa muumini. Paulo alimtia moyo Filemoni katika upendo wa kikristo kumukubali Onesmo kurudi kama kaka katika Kristo.

Alipotibu tatizo hili, Paulo aligundua kuwa alikuwa na mamlaka ya kumwambia Filemoni kubadilika, Paulo alitaka kumshawishi kuchukua nafasi mpya kwenye utumwa wake. Katika njia sawa, wakati Paulo alipofundisha katika shule ya Tiranusi, maandiko yanasema kwamba “alifikiri” au “alijadili” (Matendo 19:9). Ingawa inaweza kuwa vigumu zaidi, kuna mafanikio zaidi kuwasaidia watu taratibu kubadili mivuto yao kuliko tu kuwaambia la kufanya. Harakati mara nyingi zinaenda zaidi wakati watu wanaposogeza mbele injili kutoka kwenye mivuto yao kuliko tu kutii amri kiupofu.

Kutokana na mahusiano yao kama marafiki na makaka katika Kristo, kuliko tu kutoka kwenye nafasi ya mamlaka, Paulo aliweza kumtia moyo Filimoni kubadili mvuto wake na kumpokea Onesmo kama kaka. Kanuni hii hii inaweza kutumika katika kutatua maswala nyeti ya kisiasa katika kanisa leo. Ni nini baadhi ya maswala yanayokukabili katika kanisa lako, na ni mipaka ipi kutoka kwenye mfano huu unaoweza kutumia kuyatatua?

5. *Maono ya Yohana katika kisiwa cha Patimo*

Ufunuo ulitolewa kwa mtume kwa makanisa ya Asia wakati Yohana akiwa uhamishoni katika kisiwa cha patimo. Makanisa saba (Efeso, Smirna, Pergamo, Thiatira, Sardi, Filadelfia, na Laodikia ) yanawakilisha kizazi kijacho baada ya harakati za upandaji kanisa

Bwana Yesu yeye mwenyewe aliyaambia makanisa ni nini hasa chenye maana kwake. Kwa kuangalia kwa karibu sana kwenye tathimini yake ya makanisa, tunaweza kufanya kazi kupanda makanisa yanayompendeza. Wapanda kanisa lazima wafundishe kusanyiko lao hadhi ambazo Bwana anatukuza ili kuepuka upinzani ambao Yesu anakemea kwenye makanisa saba. Kwa Biblia ya kiidini, au mtazamo wa kanisa, kurasa za 2-3 za Ufunuo ni za muhimu.

Maono ya nyakati za mwisho ya Yohana yaliyoandikwa katika Ufunuo 4-22 ni sehemu ya kipekee katika Agano Jipya ambayo kwa njia nyingi ni vigumu kuyatafasiri. Lakini ujumbe wa maono una kisa kimoja kinachojirudia kuhusu kutokuwa na mashaka—**Yesu atalijenga kanisa lake!** “Mataifa yote yatakuja na kumwabudu” (15:4). Hili linatakiwa liwe faraja kuu kwa waumini katika misuko suko yote.

### E. Barua kwa Warumi

Ingawa Urumi haikuwa sehemu ya eneo lolote ambalo Paulo aliinjilisha wakati wa kipindi cha safari yake ya kimishenari, kanisa lenye nguvu lilianza pale kama matokeo ya kazi ya wengine. Barua ya Paulo kwa Warumi ni moja ya maandiko yenye thamani zaidi. Kwa undani zaidi, Paulo alielezea maana ya injili alivyoichukulia "siionei haya" (Rom 1:16). Paulo alijua nguvu ya injili, kwa kuwa ilibadilisha maisha yake, vile vile na maisha ya maelufu ya wengine. Ni kwa nini ni kwamba hatuoni Mungu akitenda katika njia yenye nguvu leo? Pengine sehemu ya jibu ni ukweli kwamba tunashindwa kuelewa kikamilifu na kutoa injili katika huduma.

**MFANO**

Kitabu chenye nguvu cha Warumi kimekuwa cheche zilizowasha harakati kadhaa za kiroho. Katika karne ya 16 kijana mjerumani wa katoliki aliyejihusisha na mambo ya Mungu na mkufunzi wa seminari aliyeitwa Martin Luther alikuwa na haja ya kuwa karibu na Mungu. Tatizo, kwa jinsi hiyo, ilikuwa kwamba hakujua ni kwa jinsi gani na ilionekana kwamba hata viongozi wa siku hizo hawakujua. Luther alipata jawabu alilokuwa akilitafuta katika 1515 wakati akielezea juu ya barua ya Paulo kwa Warumi. Alipokuja kwenye ukurasa wa 1, mstari wa 17 aligundua upya mafundisho ya kiblia ya 'kuhesabiwa haki kwa imani.' Luther aliendelea kufundisha injili ya wokovu kama zawadi ya bure mbali na matendo mema. Kadiri injili ilivyohubiriwa, maisha yasiyohesabika yalibadilishwa kimilele na Ulaya ilibadilishwa.

**MFANO**

Katika mwaka 1735 mtumishi kijana wa Kiangilikana aliyeitwa Yohana aliondoka Uingereza kuhudumu kwa miaka mitatu kama mmishenari miongoni mwa watu asili ya Marekani, mahali alipokutana na ugumu mwingi. Karibia na kurudi Uingereza kwa kukatishwa tamaa sana, alikwenda kwenye mkutano wa Aldersgate mahali ambapo kundi la waumini walikuwa wakisoma utangulizi wa tafsiri ya Martin Luther juu ya Warumi. Hapa na pale, mwezi wa tano 24, 1738, John Wesley alisikia injili pengine kwa mara ya kwanza. Wesley aliendelea kusoma moja ya uamsho mkuu ambao ulimwengu umepata kuona.

## III. KULINDA DHIDI YA MAFUNDISHO YA KINYUME

Kama ambavyo tumeshaona, maswala ya kimafunsisho ndiyo baadhi ya matatizo harakati za upandaji kanisa zitakutana nayo (1Tim 1:3-5). Inawezekana kupanda makanisa mengi, lakini kama hayana nguvu, matatizo makubwa yanaweza kutokea. Ushupavu kupita unaweza kwenda kutoka kuhalarisha mpaka kutokuelezeka. Mafundisho yote hayo lazima yachujwe kwa maandiko.

### A. Sanamu ya Kristo

Sanamu ni picha barabara ya mtu fulani. Picha ya kuchekesha, kama za kwenye magazeti na katuni za kwenye vijitabu zinachengesha kivuli barabara kusisitizia tabia moja au mbili za mtu mwenye kivuli. Kuwafundisha viongozi kuambatana na mazuri, Mafundisho imara ya Biblia, yatasaidia kanisa kuwa picha barabara ya Kristo. Mara nyingi, kwa sababu kuhalarisha, au uzoefu, picha halisi ya Bwana inachengeshwa kuwa iliyogeuzwa. Hii inaweza kutokea wakati dhahebu au kundi la makanisa kwa nguvu vinawathibitishia wajumbe kufata moja au sehemu ya maandiko, au kusisitizia uzoefu. Kumbuka:

1. *Uzoefu unatakiwa utafasiliwe na maandiko na siyo vinginevyo. Maandiko ndiyo chimbuko la kufundisha na kuzoeza (2Tim 3:16-17).*
2. *Epuka kuhalarisha kupindukia au kutokueleweka (Kol 2:18-23). Badala yake, mfanye Yesu Kristo kuwa kitovu cha kila kitu (Kol 1:27-29; 2:2-3,6-9; 3:4,15-16).*
3. *Epuka mafundisho yasiyo ya kweli ambayo yanaweza kuharibu kanisa.*

### B. Ukristo wa Kweli Unahitaji Upendo Miongoni mwa Wakristo Vile Vile na Mafundisho Sahihi

Kufuatana na mazoea ya kanisa, Mtume Yohana aliandika Yohana Kwanza, na ya Pili, na ya Tatu akiwa Efeso. Yohana anazungumzia kwa nguvu dhidi ya hao wanaopotosha mafundisho ya Kristo (1Yn 2:22) na wasiokuwa na uhusiano unaoonyesha upendo wa Kristo (1Yn 2:9).

Watu waliochanganya ukristo na falsafa za kawaida za siku zilipotosha mafundisho sahihi (1Yn 4:1-3). Watu kama Diotrephes (3Yn 9) walikuwa viongozi katika kanisa waliosababisha ukaidi na mgawanyiko,walitaka kuwa muhimu zaidi, na hawakuutumia upendo wa kikristo katika mahusiano yao. Mtume wa zamani alihakikisha kuwa imani iliyoweka katika ukristo na uhusiano wa upendo wa kikristo ni alama ya harakati ambayo inafanya ukristo sahihi (1Yn 5:1-2)

## IV. KUFADHILI

Moja ya maswala katika harakati za KUM inahusu uhamasishaji wa rasilimali. Rasilimali ikiwa ni pamoja na fedha, vifaa, maandishi, ujuzi, n.k. Watu wanapokosa rasilimali za kufanyia kile Mungu alichowaitia kufanya, hawawezi kuweka maono ya KUM. Kanuni mbili zinaongoza rasilimali katika harakati za upandaji kanisa.

### A. Kanuni ya Kujisaidia

Maandiko yanafundisha kwamba utoaji wa hapo ulikuwa sehemu ya harakati za upandaji kanisa katika karne ya kwanza. Paulo alitarajia makanisa kusaidia viongozi wao kifedha (1Tim 5:17, 1 Kor 9:3-12). Rasilimali za huduma, ikiwemo fedha, zinaweza kutolewa kwenye vyanzo vya nje ili kuweza kuanzisha kazi mpya. Kwa jinsi hiyo, Utimizaji wa Utume Mkuu katika eneo unatakiwa ufanyike kimsingi kwa raslimali na uanzilishi wa waumini wa eneo hilo. Kati kati ya moyo wa swala la rasilimali ni ukweli wa kimsingi kwamba watu wa Mungu wenyewe wanatoa njia ya msimgi kwa ajili ya kazi ya injili. Sehemu yao wenyewe ya kumi na sadaka inatakiwa itumike kusaidia kazi yao.

Kama Yesu alivyosema, 'Kwa kuwa palipo na mali yako, ndipo moyo wako utakapokuwa *"* (Mt 6:21). Mtu anapotoa kulingana na njia yake*,* watu hao wanajitoa kwa mioyo yao kwa kile wanachotoa kwa ajili yake. Kama watu hawatoi kwa kujitoa kwenye huduma zao, kisha kazi haina kujitoa kwa moyo. Kitu fulani chenye nguvu sana kinatokea wakati watu wanapoamua kuwa huduma au kipindi ni chao na kwamba kinafaulu au kushindwa inategemeana na kazi ya Mungu kupitia wao.

### B. Kanuni ya Kuchangia

Makusanyo kutoka Galatia, Asia, Masedonia na Akia kwa waumini wahitaji Yerusalemu (1Kor16:1-2; 2Co 8,9) inaonyesha kwamba makanisa yalitarajiwa siyo tu kusaidia huduma ya hapo, lakini pia kutoa kwa wengine wenye mahitaji. Wakati ni kawaida leo kwa "makanisa mama" kutoa kwa ajili ya mahitaji ya fedha ya "makanisa binti", tunaona kwamba kinyume kilitokea wakati Paulo alipokusanya fedha kwa ajili ya kanisa la Yerusalemu. Kumbuka kwamba makusanyo haya hayakuchokoza kanuni ya kujisaidia (2Kor 8:13-15).

Paulo kawaida alijisaida mwenyewe kifedha ili kutokuwa mzigo kwa wengine (Ac 18:2,3: 1Co 4:12). Kwa jinsi hiyo, alipokea msaada kutoka kwa Wafilipi waumini (Flp 4:15-20). Inashangaza kufahamu kuwa kifungu kilichorudiwa kila mara *"Mungu wangu atakupa mahitaji yako yote…" kama* inakuwa katika mandhali ya Paulo akiwapongeza Wafilipi kwa utoaji wao kwenye huduma ya upandaji kanisa

Utoaji fedha ni taratibu za msingi za maisha ya kikristo yanayowezesha kanisa kuhudumu, kufika nje, na kupanda makanisa zaidi. Waumini kamwe hawakutakiwa kuwa bahili (1Tim 6:3-10), na "ni baraka zaidi kutoa kuliko kupokea" Tazama matendo 20:32-35). Kwa hakika, utoaji ulio mwingi kwenye Agano Jipya ulifanywa na masikini, au angalau nje ya njia ya mtu. Watu matajiri pia wana nafasi muhimu katika harakati za upandaji kanisa. Kwa jinsi hiyo, hao wasio na kitu lazima waelewe kwamba 1 Timotheo 6:17-19 ni pamoja na maelekezo sita ya watu matajili wanaomrudia Kristo: kutokuwa na kiburi, kutokuweka tumaini lao kwenye utajili, kumtumaini Mungu peke yake, kufanya matendo mema, na kuwa wakarimu na kuwa tayari kuchangia. Umewaambia watu matajili kanisani kwako kuhusu amri sita zinazowalenga?

## V. MIKAKATI YA KIINJILI NA UPANDAJI KANISA

Jinsi gani moyo wa bidii wa kiinjilisti unavyoweza kuwasha harakati za upandaji kanisa kusalimika? Hili ni swala jingine ambalo viongozi wapanda kanisa wanakutana nalo.

### A. Kuzungumzia Kawaida Watu Walivyo na Matumaini (Matendo 2:14-40)

*Maneno sahihi yanayotolewa katika wakati muafaka yanagusa watu.* Paulo aliliuliza kanisa Efeso kuomba kwamba aweze kutumia maneno sahihi katika kuhubiri kwake injili (Efe 6:19). Katika kila utamaduni, miongoni mwa kila watu, Yesu ni jibu. Kitu chochote cha ajabu na swali la ndani la kabila la watu inaweza kuwa, kuna ujumbe wa msingi ambao, unapozungumzwa katika mda muafaka, utatikisa wengi kufanya uamzi wa maisha kwa Yesu Kristo.

Katika siku ya Pentekosti katika Matendo 2, mtume Paulo alizungumzia kawaida watu walivyo na matumaini (Mdo 2:14). Katika wakati huo, watu walikuwa wakiugua kwa matarajio ya mda maalumu wakati Mungu angetembelea watu wa Israel waliotekwa na kutawanyika. Petro alizungumzia nyakati mpya wakati Roho wa Mungu atakapokuwa hazungumzi tena isipokuwa tu kupitia kuchagua jumuia ya kinabii, isipokuwa kupitia mabinti na vijana, wazee na vijana na hata watumishi wangu!, (Mdo 2:17-21). Baadaye, Stefano, akijua jinsi Wayahudi walivyothamini historia yao, alielezea jinsi ambavyo wangeweza kupata kusudi lao la pamoja (Mdo 7). Paulo aliitikia kwenye kiu ya Wayunani ya ukweli mpya na wa kimaajabu alipowaambia waathene kwamba sasa wanaweza kujua maajabu ya Mungu asiyejulikana (Mdo 17:22-33).

Kueneza upandaji kanisa kunapata nafasi iliyotayari katika taifa wakati wapanda kanisa wamejifunza kuzungumzia juu ya jinsi watu walivyo na kuzungumzia matumaini yao. Wakati injili inapoelezewa katika mandhali ya historia ya nchi hiyo na maana kiutamaduni, inakuwa na mvuto wake mkubwan na nguvu. Njia nyingine ya kuonekana kutumia kanuni hii ni wakati 'wito kwenye utekelezaji' unapoweza kuzungumzia watu walivyo na matumaini, kisha huonekana kuwavutia.

### B. Tumia Matukio Maalumu na Mida

Matukio makubwa na sherehe katika taifa, eneo, au mji au kijiji yanaweza kupunguza kiasi cha juhudi na mda kwa wapanda kanisa. Kanisa lilizaliwa wakati wa sherehe kuu wakati maelfu ya Wayahudi, waongofu na wanaomuogopa Mungu walipokuja Yerusalemu kutoka ulimwenguni kote (Mdo 2). Baada ya mda wao Yerusalemu, wahija hawa walichukua imani mpya kupeleka nyumbani kwao. Hii inaweza kueleza jinsi kanisa huko Urumi lilivyokuwa limeanzishwa kabla ya mtume yeyote kufika pale.

Wakati Paulo aliporudi Yerusalemu mara ya mwisho, alitamani kuwahi pentekosti ikiwezekana (Mdo 20:16), pengine kwa sababu Wayahudi kutoka ulimwenguni kote wangekuwepo. Wakati Wayahudi kutoka Asia walipomtambua, walimshutumu Paulo na kumpa nafasi ya kutoa ushuhuda wake kwenye umati wa mataifa yaliyokusanyika hekaluni (Mdo 21:27ff). Paulo hakulipanga hivyo, lakini alichukulia nafasi ya hali hiyo kuendeleza injili.

Matukio makuu kama kombe la dunia, sherehe za kitaifa na siku za mapumziko ambazo tayari zinawavutia umati, na hasa umati wa kimataifa, ni nafasi bora ya kufikia nje. Makanisa yanaweza kupandwa kwa ufanisi wakati watu wanaokubali wameshafika kwenye tukio kuu, kama inavyopingwa kwa wapanda kanisa kupanua nguvu zaidi kutafuta na kuvutia watu au kuandaa mkutano mkubwa zaidi wa nje na wa gharama. Kwa kipimo kidogo, siku za kuzaliwa, kusherehekea, arusi za kikristo au misiba zinaweza kuwa nafasi za kufikia watu. Pamoja na ufatiliaji unaofaa, inaweza kusaidia yote upandaji kanisa na ukuaji.

### C. Injilisha Watu Walio katika Mamlaka

Watu kwenye mamlaka lazima wahusishwe katika kila aina ya kufikia kiuinjilisti. Yesu alimpa Paulo mbinu zake za kiunjilisti aliposema, “Ni chombo changu kiteule kuchukua jina langu kwa mataifa na wafalme” (Ac 9:15). Paulo aliweka mbinu hii wakati aliposhuhudia ubalozi wa kipro, Sergio (Ac 13:7), vilevile na kwa Felix, mtawala aliyepotoka wa Yudea, na mfanikishaji wake, Tertulo Festo (Mdo 24), kwa Herodi Agripa (Mdo 25, 26), na Publio,mtu aliyemwongoza Malta (Mdo 28:7-10). Ingawa mambo hayakuandikwa, Tunaweza kuwa na hakika kuwa Paulo alimshuhudia Kaisari wa Urumi, Nero, vilevile (Ac 27:24). Katika kwenda Urumi na kukata rufaa kwa Kaisari, misheni ya Paulo ikabadilika kutoka kwenye mkazo wa eneo mpaka kugusa mataifa (Ac 19:21, Ro 1:15).

Kabla ya makanisa ya kitaifa kushuhudia kwa viongozi wa kitaifa, makanisa haya yanatakiwa kuwaombea hadharani (1Ti 2:1-2). Hii itapelekea jamii inayokubali kuishi “maisha ya amani na utulivu na wema wote na heshima." Zaidi ya haya, watu kwenye mamlaka wanapojifunza injili kwa ushuhuda wazi wa waumini wa kitaifa, viongozi hawa wa serikali, ingawa hawataki kutubu, bado wataelewa jinsi Ukristo unavyoigusa jamii. Na kama viongozi wa taifa wana mtazamo mzuri wa uongozi wao wa nchi, watakuwa na huruma na kuheshimu thamani ya yale wanayoyafanya wakristo.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini baadhi ya maswala harakati za upandaji kanisa zinakumbana nayo? Jinsi gani Biblia inatusaidia kuitikia kwenye maswala haya?
- Ni mafundisho gani ya kiuzushi yanatishia kanisa katika eneo lako? Ni sehemu ipi ya maandiko inagusia maswala haya?
- Ni nini baadhi ya matumaini na ndoto za watu unaowahudumia?
- Una mpango wa kieneo wa kupanda makanisa katika miji inayozunguka?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Orodhesha matukio matatu makuu katika utamaduni wako na sema jinsi unavyoweza kuyatumia kama sehemu ya mbinu za upandaji kanisa.

# KANISA

KANISA

SOMO LA 12

# Nguvu ya Kanisa Linaloibuka

## NI WAKATI GANI LINAKUWA KANISA?

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea nguvu ya mpito kundi la waumini linapogeuka kuwa kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Kundi bila kusita linatakiwa liwe kanisa, badala tu ya kufanya mabadiliko mara moja na wakati mwingine likiwa bado changa.
- Huduma ya pekee na vikundi kiini vinatakiwa vibakie kuwa sehemu nyeti ya kanisa jipya.
- Kanisa jipya ni mwanzo wa utimizaji wa Utume Mkuu—siyo mwisho.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa tafsiri tofauti za kanisa
- Kujitoa kwenye vikund kiini vinavyoenbdelea kutumika.
- Kujitoa kwenye kuzidishwa kunakoendelezwa kwa kanisa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Itasaidia kurejea kwenye mwongozo huu kwenye somo la Uwakili la 2, “Uwakili wa Kifededha”, Sehemu ya III. “Pesa za Kanisa la mtaa." Sehemu hii ina baadhi ya mawazo yanayofanana juu ya kanisa linalojisaidia na kutoa heshima ya majadiliano katika somo hili kuhusu upitishaji wa pesa.

**UTANGULIZI**

Kama tu kulivyo kuzaliwa kwa mtu pekee, moja ya nyakati zinazosisimua zaidi katika maisha ya kanisa ni pale linapokuwa “limezaliwa” kiofisi. Kuzaliwa kwa kawaida kwa kanisa mara nyingi siyo tukio la bahati. Kama ilivyo katika maisha ya kibaolojia ni utaratibu wenye nguvu ambamo baadhi ya vitu kawaida vinatokea kabla au baadaye. Katika somo hili tutatafiti utaratibu huu.

### I. NI WAKATI GANI KANISA NI KANISA?

Kwa baraka za Mungu, mpanda kanisa anatakiwa aweze kuanzisha vikundi kiini kadhaa katika eneo analolenga. Wakati mwingine kutakuwa na waumini wa kutosha wa kuanzisha utaratibu wa kuvipanga kuwa kanisa la mtaa. Kuna maswala muhimu kadhaa ya kufikiri kwa wakati huo.

#### A. Nani Anaamua Lini kanisa ni Kanisa?

Swala la kwanza linahusu nani mwenye haki ya kuita kazi mpya kama “kanisa la mtaa.” Kuna angalau vyanzo vikuu vitatu vya mawazo kuhusu nini hasa kinalisimamisha kanisa.

1. *Matakwa ya Halali*

Serikali ya kila nchi pengine ina sheria maalumu zinazohusu ni aina gani ya kundi linaloweza kupokea kibari halali cha kanisa. Kibiblia hakuonekani kuwa na sababu yeyote kwa nini kanisa litahitaji kujisajiri kwenye serikali ili liwe kanisa. Kwa jinsi hiyo, mara kwa mara ni muhimu au inasaidia kiofisi kulisajili kanisa ili kuepuka karaha zisizo za lazima za haki. Mahitaji ya serikali ya kusajili kanisa yanatofautiana kutoka nchi hadi nchi, kama

zilivyo faida na hasara za kusajili. Swala hili litahitaji kutolewa uamzi kama chimbuko la jambo katika kila eneo, kikawaida kwa baraza la halmashauri la viongozi wenye uzoefu wa kanisa.

2. *Matakwa ya Kidhehebu*

Kama jengo la kanisa jipya limeanzishwa chini ya himaya ya kidhehebu, au kama litaendana na dhehebu lililolinzisha, dhehebu kawaida litakuwa na mipaka yao ya nini kinalijenga kanisa. Wanaweza kuweka pamoja na matakwa ya chini ya uanachama, utawala wa kanisa, kiwango cha pesa, mafundisho, au mashauri mengine. Tena, haya yanatofautiana kwa upana zaidi kwamba mpanda kanisa atatakiwa kuyafanyia kazi katika hali yake maalumu.

3. *Matakwa ya Kibiblia*

Mkazo wa somo hili ni katika kuelewa kanisa kibiblia kuliko tu kidhehebu au kihalali. Mawazo haya tofauti ya kanisa yanaweza kutazamwa kama mwendelezo:

**Mchoro12.1 Tabia ya Kanisa**

| ***Kama kanisa linatimiza tabia hizi:*** | ***Ni kanisa kwenye macho ya:*** |
|---|---|
| *Kibiblia* | *Mungu* |
| *Kibiblia + Kidhehebu* | *Mungu & Dhehebu* |
| *Bibllia + Dhehebu + Sheria* | *Mungu & Dhehebu & Serikali* |

Kila mpanda kanisa atatakiwa kuamua ipi kati ya ngazi hizi za kukubalika ni muhimu kwa kazi mpya katika hali yake maalumu. Kati ya sura tatu, kwa jinsi hiyo, ya kibiblia ndiyo ya kimsingi zaidi na muhimu. Kundi lolote ambalo halitimzi tafsiri ya kibiblia ya kanisa ni ibada za mazoea mbele za macho ya Mungu—bila kujali endapo au la dhehebu au serikali inalikubali. Kwa hiyo tabia ya kibiblia kwa kanisa ni nyeti kuielewa.

## B. Tafsiri ya Kanisa la Mtaa

Somo la 4 la kanisa “Kutafsiri Kanisa la Mtaa” (Mwongozo wa Kwanza) umajadili tafsiri ya kanisa kwa undani. Tafadhali rejea kwenye somo hilo kwa maelezo ya undani. Utataka pia kurejea kwenye tafsiri ya kanisa uliyoanzisha katika somo hilo. Kwa kuwa tafsiri zitatofautiana kihakika, somo hili litatumia tafsiri ya msingi kwa ajili ya majadiliano wakati wa somo. Unatakiwa ulifanyie kazi somo hili tena na tafsiri yako mwenyewe.


Kanisa la mtaa mara nyingi linatafsiriwa kama mwili *uliopangwa wa hao waliokiri imani yao katika Yesu Kristo, waliobatizwa, na wanaokutana pamoja mara kwa mara kushirikiana, kuabudu, maelekezo kwenye neno na kuyafanya yaliyoagizwa.*

Jinsi kanisa linavyopangwa na anayeongoza mwili vinaweza kutofautiana kutoka kundi moja hadi jingine.

## C. Kutofautisha Kundi Kutoka Kwenye Kanisa

Mawazo yanatofautiana kimapana ya ni lini kundi limepangwa vya kutosha kufaa tafsiri hiyo hapo juu na kisheria kudhaniwa kama kanisa. Kila jengo la kanisa linasogea kupitia hatua katika kielelezo 12:2, kusogea kutoka kwa binafsi, kwenda vikundi, kisha kanisa la mtaa.

**Kielelezo 12.2 Kutoka kwa Binafsi kuwa kanisa**




Kunaweza kukawa na vikundi kadhaa tofauti vilivyohusika katika jengo la kanisa jipya, vikiwemo vikundi kiini na vikundi vidogo. Vikundi kiini vinatoa ukuaji kwa kanisa jipya kupitia uinjilisti unaoendelea, ambacho siyo jambo kwa vikundi vidogo. Baadhi ya vikundi vinatoa mkazo wa huduma maalumu, kama vile malezi ya kawaida, vijana au familia. Ingawa maombi na mawazo yanatakiwa yatolewe kwenye kutumia vikundi kiini na/vikundi vidogo katika huduma ya upandaji kanisa, muundo wa vikundi siyo muhimu kama walivyo watu humo. Kanisa ni watu—vikundi kwa kifupi vinatoa muundo na mazingira ambamo huduma inaweza kutokea humo na kupitia watu hao.

Kama tunatumia tafsiri ya kawaida ya kanisa kutoka sehemu B, tunaweza kuelezea kwa undani ni katika hatua gani katika utaratibu kikundi kinakuwa kanisa. Ili kuwa kanisa hasa, kusanyiko linatakiwa liwe na kila moja ya mahitaji yafuatayo:

1. *Liwe na waumini wenye Imani katika Kristo*

   Kanisa la mtaa lazima liwe la hao waliokwisha kuweka imani zao na tumaini katika Kristo. Hao tu waliozaliwa tena ni wajumbe wa kanisa la wote, na kwa hiyo wanatakiwa wajulikane kama wajumbe wa kanisa la mtaa. Kundi la watu wasiookoka, haijalishi ni idadi gani, siyo kanisa. Katika hali halisi, hatuwezi tukawa na uhakika kabisa wa wokovu wa kila mjumbe, lakini hili linatakiwa liwe lengo letu. Biblia haielezi wazi kiwango cha chini cha wajumbe.

2. *Wanakutana Mara kwa Mara Kushirikiana, Kuabudu, na Mafundisho*

   Kanisa la kwanza lilikutana pamoja kila siku, lakini mda ulivyoendelea tunawaona wakitenga jumapili kwa heshima ya ufufuko wa Bwana kwenye siku ya kwanza ya juma. Kunaonekana kuwa na baadhi ya nafasi ya uteuzi katika mwanga wa mchango wa Paulo katika Warumi 14:5-6. Mkazo wa mkutano wao ulikuwa huduma ya neno na ibada iliyokazia katika kujitoa kwa Kristo kwa ajili ya ukombozi wao.

   Hakuna sababu kwa nini jengo ni muhimu ili kufahamika kama kanisa. Kanisa la kwanza lilikutana kwenye kiwanja cha hekalu la Wayahudi, katika masinagogi na majumbani. Wakati wa mateso ya Warumi walikutana pia katika mapango au sehemu yeyote iliyofichika iliyokuwepo. Jengo la kwanza la kanisa halikujengwa mpaka baada ya karne kadhaa baada ya pentekosti. Leo majengo mara nyingi yanatumika, lakini kwa hakika siyo ya lazima.

3. *Kuyatenda Maagizo*

   Kuna maagizo ya aina mbili—ubatizo na meza ya Bwana—ambayo makanisa yote yanakubali yanahitaji kuyafanya. Kwa jinsi hiyo, Kuna utofauti wa kufikiri katikati ya mifumo wanayotumia. Ubatizo unafanyika kwa njia tofauti tofauti, na mtiririko wa meza ya Bwana unatofautiana. Kufanya kwa kimadhehebu mara nyingi kunaathiri mifumo hii, lakini kazi lazima ifanywe na kanisa. Ili kudhaniwa kama kanisa la mtaa, lazima kuwe na mfumo unaofanyika katika nafasi kuendesha maagizo haya.

4. *Uwe na Viongozi Wenye Ujuzi*

Kanisa linahitaji kuwa na watu wa kutosha wenye ujuzi kutoshereza nafasi zozote za kiuongozi ambazo kanisa linatakiwa kuwa kanisa. Kama wanaamini katika nafasi ya kichungaji, wanahitaji angalau kuwa na mchungaji mwenye ujuzi mmoja. Kama wanaamini katika wingi wa wazee, lazima angalau wawe na wawili. Kama wanadhani waangalizi kuwa wa muhuimu, kisha lazima kuwe na wajumbe wenye ujuzi wa kuhudumu. Zaidi ya hayo, Ofisi hizo zinahitaji kuchaguliwa au kuteuliwa katika namna iliyoandaliwa ambayo inatosheleza mfumo wa uongozi uliochaguliwa na kanisa.

5. *Kuwa Imara Kifedha*

Kundi lisilojisaidia lenyewe linaweza kudhaniwa kama kanisa?

Kanisa linatakiwa kuwatunza viongozi wanaojitoa kwenye huduma mda wote kwenye kusanyiko (1 Tim. 5:17-18). Kanisa la kwanza pia kifedha lilisaidia wajane na masikini kwenye kusanyiko, kwa kuongeza, walituma pesa kwenda makanisa yenye mahitaji, kusaidia wamishenari wapanda makanisa. Kundi ambalo halijisaidii haliwezi kutimiza kazi hizi za kanisa la mtaa. Kwa sababu ya hili, wengine watajiuliza kama kundi ambalo halijisaidii linaweza kudhaniwa kama kanisa.

Takwa hili linawezekana, hata kwa kundi masikini sana. Kama kila mjumbe anatoa karibu ya asilimia kumi ya kipato chake, ingechukua familia kumi kumsaidia kiongozi mmoja. Kama kiongozi asiyemchungaji hahitaji mshahara mzima, inaweza hata ikahitaji wajumbe wachache kumsaidia.

Ni muhimu kuelewa kwamba, “kipato” siyo tu tasilimu, lakini pia hata rasilimali ambazo siyo tasilimu alizonazo mtu. Kama mtu fulani hapokei mshahara wa kila mara lakini ana shamba la viazi, asilimia ya viazi hivyo vinatakiwa vitolewe kanisani au kuuzwa kwa tasilimu ili kulisaidia kanisa. Wajumbe wa kanisa la mtaa waliojitoa wanaofanya wajibu wa kibiblia wa kutoa wanatakiwa waweze kusaidia siyo tu viongozi wao na huduma, lakini kufikia nje pia.


## II. KUPANGA KAMA KANISA

Taratibu za kupanga kanisa hasa hasa ni huo—utaratibu. Mara nyingi, wapanda kanisa kichanga wanafanya mabadiliko kutoka kuwa kundi kuwa kanisa. Kuna sababu mbili kwa nini hili ni kosa. Moja, kila kundi la waumini linatakiwa liwe linajifunza kutimiza kazi nyingi za kanisa iwezekanavyo kutoka kwenye mwanzo wa kundi. Wajumbe wa kundi wanatakiwa waendelee kukua kwenye wajibu hizi wanapokomaa kiroho na kuongeza kihesabu. La pili, kundi linatakiwa lisikome kukutana kama kikundi wanapokuwa kanisa. Vikundi kiini ni muhimu, na lazima viendelee. Mkutano wa pamoja wa kanisa unafanyika kwa nyongeza kwenye vikundi—kiini siyo baadala yake.

### A. Vipengele Vilivyomo kwenye kanisa la Mtaa Hai

Upandaji wa kanisa la mtaa katika njia nyingi unafanana na ujenzi wa nyumba (ukikumbuka kwamba kanisa siyo jengo). Nyumba ni mkusanyiko wa vipande kadhaa, ambavyo kawaida vinajengwa kwa utaratibu maalumu. Moja, Msingi unawekwa kisha vyumba vinajengwa, kisha dari inaongezwa. Mjumbe pekee, kikundi, na mikutano ya pamoja ya kanisa inaongezwa kwa mtindo unaoendana.

**Kielelezo12.3 kujenga Nyumba ya Bwana**




1. *Binafsi—Msingi*

   Kivuli cha msingi mara nyingi kimetumika katika Agano Jipya, lakini hali ya msingi inabadilika kulinagana na ukweli ulioelezewa. Katika vifungu tofauti, msingi ni Yesu Kristo (1Kor 3:11), Mitume na manabii (Efe 2:20), mafundisho ya toba (Ebr 6:1), na huduma ya Mtume Paulo katika kanisa la Wakorintho (1Co 3:10). Kielelezo 12.3 kinatumia msingi katika hisia hii ya baadaye. “Matofali ya kujengea” ya kawaida ya kanisa la mtaa ni kila muumini pekee. Kumleta mtu pekee kwa Bwana ni hatua ya kwanza katika kuanzisha kanisa la mtaa. Hata kama kundi dogo lipo, lakini hakuna waumini kati yao bado hakuna msingi wa kanisa. Msingi, kwa jinsi hiyo, unakua na kuwa mkubwa na imara kadiri “matofali” (waumini) yanapoongezwa.

2. *Vikundi—Vyumba*

   Vikundi kiini au vikundi vidogo ni badala ya vyumba kwenye nyumba. Vyumba hivi ni mahali ambapo shuguli za kanisa zinafanyika. Vikundi ni sehemu nyeti ya maisha ya kanisa, kama vile kiini hai kilivyo muundo nyeti katika mwili unaoishi. Ni hatua ya pili katika kutokea kwa kanisa mpya la mtaa. Nyumba ya kawaida ina vyumba kadhaa, kila kimoja kikitoa huduma tofauti. Kanisa linalokua pia linatakiwa kuwa na mchaguo wa vikundi kiini si vikundi vidogo, vikikidhi mahitaji kadhaa kama vile uinjilisti, ufuasishaji, kufundisha. Kama msingi (waumini) wanaongezeka, vyumba vingi vinaongezwa kadiri vinavyohitajika.

3. *Kusanyiko la Umoja—Dari*

   Kuna matofali mengi katika msingi wa nyumba, na idadi ya vyumba, lakini dari moja tu. Inafunika, inalinda kushikilia pamoja nyumba nzima. Mikutano ya pamoja ya kanisa la mtaa ni kama hili. Ni ncha ya juu ya kazi. Wakati dari (mkutano wa pamoja) inaongezwa, shughuli zote za kawaida za kanisa zinaweza kufanyika kiuhuru. Kunakuwa na kuhisi umoja na utoshelevu.

**B. Kuongeza “Dari”**

Kuna baadhi ya hali za kipekee au tamaduni ambapo dari inatengenezwa kabla ya vyumba vya nyumba. Idadi ya chini ya ncha au tegemezi za mda zinashikilia dari mpaka hapo vyumba vinapoongezwa. Baadhi ya makanisa ya mtaa hata yanaweza kuanza hivi. Wanaruka kutoka kuwa na waumini wachache kwenda “kuongoza ibada” kwenye jumapili fulani wakati kanisa, kwa kiwango chao, linazaliwa kiofisi. Hili linaweza kufanyika, lakini ni mara chache kuwa njia yenye ufanisi zaidi kufanyia kazi. Ikiwa bado mbaya, wakati mfumo kama huo unatumika, kanisa mara nyingi linashindwa kuongeza vyumba (vikundi kiini), kwa matokeo kwamba kanisa kamwe halifikii kiwango chake.

Kwa kutumia ulinganifu wa nyumba, ni rahisi kuona kwamba “vyumba” (vikundi) vinatakiwa viundwe kwanza na “dari” (mikutano ya pamoja) inatakiwa iongezwe kama njia ya kuyavuta makundi yote pamoja mara kwa mara. Hii inaruhusu faida ya wote vikundi kiini na mikutano mikubwa. Kanisa mpya linalojengwa kwa utaratibu huu litakuwa imara na lenye mafanikio.

Kabla kanisa halijaanza ibada ya kuabudu ya mara kwa mara, fikiria yafuatayo:

- Kuna msingi imara ulio na vikundi kiini kadhaa vinavyozidi vikiwa na jumla ya watu 30-40 wanaohudhuria?
- Kuna kiini cha watu waliofunzwa kama wainjilisti na wafuasishaji?
- Viongozi wa huduma wameelimika na kuwa tayari kuchukua majukumu mapya?
- Viongozi na wapanda kanisa wameungana kuhusu falsafa ya huduma kwa ajili ya kanisa?

### C. Kutunza Msingi na Vyumba

> Vikundi kiini siyo “mpango wa mda”mpaka kanisa linapotokea” ni maisha ya kanisa!

Hakuna mtu mwenye akili timamu amewahi kujenga nyumba, na akiwa amemaliza dari, anaangusha msingi na kuta. Hata hivyo tabia za kutatanisha mara kwa mara zinatokea kwenye makanisa mapya. Ukiwa umekusanya waumini wa kutosha kuendesha mkutano wa pamoja, wanaacha kukutana kama viini, na kususia uinjilisti na ufuasishaji wa mmoja mmoja. Kwa hali halisi, wanaharibu “vyumba” (vikundi) Kufanya “msingi” (waumini) kuvurugika.

Umuhimu wa uinjilisti wa mtu kwa mtu, ufuasishaji wa pekee, na vikundi kiini kwenye maisha *yanayoendelea* ya kanisa hauwezi kukaziwa vyakutosha! siyo “mipango ya mda” mpaka kanisa linapoundwa” n*i maisha ya kanisa!* Ni muhimu kwenye kuendeleza ukuaji na ukomavu wa kanisa jipya. Kanisa linatakiwa likutane pamoja kama kundi kubwa kwa nyongeza ya ukuaji binafsi na mikutano ya vikundi vidogo—mkutano mkubwa hautakiwi kuwa badala yake.

## SULUHU

Kama kundi la waumini wanatimiza mipaka ya Biblia kwa ajili ya kanisa la mtaa, ni kanisa machoni pa Mungu. Kanisa kawaida ni kundi la watu wanaomwamini Kristo, lakini kundi la watu siyo lazima kwamba ni kanisa. Baadhi ya tofauti zaidi za kawaida kati ya makundi na makanisa ziko kwenye maeneo ya maagizo (meza ya Bwana na ubatizo), aina za uongozi na kujisaidia kifedha.

Kuandaa kanisa mpya la mtaa haina maana kutafuta mahali pa kununua au kupanga na kuanzisha ibada ya jumapili asubuhi. Watu binafsi wanaunda msingi wa kanisa, na kanisa jipya linaanza mara tu wanapokusanyika kwa pamoja kutimiza kazi zote za kanisa. Makundi yanatakiwa yatumike kabla na baada ya kuzaliwa kwa kanisa jipya kutoa muundo kwenye shughuli za huduma ambazo zitatokea katika kila kanisa la mtaa.

Ili kwa harakati za upandaji kanisa kutokea kwenye mji wowote, eneo au nchi, kanisa la mtaa lazima liwe na kuzaliana kama lengo. Katika njia sawa kwamba “msingi” “vyumba” vilijengwa (katika utaratibu huo) kuunda kanisa jipya, kanisa hili pia lazima lipange na kujiandaa “kujenga” kanisa jingine jipya kwa kutumia utaratibu huu huu. Ni wapi unaandaa “msingi” unaofata?

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Elezea utaratibu ambao kikundi kimoja au zaidi kinakuwa kanisa.
- Ni nini baadhi ya vionyesho kwamba kundi liko tayari kuanzisha ibada ya pamoja?
- Kwa kudhania kuwa kanisa jipya limekuwa likianza kwa kutumia vikundi kiini, elezea nafasi ya kiini katika maisha ya kanisa jipya.

KANISA

SOMO LA 13

# Tabia za Makanisa Yanayokua

## YANAPATA WATU WAPYA, YANAWATUNZA NA KUWAPA KAZI

☞ **Kusudi la somo**

Kusudi la somo hili nikuelezea tabia ipi lazima iwepo katika kanisa jipya ili liweze kukua.

☞ **Wazo Kuu**

- Ukuaji na kuzaliana ni kitu cha kawaida kwa kila chenye afya
- Makanisa yanakua yanapowafikia watu wapya, na kuwatunza, na kuwaandaa kufika nje kwa wengine.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa. . .

- Kuelewa jinsi tabia za kanisa vizuri au vibaya zitaathiri ukuaji wake.
- Kushiriki katika vikundi kiini kuinjilisha waliopotea na kufundisha waumini katika huduma.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kazia kwamba mkao wa ukuaji ni ufunguo kwa yote makanisa mapya na ya zamani. Wakati baadhi ya tabia katika somo hili zitakuwa za ufanisi zaidi kuliko zingine katika eneo maalumu, mkao utamwezesha kila mwanafunzi kiubunifu kuanzisha njia sahihi ya ukuaji.

### I. NI NINI KANISA LINALOKUA?

Yesu aliahidi kwamba angelijenga kanisa lake na kwamba milango ya kuzimu isingelishinda. Tunapoangalia katika historia ya ukristo, tunaona kwamba amekuwa akitunza ahadi zake. Kanisa limekua kutokana na wanafunzi wachache Yerusalemu siku ya pentekosti kwenye mamia ya maelfu ya waumini walio katika mataifa ulimwenguni. Leo kanisa linaendelea kukua kwa kiwango cha ajabu Asia, Africa na Amerika ya Kusini. Katika sehemu zingine ukuaji wa kanisa ni mdogo zaidi kuuona. Baadhi ya nchi kimatendo hakuna kanisa, na kwa nyingine ukuaji umedumaa. Kwa kuwa ukuaji wa kanisa la Kristo unategemeana na ukuaji wa kusanyiko pekee, mpanda kanisa lazima aelewe baadhi ya sababu kwa nini makanisa mengine yanakuwa na mengine hayakui.

Ni muhimu kuelezea tuna maana gani kwa *kanisa linalokua* kabla ya kugundua tabia zake. Kanisa linaweza kukua katika njia kuu tatu:


1. Kihesabu—Waumini wengi au makanisa mengi
2. Kiroho—Kuongezeka kwa maarifa ya kibiblia na kutembea kiundani kiroho
3. Kijamii –Ufanisi mzuri au zaidi kama “chumvi” katika ulimwengu uliopotea

Makanisa mengi yanaridhika hata kama yanaona moja ya haya. Mengine yanatosheka hata kuona tu yapo. Yanaweza kusema, “hatujaona yeyote ameokoka, lakini tunamtumikia Bwana kwa uaminifu.” Mengine yanaweza kutekwa na ukuaji kinamba ambao unapunguza umuhimu wa kujitolea ili kukuza mahudhurio yao. Hakuna moja ya njia hizi ni ya kibiblia. Kanisa la mtaa linatakiwa liwe linakua katika kila moja ya njia zilizoorodheshwa hapo juu.

Kwa jinsi hiyo, kanisa la mtaa ambalo *linakua,* lakini *halizaliani* halikubaliki kwa Bwana. Utume Mkuu unatuelekeza kuyaleta mataifa yote katika kumtii yeye. Mzunguko wa Upandaji Kanisa katika kielelezo 12;1 unaelezea umuhimu wa upandaji kanisa katika utimizaji wa lengo hili. Makanisa yanayotaka kuwa yanamridhisha Bwana na utiifu kwenye Utume Mkuu yatatafuta kujizidisha

yenyewa kwa upandaji *makanisa binti*, ambayo matokeo yake yatapanda makanisa mengine. Wazo hili ni nyeti kwenye kuelewa nini kanisa linalokua linatakiwa kuwa.

**Kielelezo 13.1 Mzunguko wa Upandaji Kanisa**




Njia inayosaidia kanisa kukua katika nchi moja na utamaduni inaweza kushindwa vibaya sana katika nyingine. Kanisa zuri lazima liamue nini ni ya ufanisi na kufaa katika utamaduni wake. Lakini kuna baadhi ya tabia za msingi zinazoonekana kuwa za wote. Ukuaji wa mlipuko mara zote hautokei. Baadhi ya tamaduni zinapinga injili kwa karne au mda mrefu. Lakini kawaida ukosefu wa ukuaji unaonyesha tatizo la kanisa au njia zake za huduma.

## II. JINSI UKUAJI WA KANISA UNAVYOTOKEA

Mahitaji ya msingi kuwa na kanisa linalokua ni rahisi vya kutosha, ingawa inatia changamoto kuyaweka na kuyatumia. Kanisa lazima **livutie** watu wapya, **kuwatunza, kuwaandaa** kufikia wengine.

### A. Makanisa Yanayokua Yanavutia watu Wapya

Bila watu wapya, kanisa haliwi kubwa. Hili ni rahisi hata hivyo nyeti sana. Ukuaji huu kawaida hautokei kwa ajali. Lazima tupange kwa ajili yake na kuufanyia kazi. Mpanda kanisa kiuangalifu lazima afikiri juu ya wapi na jinsi gani kanisa lake linaweza kupata na kuwavutia watu wapya.

### B. Makanisa Yanayokua Yanatunza Watu Wapya


Kuwaleta watu wapya ni hatua ya kwanza. Linalofata ni kutunza watu hawa wapya na wa zamani. Vinginevyo, ni kama kujaza matundu kitakoni—juhudi za bure mpaka matundu yazibwe. Mtu yeyote kanisani ana uamzi wa kukaa au kuondoka. Kanisa linalokua litarithi kwenye kazi nzuri kama hiyo ya kutimiza mahitaji hayo ya kiroho ya waumini wapya kiasi kwamba watataka kuwa waaminifu zaidi kanisani.

### C. Makanisa Yanayokua Yanawaandaa Watu

Waefeso 4:11-16 ni kifungu cha ufunguo kwenye ukuaji wa kanisa. Inaonyesha kwamba kanisa linakua kwenye ukomavu kadiri kila mjumbe wa kanisa anapoandaliwa. Katika kanisa lenye afya viongopzi wanafikiria kwamba lengo lao kubwa ni kuwaandaa wajumbe wengine. Huduma hii ni pamoja na maeneo makuu matatu:

- Huduma katikati ya mwili
- Huduma ya kuwaleta waliopotea kwenye mwili
- Huduma ya kuanzisha kusanyiko jipya

**Kielelezo 13.2 Kanisa Linalokua**




Utekelezaji muhimu wa kanisa linalokua umeonyeshwa katika kielelezo 12.2. kanisa lako liko je, jengo la kanisa lako, kufanya katika maeneo yote haya? Wapi unahitaji kurekebisha?

## III. TABIA KUMI NA MBILI ZA MAKANISA YANAYOKUA

Hizi ni njia za kiutendaji ambazo kanisa la mtaa linaweza kukamilisha utekelezaji ulioonyeshwa kwenye kielelezo hapo juu. Kanisa zuri linatakiwa kuhusika katika kila eneo.

### A. Wanakwenda kwa Waliopotea

Hatua hii nyeti mara nyingi inasahaulika. Baadhi ya makanisa yanaamini kuwa ni jukumu la waliopotea kuja kanisani. Hili kabisa kabisa ni kinyume cha Utume Mkuu, ambao unaliamuru kanisa kwenda (Mt 28:18-20). Tunatakiwa kuacha kondoo 99 na kutafuta mmjo aliyepotea (Lk 15).

Mwindaji yeyote au mvuvi anajua jinsi itakavyokuwa upuuzi kutarajia samaki au mawindo kumfata. Wanatumia ujuzi wao wote na kuelewa ili kuona ni wapi samaki au mawindo yalipo na kuyafata. “wavuvi wa watu lazima wafanye kama hivyo.

Kanisa la kwanza lilitafuta waliopotea hekaluni, kwenye sinagogi, sokoni, na nyumba kwa nyumba. Yesu alikwenda kwenye karamu na sherehe zilizohudhuriwa na wakusanya kodi, makahaba, na wengine waliojulikana kwa tabia za dhambi. Hata hivyo, “wenye haki” hawakujua kanuni hii. Watawala wa dini walimshambulia Yesu kwa “kula na kunywa na wenye dhambi” (Lk 5:30-32). Yesu hakukemea kwamba amefanya hilo, badala, alisema kuwa kusudi lake ilikuwa ni kutafuta waliopotea. Wakati kondoo anapopotelea kwenye bwawa, mchungaji mwenye upendo atakwenda chini kwenye tope kutaka kumwendea na kumwokoa.

Inagharimu hekima na utambuzi kujua wapi tunaweza na wapi hatuwezi kwenda. Lakini huduma ya Yesu inaeleza kwamba ni muhimu kutafuta waliopotea popote watakapokuwa, hata kama inaleta upinzani kutoka kwa wenye “haki” Ni lazima tukazane kutafuta uwiano unaokubalika badala ya kutupa mbali nafasi za kuhudumu kwa waliopotea mahali walipo.

**B. Wanatumia Vikundi Kiini**

Wasioamini wote hawatahudhuria kanisa, lakini wanaweza kushawishiwa kuja kwenye mji wa rafiki mahali wanapoweza kuuliza maswali kuhusu ukristo katika hali ambayo haitishi. Makundi haya hayatakiwi kamwe kufata mtindo sawa kama wa kanisa. Vinatakiwa viwe vya kawaida, na vya kirafiki. Kusudi la kundi linatakiwa liwe kujadili ukweli wa neno la Mungu kisha kuwahubiria waliopotea. Vikundi kiini vimejadiliwa kwa undani katika zana hii.

**C. Wanashiriki katika Kazi za Kijamii na Wasioamini**

Kanisa linalotaka kukua litawatia moyo wajumbe wake kwenda kwenye matukio ya mpira, virabu vya mchezo, masoko, sehemu za kuogelea, sherehe za kuzaliwa, arusi, misiba, matembezi, na mikutano ya hadharani, n.k. Shughuli yeyote inaweza kuwa nafasi ya kukutana na kuanzisha uhusiano na wasiookoka. Wakristo wanatakiwa wajitenge na dhambi za ulimwengu, lakini si na ulimwengu. Badala, tunatakiwa kuwa ulimwenguni kama chumvu na mwanga..

**D. Wanatunza Mtandao wa Kazi na Mahusiano**

Muumini mpya anatakiwa kutiwa moyo kuishi maisha ya kweli ya kikristo na kuinjilisha marafiki zake waliopotea.

Watu wengi wanakuja kwa Kristo kutokana na kugushwa na mtu mwingine wanayemjua. Kila mkristo anatakiwa kuwa anaanzisha uhusiano na wasioamini ambao hatimaye utawaruhusu kushirikisha injili. Kama kila mjumbe anaweza kuanzisha angala uhusiano mmoja wa namna hiyo kila mwaka na kumwongoza mtu huyo kwa Kristo, kanisa lingeongezeka mara dufu kila mwaka. Waumini wengi wana uhusiano mdogo na wasioamini. Kadiri mkristo anapohusika katika maisha ya kanisa zaidi, mzunguko wa marafiki zake unabadilika na kuanza kuhusisha wakristo zaidi na wasioamini wachache. Matokeo yake, ameongeza urafiki kidogo na waliopotea na nafasi chache za kuwavutia kwa Kristo.

Chanzo kizuri cha mawasiliano na waliopotea ni kupitia waumini wapya. Hata hivyo, waumini wapya mara kwa mara wanatiwa moyo kujitenga na marafiki wasiookoka na kutumia mda wao wote na wanaoamini. Njia hii inaharibu uninjilisti vibaya sana na kurudisha nyuma ukuaji wa kanisa.

**E. Mabadiliko ili Kuwapata Waliopotea**

Kanuni ya kiroho ni wazi. Muumini anatakiwa ajitoe haki yake na mapendeleo kwa ajili ya waliopotea.

Mtume Paulo alijaribu kuwa kila kitu kwa watu wote ili kuwapata watu wote (1Kor 9:19-23). Alimaanisha nini? Kwa hakika hakugeuka kuwa mwenye dhambi kuwapata wenye dhambi. Alimaanisha nini kwa hiyo? Alikuwa tayari kubadili jinsi alivyoishi kama ilimsaidia mwenye dhambi kusikiliza injili. Fikiri hilo lina maana gani kwetu.

Badala ya waumini kubadili "tamaduni" zao kuwapata waliopotea, makanisa mengi yanatarajia waliopotea kubadili "tamaduni" zao ili kuja kanisani.

Ingawa kanuni ya kiroho ni wazi. Muumini anatakiwa ajitoe haki yake na mapendeleo kwa ajili ya aliyepotea. Na muumini jasiri anatakiwa ajitoe kwa muumini dhaifu. Hii haimanishi kwamba muumni anaweza kutenda dhambi. Lakini anatafuta kufanya kila linaloruhusiwa ili kufikia nje na kukutana na waliopotea katika namna ambayo ni ya kufaa kwao.

*Hali ya tabia ya muumini ni kuwaleta waliopotea kwa Kristo.* Kama muumini ni mzito, moyo mzito, yuko ovyo ovyo, na mwenye uchungu ushuhuda wake hautakuwa na mafanikio. Mkristo mwema anatakiwa atoe furaha bila kujali matatizo yake, upendo kwa Mungu na kwa wengine, na amani na hakika juu ya upendo wa Mungu kwake. Fikiria juu ya orodha ya hali ya tabia au matendo katika kielelezo 13.1. Ni upande upi, A au B, unaofikiri unaweza kuvutia wasioamini kwenye ukristo?

**Mchoro 13.1 Hali au tabia ya Mtu**

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| Upendo kwa wengine | Anakwenda kanisani kila jumapili |
| Furaha katika majaribu | Anavaa kitofauti |
| Uhakika wa upendo wa Mungu | Hanywi pombe |
| Amani katika nyakati za matatizo | Havuti sigara |
| Mkarimu katika maswala ya fedha na mda | Tupa tupa |
| Ndoa yenye upendo | Anaimba kwenye kwaya |
| Watoto waliolelewa vizuri | Anajua nyimbo za sifa |
| Wakutegemeka | Anajua sala ya Bwana |
| Mwenye hisani | Anaepuka dhambi |

Wakristo walio wengi watakubaliana safu zote zina wakristo wenye tabia nzuri. Hilo siyo swala. Ni tabia ipi inavutia kwa waumini? Tabia kwenye safu ya kushoto zinaelekea zaidi kuwavutia wasioamini kusikiliza ujumbe wetu. Waumini wanaoishi kwa tabia za namna hiyo wanaonekana zaidi watakuwa wafanisi katika uinjilisti.

Tabia hizi lazima ziwe zinaonekana. Muumini anayejifanya kupenda kuwa karibu na aliyepotea ili kumpata ataonekana hafai. Ukristo halisi unavutia, hata kwa wasiookoka. Hali ya tabia inaonekana wakati wa misukosuko. Tunapokuwa na matatizo, wasioamini wanaweza kuona jinsi tunavyotegemea Mungu. Wakati asiyeamini anapokuwa na misukosuko, anaweza kupata upendo wetu na msaada. Hali zote zinamvutia kwenye injili.

### F. Wanajihusisha na Wahitaji

Watu wengi wanakuja kwa Kristo wakati wa misukosuko. Wasioamini mara nyingi wanamjari kidogo Mungu wakati mambo yanawaendea vizuri. Bwana mara nyingi anatumia misukosuko kuwalazimisha kujua hitaji lao. Makanisa yanayokua yanajua kuwa watu wanakuwa wazi nyakati hizo, na wanatafuta njia za kuitikia kwa watu, wakati wanapokuwa wanaumia.

Njia hii siyo muhimu kama hasa tukionyesha upendo wetu na kujali kwa waliopotea. Wakati mwingine msaada wa vitu unahitajika kwa sababu ya kukosa ajila, moto, au matatizo mengine. Katika swala la ugonjwa au kifo, sikio la huruma inaweza kuwa njia inayoshukuriwa zaidi kuonyesha kujali. Ufunguo ni kutunza macho yetu wazi kwenye mahitaji tunayoweza kusaidia, kama alivyofanya msamaria mwema.

### G. Wanahusisha Mara Moja Waumini Wapya

Namna ambavyo wajumbe wanafanya kwa mtu mpya wakati wa kutembelea kwake mara ya kwanza kunaweza kukaonyesha vizuri kama atakuja tena. Kama anajisikia kukaribishwa na kukubalika, pengine atakuja tena. Hili mara nyingi ni kweli kwa waumini wapya na vile vile mgeni asiyeokoka. Makanisa mengi ya Mashariki ya mbali ya Ulaya yanachukua tahadhari kuhusu kukubali watu wapya. Tahadhari hii ililisaidia kanisa kupona nyakati za mateso, na hapo lilieleweka. Kwa jinsi hiyo, kuendelea kushikilia tabia hiyo kunaweza kukawa uteketezaji kwenye ukuaji wa kanisa.

Mgeni asiyeamini mara nyingi anahudhuria kanisa kwa sababu yuko wazi kwenye injili. Ni muhimu kukamata nafasi hiyo kumfanya kujisikia kukaribishwa na kutafuta kujibu maswali yake. Hili ni sawa kwa waumini mpya, wanaolinganishwa na wototo mchanga waliozaliwa (1 Pet 2:2). Pia wanahitaji upendo, kukubalika na kutiwa moyo kuwashawishi kwa ajili ya hitaji la uhusiano wa karibu na kanisa.

### H. Wana Maisha Ya Mwili Unaotikisika

Kanisa la kwanza la Yerusalemu ni mfano bora wa mwili wa kanisa la mtaa ambao ulikuwa hai na kutimiza mahitaji ya wajumbe wake. Mdo 2:42-47 tunaona kazi kuu za mwili wa kanisa ulivyoelezewa:

1. *Imara, mafundisho wazi ya kibiblia na mahubiri*
2. *Kupenda na kukubali ushirika*
3. *Sala ya moyoni kwenye meza ya Bwana*
4. *Maombi yanayobadilisha maisha*
5. *Kuchangia na makaka na madada walio katika mahitaji*

Kila mmoja anafurahia kuwa katika kundi linalowapenda na kuwajali. Hii ni moja ya faida kuu ya familia, na kanisa linatakiwa liwe familia. Wakristo wanapojaliana kama makaka na madada katika Kristo, watu watadumu katika kundi.

### I. Wanawaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Maisha

Kila mjumbe anatakiwa akomae. Kwa hili kutokea, viongozi lazima wawe vielelezo vya maisha ya kikristo kwao. Ufuasishaji wa kweli unatokea wakati wajumbe wa kimungu wanapotumia mda pamoja na wakristo wachanga na kutoa kielelezo kwao jinsi ya kukua na jinsi ya kumtumikia Bwana.

Inashangaza jinsi gani ibada hasa ya kanisa inavyokusudiwa kuinjilisha waliopotea, ingawa walio wengi kwenye kusanyiko ni waumini. Mahubiri ya kiinjili yanafanya kidogo kusaidia waumini kukua kwenye ukomavu. Wakati injili inatakiwa ihubiriwe kanisani, msisitizo mkubwa unatakiwa uwekwe kwenye ujumbe hasa kwa ajili ya waumini. Kama mafundisho yanafaa kwenye mahitaji ya waumini, wataendelea kuhudhuria kanisa.

### J. Wanawaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Huduma Kwenye Mwili

Huduma ya kanisa inatakiwa kufanywa na wajumbe wa kanisa—siyo na viongozi. Kama tulivyojadili katika Somo la 9 na 10 la Kanisa (Mwongozo wa Tatu), Mungu amewajalia waumini wote kwa vipawa vya kiroho kutumika katika huduma. Kusudi la viongozi, kwa hiyo, ni kufundisha na kuandaa wajumbe wa kanisa kutumia kwa ufanisi vipawa vyao vya kiroho kwenye huudma. Kanuni hii inapofatwa na wajumbe wote katika mwili wana juhudi katika kuhudumiana na kuwafikia waliopotea, kanisa litakua. Mwili wote wa kanisa unaweza kukamilisha zaidi ya viongozi peke yao.

### K. Wanawaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Huduma kwa Waliopotea

Waumini wanatakiwa kusaidia kanisa kukua. Yohana 15, Yesu alisema kwamba waumini wanatakiwa wazae matunda na kwamba angeyasafisha matawi ili kwamba yazae zaidi. Mapenzi ya baba ni kwamba tuzae matunda. Hii inawahusu waumini wote—na siyo viongozi tu. Yesu hakutafsiri tunda katika Yohana 15, lakini alituamuru kwenda na kufanya wafuasi. Hakika matunda ni pamoja na kuwaleta waliopotea.

Waumini wanachache wamewahi kuleta mtu kwa Kristo. Kuna sababu nyingi kwenye hili. Baadhi ya yale ya kawaida ni:

- Hawajafundishwa kuinjilisha mpaka wawe wamekuwa wakristo kwa mda wa kutosha kupoteza –mawasiliano yao na wasio wakristo.
- Wamefundishwa kidogo sana juu ya maisha ya kikristo kiasi kwamba wanaogopa kujaribu kuyaelezea kwa wasioamini.
- Hawakuwahi kufundishwa njia yoyote ya ufanisi ya kutoa injili.
- Wanadhani kuwa uinjilisti ni kazi ya viongozi.
- Baadhi ya waumini wanashindwa kushuhudia kwa sababu ya dhambi ambayo haijatubiwa katika maisha yao wenyewe.

Mashina yote haya yanatokana na maandalizi mabaya ya waumini katika huduma. Mpanda kanisa mzuri atakuwa mwangalifu kuwaandaa wajumbe wake kwa ajili ya huduma, kuwavutia, kutoa kielelezo cha—moyo wa kuleta roho na kuwatia moyo wanapohudumu. Kwa njia hii, atazidisha huduma yake.

### L. Wanaandaa Wajumbe kwa Ajili ya Huduma kwenye Kusanyiko Mpya

Wakati ukuaji wa kanisa la mtaa ni mzuri, kuzidi kwa makanisa ya mtaa ni bora. Kanisa lenye afya halitakiwi tu kukua katika ukubwa lakini pia kuzaliana lenyewe mara nyingi. Kuna idadi ya

sababu Kwa nini uanzishaji wa kusanyiko jipya unatakiwa zaidi kuliko tu ukuaji rahisi wa kanisa mama.

1. *Kusanyiko Jipya Linakua Haraka*

   Ni ukweli kwamba makanisa mapya karibu mara nyingi yanakua kwa haraka zaidi kuliko yale ya zamani. Kuna maelezo mengi ya hili kwa nini linatokea.

   - Makanisa machanga kawaida yanakuwa katika eneo ambalo hakujawahi kuwa na kanisa, na kwa hiyo karibu na ambao hawajainjilishwa. Ni kama kuchuma zabibu na kukuta kiunga ambacho hakuna ambaye amewahi kukichuma.

   > Muumini mpya anatakiwa kutiwa moyo kuinjilisha rafiki zake waliopotea na anaokuwa nao wakati akingali bado ana uhusiano nao.

   - Makanisa mapya ni huru kutokana na matatizo ya zamani. Ingawa makanisa ya zamani yana majereha mengi, matatizo au mikasa. Wasioamini wanaweza kutumia haya kama udhuru wa kutokuhudhuria. Kwa jinsi hiyo, wanaweza wakawa tayari kujaribu kanisa mpya lenye sifa safi.
   - Makanisa mapya lazima yakue kusaza, na kwa hiyo wajumbe wake wana moyo wa kiuinjilisti. Wanafahamu nafsini juu ya waliopotea na wako tayari zaidi kuwafikia. Hawajaridhika bado.
   - Watu wanapenda kuwa sehemu ya kanisa ambapo kuna watu wa utamaduni unaofanana. Mengi ya makanisa yaliyoanzishwa yameanzisha vipindi na mtindo wa kuabudu ambao unaendana na wa kuvutia kwa wajumbe wake hasa. Watu wa lika tofauti, elimu au historia wanaweza wakawa hawavutiwi na kanisa hili. Makanisa mapya yanaweza kuandaa mifumo ya huduma ambayo inaendana na watu hawa wengine ambayo kanisa lililokwisha kuanzishwa haliifikii. Kwa ajili ya hili, kawaida ni vizuri kama mifumo ya kanisa jipya haiendani sawasawa na ya zamani.
   - Makanisa mapya kawaida hayana sehemu zao za kufanyia mikutano na wanalazimika kufanya huduma zao nyingi majumbani na kwenye vikundi kiini. Katika hali halisi, huduma ya kikundi kiini ni njia boro yenye ufanisi zaidi ya kufikia waliopotea na kuinjilisha waumini wapya. Kwa hiyo ukosefu wa mahali unageuka kuwa mali badala ya kuwiwa.

   > Utoaji na juhudi zinazohitajika kujenga na kutunza mali kubwa unazidi nguvu na rasilimali nyingine ambazo zingeelekezwa kwenye uinjilisti.

   - Makanisa yaliyoanzishwa yana matazamio ya majengo. Utoaji na juhudi zinazohitajika kujenga na kutunza mali kubwa unazidi nguvu na rasilimali nyingine ambazo zingeelekezwa kwenye uinjilisti.

2. *Makanisa Yanayozaliana Yanakua Haraka*

   Wakati makanisa ya zamani ni mara chache sana kukua haraka kama makanisa mapya, yanakua haraka yanapokuwa yanajihusisha na upandaji kusanyiko jipya. Hili ni gumu kwa wengine kuamini, lakini ni kweli. Wengi kimakosa wanadhani kwamba kusaidia kuanzisha kanisa mpya itadhoofisha la zamani. Badala, msisitizo ulioongezwa kwenye uinjilisti, kufikia nje na ufundishaji unaohitajika kwa kazi mpya karibuni mara nyingi inaletea ukuaji wa kanisa la zamani! Shauku kwenye ukuaji inaambukiza sana kwamba kanisa linalodumaa linaweza mara nyingi kujiifufua lenyewe kwa kuhamasisha upandaji kanisa.

   Kanuni hii pia inahusu makanisa mapya. Mpanda kanisa anatakiwa kufundisha kusanyiko mpya juu ya haja ya kuzaliana kuanzia mwanzoni na kuwatia moyo kuanzisha kundi jingine upesi iwezekanavyo. Akili kama hiyo itatunza kazi yake mpya ikichanua na kukua.

## IV. KUTATHIMINI NA UFUATILIAJI WA UKUAJI WA KANISA

Wazazi wote wanajua kuwa ni muhimu kwa watoto wao kupimwa uzito na kuangaliwa na daktari mara kwa mara kuona kama mototo ana afya na anakua sawasawa. Hili ni sawa kwa kanisa. Kwa kukusanya na kuainisha aina fulani ya ukuaji wa hesabu, wapanda kanisa wanaweza kupata utambuzi wa maana kwenye afya na ukuaji wa makanisa yao. Kwa mfano, hesabu ya ubatizo kwa mwaka kwenye kanisa ni kionyesho cha “ukuaji wa kukata shauri” na kuonyesha jinsi gani kanisa

linaleta watu wapya kwa ufanisi. Kuongezeka au kutoongezeka kwa uanachama na mahudhurio vinaweza kuonyesha kama kanisa linatunza na kuandaa wajumbe. La mwisho, kuweka orodha ya idadi ya vikundi kiini, kanisa jipya lililopandwa au huduma nyingine nje ya kanisa zinaweza kuonyesha kama kanisa linafanikiwa kuhusisha wajumbe katika kazi ya injili. Kutathimini takwimu hizi ni njia pekee ya kutegemewa kujua kama kanisa linafanya sehemu yake kutimiza Utume Mkuu.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kanisa lako linakua? Kwa namna gani? Kihesabu? Kiroho? Kijamii? Baadhi ya haya? Yote kati ya haya?
- Ninatimiza wajibu wangu kuwaandaa waumini kwa ajili ya huduma, au ninajaribu kufanya hili mwenyewe? Jinsi gain ninawaandaa? Inafanya kazi?
- Kwa nini asiyeamini atake kuja kanisani kwangu? Kwa nini muumini mpya atake kubakia? Ninaweza kufanya kanisa langu kuwa zaidi la kuwapokea?
- Nimeanzisha jengo la kanisa tayari? Vikundi kiini? kama siyo, ni nini ninachosubiri?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Hudhuria kanisa jingine na jifikilie kuwa hauko muumini. Utaweza kurudi kwenye kanisa hilo? Kwa nini au kwa nini siyo? Jinsi gani inalingana na kanisa lako? Ni nini ulichojifunza kutokana na hili ambacho kitakusaidia kanisani kwako?
- Fikiria juu ya makanisa katika eneo lako, ni lipi kati yake linakua, na lipi halikui. Linganisha tabia za kila moja kwenye hali katika somo. Ni tabia ipi inaonekana kuwa sababu kwenye ukuaji wake au kutokua? Unaweza kutafsiri baadhi ya tabia zingine zinazosaidia?

KANISA

SOMO LA 14

# Utawala wa Kanisa na Ofisi

## NANI ANAWAJIBIKA?

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea aina kuu za utawala wa kanisa na hitaji la watawala wa kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Aina kuu mbili ni serikali ya kanisa na watu waabuduo
- Wazee na mashemasi lazima watimize matakwa ya kibiblia

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuwa na ufahamu wa aina tofauti za utawala wa kanisa
- Kuelewa namna ya kuainisha viongozi nyeti.
- Kuelewa majukumu na upendeleo wa viongozi wa kanisa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kusudi la somo hili siyo kujaribu kushawishi wapanda kanisa kuchukua mfumo wowote maalumu, lakini kumsaidia kufikilia matokeo kwa ukuaji wa kanisa na kuzidisha kwa uchaguzi wake wa utawala wa kanisa na viongozi.

## I. KANISA NI NINI?

Kanisa la Yesu Kristo ni kwamba mwili usioonekana wa waumini waliozaliwa upya katika Yesu Kristo—aliyekufa anayeisha na bado kuzaliwa kutoka katika kila kabila, lugha, watu na taifa duniani. Kanisa hili mara nyingi linaitwa kanisa la wote. Makanisa ya mtaa ni muonekano unaoonekana katika mda na sehemu ya kanisa la wote. Tafsiri moja ya kanisa la mtaa ni "mpangilio wa mwili wa waumini waliobatizwa, wakiongozwa na mchungaji anayefaa kiroho, wakidhihirisha uhusiano wao kwa Bwana na kwa mmoja kwa mwingine kwa kule kutumia meza ya Bwana mara kwa mara, waliojitoa kwenye mamlaka ya neno la Bwana, wanaokusanyika mara kwa mara kwa ajili ya ibada na kujifunza neno, kuugeukia ulimwengu kushuhudia. "Ni wangapi wanaohudhuria ambao lazima liwe nao, jinsi gani hasa limeandaliwa na nani anaongoza mwili wanatofautiana sana kutoka kundi moja hadi jingine.

Tofauti za kimafundisho na matendo mara nyingi inawapeleka waumini kwenye eneo moja la ndani kuunda mikusanyiko ya kitofauti kabisa na ya pekee. Kutofautiana kuelewa maandiko kumepelekea kwenye mchanganyiko tofauti wa mtindo wa kanisa na utawala. Somo hili litajaribu kuweka kwa kifupi mifumo tofauti ya serikali ili kwamba wewe, mpanda kanisa, unaweza kufikiri bila mzaha juu ya mfumo gani utafanya vizuri kwa kanisa lako na mifumo gani itapelekea kuzidi kwa haraka kwa makanisa.

## II. AINA ZA UTAWALA WA KANISA

Serikali ya kanisa inaweza kugawanywa katika aina kuu mbili zikiwa na utofauti kadhaa kwa kila moja. Kanisa linaweza au kutoweza kufahamu ni mtindo upi wa serikali linaotumia, lakini kila kanisa kwa ujumla litaingia katika moja ya mifumo hii, au baadhi ya tofauti kuwepo. Utaratibu kadhaa unatofautishwa zaidi kwa kiwango cha utawala wa kila kanisa la mtaa.

**A. Utawala wa Serikali ya Kanisa**


Mifumo ya utawala wa serikali ya kanisa inatofautiana katika mtindo, lakini kwa ujumla inaonyesha mamlaka ya "juu kwenda chini". Usimamizi unatiririka kutoka kwa viongozi au kiofisi kwenda chini kwenye kusanyiko na kwa mjumbe pekee. Kuna aina kuu mbili za utawala wa serikali ya kanisa:

1. *Episcopal*

Mfumo wa Episcopal wa utawala ni pamoja na serikali ya kanisa inayosimamia kanisa la mtaa. Mamlaka yanafanyika kupitia askofu wa kanisa. Mamlaka yanatirirka kwenda chini kutoka maaskofu kwenda kwa makasisi kwenda kwa waangalizi na mwishowe kwa wajumbe wa kanisa. Maaskofu wana mamlaka siyo tu kuteua makasisi na waangalizi wanaohudumu chini yao lakini pia kuteua maaskofu wawezeshaji. Katika njia hii, wanadumisha madaraka yao. Muundo wa Kiepiscopal unatumiwa na makanisa ya methodisti, Orthodox, Anglikana, na wakatoliki.

Madaraka haya ya maaskofu mara nyingi yanatokana na mafundisho ya mfuatano wa kitume au imani inayofanana. Hii ni, wanaamini kwamba mamlaka ya maaskofu yameletwa chini kupitia historia kutoka kwa mtume Petro, ambaye yeye mwenyewe alikuwa ameteuliwa kuwa kichwa cha kanisa na Yesu (maandiko yanayoendana: Matendo 14:23 na Tito 1:5).

**Kielelezo 13.1 Mtiririko wa Mamlaka**




2. *Presbyteriani*

Mfumo wa utawala wa Presbyterian pia una mtindo wa serikali ya kanisa, lakini serikali hii haiteuliwi kutoka juu. Badala, mamlaka yanawekwa daima kwa mawakala waliochaguliwa na watu wote wenye madaraka na wasio na madaraka, wanaotenda kwa manufaa yao. Kanisa linachagua wazee wake watawala. Wazee hawa pamoja na mzee anayefundisha (mchungaji) wanaunda kipindi. Mzee anayefundisha na mwakilishi wa wazee watawala kutoka eneo la makanisa ya mtaa wanaungana pamoja kuunda kasisi, ambaye ana madaraka juu ya vipindi vya mtaa. Wawakilishi kutoka kwa makasisi kadhaa wanaunda sinodi, na wawakilishi kutoka katika kila sinodi wanaaunda kusanyiko kwa ujumla, ambalo ndilo lenye mamlaka ya juu.

Ingawa utawala wa Presbyteran unateuliwa kutoka chini, haufanani na mfumo wa Episcopal, kuna tofauti moja. Wakati kusanyiko linachagua wazee wake watawala wa Presbyteria wanawekea mikono wazee wa kufundisha—vilevile wanaojulikana kama watumishi au wachungaji. Wazee hawa wa kufundisha kitheolojia wanalingana katika madaraka kwa wazee wanaotawala. Kwa kifupi wana kazi tofauti. Wazee wanaofundisha wanawajibika kwenye kufundisha neno na kuandaa meza ya Bwana. Wazee wanaotawala wanawajibika na maamzi mengine yanayohusu uendeshaji wa kanisa.

Msaada wa muundo huu kawaida unapatikana kwenye baraza la Yerusalemu Matendo 15).

### B. Kutano

Katika mfumo wa utawala wa kutano la kanisa, mamlaka yanatoka "chini kwenda juu". Utawala na majukuimu ya kutawala kwa kanisa la mtaa yanabakia kwa wajumbe wa kanisa hilo. Mamlaka hayo hatimaye yanatoka kwa Kristo pekee yake, kichwa cha kanisa, na siyo kutoka kwa mwili wa mwanadamu awaye yote au mtu pekee. Wajumbe peke yao wanafanya maamzi ya lazima kwenye mwili wao na kuchagua viongozi wao wenyewe. Katika kutenda hasa, wanaweza kuwaruhusu viongozi wao uhuru wa kufanya maamzi kwa kuwafikiria, lakini bado wanawajibika kwenye kusanyiko, ambao lazima ndio wapitishe maamuzi makuu.

Msaada wa hili kawaida unapatikana katika kifungu cha Matendo 6:5 ambapo kusanyiko linaonekana kutia saini kwenye maamzi ya viongozi.

## III. OFISI KWENYE KANISANI

Kuna idadi ya maneno yaliyotumika kwa viongozi wa kanisa kwenye Agano Jipya: wazee, mashemasi, makasisi wangalizi, maaskofu, wachungaji, waalimu. Sifa tatu tu kati ya hizi ndizo zimeorodheshwa kwenye maandiko, kwa hiyo tutaangalia hizi 3, Paulo anatoa sifa kwa waangalizi. Katika Tito 1, anatumia sifa zile zile kwa wazee, lakini katikati ya orodha alitumia sifa kwa waangalizi. Ushauri huu kwamba mipaka hii haibadiliki inaweza ikatusaidia katika kuonyesha ofisi katika kanisa. (Tazama Matendo 20:17,28 and 1Pet 5:1,2).

### A. Sifa kwa Waangalizi (1 Timotheo 3:1-7)

Sifa za mwangalizi (wakati mwingine askofu) zimeelezewa katika 1Timotheo 3:1-7 na kuorodheshwa kama ifuatavyo:

- Njia ya hapo juu
- Kuwa na mke mmoja
- Kujiweza
- Kuwa na kiasi
- Anayeheshimika
- Mkarimu
- Anayejitoa kufundisha
- Asiwe mlevi
- Asiwe mwenye fujo, lakini mpole
- Siyo mchokozi
- Asiwe anapenda fedha
- Anaongoza familia yake vizuri
- Anayeona kwamba watoto wake wanamtii kwa heshima
- Siye aliyekata shauri mpya
- Awe na sifa njema kwa watu wa nje

Mtu anayechaguliwa kama mwangalizi lazima aonyeshe sifa hizi katika maisha yake. Msisitizo ni kwenye tabia yake ya sasa. Kama amewahi kuwa na sifa mbaya katika maisha yake ya nyuma, kunahitajika kipindi hakika cha kuishi utakatifu kushawishi kusanyiko kwamba hakika amebadiri njia zake na kutokuendelea kuanguka dhambini.

### B. Sifa za Wazee/Waangalizi (Tito 1:5-9)

Katika waraka wake kwa Tito, Paulo anairudia orodha yake ya sifa kwa wazee na waangalizi. Tambua kuwa orodha hii ya sifa ni sawa na orodha iliyopanuliwa iliyotolewa katika 1 Timotheo 3:1-7

- Asiye na lawama
- Mme wa mke mmoja
- Watoto wanaamini na siyo wenye fujo na wasiotii
- Asiyechukua zaidi
- Siyo mwepesi wa kughafirika
- Asiyejitoa kwenye ulevi
- Siyo mwenye fujo
- Asiyefanya kazi ya mapato yasiyo ya halali

### C. Sifa za Mashemasi (1 Timotheo 3:8-13)

Sifa za mashemasi ni sawa na za wazee, isipokuwa tu mashemasi hawatakiwi kufundisha. Mahitaji makuu kwa mashemasi yamneorodheshwa katika 1 Timotheo 3;8-13 kama:

- Kuheshimiwa
- Mwaminifu
- Asiyekunywa kupindukia
- Siyo mchoyo wa fedha
- Awe na dhamiri njema
- Aliyejaribiwa
- Awe na mke mmoja
- Anayeangalia watoto wake na nyumba yake vema

Mahitaji ya kiroho ni ya sharti kama yalivyo ya wazee. Lazima pia wawe wamehakikishwa tabia njema. Tofauti pekee, ya kutokutakiwa kufundisha, tayari inaeleweka kwa kuangalia majukumu yao. Neno la Kiyunani *diakonos*[1] lililotafasiliwa kama mashemasi inamaanisha anayehudumu. Kuonekana kwa kwanza kwa mashemasi kunaonekana katika Matendo 6. Wakati huo kulikuwa na tatizo kanisani. Baadhi ya wajane wa mataifa walikuwa hawajaliwi katika ugawaji wa chakula kwa wahitaji. Mitume waliolielekeza kanisa hawakufikiri kama ilikuwa sawa kwao kuacha madaraka yao na majukumu ya kufundisha na kuomba. Badala yake, waliliomba kusanyiko kuchagua watu saba wanaoweza kuamiwa kwa kazi ya ugawaji chakula.

Kwa hiyo tunaelewa kwamba mashemasi wa Agano Jipya waliwajibika kwenye vitu na mahitaji ya kijamii kanisani. Kwa kuwa waliweza kuangalia mambo ya fedha za kanisa, mkazo wa hitaji la kiroho na hitaji la kujaribu linaeleweka. Kusudi la mashemasi ni kuwapa mda wazee wa kukazania kwenye mahitaji ya kiroho ya kanisa.

Katika 1 Timotheo 3:11 mfumo wa kike wa *diakonos* unatumika. Baadhi ya makanisa wanalichukulia hili kumaanisha “mke wa shemasi.” Wengine wanalitafsiri kumaanisha shemasi wa kike., au “ushemasi” (Tazama pia Warumi 16:1 Foibe anapoitwa shemasi.) makanisa yenye mashemasi wa kike, wana wajibu wa kutumika unaofanana na wa mashemasi.

## IV. MAJUKUMU NA UPENDELEO WA VIONGOZI WA KANISA

### A. Majukumu

1 Petro 5 anayaweka majukumu ya wazee/wachungaji/waangalizi: kuchunga kundi la Mungu. Baadhi ya mambo maalumu wanayotakiwa kufanya ni kama ifuatavyo:

---

[1] Διακονος

- Kufanya kazi ya uinjilisti (2Ti 4:5).
- Kutawala—neno la Kiyunani lililotafsiriwa tawala au utawala ni *proistemi*[2], ambayo ina maana "kuwa juu ya, kusimamia, wa mkuu wa, kuwa mlinzi au mwangalizi." Tambua kuwa Petro analiweka wazi kwamba katika kutimiza kazi hii Timotheo hatakiwi "kulundikia watu wake, lakini kuwa mfano kwao.
- Kusoma neno hadharani (1Tim4:13).
- Kulihubiri neno (2Ti 4:1-2).
- Kulifundisha neno (Tito 2:1).

### B. Nafasi

Viongozi waaminifu wanastahili heshima. Heshima inatokana na maisha ya kimungu yaliyohakikishwa waliyoishi ili kuchaguliwa kama viongozi. Baraza lao linatakiwa bila mzaha kufikiriwa na kusanyiko. Nyongeza, watu wanatakiwa kuwa waangalifu juu ya kuwalaumu juu ya mabaya wanayofanya isipokuwa yawe yameshuhudiwa na mashahidi wawili (1Tim 5:19-20). Kwa jinsi hiyo, kama wamehakikishiwa dhambi, wanatakiwa waonywe kwa ukali kuliko mjumbe wa kawaida. Hii ni katika kutunza nafasi yao ya hadharani. Wana nguvu kubwa ya kuwagusa watu kwa uzuri au ubaya, na kwa hiyo wanapata lawama kali kama wanaanguka.

Wazee waaminifu wanaofundisha wanastahili kusaidiwa kifedha. Paulo analiweka wazi 1 Wakorintho 9:7-12 kwamba kanisa jipya lilitarajiwa kusaidia hao wanaotumika kuwafundisha. Makanisa mara nyingi yanadharau mafundisho haya, na kutarajia wazee wao, wachungaji au wapanda kanisa kutafuta chanzo kingine cha kipato. Matokeo yake, wazee wanaweza kufanyishwa kazi zaidi au kutopata mda wa kutosha kwenye kazi ya usimamizi na kufundisha. Kuongoza na kufundisha kanisa ni kazi isiyo ya mzaha. Ni lazima kuyakinisha kwenye mandhali ya kanisa lako jinsi ya kutimiza majukumu haya kwa wazee wako. Lengo linatakiwa liwe kuwaunga mkono ili kwamba waweze kujitoa kwenye huduma ya mda wote kwenye kanisa. Ingawa Paulo alikuwa tayari kufanya kazi kama mtengeneza matenti wakati kulipokuwa hakujawa na kanisa la kumsaidia, mara moja alihamia kwenye huduma ya mda wote mara tu ilipowezekana. Hili linaonekana kuwa swala katika Matendo 18:1-5 wakati Sila na Timotheo hatimaye walipoleta zawadi kutoka makanisa ya Masedonia (cf. 2Kor 8:1-4).

Ni kiasi gani kinafaa? Paulo anatumia neno "tunuku mara mbili" Timotheo 5:17-18. Ingeweza kumaanisha "mara mbili ya mshahara," lakini ilionekana zaidi kurejea kwenye tunuku kwa mifumo miwili—heshima na zawadi ya fedha. Katika swala hilo, wanastahili angalau kiasi ambacho mtu wa kawaida kwenye kusanyiko anachopokea. Kama hawana hitaji la kifedha, wanaweza wakakataa sehemu hiyo ya tunuku kama Paulo alivyofanya (1Kor 9:12) lakini hiyo ni haki ya mzee, siyo ya kanisa. Ni jukumu la kusanyiko kuwahudumia kwa njia hii, na kwa hiyo kuonyesha heshima yao kwenye kufundisdha neno. Kama wakikataa, kanisa linatakiwa litumie fungu hilo kusaidia upandaji wa kanisa jingine, kama Wamasedonia walivyofanya kwenye mfano hapo juu.

## V. UFUPISHO

Ingawa Agano jipya lina kila moja ya aina hii ya utawala na wazee, haina amri maalumu juu ya jinsi kanisa la mtaa linavyotakiwa liandaliwe. Kama mpanda kanisa, unatakiwa kiungalifu na kimaombi kufikiria uchaguzi mwingine. Historia yako ya nyuma na dhehebu unalofata litaweza kugusa zaidi maamzi yako ya utawala wa kanisa. Sehemu ya wajibu wako katika kuandaa kikundi kiini chako kugeuka kuwa kanisa ni kuwafundisha juu ya utawala wa kanisa na hasa aina ya utawala wao kama kanisa jipya watakaokuwa nao.

---

[2] προιστημι

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Unapofikiria aina ya utawala wa kanisa ulioelezewa katika somo hili, ni baadhi ya mambo yapi bayana ambayo yangeweza kuchangia kwenye kuzidisha? Nini baadhi ya vitu vya kinyume ambavyo vingeweza kuzuia kuzidishwa kwa kanisa?
- Unakubaliana na mausia ya Paulo ya kuwalipa wazee wanaofundisha? Ni nafasi ipi kanisa unalopanda litayochukua katika hili?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Ainisha wanaume (wawili) kwenye jengo lako la kanisa ambao unadhani wana umuhimu kuwa wazee. Anzisha mpango wa kufuasa na kuwajaribu kwenye hali ya tabia maalumu zinazohitajiwa kwa mzee.

# TABIA YA KIROHO

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 11

# Upendo Kama Msingi kwenye Huduma

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuzalisha watu wanahudumia kutoka kwenye moyo wa upendo.

☞ **Wazo Kuu**

- Uhusiano wetu na Mungu unagusa jinsi tunavyojihusisha na wengine
- Upendo usio na sababu alio nao Mungu kwetu kama ulivyoelezewa kwenye injili ni kielelezo chetu cha kuhusiana na wengine.
- Moja ya kitu cha kuvutia cha kanisa jipya kinatakiwa kiwe uhusiano wa upendo uliopo miongoni mwa waumini.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Kwa matokeo ya somo hili wahusika wanatakiwa:

- Kuwa wanaopendana na wenye neema kwa wengine.
- Kuelewa jinsi ya kuhudumu kwa wengine kutoka kwenye moyo wa upendo kwa watu.

## UTANGULIZI

Tumekuwa tukijifunza jinsi injili inavyogusa kutembea kwetu na Mungu. Tumezungumzia jinsi Mungu anavyotupenda kama baba anavyopenda mtoto kupitia neema na rehema. Uhusiano wetu na Mungu unagusa jinsi tunavyohusiana na wengine. Mtu anayeishi kwa imani hafungwi na sheria, lakini upendo. Imani yake inazalisha ndani yake upendo wa kweli. Kwa hiyo tunaona sifa hizi zisizotenganishwa za imani na upendo zikifanya kazi pamoja.

## I. INJILI KAMA KIELELEZO CHA UHUSIANO

Maisha yetu ya kiroho yanaanza na kuzaliwa kiroho. Kabla ya kuzungumzia injili kama kielelezo cha mahusiano, tunahitaji kufanya marudio ya kile ambacho injili imefanya katika maisha yetu. Kama jedwali la 11.1 linavyoelezea, kuna aina mbili za msingi lakini njia tofauti za kuhusiana na Mungu. Njia hizi mbili zinadhuru jinsi tunavyohusiana na Mungu vilevile na wengine.

**Jedwali 11.1 Injili na Dini**

| Injili | Dini |
|---|---|
| *(Mungu kwa nguvu zake anajaribu kumfikia mwanadamu)* | *(Mwanadamu kiasili anajaribu kumfikia Mungu)* |
| Neema | Matendo |
| Imani | Utii |
| Upendo usio na sababu | Kuhukumu |
| Roho Mtakatifu anayebadilisha | Juhudi za binafsi |
| Neema inapelekea utii | Utii unapelekea neema |

### A. Injili Inaokoa

Ujumbe wenye nguvu wa injili unatubadilisha kwa njia nyingi. Tumetangaziwa haki kwa imani kwenye injili inayotuokoa kutoka kwenye hukumu ya Mungu na kuhakikisha maisha ya milele.

### B. Injili Inabadilisha

Injili inagusa zaidi ya mwisho wetu wa milele. Ujumbe wa injili unatubadilisha siku hadi siku. Tumefanywa watakatifu kwa damu ya mwokozi wetu kwa msalaba ambao umewahi kutokea mbele yetu kama kitovu cha maisha yetu ya kiroho. Tunatembea kwa imani tukiamini kwamba Mungu anatupenda. Nje ya shukurani zetu za wokovu kwa njia ya injili, tunaishi maisha ya utii kwenye mapenzi ya Mungu. Kwa kuelewa nafasi yetu katika Kristo, tunapata nguvu za kushinda dhambi na kukua katika ukomavu.

### C. Injili Inatoa Kielelezo cha Uhusiano

La mwisho, injili inagusa uhusiano wetu na wengine. Injili ni upendo usio na sababu iliyosogezwa kwetu. Upendo huu usio na sababu kisha unaweza kuwa kielelezo ambacho tunahusiana na wengine. Katika kuliandikia kanisa alilokuwa amepanda Efeso, Paulo alitoa ushauri kuu akisema "muwe wakarimu na wenye huruma mmoja kwa mwingine, mkisameheana kama katika Kristo, Mungu ametusamehe" (Efe 4:32). Yesu aliwafundisha wanafunzi kuomba wakisema, "tusamehe makosa yetu kama nasi tunavyosamehe wadeni zetu" (Mt. 6:12).

Jinsi gani injili inaweza kuwa kielelezo cha uhusiano? Jinsi gani tunaweza kuwa wakarimu mmoja kwa mwingine? Kama tutakavyoona, Yesu alitufundisha jinsi gani.

## II. UPENDO WA MUNGU WA KUJITOA, USIO NA SABABU

Upendo wa Mungu wa kujitoa na usio na sababu umeelezewa kwa undani zaidi kwenye maisha na mafundisho ya Yesu.

### A. Amri Kuu

Wakati Yesu alipokuwa akihojiwa na mafarisayo kuhusu amri iliyo kuu, Alifupisha kwa kunukuru kutoka Kumbukumbu la Torati 6:5: *"Mpende* Bwana kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote." Kisha aliongeza amri kuu ya pili, iliyochukuliwa kutoka Walawi 19:18, ambayo ilifupisha sheria zilizobaki za Agano la Kale, "Mpende jirani yako kama unavyojipenda" (Mt 22: 34-40, Mark 12:28-31). Kwa pamoja hii mara nyingi inaitwa amri kuu. Amri kuu ndivyo Yesu anavyotaka tufanane: kufanana na Kristo. Ni ufupisho wa sheria: utakatifu.

Katika jitihada zao za kutunza sheria, mafarisayo walionekana kusahau amri hizi mbili. Walizipenda sheria lakini si mtoaji wa sheria, na jirani kidogo sana. Hata hivyo, amri hizi zilikuwa mipaka kwenye uhusiano wa watu na Mungu na mwanadamu mwenzake.

### B. Amri Mpya

Mda mfupi kabla ya kifo chake, Yesu aliwapa wanafunzi wake baadhi ya maelekezo maalumu ambayo yangekuwa mipaka ya kuwaonyesha jinsi ya kuhusiana mmoja kwa mwingine. Mipaka hii inapatikana katika Yohana 13-17. Alianza kwa kutoa amri mpya, "***Pendaneni.*** Kama *nilivyowapenda*,. Ndivyo mnavyotakiwa kupendana" (Yh 13:34). Hii ni sawa na amri kuu. Lakini, kuna tofauti kuu mbili:

1. *Upendo ni miongoni mwa waumini.*

Katika amri kuu, tumefundishwa kumpenda Mungu na majirani zetu. Katika amri hii mpya, tunaona kwamba kunatakiwa kuwa na upendo maalumu miongoni mwa wafuasi wake: watoto wangu…pendaneni" (Yh 13:33-34).

> Tunapokuwa hatupendani, watu wanashangaa, I wapi nguvu ya injili?

Yesu aliendelea kueleza ushuhuda kwamba upendo huu miongoni mwa waumini ni kwa waliopotea aliposema, "Kwa hili watu wote watajua kwamba mu wafuasi wangu, kama **mnapendana"** (Yh. 13:35). Wakati wakristo wanapokuwa hawapendani, ni moja ya shuhuda mbaya zaidi. Kama hao wanaoamini injili hawapendani, kisha ni namna gani wasioamini wataelewa kuwa injili inaleta amani na Mungu? Tunapokuwa hatupendani,

watu wanashangaa I wapi nguvu ya injili? Inaleta amani kati ya mtu na Mungu… haitakiwi pia kuleta amani kati ya watu? Makanisa yetu yanatakiwa kuwa picha ndogo ya ufalme wa Mungu duniani, mahali ambapo upendo wa Kristo wenye nguvu unaonekana.

2. *Kiwango cha Upendo.*

Katika amri kuu, kiwango cha kupenda wengine kilipimwa na upendo wa kujipenda. Lakini katika amri mpya, upendo wa Kristo wa kujitoa kinakuwa kiwango chetu cha jinsi tunavyotakiwa kupendana.


Yesu ana maana gani anaposema anatoa amri mpya? (Yn 13:34). Katika Kiyunani, kuna maneno mawili tofauti yanayoweza kutafsiriwa “mpya." Ya kwanza, *neos*[3], inamaanisha ambacho hakijawahi kuwepo kamwe. Lakini neno la upya Yesu alilotumia lilikuwa neno jingine, *kainos*[4], *linalomaanisha* “upya katika kiwango." Alielezea kiwango kipya cha upendo katika Yohana 15:12,13: *“Amri yangu ni hii: pendaneni kama nilivyowapenda. Hakuna upendo ulio mkuu kama huu wa mtu kutoa maisha yake kwa ajili ya rafiki zake."* Kufuatana na mfano wa Yesu, watoto wake lazima wawe na upendo mmoja kwa mwingine unaopimwa na upendo Bwana alionao kwetu.

## III. UPENDO WA MUNGU ULIHUSISHWA KWENYE UHUSIANO

Uhusiano kati ya mtu na Mungu utakuwa na mguso wa moja kwa moja kwenye uhusiano na wengine.

Uhusiano kati ya mtu na Mungu utakuwa na mguso wa moja kwa moja kwenye uhusiano na wengine. Katika kielelezo 11-2, tunaona mchoro rahisi unaelezea hili. Msitari wa wima unasimama badala ya sehemu ya kwanza ya amri kuu *“Mpende Bwana Mungu wako…”* na sehemu ya pili ya Agano Jipya “…kama nilivyowapenda.” Mstari wa ulalo unawakilisha uhusiano wetu kwa wengine ambao tunatakiwa kuwapenda kama Yesu alivyotupenda. Tao lenye nukuta inawakilisha ukweli kwamba njia ambayo tunahusiana na wengine ni sawa na uhusiano wetu na Mungu.

**Kielelezo 11.2 Kumpenda Mungu na Kuwapenda Wengine**




Kama mtu anahusiana na Mungu kiuhalali—kutakuwa na kawaida ya kuhusiana na wengine kwa njia sawa. Kama mtu anaamini kwamba Mungu ana hasira nao, kisha kuna uwezekano wa kuwachukia wengine. Kwa upande mwingine, kama mtu anaelewa kuwa Mungu anawapenda bila sababu, kisha atakuwa huru kuwapenda wengine kwa njia sawa.

[3] νεος
[4] καινος

Njia moja ya kupima ukuaji wa kiroho kisha ni kupima jinsi mtu anavyohusiana na wengine. Inawezekana kuwa mkristo mzuri lakini bila kupatana na wengine vyema? Kwa sababu ya amri mpya, haionekani hivyo. Tunatakiwa kumpenda Mungu na wengine.


Inaonekana kwamba upendo kama sehemu ya kufanana na Yesu mara nyingi inachukuliwa vibaya. Kwa nini ni hivi? Inawezekana, kwa sababu ni rahisi kutii orodha ya sheria kuliko kufanya mioyo yetu kubadilika. Aina ya watu wengi wanaweza kutii sheria na taratibu, lakini inahitaji moyo kubadilishwa na Mungu ili kupenda.

## IV. UPENDO KAMA MSINGI WA HUDUMA

Upendo wa Mungu usio na sababu unatakiwa uwe msingi wa huduma. Kwa kuwa Mungu ametupenda hivyo kwa upendo usio na sababu, tumeitiwa kuwapenda wengine kwa njia sawa. Mungu ametugusa kiasi hicho kwa upendo wake kwamba tuweze kusukumwa kutoa upendo kwa wengine kwa njia ambayo inakuwa na ushuhuda kwa Kristo wa alichofanya kwa ajili yetu.

Ni akina nani hao katika huduma ambao tunaonyesha upendo huu? Ni akina nani “wengine” ambao Mungu amewaweka katika maisha yetu?  Kadiri Mungu alivyowaweka karibu, ndivyo tulivyo na wajibu mkuu wa kuwapenda na kugusa maisha yao kwa njia ambayo Mungu amefanya kwetu. Mpanda kanisa halisi kisha anaweza kuwa na maeneo yafuatayo ya huduma kama yalivyoonyeshwa katika kielelezo 11-3.

**Kielelezo 11.3  “Akina Nani Tunaowapenda?**




Inaweza kuwa kitu cha kawaida kwako kutokuwapenda baadhi katika kusanyiko lako. Huduma ni ngumu. Lakini upendo wa Mungu usio na sababu unapohusisha mahusiano, ni wazi kwamba Mungu yuko kazini. Hii kisha ni ushuhuda kwa waliopotea. “Kwa hili watu watajua ya kuwa mu wafuasi wangu, kama mnapendana" (Jn 13:35).

Kitu kinachovutia zaidi kuhusu jengo lako la kanisa kinapaswa kuwa hadhi ya uhusiano ambao umeanzishwa. Upendo wa kujitoa na usio na sababu unapaswa kuwa kawaida kuanzia kwenye uongozi wa kanisa. Hivi ndivyo Mungu anavyotupenda na jinsi tunavyopaswa kuwapenda wengine.

Kitu kinachovutia zaidi kuhusu jengo lako la kanisa kinapaswa kuwa hadhi ya uhusiano ambao umeanzishwa.

### SULUHU

Ukuaji kiroho ni zaidi ya ukuaji wote kwa kitu kimoja—katika upendo wa Mungu *usiojali.* Kutokukomaa kiroho ni kwa kwanza katika kutokukomaa kote katika upendo wa Mungu. Kuanguka kiroho kunatokana na kukosa kuelewa upendo wa Mungu. Na kukua katika upendo huu ndiyo tiba pekee. Wengi imani yetu katika Yesu Kristo, Bwana na mwokozi wetu, inajionyesha yenyewe katika matendo ya upendo, upendo kwa familia zetu, makaka na madada katika Kristo, kwa makanisa yetu, kwenye ulimwengu unaopotea. Bwana aweze kuimarisha imani katika mioyo yetu.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani unaweza kueleza "jirani" kama ilivyotumika katika amri kuu (mpende jirani yako kama unavyojipenda)? Ni nini ingekuwa matokeo kama kanisa lako lote lingetii amri hii?
- Yesu alimaanisha nini aliposema pendaneni "kama nilivyowapenda?"
- Ni muhimu kwa viongozi kutii amri hii kuliko kwa wengine kanisani? Kwa nini na kwa nini siyo?
- Jinsi gani unawapenda watu vyema?
- Fikiria tofauti upendo inaofanya kwenye hali zifuatazo: familia/marafiki; waumini na wasioamini? Wajumbe wa kanisa/viongozi?
- Jinsi gani imani yetu inayokua inavyogusa jinsi tunavyowapenda wengine?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Muulize Mungu akuonyeshe baadhi ya waumini ambao utaonyesha aina ya upendo Yesu alioamuru. Andika majina yao na nini utafanya. Acha nafasi ya kuandika matokeo wakati hili linapokamilika.
- Muulize Mungu akuonyeshe baadhi ya "majirani" ambao unatakiwa kuwaonyesha upendo. Andika majina yao na nini utafanya kuonyesha upendo kwao. Acha nafasi ya kuandika matokeo hili linapokamilika.
- Fikiria mtu ambaye uko karibu naye (mwenzi, mzazi, au mtoto). Jinsi gani unampenda mtu huyu? Ni kwa njia zipi ukosefu wako wa imani katika injili umeathiri jinsi ulivyowapenda? Ni dhambi ipi unahitaji kuitubu kwao? Fikiria njia thabiti unayotaka kumpenda mtu huyu kwa sababu ya imani yako iliyolejezwa kwenye injili.

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 12

# Kuuelewa Moyo wa Baba

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kwamba sisi kama viongozi tunatakiwa kuwa wenye upendo, wenye huruma kwa watu wanaofurahi wakati mwenye dhambi aliyepotea anapopatikana

☞ **Wazo Kuu**

- Mungu anawapenda watoto wake bila sababu
- Tunatakiwa kupenda kama baba anavyopenda

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuuelewa upendo wa baba kwa waliopotea.
- Kujua kwamba kama kiongozi wa kikristo tunatakiwa kuendelea kuchunguza tabia zetu na matendo yetu kwa waliopotea.
- Kumuuliza Mungu kutupa neema ya kupenda kama Mungu anavyopenda.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Mistari ya kwanza ya Luka 15 ni ya lazima katika kuelewa mfano wa Yesu anaofundisha katika ukurasa huu. Chukua mda mwanzo wa kipindi kuwafanya wafunzwa kufikiria maandalizi ya wakusanya kodi na "wenye dhambi" waliozunguka kumsikiliza Yesu. Fikiria mafarisayo kwenye masimulizi ya mwanzo wakiupinga uhusikaji waYesu na watu hawa. Fanya kipindi hiki kuwa cha mwingiliano kwa kusimama kujadili maswali yaliyowekwa kwenye somo. Acha mda mwishoni kwa ajili ya tathimini ya binafsi na matumizi.

## UTANGULIZI

Katika Biblia yote, Agano Jipya na la Kale tunaona kwamba upendo wa Mungu unapita siyo tu dhambi zetu, lakini kutokuwa na shukurani kwetu kwa upendo huo. Tumeitiwa kuwapenda wengine kama Mungu anavyotupenda. Lakini tunaelewa hasa hilo lina maana gani? Yesu, katika maisha yake ya mfano, anatufundisha zaidi hili lina maana gani. Moja ya fungu dhahiri na wazi zaidi linalozungumzia aina hii ya upendo ni mfano wa mwana mpotevu (Lk 15:11-31). Ni muhimu sana kwetu kuelewa upendo wa Mungu kwetu kama tunataka tutoe aina hiyo ya upendo kwa wengine.

## I. MIFANO MITATU YA VITU VILIVYOPOTEA -LUKA 15

### A. Mandhali ya Luka 15

Mistari ya kwanza miwili ya Luka 15 inatoa mandhali ya mafundisho ya Yesu kwenye mistari ya mwisho. Hapa tunaona Yesu akiwa amezungukwa na wakusanya kodi na wenye dhambi" wakiwa tayari kusikiliza mafundisho yake (Lk 15:1). Fikiria itakuwaje kwa Yesu kukaa akiwa anasimulia wakusanya kodi na "wenye dhambi." Hili lingefanyika wapi—nje? Kwenye uwanja wa nyumba kwenye aina ya nyumba za kimediteraniani? Kwenye dari? Ni aina gani ya watu wangekuwa kwenye kundi la waliokaa kumzunguka Yesu? Nini kingekuwa mezani? Kungekuwa na chakula" unasikia vicheko? Watu wanajaribu kumridhisha Yesu kwa masimulizi yao?

Baada ya kuwa na picha akilini mwako ya Yesu akiwa amekaa na wakusanya kodi na wenye dhambi, Sasa fikiria mafarisayo na walimu wa sheria (Lk 15:2). Wapi wangekuwa

wamesimama au kukaa? Kwa hakika siyo katika chumba kimoja na wakusanya kodi na wenye dhambi. Mafarisayo wasingeweza kuchanganyika na wenye dhambi. Pengine wangesimama nje gizani au kwenye matamvua ya umati umbali fulani –ili kutogusa mojawapo wa wenye dhambi. Ni nini Mafarisayo wananung'unikia?

Jiruhusu mwenye kuhisimguso wa tukio hili, na mkazo kati ya Yesu, umati uliokusanyika na Mafarisayo. Ukiweka tukio hili akilini, soma mifani ambayo Yesu anasimulia mwishoni mwa ukurasa.

### B. Mifano

Mifano mitatu katika Luka 15 ni pamoja na mfano wa kindoo aliyepotea (vv. 3-7), mfano wa sarafu iliyopotea (vv. 8-10), na mfano wa mwana mpotevu (vv. 11-32). Wazo kuu la mifano mitatu linapatikana katika Luka 15:10, *"Ninawaambia, kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa mwenye dhambi mmoja anayetubu."* Tambua ulinganifu ufuatao na utofauti kwenye mifano hii.

> "Ninawaambia, kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa mwenye dhambi mmoja anayetubu."

- Masimulizi yote matatu ni juu ya kutafuta vitu vilivyopotea (kondoo mmoja nje ya 100, sarafu moja nje ya 10, mwana mmoja nje ya wawili). Vitu vyote vilivyokuwa vimepotea vilikuwa na thamani. Kama Yesu anavyoisimulia mifano, anaanza na upotevu wa (kondoo mmoja kati ya 100), kisha upotevu unaendelea (sarafu moja kati ya 10), kisha mwishoni moja ya upotevu mkuu mtu anaoweza kuupata (mwana mmoja kati ya wawili).
- Vitu vilivyopotea katika mifano yote hatimaye vilipatikana.
- Kufurahia na kushangilia na wengine kulitokea wakati vitu vilivyopotea vilipopatikana. Jinsi gani unaweza kufikiria mchungaji, mama na baba walivyojisikia wakati walipopata vitu vyao vilivyokuwa havipo? Ni aina gani ya furaha unadhani ilitokea? Ni aina gani ya sherehe ungefanya kama ulikuwa umepoteza kitu fulani cha thamani kubwa na kisha kukipata tena?
- Kuna tofauti moja kati ya mifano ya kwanza miwili (kondoo aliyepotea, sarafu iliyopotea) na wa mwisho (wa mwana aliyepotea). Siyo sawa na ya kwanza miwili, katika mfano wa mwana mpotevu, hakuna anayekwenda kumtafuta. Kwa nini ni hivyo? Watu wengi wanadhani kuwa sababu kwa hili ni kuonyesha kwamba mtu anatakiwa awajibike kwenye matendo yake mwenyewe na "kuja nyumbani" Hili linaweza kwa sehemu kuwa kweli, lakini siyo wazo alilokuwa akifanya Yesu hapa. Kuna sababu ya undani ambayo inatakiwa iwe wazi tunapoangalia kwa karibu kwenye fungu.

## II. MFANO WA MWANA MPOTEVU

Kama ilivyo kawaida yake, Yesu anaweka msistizo wake kwenye tabia. Ukiangalia tabia ya kila mmoja wa watu hawa watatu kutatusaidia kuelewa nini Yesu alikusudia wasilkilizaji wake wajifunze kutoka kwenye mfano.

### A. Baba

Mfano huu wakati mwingine unaitwa mfano wa upendo wa baba. Baba wazi wazi alikuwa mtu mwenye upendo aliyempa mtoto uhuru wa kuchagua—hata alipofanya uchaguzi mbaya. Aliendelea kuonyesha upendo usio na sababu kwa kijana wake, kumkubari kurudi, akasahau yaliyopita. Upendo usio na sababu wa baba uliyeyusha ugumu wa moyo wa kijana, ulifungua milango ya tumaini lake kurudi, ulionyesha njia na kufanya utaratibu wa toba kuwa rahisi.

Mfano huu unatuambia siyo tu juu ya upendo wa baba. Kristo anatoa ndani yake picha bora ya jinsi gani mtu anaitikia kwenye upendo, ulioonyeshwa kwake na baba yetu wa mbinguni, Mungu. Urejeo wa vijana wawili unatuonyesha wanadamu wawili wanavyoitikia kwenye upendo wa baba.

### B. Kaka Mdogo

Mwitikio wa kaka mdogo ulionyesha mtu ambaye hasa alikuwa mchoyo. Hakuwa anajali baba yake anavyojisikia au wajibu wake kama mmoja wa familia. Katika utamaduni wa Wayahudi, baba anaweza kugawanya urithi lakini ana haki ya kutunza haki zote mpaka atakapokufa. Kwa

kijana kuuliza juu ya urithi wote na kipato chake wakati baba alikuwa bado anaishi ilikuwa kuonyesha kwamba alimfanya baba yake kama aliyekwisha kufa.

Ubinafsi wa kijana ulionyeshwa kwenye ufujaji wa mali bila kujali ni kwa ugumu kiasi gani baba yake aliupata kufanya kazi kuzipata fedha hizo. Hata hakuweza kufikiri kwamba kutokuwepo kwake kutamfanya kaka yake kufanya kazi sana.

> Mwana mpotevu ataweza tena kamwe kumkimbia baba?

Karibu kikawaida, ubinafsi wake hatimaye ulipelekea chukizo kwake na kukata tamaa. Alipofika mwisho wake mwenyewe, alikuwa mwenye toba. Wazi alikiri dhambi yake na kutofaa mbele ya baba (v. 21). Upendo ulioonyeshwa na baba na jinsi alivyompokea hakika kulifanya mguso wenye nguvu kwa kijana na kubadili maisha yake milele. Unafikiria nini…mwana mpotevu ataweza tena kamwe kumkimbia baba? Wengi wetu tutakubaliana kwamba ni mashaka kama ataweza kukimbia tena, kwa sababu amepata kile ambacho kila roho inatamani—upendo. Upendo ni kivuto kikuu kinachojulikana kwetu (vinginevyo mungu asingekuwa pendo, 1Yh 4:8). Upendo huu ulikuwa unapatikiana kwa mwana mpotevu bila masharti kutoka kwa baba yake. Ni kijana harisi upande wa kiroho. (Tazama Tabia ya Kiroho Somo la 6 "Kuishi kama Mwana Badala ya Mayatima" na somo la 7 "Yatima Anajifunza kuwa Mwana "kwenye Mwongozo wa Pili.)

### C. Kaka Mkubwa

Mara nyingi tunapendelea kijana mkubwa, ambaye matendo yake yanaonekana kuwa ya adabu kwetu. Kweli, alionyesha kuwajibika, alifanya kazi kwa juhudi kamwe hakuwahi kuiacha familia kama kaka yake mdogo alivyofanya. Hata hivyo, kaka mkubwa alikuwa pia anajijali mwenyewe. Hakujali kuteseka kwa baba yake au kwa kaka yake aliyepotea. Haielezeki ukweli kwamba alijaribu kamwe kutafuta kaka yake na kumrudisha. Hata hakuwa anamuita kaka yake, lakini badara yake alimrejeza kama "kijana mdogo" anapokuwa anaongea na baba yake (v. 30). Tabia yake ilikuwa ya mwenye wivu kwa kaka yake na chuki kwamba baba yake angemtunukia kaka yake badala ya yeye. Alijihesabia haki mwenyewe kwa misingi ya kazi alizomfanyia baba yake.

Kwa ndani zaidi, kaka mkubwa alimuonea fitina kaka yake na kujisikia kuchokozwa wakati baba aliposherehekea kurudi kwa "mwana mpotevu". Alikuwa akifikiria kuwa alistahili kutendewa hivyo kutokana na kazi zake za juhudi kwa baba yake (v.29). Uamzi kama huo kutoka kwa kaka mkubwa unadhihirisha kwamba kwa miaka mingi, amekuwa akimfanyia baba nje ya hisia za utii, siyo upendo. Kusemea kiroho, mtoto huyu ni yatima (tazama Somo 6 na 7 la Tabia za Kiroho).

Moyo wake ulibakia kuwa baridi na kujifikiria, ambako kuliua uhusiano wake na familia yote. Kama kaka yake mdogo, alihitaji kutubu.

### D. Ufafanuzi

Mungu anawapenda watoto wake sawa na kama baba kwenye mfano anavyofanya—bila sababu. Kwa mfano huu, Yesu anajibu mashitaka ya viongozi wa dini (Mafarisayo na Masadukayo). Mwana mpotevu, ni alama ya wenye dhambi ambao Yesu alikuwa na ushirika nao. (Luka 15:1-2) Katika kusimulia mfano, Yesu aliwaelezea washutumu wake kwa nini alikuwa na ushirika na wenye dhambi—aliwapenda bila sababu. Viongozi wa dini waliomshitaki Yesu kwa kuwa na ushirika na wenye dhambi walikuwa wakifanya kama kaka mkubwa mwenye chuki na mwenye kijihesabia haki, wakati wangeweza kuwa kama baba, aliyejaa upendo usio na sababu na anayefurahia wakati aliyepotea anaporudi nyumbani.

## III. MATUMIZI—TUNAPENDA KAMA BABA ANAVYOPENDA?

Hatari halisi kwa waumini ni kwamba ingawa wote tumeshawahi kuwa wapotevu na kurudi nyumbani, tuna mazoea yenye nguvu ya kuwa kama kaka mkubwa <u>baada ya mda</u>. Yesu anatutaka tutubu kama kijana mdogo alivyofanya na kuwa na upendo ambao baba alikuwa nao. Maswali yafuatayo yatakusaidia kuonyesha hali yako ya kweli (kama au la umekuwa kama kaka mkubwa kwenye mfano).

1. Ni nini tabia yangu kwa waliopotea? Ninawadharau? Ni mwenye kuhukumu? Ni mwenye huruma na mwenye kusamehe ? Fikiria nyakati ambazo umewahi kuwa karibu na watu "wasiopendeka". Nini ulichofanya?

2. Ninawatafuta waliopotea kwa juhudi au kuwasubiri tu “waje?” Linganisha maneno ya Yesu katika Luka 19:10.
3. Nimeridhika “kula na wenye dhambi? Ninajari zaidi kile ambacho watu watasema juu yangu kuliko nilivyo kwa wenye dhambi?
4. “Ninakimbia kukutana na wenye dhambi” na kuwaonyesha huruma, au ninawakataa pamoja na dhambi zao? (Kwa mfano, nitafanya nini kama kahaba au mlevi wa madawa anapokuja kwenye ushirika wangu?)
5. Upendo wangu kwa baba ni kama ninavyowapenda hao anaowapenda? Wakati wenye dhambi wanapotubu, ninafurahi na kuwakubali kama makaka na madada?
6. Niko nanung’nika kwa ndani jinsi gani ninafanya kazi kwa juhudi na jinsi nisivyoshukuriwa badala ya kufurahia na kushangilia pamoja na Bwana?

**UTEKELEZJI WA AZIMIO**

Soma Luka 15. Kisha soma tena na jibu maswali kwenye matumizi. Tumia mda katika maombi na muulize Mungu akupe moyo sawa wa huruma kwa watu alionao Mungu. Kama kuna vitu unavyohitaji kukiri kwake, fanya hivyo. Kama unahitaji kukiri kwa wengine au kufanya mpango wa hatua makini kuhusu kuhusiana na wengine kama Mungu anavyohusiana nawe, andika hili pamoja na jinsi gani utafanya.

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 13

# Neema ni kwa Wanyenyekevu

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha jinsi maisha ya kikristo lazima kuishi kwa unyenyekevu. Nguvu zinakuja kutokana na udhaifu… na maisha ya kikristo lazima yatokane na unyenyekevu.

☞ **Wazo Kuu**

- Wakristo wanatakiwa wawe na tabia ya unyenyekevu.
- Tumeitwa kuhudumu si kwa nguvu zetu, lakini kwa nguvu za Roho Mtakatifu.
- Maombi yanaonyesha unyenyekevu kwa Mungu.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa jinsi ya kutumika kwa unyenyekevu.
- Kujua kanuni inayoimarisha inatoka katika udhaifu wetu.
- Kujitoa kwenye kutegemea uhusiano na baba.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Jaribio la unyenyekevu lina nguvu. Linaweza kufikisha kwenye nyakati za toba kwa washiriki. Angalia uwezekano wa kushughulika na mtu kwa maswala ya kiroho kila inapowezekana. Angalia njia nzuri za kuelezea wazo katika somo hili kutokana na uzoefu wako mwenyewe.

**UTANGULIZI**

Wakristo wengi wanahangaika katika kutunza unyenyekevu. Baadhi ya wakristo—hata viongozi—wanaanza kwa unyenyekevu, lakini baada ya baadhi ya mafanikio katika huduma, wanaanza kiburi cha uerevu au kujifanya jasili ambako kunapingana na unyenyekevu wa kikristo. Pengine hakuna kilicho cha kufisha zaidi kwa mkristo kama kiburi—na wapanda kanisa hawajatolewa pia katika hili. Siyo tu kwamba kiburi kinaunda mipaka kati ya wakristo makaka, lakini pia ni moja ya vitu hivyo ambavyo Bwana anavichukia (Mit 6:16-17).

Yesu aliliweka wazi kwa wafuasi wake kwamba wanatakiwa wasiwe wanajitumikia (Mt 20:20-28; Yn 13:1-16). Viongozi wengi wa kidunia wanatumia kuabisha au tabia ya ukubwa kuwafanya wafuasi kuwa chini. Vitu hivi vinatakiwa kamwe visiwe tabia ya mkristo (Mt 20:25,28; 1Pet 5:1-7). Kinyume chake, unyenyekevu inatakiwa iwe alama ya wakristo wote, na viongozi wakitoa mfano kama Kristo alivyofanya.

## I. UNYENYEKEVU—NI NINI?

> Kimakusudi kuchukua nafasi ya chini inaonekana makosa kwa ulimwengu…

Ni nini kinakuja kwenye akili yako unaposikia neno “unyenyekevu?” watu wengi wanafikiri unyenyekevu kama kuwa wa chini. Mara nyingine tunaelezea aliyevaa vibaya, aliyelishwa vibaya, mtu masikini kama ‘myenyekevu'' Wakati Mungu akitutaka kunyenyekea, hataki tujifikirie wenyewe kama masikini ombaomba, au fukara. Maandiko yanatuambia kuwa tu watoto wake na warithi pamoja katika ufalme wake na Kristo. Kuamini kitu kingine zaidi ni upotofu mkubwa wa ukweli wa kibiblia.

Unyenyekevu 'siyo kujifikiria mwenyewe kuliko unavyostahili' (Rum 12:3). Mtu mnyenyekevu hajivutii mwenyewe, wala kufanya vitu vya kuelezea umuhimu wake. Kimakusudi kuchukua nafasi ya chini inaonekana makosa kwa ulimwengu—na pengine hata kwa baadhi yetu. Lakini ni njia kwenye haki na njia ambayo wakristo, hasa viongozi, wanaonyesha injili kwa hao wanaowazunguka. Miili yetu inadharau sehemu ya chini na tuna vita mikononi mwetu kuchukua sehemu ya chini. Lakini ni sehemu wanyenyekevu watapata neema (Lk 14:10).

***"Mungu anapinga kiburi, lakini anawapa neema wanyenyekevu "*** (1Pet 5:5). Hatuachi katika hali yetu ya kiburi cha ujinga. Anatutaka tuwe wanyenyekevu. Ni kutoka katika sehemu ya wanyenyekevu tunapoelewa jinsi gani Mungu alivyo mkuu. Umewahu kujiona mwenyewe ukiwa katika mkwaluzano na Mungu? Inaweza ikawa kwamba baadhi ya mahangaiko tunayokutana nayo ni juhudi za Mungu kutufundisha unyenyekevu?

Pengine njia nzuru ya kuelewa unyenyekevu ni kujichunguza wenyewe. Maswali kumi na mawili yaliyoorodheshwa katika jedwali 13.1 yatatusaidia kuelewa unyenyekevu wakati yakidhihirisha baadhi ya njia tunazoshindwa. Tafakari kila swali kwa uangalifu

**Jedwali 13.1 Mtihani wa Unyenyekevu**

1. Jinsi gani unachukulia upinzani?
2. Watu wanaona rahisi kuja kwako? Unaingilika?
3. Mara kwa mara unajihusisha na mahangaiko ya madaraka na mabishano?
4. Unajikuta ukifikiri kuwa kila mmoja ana makosa isipokuwa wewe?
5. Je hasira inajibanza karibu na maisha yako?
6. Unaweza kufurahia unaposikia mafanikio ya wengine?
7. Wengine wanaweza kukudhania kama mtu mpinzani?
8. Unajikuta ukijitetea mwenyewe kwa wengine?
9. Ni msikilizaji mzuri, unayweza kukazania wengine badala tu majibu yako au ni nini kitu sahihi cha kufanya?
10. Kimakusudi unachukua sehemu ya chini? (Luke 14:7-11)
11. Ni mwenye rehema na mpole, au kuna ukingo mgumu kwenye utu wako?
12. Maombi ni harakati zako za kwanza kwa moyo wako?

## II. MIFANO YA UNYENYEKEVU

### A. Yesu

Mtume Paulo wazi anaelezea kuwa Yesu ni mfano wetu wa unyenyekevu. Tunajifunza katika Wafilipi 2:5 kwamba tunatakiwa tuwe na tabia sawa kama ya Yesu Kristo, aliyejinyenyekeza mwenyewe hata kiasi cha kufa.

> Unyenyekevu ni kukubali kwamba " ni mtegemezi juu ya Mungu kwa lolote ninalotaka kukamilisha."

Mfano wetu wa uyenyekevu, Yesu, alikuwa mkamilifu katika vitu vyote. Hata hivyo, **mtu mkailifu—Yesu Kristo—alikuwa mtegemezi halisi!** Tambua Yesu alichosema juu yake mwenyewe: *"Nitawaambia ukweli, mwana hawezi kufanya lolote peke yake; Anaweza kufanya yale tu anayomuona baba anafanya, Kwa sababu kila baba anachofanya, mwana pia anafanya"* (Yn 5:19-20). Kama mtu yeyote hakuhitaji kutegemea, Yesu alikuwa mmoja wapo. Lakini utegemezi siyo dalili ya udhaifu, lakini badala yake dalili ya uwezo. Hii ni njia ya juu-chini ya kuangalia yote uongozi na maisha ya kikristo.

Unyenyekevu ni kukubali kwamba "siwezi kufanya peke yangu. Ni mtegemezi juu ya Mungu kwa lolote ninalotaka kukamilisha." Katika ulimwengu tuna mahangaiko na wazo la unyenyekevu. Tunauruhusu ulimwengu kuweka viwango vyetu, na siyo Mungu.

**B. Paulo**

Mpanda kanisa mkuu Paulo alikuwa na mengi ya kujivunia kwa kiwango cha mwanadamu (Flp 3:4-11, 2Kor 11:22-29). Kwa jinsi hiyo, tunaweza kuona kwamba Paulo alikua katika unyenyekevu kwa kipindi chote cha huduma yake. Ukigundua kuwa mwanzoni mwa huduma yake anajieleza mwenyewe kama “mdogo kuliko mitume wote” (1Co 15:9). Baadaye, kwenye barua yake kwa Wefeso, anajiita mdogo kuliko watakatifu wote” (Efe 3:8). Na katika hatua ya mwisho ya maisha yake anajieleza kama mkuu wa wenye dhambi” (1Tim 1:15).

Paulo pia alikuwa na ”mwiba” ambao hatuuelewi kabisa, lakini anamuuliza Mungu kuuondoa. Tambua mchango wake kuhusu ombi hili: “*Lakini akaniambia, neema yangu yatosha kwako, kwa kuwa uwezo wangu unadhihirika kwenye udhaifu.’ Kwa hiyo nitajivuna zaidi juu ya udhaifu wangu ili kwamba nguvu ya Kristo ikae ndani yangu. Hii ndiyo sababu, kwa ajili ya Kristo, ninafurahia udhaifu, matokeo yake, katika ugumu, katika mateso, katika matatizo. Kwa kuwa ninapokuwa dhaifu, ndipo nina nguvu"* (2Kor 12:9-10). Ilikuwa muhimu zaidi katika mtazamo wa Mungu kwa Paulo kushuhudia kwa njia ya “mwiba” na kuishi kwa unyenyekevu wa kumtegemea Mungu, Kuliko Paulo kuwa huru kutokana na mwiba na kuwa na kiburi. Mungu anawataka watoto wake wamtegemee. Mungu anatutaka wewe na mimi tumtegemee.

Haki zetu ni mfumo mwingine wa kutotegemea. Linganisha na tofautisha mtu ambaye ana nguvu kwa nje (kuwa na nguvu mwenyewe) lakini dhaifu kwa ndani na kiongozi ambaye kwa nje ni dhaifu lakini kwa ndani mwenye nguvu Kielelezo 13.2).

**Jedwali 13.2 Sauli and Paulo**

| **Sauli:**<br>***Kwa nje mwenye nguvu kwa ndani mdhaifu*** | **Paulo:**<br>***Kwa ndani mwenye nguvu kwa nje dhaifu*** |
|---|---|
| Mtu huyu alikuwa na nguvu katika kusudio la “kufanya mambo sawa.” Jitihada zake hata zilimwendesha kupeleke wakristo jela. Kama Mfarisayo, alifata sheria bila mzaha. Anaweza kuwa alikuwa hana waa kwa nje, lakini kwa ndani alikuwa akiharibika Flp 3:4-11). | Paulo alipokata shauri, aligeuka kutotegemea sana juhudi zake kukamilisha mambo na kutegemea zaidi katika nguvu za baba zinazofanya kazi ndani yake. Hakuwa tena anajali jinsi alivyokuwa akidhaniwa kwa nje na kuchagua kuchukua sehemu ya chini. Fikiria jinsi Paulo alivyojinyenyekeza mwenyewe kwa Wakorintho. *“Nani aliyedhaifu nisiwe dhaifu na mimi? Ni nani aliyekwazwa, nami nisichukiwe?" (2Kor 11:29). “Lakini mimi hasha nisione fahari katika kitu chochote isipokuwa katika msalaba wa Yesu Kriato." (Gal 6:14).* Tunaona mtu aliyekuwa mwenye nguvu kwa sababu hakujali kile wengine walichomfikiria. Alijali tu kile Yesu alichomdhania na matokeo yake, akawa mtu mwenye nguvu aliyetumiwa na Mungu katika namna ya ajabu. |

**III. MAOMBI YANAONYESHA UNYENYEKEVU KWA MUNGU**

Wakristo wengi wana ufahamu mdogo wa jinsi ya kuishi kwa kutegemea na kutumaini wakati maisha yanapokuwa nje ya uwezo. Hata hivyo, maombi yanaweza kuwa njia nyingine ya sisi kuonyesha kutotegemea. Wakati mwingine tunaomba kupata kuzuia hali ambazo ziko nje ya uwezo. Lakini hasa maombi ni juu ya Mungu kuwa juu ya utawala. Ni kukubabali utegemezi kamili kwa Mungu. Mtu mnyenyekevu haombi kujaribu kupata uwezo kudhibiti hali. Badala, anaomba kuunganishwa kwenye kusudi na mpango wa Mungu. Hili linaeleza maombi yako?

**IV. MAISHA YA KIKIRISTO YENYE TABIA YA UNYENYEKEVU**

Kiburi kinatufanya kutogundua hitaji letu la kutegemea Mungu. Tulianza maisha ya kikristo kama waombaji na Mungu akatupa mkate wa kula. Alitoa kwetu vya kutosha kama alivyotoa kwa Waisraeli walipokuwa wakitangatanga jangwani. Kila siku walihitaji mkate kutoka kwa baba kuwawezesha. Hii ni hali sawa tuliyomo. Lakini tunapoamua hatuhitaji mkate, tunaingia kwenye matatizo. Si waombaji tena lakini badala yake tuna vyanzo vyetu wenyewe vya mkate. Hii ni kujitegemea na inatokana na upendo wetu kwa haki zetu wenyewe.

Kiburi na kujitegemea pia kunawafanya viongozi kuwa wagawaji wa mkate badala ya kuelekeza mkate ulipo. Hii ni hatari ya kutoka nje ya injili. Tunadhani kuwa tuna kile ambacho watu wanahitaji badala ya Yesu kuwa nacho. Tunashauri utegemezi kwetu badala ya Yesu. Kama viongozi, tunahitaji kuwapeleka watu kwa aliye na nguvu, chakula, faraja na msamaha.

Kiburi na kujitegemea pia kunawafanya viongozi kuwa wagawaji wa mkate badala ya kuelekeza mkate ulipo.

1 Petro 5:1-4 anatoa baadhi ya kanuni kwa hao wanaotaka kuwa wazee wa kanisa au viongozi. Wanatakiwa waelezeke katika njia nne zifuatazo:

- Mchungaji
- Aliyetayari kutumika
- Asiyewarundikia wengine
- Mfano

Aina ya uongozi ulioelezewa juu ni hakika wa upendo na wa utumishi. Mfuasi kikawaida atataka kuitikia kiupendeleo kwa kiongozi anayefikia sifa hapo juu. Watu kikawaida hawataki kumuumiza mtu mwingine anayewapenda. Hii ndiyo sababu ni ya asili hasa kwa Petro, kwenye msitari tu unaofatia (1Pe 5:5), kumtia moyo kijana, hakuna shaka wafuasi wa wazee, kunyenyekea kwenye uongozi wao.

Pia tunajifunza katika mstari wa 5 na 6 kwamba "wote" tunahitaji kutafuta unyenyekevu: *Kujivika mwenyewe unyenyekevu.*" Kwa maneno mengine "utafute." *"Jinyenyekeshe mwenyewe"* (vs. 6) ni amri, siyo uchaguzi, kutoka kwa Roho Mtakatifu. Mausia haya siyo tu kwa viongozi au kwa wafuasi. Ni kwa kila mmoja.

Jedwali lifuatalo linaweza kusaidia kuonyesha tofauti kati ya wakristo wanaoishi kwa kujitegemea na yule anayeishi kwa kumtegemea Mungu.

**Jedwali 13.3 – Kujitegemea dhidi ya Utegemezi**

| Kujitegemea—KIBURI | Utegemezi—UNYENYEKEVU |
|---|---|
| • Mtu anayejitegemea ana mafanikio/kushindwa "mtazamo wa vitu.<br>• Kutokuamini ni kipande kwa mtu huyu kwa sababu anajua ana kikomo. | • Mtu anayemtegemea Kristo anaelewa kwamba Yesu yuko juu. Anaishi na ujasiri huu.<br>• Imani ni kitovu cha maisha kwa mtu huyu. Kushindwa ni kutokuamini. |

## SULUHU

Umejawa na kiburi au una tabia ya unyenyekevu? Kama si munyenyekevu, kisha unaacha baraka kuu za Mungu mwenyezi anayetoa neema kwa **wanyenyekevu**. Zungumza na mshauri wako juu ya hitaji lako la kuwa mnyenyekevu mbele za Mungu. Fanya hili kuwa kitu cha kuombea.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini unadhani wakristo wengi, wakiwemo viongozi, wanahangaika na unyenyekevu?
- Ni katika njia zipi unakuta kwamba ni vigumu kuwa mnyenyeklevu?
- Kwa nini Mungu anataoa neema kwa wanyenyekevu?
- Ni tofauti gani unyenyekevu unafanya katika maisha ya mpanda kanisa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Tafuta mtu wa kuwajibika kwake, mtu ambaye unaweza kushirikisha kwa ukweli na uaminifu.
- Muulize mshiriki wako wa kuwajibika kukusaidia kumulika vitu vilivyo kwenye mtihani wa unyenyekevu.
- Katika kumbukumbu zako za kiroho, andika mabadiliko unayoyaona yakitokea katika maisha yako.

# MAOMBI

MAOMBI

SOMO LA 8,9

# Kongamano la Maombi

## KUOMBA KIBIBLIA

☞ **Kusudi la Somo**

Kutoa mwanya kwa wafunzwa wapanda kanisa kuungana pamoja katika kuomba kwa ajili ya utimilifu wa Utume Mkuu—siyo tu katika eneo lao, lakini "mpaka miisho ya dunia"

☞ **Wazo Kuu**

- Maombi yalikuwa kianzio cha kuenea kwa injili katika Matendo.
- Kibiblia maombi yanatakiwa yahusishe maombezi kwa ajili ya kazi ya Bwana ulimwenguni kote.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati anaposhika yaliyomo katika somo, kila mshiriki ...

- Atakuwa na ufahamu zaidi wa upeo wa injili.
- Awe ameshawishika zaidi kwamba maombi ni ufunguo wa kuona Mungu akifanya kazi kwa nguvu leo kama alivyofanya katika kitabu cha Matendo.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Tambua kuwa hiki ni kipindi cha awamu mbili kinachounganisha mafundisho na kuomba. Kila sehemu inatoa kanuni za kibiblia ambazo zinahusiana na maombi kwa upandaji kanisa. Mara baada ya kila kanuni kutambulishwa, mda unatakiwa uchukuliwe kuomba juu ya somo. Unaweza kutaka kubadilishana wakati wa kuomba kwa kundi lote na kugawanyika katika makundi madogo.

### UTANGULIZI

Kila mpanda kanisa anayetamani kufanikiwa lazima awe amejitoa kwenye maombi. Kiburi na kujitegemea pia kunawafanya viongozi wagawaji wa mkate badala ya kuelekeza mkate ulipo. Maombi ni chanzo cha yote nguvu na maelekezo kutoka kwa Mungu. Hakuna kitu cha kudumu cha kiroho chenye thamani kitakachokamilika bila maombi. Kwa jinsi hiyo, inawezekana kuomba mara kwa mara na kwa uaminifu, lakini siyo kuomba kwa vitu muhimu. Wakati ni kweli kwamba Mungu anataka tuombe kwa ajili ya mahitaji yetu, hilo peke yake halitoshi. Anatutarajia pia tuombe kwa ajili ya mahitaji ya wengine, na kwa utimizaji wa mpango wake kufikia mataifa yote—hii ni, Utume Mkuu.

### I. INJILI KWA WATU WOTE

Moyo wa Mungu unatamani wote wasikie habari njema ya injili. Yesu Kristo aliacha mbingu ili kutoa wokovu kwa damu yake iliyomwagika, na mitume walisafiri ulimwenguni kote kulikojulikana kwa nyakati zao kutangaza ukweli huo. Waumini wengi leo wameridhika kuangalia mahitaji yao wenyewe au mahitaji ya hao walio karibu nao na kudharau hitaji la ulimwengu. Katika baadhi ya njia, kanisa la kwanza lilihangaika na tatizo kama hili. Waumini wa kwanza walikuwa kabila la Wayahudi, na walikuwa na wakati mgumu kuamua kupeleka injili kwa mataifa mengine. Nini hatimaye kiliwashawishi? Katika neno, maombi. Kuna matukio manne magumu sana katika Matendo mahali maombi yalipotoa nguvu na mvuto kwenye ushuhuda, au yote.

#### A. Wafuasi 120 katika Matendo 1:12-14

Amri ya mwisho ya Yesu kabla ya ufufuko wake ilikuwa ni kwa mitume kusubiri Yerusalemu. Walitumia mda wao pamoja " *wakiomba bila kukoma*" kwenye chumba cha juu. Matokeo ya

maombi haya ya mkutano wa mda mrefu ilikuwa kuja kwa roho Mtakatifu, mahubiri yenye nguvu ya Paulo, na kukata shauri kwa watu 3000 kwa siku moja!

### B. Kanisa la Yerusalemu katika Matendo 4:23-31

Kanisa changa la Yerusalemu lilikutana na upinzani mkuu kutoka kwenye mamlaka ya kidini, waliowaamuru kuacha kueneza injili ya Yesu Kristo. Katika Mwitikio, waumini walikutana pamoja na kumwaga haja zao kwa Mungu. Matokeo yake ilikuwa ni kumwagika kwa nguvu ya Roho Mtakatifu na kusindikizwa na ujasiri wa kuendelea na ushuhuda wao bila kujali upinzani.

### C. Petro Darini katika Matendo 10:9-15

Katika hatua hii katika Matendo, injili ilikuwa haijapenya kupita kwa Wayahudi. Kwa mara nyingine, Mungu alitumia maombi—wakati huu maombi ya Petro peke yake—kuleta haja hata ya kuwafikia Mataifa. Petro hakuwa hata tayari *kuingia nyumba ya Mataifa au kula naye,* alipelekwa mwenyewe kumshuhudia. Lakini baada ya Mungu kukutana na Petro katika mda wake wa kuomba, hakuwa tu tayari kwenda kwenye nyumba ya Korneli na kufungua mlango wa imani kwa Mataifa, lakini hata alitetea haki za Mataifa kuokoka mbele ya Wayahudi wakatili walioamini (Mdo 11).

### D. Paulo and Barnaba Huko Antiokia Matendo 13:1-3


Jaribio bila mzaha la kwanza na kanisa kujaribu hasa kushughulika na Utume Mkuu na kuchukua injili kwa *Mtaifa yote* Inapatikana katika safari ya kimishenari ya mtume Paulo. Safari hizo zilikua kutokana na mkutano wa maombi ya kanisa la Antiokia. Katika tukio hili, Biblia hasa inasema kwamba walikuwa wanafunga. Somo la 5 la Maombi limeelezea kwamba kufunga kawaida kulikuwa kutokula chakula au vinywaji kwa kuonyesha kusudi la maombi *yasiyokatizwa na ushirika na Mungu.* Ilikuwa ni wakati wa kipindi hiki chenye mkazo wa ushirika na Bwana alipowaelekeza kumtenga Paulo na Barnabas kwa ajili ya kazi ya kimishenari. Kanisa mara moja lilikubaliana na *kuwatuma kwa maombi.*

## II. KUOMBA KWA AJIILI YA ULIMWENGU

Ilichukua kanisa la kwanza mda mrefu kuelewa wajibu wao kuyafikia maifa yote. Huu ni mfano mmoja wa kibiblia ambao hatuhitaji kuurudia. Wakati huo huo Yesu aliwaambia kusubiri Roho Mtakatifu, aliwaambia pia *wapi* na *nani* walitakiwa wamuhubirie injili. Ilikuwa kwenda kwa hao walio <u>Yerusalemu</u>, <u>Yudea</u>, <u>Samaria</u> na <u>miisho ya dunia</u>, (Mdo 1:4-8). Na hata hivyo tunafata historia ya kanisa kwenye kurasa kumi na tatu za Mtendo kabla hawajalichukulia hili bila mzaha. Jinsi gani inasikitisha!

Kusudi la kongamano la maombi yafuatayo ni kukazia siyo tu katika mahitaji yetu binafsi na ya hapo hapo lakini pia kupanua maombi yetu mpaka “miisho ya dunia.’ Hili lilikuwa ndilo kusudio la Bwana. Unapoangalia katika kielelezo hapo chini, fikiria juu ya eneo gani linaweza kuwa linakuwakilisha wewe, na jaza kwenye nafasi wazi kulingana. Rejea nyuma kwenye haya unapoendelea kwenye mda wa maombi.

**Kielelezo 8.1 Matendo 1:8 Kuomba**




## III. KONGAMANO LA MAOMBI – KUOMBEA ULIMWENGU WOTE

Kipengele kifuatacho kinatoa mambo ya kibiblia ya kimkakati ya maombi ambayo wawezeshaji na viongozi wanaweza kutumia kama msingi kwenye mkazo na kiongozi kiufanisi zaidi kwa vikundi vyao vya maombi na mtandao. Tumia utaratibu huu kama kiongozi kwenye kongamano la maombi ya siku hizi.

### A. Ombea Mahitaji Binafsi na Matatizo

Hata kama vikundi vyetu vya maombi vitaombea kueneza upandaji kanisa, wakati mwingine tunatakiwa kuachilia mizigo yetu ili kwanza tuweze kuweka akili zetu kwenye vitu ambavyo viko kwenye moyo wa Mungu kwa mataifa yetu, maeneo, miji, jiji, vijiji na ujirani. Wafilipi 4:6-7 inatuambia kuwa tunapokuwa tunaomba juu ya mashaka yetu amani ya Mungu italinda mioyo na akili yetu kwenye vitu vya Kristo.

**Gawanyika katika makundi ya wawili au watatu, kwa kifupi shirikisha mahitaji yako ya binafsi, na chukua mda katika kuombeana.**

### B. Ombea Kanisa la Mungu

Tunapoangalia hitaji la kanisa, tunaweza tukashawishika kuombea vitu vinavyotusumbua kibinafsi au kuomba kwa tabia ya upinzani. Hii siyo hekima kwa kuwa kanisa ni bibi arusi wa Kristo (Waefeso 5:22-32) na hakuna bwana arusi anayekubaliana na tabia isiyo sawa kwa bi arusi mpendwa. Mahitaji ya maombezi yafuatayo yanaweza kutusaidia kuongoza maombi yetu kwa kanisa.

**Tumia dakika chache mkiomba kwa pamoja kama kundi kwa kila moja ya maeneo haya:**

*1. Omba kwa Ajili ya Umoja*

Wakati Yesu alipowaombea waumini, aliomba kwa ajili ya umoja. Aliomba kwamba tuwe umoja kwa sababu ya upendo wetu kwake na kwa baba, na upendo wetu kwa mmoja kwa mwingine ambao unafanana na upendo kati ya Yesu na baba (Yn 17:20-23). Hili linachangia kwenye kueneza upandaji kanisa kwa sababu kwa kupitia muungano huu ulimwengu utajua kuhusu Yesu

2. *Omba kwa Ajili ya Upendo wa Kristo*

   Mtume Paulo aliomba kwa ajili ya kanisa la Filipi kuungana katika upendo, lakini siyo katika upendo kipofu. Aliomba kwa ajili ya upendo wenye akili na ufahamu wa ndani na busara (Flp 1:9). Hili linachangia kwenye kueneza upandaji kanisa kwa sababu tunapopendana watu wote watajua kwamba tunamfuata Yesu (Yn 13:35).

3. *Omba kwa Ajili ya Utii*

   Paulo aliomba kwamba kanisa la Efeso litaelewa wito wake, na tumaini kuu ambalo wito wa Mungu unalo (Efe 1:18). Hili linachangia kueneza upandaji wa kanisa kwa sababu kanisa linapoelewa wito wake, litazaliana na kuichukua injili ulimwenguni (Mt 28:18-20).

### C. Omba kwa ajili ya Watenda Kazi Wengi kwa Ajili ya Mavuno ya Mungu

Hii ni amri ya moja kwa moja kutoka Mathayo 9:38. Kama Yesu anatuamrisha kuombea kitu fulani, na tunakuwa waaminifu kuomba, atakuwa mwaminifu kujibu? Kunaweza kukawa kwamba kuna upungufu kiasi hicho cha watenda kazi kwa sababu kuna ukosefu wa maombi wa kitu hiki ambacho Bwana Yesu mwenyewe ameamru? Fikiri juu yake.

**Muulize Bwana kutuma watenda kazi zaidi kwenye mavuno yake yote hapa na ulimwenguni.**

### D. Omba kwa Ajili ya Wapanda Kanisa

Paulo alikuwa mtume mpanda kanisa. Akijua hitaji la wito wake, aliliomba kanisa la Efeso kumuombea kwamba aweze kuwa na maneno sahihi ya kusema na ujasiri wa kutangaza injili (Efe 6:19-20).

**Omba kwa majina kwa hao miongoni mwenu na wengine unaowajua wanapanda makanisa mapya.**

### E. Omba kwa Ajili ya Siasa, Jamii, na Viongozi wa Dini

1Timotheo 2:1-5 inatoa maelekezo wazi kwa wakristo kuomba kwa ajili ya viongozi wa kiserikali na hao walio katika madaraka. *Kusudi* la maombi haya ni kwamba kuwe na amani—inayopelekea *wokovu wa wengi*.

**Gawanyika katika makundi madogo na omba kwa ajili ya serikali yako na kwa viongozi wengine kwa majina, ukiuliza kwamba Mungu aweze kuwatumia kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuhubiri injili.**

### F. Omba kwa Ajili ya Taifa Lako na Mataifa ya Ulimwengu

Paulo alihubiri kwa mataifa, lakini ki wazi alieleza kwamba aliomba kwa Mungu kwa ajili ya taifa lake, la Israeli. Katika Warumi 10:1 aliandika, "ndugu zangu, haja ya moyo wangu na maombi kwa Mungu kwa Waisraeli kwamba waweze kuokoka." Katika mfano mwingine, ukifuatia maombi ya watatkatifu mbinguni, Mungu alibariki kuomba kwao kwa kuwanunua watu kutoka mataifa yote kwa ajili yake mwenyewe kwa damu ya Yesu Kristo (Uf 5:8-10). Tunapoombea taifa lote, tunachangia kuenea upandaji wa kanisa mbele ya kiti cha enzi cha Mungu.

**Funga kongamano hili la maombi kwa kuchukua mda uliobaki kuomba kama kikundi kwa ajili ya wokovu wa watu wenu wenyewe, na pia kwa ajili ya watu wa makundi mengine katika nchi yako na ulimwenguni kote. Mtaje kila mmoja maalumu na kwa majina kama Mungu anavyowaleta kwenye akili yako.**

# UONGOZI

UONGOZI

SOMO LA 6

# Uongozi wa Kitumishi

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kujadili umuhimu na muonekano halisi wa kiongozi mtumishi kama tabia kwa uongozi kwenye harakati za upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Uongozi ni "Nini" na kiongozi mtumishi ni kwa "jinsi gani"
- Uongozi wa kitumishi ni kielelezo cha kibiblia kwa viongozi wakristo.

☞ **Matokeo yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua tofauti kati ya uongozi wa kidunia na uongozi wa kitumishi.
- Kujitoa kuongoza kama mtumishi badala ya bosi.

☞ **Ziada**

6A Orodha ya Kiongozi Kuangalia

**UTANGULIZI**

Moja ya hitaji kuu zaidi la harakati za upandaji kanisa ni uongozi uliovutiwa kibiblia. Wakati njia za kidunia za uongozi zinapoletwa kanisani, au wakati watu wanapokalia maelekeo ya kiasili badala ya neno la Mungu, mazoea yanapelekea kwenye kuvutiwa madaraka, viongozi wanaokandamiza. Kama hatuvunji nira hii ya viongozi wasio wa kibiblia na kuachia rasilimali za mwili wa Kristo, kuna tumaini kidogo kwamba ulimwengu unaweza kuinjilishwa na kuletwa chini ya milki ya Kristo katika mda wetu wa kuishi.

Kristo alituacha na mfano wa jinsi ya kuongoza wengine, na kipeo chetu cha uongozi kinatakiwa kitoke kwenye mfano wake. Uchukuliaji wake wa uongozi ulihusisha kujitoa mwenyewe kwa wafuasi wake.

## I. UONGOZI WA KIDUNIA

> Ulimwengu unatazama uongozi kama jambo la madaraka.

Kuna mazoea ya kuutazama uongozi kama kitu cha madaraka. Wengine wanajisikia kuwa madaraka yanawapa haki ya kuongoza kwa kuamrisha wengine. Kwa kufikiria njia hii inaweza kuletea upotovu na uongozi wa kujitumikia. Tunaona mifano ya hili katika siasa, elimu, biashara n.k., ambako kunaweza kuunda mazoea kwetu ya kuongoza kama njia ya ulimwengu, kwa kuwa njia hizo zinaeleweka kwetu.

Uongozi wa kidunia unatokana na dhana fulani, kuhusu jinsi watu wanavyovutiwa kama vile:

- Huwezi kuwatumaini watu kufanya yale unayotaka wafanye.
- Kama unawatumaini wengine kupita, watachukulia manufaa kwako.
- Viongozi wanajitwalia madaraka kwa kuzingatia nafasi zao au kwa hadhi zao.
- Watu watafanya unachowataka kufanya wanapokuwa wamevutiwa na malipo, kutishika kwa adhabu.

- Viongozi wanatakiwa waepuke mawasiliano ya karibu na wafuasi wao, au wafuasi wao watawaona wao kama dhaifu.

Unakubaliana na mojawapo ya maelezo haya? Kwa nini na kwa nini siyo?

Dhana hiyo hapo juu ni ya kawaida kwa viongozi wengi. Wana weza wasiliseme kwa nje, lakini kwa undani, wanaweza kuifikiria kazi yao ya uongozi wao kutoka katika mtazamo wa uchoyo, na wa kiukandamiozaji. Sikiliza kwenye 'majigambo' ya viongozi wafuatao na jadili jinsi kila mmoja alivyo mchoyo:

- *Ninajua zidi kinachohitajika kufanyika. Baada ya yote, ni mwenye kufunzwa zaidi, mwenye uzoefu zidi, na ninayejua vema kazi yetu kuliko yeyote awaye. Wafuasi wangu wanatarajia hayo kutoka kwangu.*
- *Kama kiongozi siwezi kufanya kila kitu mwenyewe, kwa hiyo ninahitaji msaada kutoka kwa wafuasi wangu kufanya kazi, lakini sihitaji mawazo yao au mipango yao kuweka kinachohitajika kufanyika.*
- *Nadhani nahitaji kuwasikiliza wafuasi wangu. Siku hizi wanatarajia yote hayo kutoka kwangu. Lakini, sitarajii kusikia chochote kipya. Ninaujasiri hakika wa kuishia kufanya ninavyotaka.*
- *Ndiyo, Ni mimi ninayeshikilia mambo na kusimamia wayo wa mikutano yote. Baada ya yote, michango yote ni yangu na nimeshaipitia kila moja tayari.*

## II. UONGOZI WA KITUMISHI


Yesu alichukua mda wa kueleza wazi njia ya ulimwengu ya kuongoza (Mt 20:25-28). Alitangaza "*siyo hivyo kwako*" na kuweka wazi kwamba wanafunzi hawakutakiwa kuweka kamwe njia nzito, ya kibinafsi ya uongozi. Badala yake, hao wanaomfuata Yesu wanatakiwa kuwa "watumishi kwa wote."

### A. Utumishi na uongozi unaweza kuwepo

Muonjo wa kwanza wa maneno "kiongozi mtumishi" na "Uongozi" yanaonekana kwa namna fulani kugongana. Kwa upande mmoja, mtumishi ni mtu aliyeajiliwa na mwingine, anayefanya mapenzi ya mwajili. Usalama wa kazi yake unategemea hiyo, vilevile na heshima yake kama mtumishi aliyeajiliwa. Utumishi unamaanisha kuitikia shughuli, nafasi inayofaa, na roho ya kuachilia.

*Uongozi,* kwa upande mwingine, inamaanisha uanzislihi. Inahusisha mwelekeo, mguso na mvuto. Inahitaji---, mazingira ya ubunifu, mkazo, na kuwajenga wengine ili kwamba kwa pamoja wanaweza kuzalisha zaidi ya ambavyo kila mmoja angeweza peke yake. Uongozi ni *kujua wapi mtu anakwenda, na kuwa na uwezo wa kuwavutia wengien kuongozana.*

**Kielelezo 3.1 Kiongozi mtumishi**



Kwa hiyo jinsi gani wawili wanaweza kufaa pamoja? Wakati uongozi unaeleza 'kwa nini' ya kazi yetu, utumishi kimsingi unazungumzia 'jinsi' ya kazi yetu (mahitaji ya wengine). Tunaongoza kama watumishi. Kuwa "kiongozi" katika mtazamo wa kidunia hakuhitaji moyo wa utumishi. Kwa jinsi hiyo, katika kazi ya kuzalisha harakati za upandaji kanisa, ni kitu cha lazima.

### B. Kanuni za kikristo kuhusu mvuto na uongozi

- Watu wameumbwa kwa mfano wa mungu na kwa hiyo kuwa na thamani halisi (Ge 1:27-28).
- Watu wanavutiwa kutenda kwa ubora kwa kutambua kuwa kila kitu kitafanyika kwa utukufu wa Mungu (Col 3:23).
- Watu hawatakua na kuendelea mpaka waaminiwe na kupewa uhuru wa yote kufanikiwa na kushindwa.
- Kiongozi anateuliwa na Mungu na kuchukua madaraka kutoka kwake (Rom 13:1).
- Viongozi wenye mafanikio wanawaona wenzao kama marafiki, na siyo kama wa chini, na kuzungumza nao kwa roho ya uwazi na unyenyekevu (Yn 15:15).

## III. MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA JUU YA KIONGOZI MTUMISHI

Yesu na mitume siyo tu walifundisha juu ya uongozi wa kitumishi, lakini pia waliuonyesha kwa maisha yao. Mfano wao unatakiwa uendelee kututia changamoto tunapokuwa tunahudumu leo.

### A. Mfano na Mafundisho ya Yesu

Uongozi wa Yesu hautakiwi kuwa wa kujitumikia (Mt 20:25-28; Yn 13:1-16). Yesu aliweka pembeni heshima yake ili kutumika—ya kuelezeka zaidi kwenye chumba cha juu alipoosha miguu ya wanafunzi. Hatimaye, huduma yake ya kipekee ilimpelekea kufa kwa kimwili kwa hao waliokuwa chini ya uangalizi wake (Plp 2:1-11). Alichukua mfumo wa mtumishi ili kuchukua mzigo wa dhambi. Aliwakaribisha waliopotea kuja kwake na kupata pumziko kutoka kwenye mizigo yao, *"Njono kwangu ninyi nyote mnaolemewa na mizigo, nami nitawapimzisha*. *Jitieni nira yangu na mjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa kuwa nira yangu ni laini na mzigo kwangu ni mwepesi" (Mt 11:28-30).*

Kama kiongozi mkuu Yesu aliwasha harakati za ajabu za mda wote, harakati zake za kanisa ulimwenguni kote. Hata hivyo bado Yesu alikuwa mtumishi. Jinsi gani hiyo ilihusika katika hatua hii Yesu kama mtumishi alianzisha harakati tunazojadili leo.

Yesu anawaita wanafunzi wake "rafiki" na yeye mwenyewe "mtumishi" (Yn 15:15). Wanafunzi hawakuhitaji hili kutoka kwake. Wajibu wa wanafunzi ilikuwa ni heshima ya ndani na utii. Katika mahusiano ya kawaida, majukumu haya mara nyingi yanatunzwa. Kiongozi anataka heshima na utii kadiri wafuasi wanapomtafuta rafiki na mtumishi.

Yesu pia aliwafundisha wanafunzi wake umuhimu wa kuwa kiongozi mtumishi. Katika Mathayo 20:25-28, aliwaonya kutofata mfumo wa kiulimwengu wa uongozi. Badala yake, aliwapa changamoto kufata mfano wake kwa kutoa maisha yao kutafuta na kuokoa waliopotea.

### B. Mfano na Mafundisho ya Paulo

Pengine mfano bora wa moyo wa Paulo wa utumishi unaonekana katika barua yake ya pili kwa Wathesalonike. Angalia kwa karibu jinsi alivyoelezea huduma miongoni mwao.

> *"Hatukutafuta utukufu kwa wanadamu, wala kwenu, wala kwa wengine tulipokuwa tukiweza kuwalemea kama mitume wa Kristo. Bali tulikuwa wapole katikati yenu, kama vile mlezi awatunzavyo watoto wake mwenyewe. Vivyo hivyo nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tulio na furaha kuwapa, si injili ya Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu. Maana, ndugu, mnakumbuka taabu zetu na masumbufu yetu; kwa kuwa mchana na usiku tulifanya kazi tusije tukamlemea mtu wa kwenu awaye yote, tukawahubiri hivi injili ya Mungu"* (1The 2:6-9).

Wazi Paulo alijisikia kwamba nafasi yake kama mtume ilimfanya kuwatumikia wengine na kubeba mizigo yao, badala ya kutumikiwa. Alitufundisha kufanya sawa:

- *“Sisi tulio na nguvu tunapaswa <u>kuchukua udhaifu wa wasio na nguvu</u> wala haitupasi kujipendeza wenyewe (Rum 15:1).*
- *“Ndugu, twawasihi, waonyeni wale wasiokaa kwa utaratibu, <u>watieni moyo walio dhaifu</u>, watieni nguvu wanyonge vumileni na watu wote”* (1Th 5:14).
- *“Ndugu zangu, mtu akighafilika katika kosa lolote, ninyi mlio wa roho mrejezeni upya kwa roho ya upole, ukijiangalia nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe. <u>Mchukuliane mizigo</u> na kuitimiza hiyo sheria ya Kristo”* (Gal 6:1,2).

### C. Mfano na Mafundisho ya Petro

Katika walaka wake wa kwanza, Petro anaweka wazi kwamba viongozi kanisani wanatarajiwa kuwa viongozi watumishi (1Pet 5:1-4). Petro anasihi kama aliyeona mateso ya Yesu mara ya kwanza na hata anataja mafundisho ya Yesu juu ya uongozi (Mt 20:25-28) kwa kuwaelekeza wazee hawa ‘wasiwarundikie’ hao waliowaamini.

Maisha ya Petro yanahakikisha kuwa aliamini kile alichofundisha. Aliteseka sana katika kumtumikia Bwana. Mapokeo yanasema kwamba Petro alisulubiwa juu-chini kwa *upendeleo wake,* Kwa sababu hakujisikia kama alikuwa anafaa kusurubiwa kwenye nafasi moja kama ya Kristo.

## IV. MATUMIZI

Uongozi wa kitumishi ni njia ya kibiblia kwenye uongozi. Kwa maneno rahisi, uongozi wa kitumishi una maana kwamba kiongozi anaweka wafuasi wake vyema mbele yake mwenyewe. Viongozi wa kikristo ni watumishi wa kwanza na wa mbele. Vitisho, ukubwa, na nguvu hazitakiwi kamwe kuwa tabia ya kiongozi mkristo (Mt 20:25-28, 1Pet 5:1-7). Kiongozi mkristo siyo “mtawala” kwa namna ya mabavu (neno mtawala” (mzizi wa Kiyunani ‘hila’’) halikutumiwa kamwe katika Agano Jipya kueleza uhusiano kati ya wakristo]. Badala yake ni mtumishi.

> Uongozi wa kitumishi una maana kwamba kiongozi anaweka wafuasi wake vyema mbele yake mwenyewe.

**Sifa na Tabia za Kiongozi Mtumishi**

- Kiongozi mtumishi anatunza na kujenga umoja (Efe 4:3). Anaepuka mabishano yasiyo ya lazima juu ya umilikaji wa mali au ngome.
- Viongozi watumishi hawatishwi na uwezo na makamilisho ya wengine. Badala yake, wanatambua thamani ya uwezo huu na kuutumia kufaulu malengo ya kikundi.
- Kiongozi mtumishi ni “mjenzi” wa wengine. Kiongozi mtumishi anafanya kazi kuwatia moyo na kuwainua wengine kwa kila njia inayowezekana. Wanashangilia mafanikio ya wengine, bila kujali ni madogo kiasi gani.
- Viongozi watumishi ni wa mstari wa mbele kusogeza maswala mbele, wakati wakitunza upole na kuwafikiria wengine.
- Kiongozi mtumishi anawazungumza wengine vizuri kila wakati.
- Kiongozi mtumishi anatafuta kujenga msingi mpana wa viongozi kuongoza pamoja naye.
- Viongozi watumishi wanatambua na kutumia mamlaka inavyopaswa (kinafasi, kimahusiano, kiuzoefu, kibinafsi, kiroho).
- Kiongozi mtumishi hajipatii umaarufu, kufaa, sifa kutokana na nafasi anayoshikilia.
- Kiongozi mtumishi hafanyi maamzi kutokana na maendeleo yake, kusonga mbele, faraja. Kuzidi kwa mamlaka au nafasi kwa gharama ya hao anaotumikia.
- Kujitoa kwa kiongozi mtumishi kwa wafuasi wake kunasonga mbele, huduma yao, na kuongezeka kwao ni ufunguo wa kuonyesha upendo wake.
- Kiongozi mtumishi anawaendeleza viongozi wenzake, ili kutoa msingi imara wa uongozi kwa makanisa mapya yanayozaa.

### SULUHU

Tabia ya kiongozi mtumishi ni kwamba kazi yake ni kuongoza wengine kufanya anachotaka Mungu kutoka kwao. Kazi yake siyo 'kulundikia' wengine, au kuwafanyisha anachodhani kuwa ni bora. Badala yake, anatakiwa kuwajenga wengine katika maeneo yote ya maisha na huduma. Mafanikio ya kiongozi mtumishi yanapimwa kwa yale aliyokamilisha katika maisha ya wale anaowaongoza.

> Kiongozi mtumishi lazima kuwajenga wengine katika maeneo yote ya maisha na huduma.

Kiongozi mtumishi anatambua mbele ya Mungu, yuko kwenye ngazi moja na wale anaowaongoza. Mamlaka yake kuongoza siyo yake hasa lakini yanatoka kwa Mungu, kwa hiyo hayuko huru kutumia mamlaka hayo katika njia yoyote anayotaka. Lazima atumie mamlaka haya katika njia sawa na Yesu alivyofanya, kama mtumishi kwa hao aliokuwa anawaongoza.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini ni vigumu kwa kiongozi kuwa kiongozi mtumishi?
- Nini baadhi ya mizigo ambayo mpanda kanisa anatakiwa awe tayari kuibeba kwa ajili ya wengine?
- Elezea namna gani mpanda kanisa atakavyokuwa aliyekuwa kiongozi mtumishi.
- Nini mabadiliko katika maisha yako mweyewe na huduma unayohitaji kufanya kuwa kiongozi mtumishi bora?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Kamilisha Ziada 6A, "Orodha ya Kiongozi." Tathimini mtindo wa uongozi wako kulingana na matokeo ya orodha hii. Kama kiongozi, onyesha maeneo katika maisha yako na huduma ambayo yanahitaji kubadilika.

### VYANZO

Engel, James F., Jane Overstreet, and Terry Sparks. *Leadership: Making Human Strength Productive*. St. Davids, PA: The Center For Organizational Excellence, Eastern College, 1996.

**UONGOZI**
***ZIADA***
**6A**

# Orodha ya Kiongozi

Tumia mzani hapo chini kutathimini sifa zako kama kiongozi mpanda kanisa. Zungushia namba moja (kutoka 1 – 5) ambayo inaonyesha zaidi jinsi kila maelezo yanavyokuelezea. Inaweza pia ikasaidia kumruhusu mmoja unayemjua na kumwamini kutathimini ukweli wako, kama mwenzi wako au rafiki wa kiroho. Kisha linganisha matokeo kuona mahali panapokubaliana na pasipokubaliana. Kutokana na hili unaweza kuhitaji kufanya baadhi ya mabadiliko katika mtindo wako wa huduma ili kuwa mfanisi zaidi kwenye upandaji kanisa.

**Zungushia namba moja kwa kila swali**

| | | **Chini** | | | | **Bora** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Niko tayari wakati wote kwa vyovyote kwa ajili ya Mungu. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 2. | Nina uwezo wa kuwakilisha maono niliyopewa na Mungu kwa wengine. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 3. | Nimejitoa kwenye uinjilisti, upandaji kanisa na kuanzisha vikundi kiini. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 4. | Ninapenda kuchukua hatua | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 5. | Niko tayari na ninaweza kushughulikia migongano kati ya watu. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6. | Ninaweza kuunda umiliki wa huduma kwa wengine. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 7. | Ninaweza kutumia vipawa vya kiroho na uwezo wa wengine. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 8. | Ninatembea na Kristo. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 9. | Ni kiongozi mtumishi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 10. | Nina ushirikiano kamili na msaada kwa familia yangu. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 11. | Ninahusiana vema na wasio wa kanisa na ambao hawajakata shauri. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 12. | Ninakabili changamoto kama "nafasi" badala ya "matatizo." | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 13. | Ninaendana na malengo niliyoweka na wengine. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 14. | Sikai kimya ninapokutana na nyakati ngumu. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 15. | Nina "wito kutoka kwa Mungu" kufanya upandaji wa kanisa. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 16. | Ninajua jinsi ya kuwagawia watu. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 17. | Ninawafundisha wengine kutumia vipawa vyao kwa ufanisi zaidi. | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

UONGOZI

SOMO LA 7

# Nguvu ya Uongozi

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea jinsi kiongozi, kundi na kazi vinavyohusiana, na jinsi kwa pamoja vinavyogusa utaratibu wa upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Kiongozi, kundi, na kazi vyote vinagusa utaratibu wa uongozi.
- Mitindo ya uongozi inayotofautiana inafaa katika hali tofauti, lakini uongozi wa kundi wa upandaji kanisa unatakiwa kuzingatia kikundi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa...

- Kujua mtindo wake wa kawaida wa uongozi.
- Kuujitoa kuanzisha 'vikundi' zaidi katika uongozi wake.

## UTANGULIZI

Ni kwa nini baadhi ya viongozi wanashindwa na wengine wanafaulu? Kwa nini baadhi ya viongozi wanazidi katika baadhi ya hali na kushindwa katika nyingine? Katika njia sawa, inawezekana kabisa kuelezea aina ya kiongozi wa kijamii atakayekuwa mfanisi katika hali zote na katika tamaduni zote? Tunaweza kufanya maelezo ya ujasiri kama vile "kiongozi kawaida lazima…?" Wengi wamejaribu kufanya kama hivyo, na kushindwa. Kujifunza uongozi kunakoangalia tu kwenye ujuzi na sifa za kiongozi kunaacha sehemu muhimu ya kulinganisha.

Jibu la swali hapo juu lina utata kwa sababu vigezo kadhaa vinagusa ufanisi wa viongozi, ambapo ujuzi wa kiongozi ni sehemu moja tu. Badala yake, Uongozi unahusu mwingiliano wa vigezo vitatu, kama yalivyoonyeshwa katika kielelezo 7.1:

- Tabia za kiongozi.
- Tabia za kundi.
- Asili ya kazi.

Ili kwa kiongozi kuliongoza kundi lake kukamilisha kazi yake kwa ufanisi, vigezo hivi vitatu lazima viende pamoja. Kiongozi lazima aweze kuongoza kundi na kuelewa jinsi ya kuendea kazi. Kundi lazima liwe linaweza kukamilisha kazi na kuwa tayari kumfata kiongozi. Ili kuhakikisha kwamba kundi lililojitoa kwenye upandaji kanisa limeandaliwa kifikira kwa kazi hiyo, ni lazima kutathimini 'tabia' ya asili zote hizi tatu.

Ili kwa kiongozi kuliongoza kundi lake kukamilisha kazi yake kwa ufanisi, vigezo hivi vitatu lazima viende pamoja.


## I. TABIA ZA KIONGOZI

Kiongozi, wakati siyo kigezo peke yake, ni geuzi muhimu zaidi katika utaratibu wa uongozi. Machache yanaweza kutokea bila uongozi, na kiongozi sahihi anaweza kufanya mabadiliko yote ulimwenguni. Wakati mwingine kundi halina kiongozi wazi. Hili ni tatizo la kawaida la huduma—hakuna anayeibuka kuchukua uongozi. Kama, kwa hiyo, kundi linakamilisha kazi, mjumbe mmoja au zaid wa kundini pengine anashikilia nafasi ya kiongozi—hata kama hili halitambuliki. Ukweli,

Kuna hali ambazo watu kadhaa wataelekeza kazi kwa mapatano, kwa makusudi kuamua kutokuwa na kiongozi. Wakati hili linafanya kazi mara chache, ni vigumu kusonga mbele kwenye kazi yoyote bila mtu mmoja kuunganisha na kuhakikisha kuwa uamzi wa vikundi unafatwa. Hii ni sababu ya msingi kwamba halmashauri ina sifa mbaya ya kutofanya vya kutosha.

Somo hili linajitwalia kwamba kundi lako la upandaji kanisa lina kiongozi—hata kama tofauti katika madaraka kati ya kiongozi na wajumbe wengine ni kidogo. Pia inadhaniwa kwamba pengine wewe ni kiongozi, na kwamba unatamani kufanya kazi nzuri ya kuongoza. Ni vigezo gani muhimu kwenye uhusiano kati ya kiongozi, kikundi na kazi?

**Kielelezo 7.1 Vigezo Vitatu vya Mafanikio ya Uongozi**




**A. Utu wa Kiongozi**

Tabia ya kiongozi imeshashughulikiwa kwenye somo la nyuma, kwa hiyo tutaligusia tu hapa. Hii haina maana kwamba siyo muhimu. Kinyume chake, tunapokuwa tunashughulika na kazi ya kiroho ya upandaji kanisa, moyo wa kiongozi pengine ni kigezo pekee muhimu zaidi kwenye mafanikio ya kikundi. Ndiyo maana ni muhimu hiyo kwa Bwana, na kwa nini inatakiwa iwe kipaombele cha juu kwetu (1Sam 16:7).

Kufuatana na yaliyokwisha kujadiliwa kwenye somo la nyuma la uongozi kwenye Mwongozo wa Pili, fikiria yafuatayo:

- Kwa mapana gani unafaa kwenye 'sura' ya kiongozi kwenye mandhali ya upandaji kanisa kama yalivyojadiliwa kwenye somo la uongozi la 2, "sura ya kiongozi"?
- Ni wazi kwamba hakuna anayefaa sura kikamilifu. Jinsi gani kama kiongozi unavyoshughulika na maeneo ambayo hujajaliwa?
- Unafata kanuni za kibiblia za uongozi kama zilivyodokezwa kwenye somo la 1 La uongozi, "Kanuni za Kibiblia za Uongozi"?

**B. Jinsi Kiongozi Anavyojihusisha kwenye Kikundi**

Mtindo wa uongozi unatofautiana kutoka kiongozi hadi kiongozi. Kielelezo 7.2 kinafafanua mitindo mitano ya uongozi ambayo ni ya kawaida. Mtindo wa kiongozi unaweza kuelekea kutoka "mkao wa kuongoza mpaka "mkao wa kikundi" kutegemeana na kiasi gani kiongozi anachangia yanalinda kikundi.

Inaweza kutolewa hoja kwamba kuna mda na nafasi ya kila moja ya mitindo hii mitano ya uongozi. Kwa jinsi hiyo, 'mkao wa kuongoza mwisho wa mzani kawaida utaweza kufaa tu wakati kundi linapokosa ukomavu au kuelewa kufanya maamzi mazuri, au pengine kwenye hali ya misukosuko.


> Kuna mda na nafasi ya kila moja ya mitindo hii mitano ya uongozi.

Kwa kusudi la upandaji kanisa, kunatakiwa kuwe na kiwango cha ajabu cha ukomavu wa kiroho kwenye sehemu hiyo ya wote wanaohudumu na kuelekeza kazi. Kwa hiyo, kiongozi wa kundi la upandaji kanisa anatakiwa kutarajia kutumia zaidi mtindo wa "kukazia kundi" wa uongozi. Tatizo linatokea wakati kiongozi wa jengo la kanisa akiwa ameridhika tu kwa "mkao wa kiongozi". Kwenye hali hiyo, kiongozi ana chaguzi nne. Anaweza:

- Kujifunza kubadili mtindo
- Kuachilia nafasi ya uongozi
- Kufanya kazi peke yake
- Kulichanganya kundi lote na kurudisha nyuma upandaji wa kanisa

Unapoangalia kielelezo 7.2 na kusoma majadiliano ya kila mtindo wa uongozi, tathimini mtindo wako unaopendelea. Tunasema "unapendelewa" kwa sababu ingawa viongozi wanaweza kutumia mitindo tofauti, wanakuwa na uhuru zaidi katika mmoja wake.

**Kielelezo 7.2 Mitindo Mitano ya kawaida ya Uongozi**




1. *Kuambia*

   Viongozi wanaainisha matatizo, wanafikiria uwezekano, wanachagua suluhu moja, na kuwaawambia wafuasi wao nini cha kufanya. Viongozi wanaweza kufikilia maoni ya wajumbe, lakini wajumbe hawashiriki moja kwa moja kwenye kufanya maamuzi.

2. *Kushawishi*

   Viongozi wanafanya maamzi na kujaribu kushawishi wajumbe wa kikundi kuyakubali. Kiongozi anayetumia mtindo huu anaweza kusema kwamba wamefikiria malengo ya chama na mapendeleo ya wajumbe wa kikundi. Hata wanasema jinsi wajumbe watakavyofaidika kwa kuyachukua maamzi.

3. *Kushaulisha*

   Wajumbe wa kikundi wana nafasi ya kugusa ufanyaji wa maamzi tokea mwanzoni. Viongozi wanaotumia mtindo huu wanatoa matatizo na habari za nyuma zinazoendana. Wanakaribisha kundi kutoa mawazo ya uwezekano wa kufanya. Kisha viongozi wanachagua utatuzi unaotumainisha zaidi.

4. *Kushiriki*

   Viongozi wanashiriki kwenye maamzi kwa kiwango sawa kama wajumbe wengine, na kukubaliana kabla ya kufanya uamzi wowote kundi linaofanya.

5. *Kugawa*

   Viongozi wanatafsiri mipaka watakayotatulia matatizo au kukamilisha kazi. Kisha wanaigeuzia kwenye kikundi kufanyia ufumbuzi au kuweka kazi.

> Kiongozi wa kupanda kanisa kawaida anatakiwa awashirikishe hao anaofanya nao kazi.

Kumbuka kwamba hakuna moja ya mitindo hii mitano imerithiwa kihaki au kimakosa. Jeshi, kwa mfano, limekuwa na mafanikio makuu katika *kuwaambia* wanajeshi cha kufanya, bila kuruhusu majadiliano. Hata katika hali ya upandaji kanisa, kunaweza kukawa na baadhi ya mda ambapo ni bora na rahisi kama kiongozi anafanya maamzi fulani bila kushirikisha kikundi. Kawaida hili linatokea kunapokuwa na dharura ya kufanya maamzi *wakati huo*! Kwa jinsi hiyo, Katika yote lakini hali iliyopindukia, kiongozi wa kupanda kanisa  anatakiwa awashirikishe hao anaofanya nao kazi. Kiongozi mzuri anahitaji kujua lini kila mtindo unaweza kufaa, na kuwa anakua katika uwezo wake  wa kutumia mitindo mingine kuliko yake ya kawaida inapokuwa lazima.

### C. Kuielewa Kazi   kwa Kiongozi

Inatakiwa iwe kawaida kwamba kiongozi lazima aelewe kazi inayotakiwa kukamilishwa na kujua jinsi ya kuifanya. Kwa jinsi hiyo, viongozi mara nyingi wanateuliwa kipekee kuzingatia hadhi au uwezo wa nyuma wa kuongoza, hata kama hawaelewi kazi iliyopo. Wengine wanaweza kuwa na uwezo vya kutosha kujifunza haraka na kufanikiwa, lakini wengi wanashindwa katika hali hii. Inatakiwa kwa hali na mali kwamba kiongozi anatakiwa awe na kuelewa kazi.

Upandaji kanisa ni kazi muhimu sana kuikabidhi kwa viongozi ambao hawaifahamu, au ambao hawako tayari kujifunza juu yake. Kwa hakika, kiongozi ambaye siyo wa kujifunza mara chache sana ataelekeza kundi kwenye ufanisi wa ukamilishaji kazi yake. Kwa hiyo, kiongozi wa upandaji kanisa *lazima* aelewe utaratibu wa upandaji kianisa, na kukua katika ufahamu wake. Nafasi ya kiongozi ni nyeti. Kama kiongozi ana mapendekezo au mawazo ya kimakosa, kupanda kanisa pengine kutashindwa.

> Siyo lazima kwamba kiongozi anajua kila kitu kuhusu upandaji kanisa.

Siyo lazima kwamba kiongozi anajua *kila kitu* kuhusu upandaji kanisa. Kama ni hivyo, hakuna kanisa ambalo kamwe lingepandwa—kwa ukosefu wa viongozi. Kwa njia sawa, hata siyo lazima kwamba kiongozi anajua zaidi kuliko mjumbe awaye yote wa kikundi. Pengine mjumbe mwingine ni ‘mupanda kanisa mjuzi’, lakini siyo hasa kiongozi mwenye uwezo. Suluhu bora kwenye hali hiyo ni kwa viongozi zaidi waliojaliwa kutwaa madaraka ya uongozi wa kikundi, lakini kuhakikisha kwamba anarithi mtindo wa ‘mkao wa kundi’ ili kwamba kundi lifaidike kutoka kwenye uzoefu wa mjumbe mwenye kujua.

## II. TABIA ZA KIKUNDI

Kusema ‘kikundi’ tuna maanisha yeyote anayeongozwa na kiongozi.’ Kiongozi anaweza asiwe kwenye kudhibiti kigezo hiki. Unaweza kufanya kazi na watu ambao hukuchagua, lakini Mungu amewaongoza pamoja. Kama wewe mwenyewe unachagua wajumbe wa kundi au la, unaweza ukaimarisha uongozi wako na mafanikio ya kikundi kwa kufahamu asili ya kundi.

> Kama kuna upungufu kwenye eneo moja au zaidi, utahitaji kutafuta njia ya kuanzisha ustadi wa kazi hizo.

Kundi la upandaji kanisa lazima liongoze maisha ya kimungu, na kuweza kufanya kazi za msingi kama uinjilisti, kufuasa, na kujenga mahusiano. Kama wajumbe wana uwezo kwenye maeneo haya, kazi yako kama kiongozi kwa kifupi itakuwa kuwafanya kukazia kwenye lengo la upandaji kanisa. Kama kuna upungufu kwenye eneo moja au zaidi, utahitaji kutafuta njia ya kuanzisha ustadi wa kazi hizo. Kwa hiyo, tathimini ya uangalifu ya kikundi itakuwa ya kufaa, na kuzidisha nafasi zao za kuanzisha kanisa imara linalokua. Kuna maeneo kadhaa ya kufikiria,

### A. Ujuzi na Uwezo wa Wajumbe wa Kikundi

Angalia kundi unalofanya nalo kazi na fikiria maswali yafuatayo:

- Ni uzoefu kiasi gani wajumbe wa kundi wanao kwenye uinjilisti, ufuasishaji n.k.? Unahitaji kukazania kwenye kufunza?

- Ni kwa njia zipi baadhi yao wako tayari kutolewa kwenye huduma?
- Wajumbe wako wanafahamu vipawa vyao vya kiroho?

Majibu kwa maswali haya yatagusa kuendelea kwa kikundi. Huwezi kuliongoza kundi mahali ambapo hawajatayarishwa kwenda. Kama kundi lako linakosa ujuzi wa huduma, utahitaji kuwafunza.

### B. Kujitoa kwa Wajumbe kwenye Kazi

Pengine una kundi la watu wenye ujuzi wa kufanya nao kazi. Wengine wanaweza kuwa wamepanda makanisa kabla, wengine ni wainjilisti wenye uzoefu au viongozi wa kikundi kiini. Lakini pengine wajumbe wako wa kikundi hawapo kushiriki katika kazi kwa sababu ya majukumu.

- Je ratiba ya ajira inagongana na mikutano na shughuli za huduma?
- Je wajibu wa familia unaingilia mkazo wa wajumbe wa kundi?
- Je wajumbe wanadhani kwamba kupanda kanisa ni kazi nyeti?

Pengine wajumbe wa kanisa wamejitoa kwenye kupanda kanisa, lakini wana mawazo tofauti juu ya aina ya kanisa wanaloanzisha. Wanaweza kutarajia aina tofauti ya mitindio ya huduma, au kuwa na maono yanayogongana ya muundo wa kanisa. Kama kundi lako halikufanyia kazi mpango wazi na mkakati, aina ya tatizo hili pengine litainuka. Utakuwa na ugumu mkubwa katika kusogeza kundi mbele mpaka wote mtakapokubaliana juu ya nini mnakoelekea.

### C. Uhusiano Kati ya Wajumbe

Uongozi zaidi ni biashara ya "watu". Sehemu kubwa ya huduma inashughulika na wengine. Kama kuna matatizo ya mahusiano miongoni mwa hao unaofanya nao kazi, itaingiliana na kazi mara moja au badaye. Viongozi wanatakiwa kuendelea kushauri uhusiano miongoni mwa wajumbe wa kundi kwa kuendelea. Kama kundi haliaminiani, kuendelea kunaweza kuzuiliwa. Kama wajumbe wanashindania kusifiwa au nafasi, ushirikiano wa kweli hautawezekana. Mchanganyiko wa vivutio na michango iliyojificha bila kujua inaweza ikaingiliana na lengo.

> Matatizo mara kwa mara yanatokea wakati mtindo wa uongozi unapogongana na matarajio.

Inawezekana pia kwamba mjumbe mmoja au zaidi anaweza kuwa na matatizo ya uhusiano na kiongozi. Hili mara kwa mara linatokea wakati mtindo wa uongozi unapogongana na matarajio. Kiongozi angeweza kutumia mtindo huo wa kuelekeza kwa kundi ambalo linathamini uhuru, na hivyo kuwafanya wajumbe kujisikia kufanywa wadogo. Au, kwenye swala la kinyume, kiongozi anaweza kutofautiana maamzi na kundi, ambapo badala yangeweza kuwa na mwelekezo imara kutoka kwa kiongozi, na kwa hiyo kujisikia kuchanganyikiwa au kusumbuka kujua nini la kufanya. Maswala yote yanatakiwa yakabiliwe na kufikia makubaliano ya kutendeka.

Jinsi gani utashughulika na migogoro kati ya watu kama kiongozi wa wengine? Kiongozi mwenye uzoefu anatoa ushauri ufuatao:

> *Ninapoona hangaiko miongoni mwa ninaowaongoza, au mmoja anapoonyesha moyo wa "ufarakani" kwenye mtazamo fulani, ninajaribu kujiuliza, "nini kinaendelea hapa?" Mda mwingi kunakuwa na kuumia, hofu au maswala kati ya watu chini ya upande unaotokeza isivyo kawaida. Pengine nimemkaza mtu huyu, au pengine anajisikia kutokuthaminiwa na kikundi. Kwa kutumia mda kidogo wa ziada na mtu anayeonekana "kusumbuliwa", pengine kuwapa nafasi ya kuwa wazi, mara nyingi ninaweza kuwahakikishia kustahili kwao na kukubalika kwao na mimi na kikundi. Mara kwa mara hii ndiyo tu muhimu kukuza ukaribu kati yetu.*

## III. ASILI YA KAZI

Kigezo cha tatu kwenye uongozi ni kazi. Kazi ndilo kusudi la kuwepo kwa kundi. Ni muhimu kwamba kazi inaweza kuwa wazi kwenye akili ya kila mjumbe. Majukumu ya kutunza lengo hili yanaangukia kimraba mabegani mwa kiongozi.

> Ni wajibu wa kiongozi kuifanya kazi kuwa wazi.

Kuna kupindukia kwa aina mbili

1) Kushindwa kuweka kazi waziwazi mbele ya kikundi, na

2) Msisitizo zaidi wa kazi kwenye madhara ya uhusiano wa kundi.

Kupindukia kwa kwanza kunasababisha kutapatapa kufanya shughuli zisizo na umuhimu, au kuzingwa na kuangalia kundi kiasi kwamba wanasahau waliopotea ambao Bwana amewaletea. Kupindukia kwa pili kunatokana na uhusiano uliojeruhiwa na kutoweza kueleleza jumuia ya kikristo.

**Kazi yako ni kueneza upandaji kanisa.** Kama kiongozi, unahitaji kuendelea kutathimini endapo kama kundi lako linasonga mbele katika upandaji kanisa. Utafiti wako unakusaidia kuelewa hali yako maalumu na kukazia juhudi zako kwenye maeneo muhimu. Kwa nyongeza ya kile ulichojifunza kwenye utafiti, unahitaji kufikiri jinsi maswala yafuatayo yanaathiri ugumu wa upandaji kanisa kwenye eneo lako unalolenga, na kurekebisha matarajio yako kufuatana.

> Kama kiongozi, unahitaji kuendelea kutathimini endapo kundi lako linasonga mbele katika upandaji kanisa.

- Unapanda kanisa miongoni mwa watu wanaopinga au wanaopokea?
- Wewe au wajumbe wa kundi lako ni "wa kuja" au "wageni" miongoni mwa watu hawa?
- Kuna hali halisi za kiuchumi zinazofanya juhudi za upandaji kanisa kuwa mgumu?
- Una habari za kutosha kuhusu mandhali yako? Wewe na kundi lako mnaelewa kazi yenu?
- Una mpango wazi na mkakati ambao unapeleka utafiti wako kwenye wajibu?
- Kuna nguvu za kiroho zisizo za kawaida ambazo lazima zikabiliwe?
- Kuna msukumo wowote wa kisiasa ambao unaathiri hali?
- Una rasilimali zinazohitajika kukamilisha kazi?
- Ni kwa njia zipi Mungu amekutayarisha wewe na kundi lako kwa kazi hii?
- Kuna 'milango wazi' yoyote ambayo inahakikisha ufanisi katika kazi, na upi unahitaji kutumia kiukamilifu?
- Watu ambao kundi lako limeshafikia wanakua na kufuaswa kwa Bwana? Ni masahihisho gani unahitaji kufanya kwenye mkakati wako ili kuwasaidia vyema?

## SULUHU

Kama unavyoweza kuona kuna vigezo vingi vinavyoathiri utaratibu wa uongozi. Kama mpanda kanisa unahitaji kuangalia uwezo wa uongozi na ujuzi, Linda na funza kundi lako na mulika hali halisi kadhaa kwenye kazi. Utekelezaji wa mpango mwishoni mwa somo hili utakusaidia kuchukua shina la vigezo vyako.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni vigezo gani vitatu vikuu vinavyoathiri mafanikio ya uongozi?
- Ni mtindo upi halisi zaidi wa uongozi wa serikali katika nchi yako?
- Ni mtindo upi halisi zaidi wa uongozi kwenye makanisa yako?
- Ni mtindo upi wa uongozi ulitumiwa na viongozi hao wakristo ambao wamekuwa na mguso zaidi wa kuonekana kwako nyuma?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Andika matokeo ya vigezo kadhaa kwenye hali ya uongozi wako kwa kujibu maswali yafuatayo. Mpatie matokeo haya mshauri wako na jadili pamoja naye kabla ya kipindi cha mafunzo yajayo.

1) Jielezee mwenyewe kama kiongozi
   - Ni mtindo upi wa uongozi unatumia zaidi?
   - Ni vipingamizi vipi unavyoviona mwenyewe unavyo? Nini unachoweza kufanya kufidia kweye vipingamizi hivi?
2) Elezea kundi lako
   - Elezea ujuzi na uwezo wao.
   - Ni kiwango gani chao kwenye kujitoa kwenye kazi?
   - Kuna aina yoyote na migogoro kati yao ambayo inahitaji kushughulikiwa?
3) Elezea kazi yako.
   - Unapanda kanisa miongoni mwa watu wanaopinga au wanaokubali?
   - Wewe au wajumbe wa kundi lako ni “wa kuja” au wageni miongoni mwa watu hawa?
   - Kuna hali halisi ya uchumi inayofanya juhudi za upandaji kanisa kuwa ngumu?
   - Una habari za kutosha kuhusu mandhali yako? Wewe na kundi lako mnaelewa kazi yenu?
   - Una mpango wazi na mkakati ambao unapeleka matokeo ya utafiti wako kwenye wajibu?
   - Kuna nguvu za kiroho zisizo za kawaida ambazo lazima zikabiliwe?
   - Kuna msukumo wowote wa kisiasa ambao unaathiri hali?
   - Una rasilimali zinazohitajika kukamilisha kazi?
   - Ni kwa njia zipi Mungu amekutayarisha wewe na kundi lako kwa kazi hii?
4) Suluhu
   - Kama matokeo ya ulichojifunza, nini unahitaji kukazania?
   - Ni mtindo upi wa uongozi unaweza kuwa wa ufanisi zaidi kwenye hali yako, na kwa nini?

**VYANZO**

D’Souza, A., and Engel, J. F. “Leadership Styles, Being a Leader” in *Leadership: Making Human Strength Productive*. St. Davids, PA: The Center For Organizational Excellence, Eastern College, 1996. (Used by Permission)

UONGOZI

SOMO LA 8

# Mitindo ya Mwingiliano

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la warsha hii ni kutambulisha mwingiliano wa mitindo, kumpa kiongozi kubuni marejeo ya kuelewa jinsi anavyoweza kufanya kazi na wengine kiufanisi zaidi.

☞ **Wazo Kuu**

- Mitindo ya kuingiliana siyo sawa na mitindo ya uongozi, lakini inaathiri uongozi.
- Mitindo yote ya mwingiliano ina uwezo wake na udhaifu.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka kila mshiriki anatakiwa...

- Kujua mtindo wake wa kuingiliana na wengine.
- Kujua jinsi migongano inavyoibuka kwa sababu ya mitindo tofauti ya kuingiliana.
- Kuainisha njia moja ya kukuza ufanisi na wengine.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili ni somo mchaanganyiko na warsha. Wafunzwa watatathimini mitindo ya mwingiliano kwa kutumia jedwali 8.1 (ruhusu dakika 15 kwa shughuli hii). Kisha rejea nyuma kwenye matokeo ya tathimini unapokuwa unafanyia kazi maelezo ya kila aina ya mtindo wa mwingiliano. Somo hili litafanyika vizuri zaidi kwa majadiliano miongozi mwa washiriki na wakufunzi.

## UTANGULIZI

Uongozi ni utaratibu wa kijamii. Viongozi wanashughulika na watu, na mahusiano kati ya watu ni sehemu kubwa ya ufanisi. Kama mpanda kanisa, ufanisi wako unaguswa na uwezo wako wa kuelewa na kujihusisha kwa watu wengine. Mitindo ya mwingiliano inakazia kwenye uhusiano kati ya watu, wakati mitindo ya uongozi inakazia katika kukamilisha kazi maalumu. Ndiyo, kuna baadhi ya kupishana, lakini zote ni fikira muhimu kwa kiongozi. Katika somo hili tutaangalia katika mitindo kadhaa ya kuingiliana na wengine. Utakuwa na nafasi ya kugundua kawaida yako ya kushughulika na wengine. Zana ya tathimini katika somo hili itatumika pia katika kuwaelewa wengine.

## I. GUNDUA MTINDO WAKO WA MWINGILIANO

Mungu ametuumba kila mtu tofauti na kutuita kwenye kazi tofauti. Hii ina maana **kila mmoja siyo kama wewe.** Tunapowatarajia wengine kutenda kama sisi, kufikiri kama sisi, na kuona vitu kama tunavyofanya, kisha tunaishia kujenga uhusiano na watu walio kama sisi. Tunashindwa kwa hiyo kuwakubali wengine na mara kwa mara kujikuta kwenye migogoro.

> Unapogundua mtindo wako unaoingiliana unaweza kuanza kufanya mabadiliko kukuza uwezo wako na kupunguza udhaifu wako.

Tunahitaji kujiangalia wenyewe ili kuona jinsi tunavyoathiri wengine. Tunaweza tukawakwaza wengine na tusijue. Tunaweza kujisikia kutokuweza kuwavutia wengine na tusijue kwa nini. Vifungu vifuatavyo ni pamoja na zoezi linaloweza kukusaidia kugundua mtindo wako wa kuingiliana na wengine. Unapogundua mtindo wako unaoingiliana unaweza kuanza kufanya mabadiliko kukuza uwezo wako na kupunguza udhaifu wako. Hii inaweza kupunguza migongano na wengine, na kukusaidia kuwa mfanisi zaidi.

### A. Mwelekeo wa Kutathimini Mtindo wa Mwingiliano Wako

Kielelezo 8.1 Kina safu nne za maelezo. Itikia kwa maelezo yote kwenye jedwali kwa kuweka 0, 1, au 2 kwenye nafasi iliyotolewa pembeni ya kila maelezo.

0 = maelezo haya kamwe hayakuelezei wewe.

1 = maelezo haya wakati mwingine yanakuelezea wewe.

2 = maelezo haya yanakuelezea wewe vema.

**Kielelezo 8.1 Kutathimini Mtindo Wako wa Mwingiliano**

| Safu1 | | Safu 2 | | Safu 3 | | Safu 4 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ninakamata picha kubwa kwa haraka zaidi kuliko wengine wanaonizunguka | ___ | Mimi ni mtu ninayeleta shauku kwa watu wanaonizunguka | ___ | Watu wanasema ninaonyesha uvumilivu na kuelewa | ___ | Ninaweza kutegemewa kuchukua kazi niliyopewa | ___ |
| Ninapenda kufanya mambo kutokea haraka | ___ | Ninafanya kazi vema ninapokuwa huru na kubanwa na wengine | ___ | Watu husema mimi ni mwepesi wa kuzoea | ___ | Moja ya uwezo wangu mkuu ni kuwa mwangalifu wa mambo mengi | ___ |
| Si mzuri kwenye mambo mengi | ___ | Mara kwa mara naweka watu mbele ya vipindi | ___ | Mimi ni msikilizaji mzuri | ___ | Kama kazi ina manufaa kuifanya, ina manufaa kuifanya vema sana | ___ |
| Mara kwa mara natia changamoto hali iliyopo | ___ | Kulinda mda ni vigumu kwangu | ___ | Watu ni muhimu kwangu kama ilivyo vipindi vya huduma | ___ | Ninahitaji kujua hasa nini kinatarajiwa kutoka kwangu | ___ |
| Inapolazimika, nitachukua tahadhali kufanya mambo yatokee | ___ | Watu wanapenda kuwa karibu na mimi | ___ | Ninafanya vema kweye hali watu wanapofanya kazi kwa mapatano | ___ | Sitaki kufanya maamzi bila kuwa na ukweli wote | ___ |
| Wakati mwingine ninakuta ni vigumu kuwa mshiriki mzuri wa kundi | ___ | Ninaamua kuchukulia mwenyewe watu wanapokuwa hawakubaliani na mimi | ___ | Zaidi ninakuwa na mafanikio wakati hali yangu ya kazi ni imara na salama | ___ | Ninakuwa na matatizo wakati wa kutoa hisia zangu | ___ |
| Baadhi ya watu wanasema kwamba si msikilizaji mzuri | ___ | Sifanyi vizuri na ukweli na kazi zenye mambo mengi | ___ | Ninafanya vema watu wanaponionyesha kwamba ninakubalika | ___ | Ni mtu mwenye tahadhari ninayesita kuchukua hatari | ___ |
| Mara kwa mara ninachoshwa wakati huduma yangu inapokuwa kila siku | ___ | Ninakuta ni rahisi kuelezea mawazo yangu na hisia zangu | ___ | Mabadiliko kupita yananitisha | ___ | Ninatenda vema kwenye mipaka inayojulikana na taratibu | ___ |
| Ninachanganyikiwa wakati watu wanapokataa mawazo yangu | ___ | Ninafanya vizuri ninapohisi kwamba wengine wananipenda hasa | ___ | Wakuu wangu wanaweza kutarajia uaminifu wangu | ___ | Ni mpinzani wakati utendaji wangu unaposhuka chini ya kiwango | ___ |
| Ninakaribisha changamoto na kubadilika—ndivyo inakuwa bora zaidi | ___ | Ninafanikiwa katika kuwavutia wengine kufanya kazi pamoja | ___ | Ninafanya kila ninaloweza kutimiza mahitaji ya hao walio karibu nami | ___ | Watu mara kwa mara wanashangaa kile ninachofikiria | ___ |
| **Jumla ya Safu 1:** | | **Jumla ya Safu 2:** | | **Jumla ya Safu 3:** | | **Jumla ya Safu 4:** | |

### B. Alama

Unapokuwa umemaliza, jumlisha majibu yako katika kila safu na andika jumla katika nafasi ya chini kwenye safu. Rejea kwenye namba hizi unapoendelea kufanya kazi ya yaliyobaki kwenye somo.

### C. Kufafanua Matokeo

Kuna mitindo minne ya msingi ya mwingiliano. Safu nne katika kielelezo 8.1 zinawakilisha mitindo hii minne. Tena, mitindo hii ya mwingiliano inatofautiana kutoka kwenye "mitindo ya uongozi" iliyotambulishwa kwenye somo la mwisho kwa sababu inafaa kwa kila mmoja, endapo ni viongozi au la.

Unaweza sasa kuonyesha mtindo wa mwingiliano wako wa kawaida kwa kujaza kwenye jumla kutoka kielelezo 8.1 kwenye nafasi pembeni "jumla ya safu…" kwenye jedwali 8.2 chini. Inayofata, tafuta namba ya juu na weka badala "1" pembeni yake kwenye nafasi chini ya "Daraja." Kisha, weka daraja la mtindo wako wa pili wa juu kama "2" ya tatu yako ya juu kama "3" na ya chini kama "4"

**Jedwali 8.2 Mtindo Wako**

| Jumla  Kutoka Kielelzo 8.1 | Mtindo | Daraja |
|---|---|---|
| Jumla kutoka safu 1: | **MTENDAJI** | |
| Jumla kutoka safu 2: | **MVUTIAJI** | |
| Jumla kutoka safu 3: | **WACHEZAJI WA TIMU** | |
| Jumla kutoka safu 4: | **ANAYEFIKIRI** | |

Sasa unajua upi kati ya hii mitindo minne ya mwingiliano ni imara zaidi na ipi ni dhaifu zaidi. Uko tayari kuangalia juu ya kila mmoja unachomanisha, uwezo kadhaa na udhaifu wake, na nini unachoweza kufanya kukuza mwingiliano wako.

## II. MITINDO MINNE YA MWINGILIANO

Hakuna mtindo kati ya hii ulio bora kuliko mwingine. Kila mmoja una uwezo na udhaifu wake. Mungu anatumia hali zote za utu katika ufalme wake.

### A. Mtendaji

*"Chukua hatua na ibuka kwenye changamoto ya kuleta mabadiliko kufanya huduma yenye ufanisi zaidi."*

Watendaji wanakuwa watu wenye uwezo, wanaoweza kukubali changamoto na kutatua matatizo kwa njia ya haraka na ya ufanisi. Ni watu wa utekelezaji na wanaweza kutegemewa kufanya mambo kufanyika. Watendaji hawaogopi kuchukua hatari; wakati mwingine wanachukua kazi nyingi zaidi na wanaweza kuonekana kutokuwa wavumilivu kunapokuwa hakuna maendeleo wakati huo.

Mfano: Paulo (Flp 4:13)

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:***<br>Uhuru, madaraka, mchanganyiko, kazi ngumu, nafasi za kuendelea, kutia moyo mmoja mmoja | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:***<br>Hutoa majibu ya moja kwa moja, hung'ang'ania kwenye biashara, hukazia maana, hutoa msukumo |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:***<br>Mdanganyifu, unayejitegemea, Mfanisi, mwenye kutenda | ***Hao waliotofauti wanaweza kukuona kama:***<br>Mwenye haraka, anayelazimisha, anayemiliki, mkali, mgumu |

*BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI*

- Kujifunza kusikiliza, kuwa mvumilivu

- Kutoa amri kidogo
- Kuendeleza kujali watu zaidi
- Kuwa wa kuingilika zaidi na kusaidia watu
- Elezea kwa nini vitu viko kama vilivyo

**B. Mvutiaji**

*"Kuvutia na kugusa wengine kufanya kazi pamoja kupata matokeo muhimu"*

Wavutiaji ni watu wanaotarajia na wenye shauku ambao ni wazuri katika kuhusiana na wengine. Mara nyingi ni makini sana na wanaweza kuelewa mawazo na uwezekano katika namna inayowavuta wengine kushiriki. Kawaida yao kuwa na msisimko juu ya vitu vipya inaweza kuwawia vigumu kwao kufatilia baadhi ya kazi

Mfano: Petro (Mt 14:28,16:16)

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:*** Fahari, urafiki wa kimahusiano, uhuru kutokana na kusimamia mambo mengi, nafasi ya kuvutia na kusaidia wengine , mtoaji wa mawazo kiuhuru | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:*** Ni marafiki na huru, kutoa sifa na kukubalika, kutafuta kushiriki kijamii |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:*** Anayeamsha, mwenye shauku, mwigizaji, mtu mchangamfu | ***Hao walio tofauti wanaweza kukuona kama:*** Anayechangamshwa, majivuno, mkasilikaji, muonevu, mzungumzaji |

*BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI*

- Uwe mwenye haraka kidogo—tathimini mawazo yako
- Uwe wa –kuangalia matokeo zaidi
- Tawala matendo na hisia
- Kazania zaidi mambo/ukweli
- Punguza, sikiliza, usiseme sana

**C. Timu ya Mchezo**

*"Shirikiana kiutayari na wengine kufanya maono na mipango"*

Timu ya mchezo inaunga mkono, watu wenye fahari walio na hisia nzito kwenye mahitaji ya wengine. Wanaweza kuhesabika kuchukua kazi kama zilivyogawiwa na viongozi na hawatakwaza hao waliojitoa kwa ajili yao. Timu ya mchezo inaweza isifanye kazi vizuri peke yake kwa kuwa wakati mwingine wanakosa uanzilishi wa kipekee.

Mfano: Barnabas (Mdo 15:37-39)

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:*** Uchaguzi wa kazi moja pekee, Kujihusisha na kundi, kuanzisha mtindo wa kazi, usalama, malengo wazi na mgao wa kazi | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:*** Hutumika kama marafiki, wanaruhuru mda wa kuzoea mabadiliko, wanaruhusu uhuru wa kufanya kazi katika mda wako,wanatoa msaada |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:*** Mwenye kutia moyo, utayari, wa kutegemeka, wa kutegemewa | ***Hao waliotofauti wanaweza kukuona kama:*** Mthibishaji, asiye stadi, mtegemezi, mzito, mnyamavu |

*BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI*

- Uwe mwepesi kidogo kwa yale wanayofikiria wengine

- Uwe mnyoopfu zaidi
- Uwe na kuhusika zaidi na kazi yenyewe
- Kutana na makabiliano na uwe mwamuzi zaidi
- Jifunze kusema hapana
- Fanya mengi kuanzisha utekelezaji

**D. Mwenye Fikara**

*"Aliyevutika kuchukua maono na kupanga kwa mchanganuo safi na kwa uangalifu"*

Wanaofikiri ni waaminifu, watu wenye mpangilio walio na wanaokamata mambo kwa wingi. Wanaweza kutegemewa kufuatwa kwenye miradi ambayo wengine wanaona kuwa ya kutatanisha. Wanaofikiri wanatiwa changamoto na mabadiliko yasiyotarajiwa na kutaka kung'ang'ania yanayoonekana kutokueleweka.

Mfano: Luka (Luka 1:1-4)

| | |
|---|---|
| ***Anatamani hali zinazoruhusu:*** Uchaguzi wa kazi moja, Uangalifu, Upangaji, ulinzi, uimara, matatizo kidogo ya kushindwa | ***Anaitikia vema kwa wengine ambao:*** Hutoa hakikisho tena, anga la usaidizi, kupambanua njia na viwango |
| ***Hao walio sawa wanaweza kukuona kama:*** Mkamilifu, shupavu, wa utaratibu, kutokuwa na mzaha | ***Hao waliotofauti wanaweza kukuona kama:*** Mpinzani, mwenye vitu, mpekuzi, si mdanganyaji, mwenye maadili |

*BAADHI YA HATUA ZA UTEKELEZAJI*

- Kukazania kufanya mambo yaliyo sahihi—siyo tu katika kufanya vitu kiusahihi
- Anaitikia haraka zaidi
- Anaanza kutumaini fikira na kukalia kidogo ukweli
- Kuwa tayari kuchukua matatizo
- Kuwa wazi zaidi na rahisi
- Usiogope kuanzisha mahusiano

Matokeo haya yanakuelezea wewe? Unaweza kutaka kumshirikisha matokeo mwenzi wako au watu wengine wanaokujua vema kuona kama wanaweza kuainisha matokeo haya. Kumbuka kwamba mitindo haiendani na watu kikamilifu. Unaweza kukuta kwamba huendani kabisa na moja kati ya mitindo hii minne. Kwa watu wengi katika makundi mawili ambayo wamepa alama za juu watawekea kivuri chepesi kwenye mitindo yao.

*Chukua mda fulani kushirikisha uliyojifunza kwa wafunzwa wenzio kuhusu wewe mwenyewe kufikia hatua hii. Katika vikundi vidogo, jibu maswali haya:*

- Ni mazingira gani unayopendelea kufanyia kazi?
- Ni watu wa aina gani ambao unaitikia kwao zaidi?
- Elezea mazingira yako halisi unayofanya kazi. Jinsi gani yanafanana na mapendeleo yao au kutofanana?
- Umekuwa na ugumu katika kugusa watu ambao unahisi mitindo yao ni tofauti na yako mwenyewe?
- Ni nini ulichojifunza kuhusu wewe mwenyewe ambacho hukujua kabla?
- Ni hatua zipi unazoweza kuchukua ili kuwa mfanisi zaidi kwa watu wanaokuzunguka? Unahitaji kuwa muwazi zaidi? Unahitaji kusikiliza zaidi? Unahitaji kuwa mchangamfu zaidi?

## UFUPISHO

Nini unachoweza kufanya, kwa sasa unapokuwa unajua vitu vichache kuhusu wewe mwenyewe, kuwa mfanisi kwa wengine? Kama ilivyokwisha kusemwa, kila moja ya mitindo hii ina uwezo wake wa kipekee vilevile na udhaifu. Utahitaji kutumia uwezo wako na kujifunza kukua kutokana na udhaifi wako.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

Kwa kila moja ya makundi manne ya watu, yanaelezea uwezo na udhaifu kwa misingi ya utaratibu wa upandaji kanisa.

- Jinsi gani watendaji wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?
- Jinsi gani watia moyo wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?
- Jinsi gani wachezaji wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?
- Jinsi gani wanaofikiri wanavyokabili kazi ya upandaji kanisa? Ni nini uwezo wao na udhaifu?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Kama njia ya kuelewa vitengo hivi vinne, chukua watu watano unaowajua kutoka kwenye mzunguko wa marafiki zako na kimya kimya wachunguze katika hali tofauti tofauti na kisiri nukuru matendo yao au maelezo yanayochanganua mtindo wao wa mwingiliano.
- Fikiria "hatua za utekelezaji" ambazo zinafatana na kila mtindo. Tambua miwili ambayo kwa uangalifu utaifanyia kazi kabla ya kipindi kinachofata cha mafunzo. Shirikisha hili kwa mshauri wako, na muulize mshauri kukupatia matokeo juu ya jinsi unavyofanya.

## VYANZO

Engel, James F., Jane Overstreet, and Terry Sparks. *Leadership: Making Human Strength Productive*. St. Davids, PA: The Center For Organizational Excellence, Eastern College, 1996. (Used by Permission)

UONGOZI

SOMO LA 9

# Hitaji ya Uongozi

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kumsaidia mfunzwa kuona ni aina gani na viongozi wangapi wanahitajika kwa makanisa ya mtaa na kwa mwili wote wa Kristo (Kanisa) katika taifa lake.

☞ **Wazo Kuu**

- Kueneza upandaji kanisa kunahitaji mchanganyiko wa viongozi.
- Kila muumini anatakiwa afunzwe kwa ajili ya uongozi, na ingawa siyo wote wataufaulu.
- Kadiri uongozi unapokuwa katika kiwango cha chini, ndivyo uongozi unavyohitajika zaidi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka kila mshiriki anatakiwa…

- Kujua aina nne za kazi ya viongozi zilizoelezewa katika somo hili.
- Kuweza kujua kuchunguza mahitaji ya uongozi katika huduma yake.

## UTANGULIZI

Kanisa linahitaji uongozi. Pengine wote tunaweza kukubaliana na maelezo haya. Lakini pia yanainua idadi ya maswali kadhaa muhimu. Ni aina gani ya uongozi unahitajika? Nani anatakiwa awe mhitimu wa kufundisha uongozi? Wapi viongozi wa kanisa wanatakiwa wafunzwe? Jinsi gani wafundishwe? Nani awafundishe? Ni nafasi zipi wanatakiwa wachukue katika maisha ya kanisa? Dwight Smith, kiongozi wa misheni, amesema kwamba, “Bila viongozi, hakutakuwa na kesho; kutakuwa na leo inayojirudia.”

> Bila viongozi, hakutakuwa na kesho; kutakuwa na leo inayojirudia.”

Wakati maswali haya ya uongozi yanapojadiliwa, kuna aina mbili za dhana za uongo za kawaida. Dhana ya kwanza ni kwamba viongozi wanaweza tu kufunzwa katika vipindi maalumu (Jumuia za Biblia au Seminari) na kisha kutumwa nje kufanya kazi katika makanisa ya mitaa. Dhana ya pili ni kwamba uongozi unamaanisha “wachungaji.” Dhana hizi zinapunguza uchaguzi uliopo wa kujaza mahitaji ya uongozi. Somo hili litajaribu kutoa kuelewa kuzuri kwa hitaji halisi la uongozi kwenye kanisa.

## I. NI AINA GANI YA VIONGOZI KANISA LINAHITAJI?

Kuelewa kwa ufinyu kwa uongozi kama mchungaji peke yake, wakati ikiwa kawaida, kunakana ukweli kwamba aina nyingi kadhaa za uongozi unahitajika kanisani kama tutatimiza Utume Mkuu. Hata siyo mapenzi ya Bwana kwamba wachungaji tu wataendesha huduma ya kanisa. Kuna angalau ngazi nne za uongozi wa kanisa ambazo zimebainika. Kwa kutumia ngazi hizi, tutaelezea kazi za viongozi pamoja na aina kadhaa za vipindi vya mafunzo yanayohitajika kuwaandaa kwa ajili ya huduma.

> Aina nyingi za viongozi, kwa nyongeza ya wachungaji, wanahitajika kama kanisa litatimiza Utume Mkuu.

Kabla hatujaonyesha ni aina gani ya viongozi kanisa linahitaji, ni lazima tukumbuke tafsiri yetu ya uongozi ambayo ilitolewa kwenye masomo ya nyuma. Uongozi ni *kugusa*. Ni lazima tuwe waangalifu tusiangukie kwenye mtego wa kufikiria uongozi kama nafasi ya awali, lakini badala yake kama kugusa. Kwa kutumia tafsiri hiyo, tunaweza sasa kufikiri viongozi wa kanisa kama watu

wanaoweza kugusa wengine kukua kiroho na kuwafikia waliopotea. Niwazi, Kanisa linahitaji idadi kubwa ya viongozi wa aina hiyo. Kwa hakika, *zaidi,* kama si wote, wakristo wanatakiwa waweze kufanya kazi hizi.

Ni muhimu kufundisha waumini kwa ujumla kwa ajili ya uongozi, badala ya kuchagua wachache.

Njia hii mpya ya kuangalia viongozi kwa ajili ya kanisa inaonyesha umuhimu wa kufundisha siyo tu 'kuchagua viongozi wachache' lakini kwa ufundishaji mpana zaidi wa waumini kwa ujumla. Siyo wote watakuwa na uwezo wa ngazi moja ya uongozi. Baadhi wana uwezo zidi wa asili wa kuongoza, au wamejaliwa kiroho kwa majukumu hayo. Wanaweza kuongoza makanisa makubwa sana au makundi ya kanisa. Wengine wataongoza katika njia za kujisikia kidogo, kama vile kwenye vikundi vidogo. Ngazi nne za uongozi ni:

**A. Viongozi wa Vikundi Vidogo au Vikundi Kiini – Wafanya Majaribio**

Viongozi hawa wana majukumu madogo ya kwawida ya uongozi kuliko kufanya ya viongozi wa kanisa, au mchungaji lakini ni moja ya nafasi nyeti zaidi. Viongozi hawa wana mawasiliano zaidi ya moja kwa moja na waliopotea, na kwa wote waumini waliokomaa na ambao bado. Kwa njia nyingi wako 'mstari wa mbele.' Ngazi ya "juu" ya uongozi ipo hasa kusaidia kufunza, kuhamasisha, na kutoa kufikira kwa kundi hili kuchukua kazi kubwa zaidi ya upandaji kanisa. Wakati kiongopzi kama huyo anatakiwa awe mkristo anayekua, kunaonekana kutokuwa na maelekezo ya mkazo sawa kwa ngazi hii ya uongozi kwa kuwa ni ya wazee. Hii ni sehemu nzuri ya kutumia waumini ambao hawajakomaa sana kwenye huduma. Itakuwa uzoefu wa kuimarishwa kwao, na wanapokomaa na kufaulu, wanaweza kuongezewa majukumu. Mengi hasa ya huduma ya kanisa la kwanza yalitokea kwenye vikundi vidogo kwa aina hii ya uongozi (Matendo 2:46-47).

**B. Viongozi wa Kanisa la Mtaa—Waandaaji**

Viongozi wa kanisa la mtaa wana majukumu ya kuandaa kusanyiko lote la mtaa kwa ajili ya huduma, na kuwaelekeza kwenye kazi hiyo. Hawakuwa kamwe wamekusudiwa kufanya kazi ya huduma wenyewe. Badala, nafasi yao ni muhimu zaidi kutumia mda "wakisubiri mezani." Hao walio katika kitengo hiki wanaweza kuitwa wafuasi wenzi, wazee, mashemasi, wachungaji, au kitu kingine, kutegemeana na muungano wa kanisa maalumu ambalo wanatoka. Kunaweza kukawa na mmoja au wengi kutegemeana na ukubwa wa kusanyiko. Wana majukumu ya ajabu mbele za Bwana, na wanatakiwa wachaguliwe kwa uangalifu. Hao tu waliohakikishwa kuwa na tabia nzuri na maisha ya kimungu wanatakiwa wafikiriwe kwa ngazi hii ya uongozi.

**C. Viongozi wa Kanisa wa Eneo—Wahamasishaji**

Kwa kipindi mtu anapoibukia kwenye hatua hii ya uongozi, wanatakiwa kuwa wanatumia mda wao ulio mwingi kuwatia moyo wengine kufanya kazi ya huduma. Kwa njia hii, wanaweza kuzidisha juhudi zao na kufanya kiwango cha juu cha mguso kwa uzoefu wao. Hao walio katika ngazi hii ya uongozi wanaweza kuitwa waangalizi, maaskofu, makasisi, au vyeo vingine vingi. Jina lina umuhimu kidogo kuliko majukumu wanayoshika. Ngazi hii pengine ndiyo inayokumbwa na dhambi ya kiburi, na kwa hiyo lazima wachaguliwe kwa uangalifu.

**D. Viongozi wa Kanisa wa Kitaifa—Wenye Kuwa na Fikara**

Viongozi wachache wana hekima ya kuweza kutimiza wajibu huu kama viongozi wa taifa.

Viongozi wa taifa ni wale wanaoweza kuwasaidia wengine kuona itakuwaje. Wanatumia mda wao wakiainisha lengo la shughuli zetu kwa ajili yetu wote. Wakati wanaohamasisha wanatunza mashine ya harakati ikiwaka, Watoa fikara wanatuchochea kuelekea kwenye kusudi la kuleta injili kwa kila taifa. Umoja na ushirika miongoni mwa waumini ni ufunguo wa kukamilisha Utume Mkuu. Yesu aliomba kwamba umoja wa waumini uwe ushuhuda ambao utahakikisha kwa ulimwengu kwamba alikuwa ametumwa na baba, na kwamba anatupenda (Yn 17:23). Hata hivyo, kutunza umoja huo bila kupatanisha ukweli wa injili ni kazi ya ukumbusho. Viongozi wachache wana hekima ya kuweza kutimiza wajibu huu kama viongozi wa taifa.

Inatakiwa itambulike kwamba kuna kutatiza kwa asili na kunakofaa kwenye mipaka kati ya kazi nne za aina nne za viongozi. Mgawanyo huu unawakilisha kazi za *msingi* za ngazi ya uongozi. Katika hali halisi, ngazi zote nne zinatakiwa zitimize nafasi zingine kwa kiwango kidogo. Kwa

mfano, Mchungaji pia anaweza kuwa na fikara. Kiongozi wa kikundi kidogo anatakiwa kuandaa. Kiongozi wa kitaifa anatakiwa kuhamasisha, na zaidi. Kwa jinsi hiyo, Wanatakiwa watumie mda wao mwingi, na kuwa wenye vipawa zaidi kwenye maeneo yaliyoorodheshwa kwa kiwango cha uongozi.


Kuna njia tofauti tofauti za kutenga ngazi za uongozi, lakini kwa kusudi letu, tutatumia hizi nne. Na ingawa zana hizi za kufundishia zinakazia kwenye ngazi mbili za kwanza, hii haina maana kwamba zile nyingine mbili si muhimu. Badala, viongozi wa kieneo na wa kitaifa kawaida wanaanzia huduma zao kwenye ngazi mbili za kwanza, na kupewa majukumu zaidi uwezo wao unapotambulika.

Inatakiwa itambulike pia kwamba mchanganyiko wa watu wanahitajika kujaza majukumu haya ya uongozi. Ili kwa harakati za upandaji kanisa kutokea, makundi mengi tofauti yanahitaji kuhamasishwa na kuongozwa. Wakati wanaume wenye sifa watahitajika kwenye nafasi nyingi, kutakuwa na hitaji kwa wanawake viongozi na viongozi wa vijana. Katika baadhi ya hali, wanaume na wanawake bachela wanaweza kuwa bora kutoa mda na nguvu zinazohitajika kwa harakati kuenea. Hili lilikuwa ni swala kwenye Agano Jipya, ambapo Bwana kwa ukubwa alimtumia mtume Paulo kama bachela.

## II. NI VIONGOZI WANGAPI KANISA LINAHITAJI?

Hitaji la viongozi kanisani linaweza kuelezewa vema kwa piramidi katika kielelezo 9.1. Kielelezo hiki kinaeleza ukweli kwamba viongozi wengi zaidi wanahitajika kwenye kina cha piramidi kuliko juu. Hii ni kwa sababu ya idadi inayoongezeka ya makundi ya kuongoza tunapokuwa tunaelekea chini kwenye piramidi. Kuna idadi kidogo ya makanisa ya kitaifa, lakini kila moja yake linaweza kuwa na maeneo mengi. Kila kanisa la kieneo linaweza kuwa na idadi kubwa ya makanisa ya mtaa. Kila kanisa hai la mtaa litakuwa na mikutano ya pamoja ya vikundi vidogo vingi na / au vikundi kiini vya kuadilishana, maombi, kuabudu, uinjilisti na shughuli zingine na mahitaji.

**Kielelezo 9.1 Piramidi ya Uongozi wa Kanisa**




Kwa hiyo, jibu la swali “Ni viongozi wangapi tunahitaji?” ni “Wengi kadiri tuwezavyo kufunza!” Tunapofikiria ngazi zote za uongozi, tunaona kwamba hitaji ni zito, na linaendelea kadiri watu wanapoletwa kwa Bwana, vikundi vidogo vinaundwa, na makanisa ya mtaa mapya kuanzishwa. Hii inapelekea kwenye swali linalofata la kimsingi.

### A. ‘Meza ya Mchanga’

Huduma itapanda au kuanguka kwa uongozi wake. Hii ina maana kwamba kabla kanisa halijaweza kuongeza wajumbe wapya, ni lazima lipanue msingi wa uongozi wake. Hili ni sawa na kujaza mchanga juu ya meza. Unaweza kujaza tu mchanga zaidi kwenye meza kabla haijajaa. Kunapokuwa hakuna nafasi zaidi kwenye meza kiasha meza imejazwa na mchanga

kuchukua umbo la piramidi na mchanga wote wa ziada uliokosa nafasi mezani. Kama unataka kuongeza mchanga zaidi na kujenga piramidi kubwa, ni lazima upanue kina cha meza.

Viongozi nyeti wanaweza kupatikana hapohapo kwenye kikundi kiini chako na kanisa. Wanachotakiwa ni kugundulika na kufunzwa.

Maana ya kanuni ya piramidi ni rahisi. Kama unataka kukua, ni lazima uanze kwa kupanua kina. Viongozi nyeti wanaweza kupatikana hapo hapo kwenye kikundi kiini chako na kanisa. Wanachotakiwa ni kugundulika na kufunzwa. Funza viongozi wapya na kanisa lako litaweza kukua kiafya na idadi. Kama kanisa lako halikui kwa hiyo inaonekana zaidi kutokuwa na viongozi wa kutosha kwa ngazi fulani. Kwa mfano, Kanisa lako lina viongozi wa kutosha wa vikundi vidogo? Kama siyo, pengine unahitaji kukazania kwenye maendeleo ya uongozi ili kwamba kanisa lako liwe na ufanisi zaidi katika kuwafikia nje kwa ajili ya Kristo.

**B. 'Kanuni ya Yethro'**

Viongozi wataalamu wa serikali wamesema kwamba kwa utekelezaji wa ufanisi wa kundi, endapo ni katika jeshi, ulimwengu wa biashara, au katika anga la siasa, asilimia 10-15% ya kundi lazima wawe kwenye nafasi za uongozi. Asilimia hii inathibitisha kwamba kundi lina mawasiliano sawa, usimamizi na mwingiliano ili kwamba waweze kutimiza kitu fulani. Kwa maneno mengine, kunatakiwa kuwe na kiongozi mmoja kwa kila watu saba mpaka kumi ambao wamesimamiwa.

Haishangazi kwamba Mungu ametupatia mifano ya kibiblia ya uwiano wa uongozi miaka maelfu kabla ya watalamu hawa wa serikali kufanya ugunduzi wao. Katika Kutoka 18, Musa alikuwa amechoka sana kutokana na kuongoza watu wa Israeli. Baba mkwe wake, Yethro' aliona hili, na kushauri njia bora ya kuongoza watu. Mfano huu tutakaouita 'Kanuni ya Yethro,' bado unafaa. Alimshauri Musa kuteua maelfu ya viongozi, mamia, kwenye hamsini na makumi. Hawa ni viongozi wangapi? Ngoja tujumlishe viongozi kwa kundi la watu 100.

**Mchoro 9.2**

| Kwa kila Watu 1000 | Aina za Viongozi | Idadi Iliyohitajika |
|---|---|---|
| **1000 ÷** | **1000 =** | ***1*** |
| **1000 ÷** | **100 =** | ***10*** |
| **1000 ÷** | **50 =** | ***20*** |
| **1000 ÷** | **10 =** | ***100*** |
| | **Jumla ya Viongozi waliohitajika** | ***131*** |

Kutoka Jedwali 9.2, Unaweza kuona kwamba kulingana na 'Kanuni ya Yethro' kutakuwa na viongozi 131 kwa kila watu 1000 wanaoongozwa. Kama tunaelezea hii kama asilimia, 131 nje ya 1000 asilimia 13.1. Idadi hiyo inaoana na kielelezo cha serikali vema sana cha asilimia 10-15. Hapa kuna mtihani rahisi kwa ajili yako. Katia kanisa lako la hivi karibuni au jengo la kanisa, asilimia 10-15 ya watu inatakiwa iwe viongozi. Zidisha namba ya watu ulionao kwa 0.15 (au 1silimia 15) kuona ni jinsi gani unafanya vyema.

| | |
|---|---|
| *Jumla ya watu kanisani kwangu (jengo):* | ________ |
| *Kuzidishwa kwa 15%:* | *X 0.15* |
| *Idadi ya viongozi unaotakiwa kuwa nao:* | ________ |
| *Idadi halisi ya nilionao sasa:* | ________ |

Unaendeleaje? Hongera hata kama una zaidi ya 15%. Kama una kidogo, ni muhimu kwamba unaanza kufanya kazi katika kuendeleza viongozi.

### III. WAPI TUNAPATA VIONGOZI HAWA?

**Kie. 8.3**




Bwana hatupi kazi ya kumaliza isipokuwa anajua kuwa inawezekana. Tuanaweza kukamilisha kazi hii inayoonekana kutowezekana kama tu waangalifu kufata maelekezo yake, na baadhi ya kanuni za msingi za kimaandiko za mafunzo ya uongozi.

Katika Matendo 5:14-30, Yesu alitoa mfano juu ya watumishi watatu. Wakati mfano una kusudi maalumu, mistari ya 21 na 23 inarudia kifungu cha maana, "Umekuwa mwaminifu kwa vichache; nitakuweka mkuu wa vingi." Wazo hili lina maana, na linaonyesha kuelezea jinsi tunavyoweza kupata viongozi tunaohitaji. Tunatakiwa tuangalie hao walio waaminifu katika 'machache' ya uongozi, na kuwapa majukumu yanayoongezeka. Tumeshaona hili tulipoangalia kwenye hatua za uongozi. Mafanikio (na uaminifu) katika ngazi za chini ilikuwa mara zote hitaji kwa majukumu ya juu.

Kwa hiyo, kuongezeka kwa hitaji la viongozi wa kikristo kwa kanisa kutahitaji kutimizwa kwa kufuasa waumini wapya na kuwafundisha kwa ajili ya uongozi. Hapa ndipo tunatakiwa kupata viongozi, na ambapo tunatakiwa kuanza kufunza. Hili siyo kuchangia kwamba wakata shauri wapya mara moja wanakuwa tayari kuhudumu kama kiongozi wa kanisa. Hawawezi, na Biblia inaonya juu ya kuwahisha utaratibu huu (Tim 3:6) Kwa jinsi hiyo, ukweli kwamba hawawezi kuhudumu mara moja kama viongozi huo ndio wajibu wetu kuanza kuwafundisha kwa uwezekano wa huduma za mbeleni. Tunahitaji kukazania kuendeleza uaminifu, tabia ya kimungu, na tabia ya kitumishi mara moja. Kama wanaume na wanawake hakikisha uaminifu, wanatakiwa wapewe yote majukumu zaidi na mafunzo zaidi kwa undani.

### UFUPISHO

Mda sasa utakuwa si wa mzaha zaidi kuhusu ufundishaji zaidi wa viongozi katika ngazi zaidi. Kukua kwa mbeleni na kanisa lenye afya linavitegemea. Hatuwezi kudhani kwamba viongozi sahihi wataibuka kutoka kwenye vyuo vya mafunzo tutakapowahitaji. Viongozi wa kanisa la mtaa wanatakiwa kuchukua hatua ya mwanzo katika hili.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Watu wangapi katika kanisa lako wanatenda katika ngazi fulani ya uongozi?
- Ni nini hitaji lako kuu katika huduma yako kwa kipindi hiki?
- Nini unaweza kufanya katika kanisa lako kufunza viongozi wa kikundi kiini na kikundi kidogo?
- Nani ni viongozi katika eneo lako? Wapi na jinsi gani wamefunzwa?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Jifunze vipindi vya mafunzo na hitaji la uongozi katika eneo lako. Ni mafunzo yapi yanapatikana kwa kila ngazi ya uongozi? Jinsi gani unaweza kufaidika kutoka kwenye vyanzo hivi katika jengo la kanisa lako? Shirikisha matokeo yako kwa mshauri wako.

### VYANZO

Womack, David A. *The Pyramid Principle.* Minneapolis, MN: Bethany Fellowship, 1977.

UONGOZI

SOMO LA 10

# Kufunza Viongozi Wapya

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kukazia majukumu ya mpanda kanisa kuzidi yenyewe kupitia kufundisha viongozi wengine. Haitoshi tu kugawa madaraka; uongozi lazima uzidi. Somo hili linaelezea ujuzi rahisi wa kufunza kazini kunakoweza kuletea kuzidi kwa viongozi.

☞ **Wazo Kuu**

- Musa, Yesu, na Paulo wote walielezea kufundisha viongozi wapya
- Kufundisha kunatakiwa kuchukulie yote mahitaji ya huduma na mahitaji ya viongozi wapya.
- Kiongozi hatimaye anatakiwa ahusuishe na kutoa wafunzwa wake.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka kila mshiriki anatakiwa...

- Kujua jinsi viongozi walivyofunzwa kwenye Biblia.
- Kujua na kutumia hatua 5 za utaratibu wa kufunza viongozi wapya katika kazi mpya.
- Kujitoa kwenye kuzidisha yeye mwenyewe kupitia kuendeleza viongopzi wapya.

☞ **Ziada**

10A Sifa za Kutia Moyo kwenye Uongozi Mpya

**UTANGULIZI**

Maendeleo ya uongozi ni moja ya kipengele muhimu cha upandaji kanisa na ukuaji wa kanisa. Bila maendeleo ya uongozi, wajumbe wa kanisa wanabakia kuwa wategemezi milele kwa mpanda kansia na timu yake. Makanisa yanayokua kawaida yana vipindi, vya kawaida na visivyo vya kawaida ambamo viongozi wanafunzwa kuchukua majukumu. Makanisa yanayodumaa mara nyingi hayana.

Kama mpanda kanisa, lazima uzidi mwenyewe kwa kuendeleza viongozi wengine. Mapema katika upandaji wa kanisa wakati mpanda kanisa anapotumia mda wake mkubwa kufanya uinjilisti, anahitaji kuanza kuainisha na kuwajenga hao wanaweza kuwa viongozi wa mbeleni. Katika hatua ya baadaye katika kanisa lililopandwa, atatumia mda wake mwingi akishughulika na maendeleo ya uongozi. Maendeleo ya uongozi ni lazima ili kuunda kanisa hai, linalokua. Jinsi gani tunafanya? Kwanza, tambua mifano ifuatayo ya kibiblia:

## I. MIFANO YA KIBIBLIA YA KUZIDISHA UONGOZI

### A. Musa na Yoshua

Musa alikamilisha vitu vya ajabu kwa ajili ya Mungu. Alikomboa watoto wa Israeli kutoka utumwani mwa Wamisri na kuwaleta katika mpaka wa nchi ya ahadi. Yoshua alikuwa upande wa Musa kama mpiganaji wa kutegemewa kutokea mwanzoni mwa uongozi wa Musa (Kutoka 17:9-14). Yoshua alikwenda na Musa kwenye mlima Sinai kupokea sheria na amri, (Kutoka 24:12-13), na kuonekana kuwa na kibari maalumu kuingia kwenye 'hema ya mkutano' ambapo Mungu alikutana na Musa (kutoka 33:7-11). Imani ya Yoshua kuu ilionyeshwa vyema wakati yeye na Kalebu peke yao walipoamini kwamba Mungu angewapa uwezo wa kuimiliki nchi ya Kanaani (He 14:6-9).

Katika hatua fulani ya maisha ya Musa alijiuliza mwenyewe swali ambalo viongozi wote wanatakiwa kujiuliza kila mara. "Nani atakuwa badala yangu?" Musa alitambua kuwa Waisraeli wangehitaji uongozi wa mbeleni, na akamuuliza Mungu wa kuwa badala. Mungu alimchagua Yoshua, ambaye alikuwa akijifunza kutoka kwa Musa, na kisha akamwambia Musa kugawa baadhi ya madaraka kwa Yoshua ili kwamba watu waweze kujua kwamba Yoshua alikuwa Mtu wa Mungu aliyemchagua (He 27:15-22).

Musa aliona nchi ya ahadi, lakini hakuingia humo. Yoshua, kwa jinsi hiyo aliona uhalali wa ndoto ya Musa alipoingia humo nchi ya ahadi na Waisrael wote. Musa anaweza akawa alikuwa na wivu kwa ukweli kwamba asingeingia nchi ya ahadi, kwamba Yoshua angeingia (Kum 1:37-38. Badala, Musa alikabidhi uongozi kineema kwa Yoshua, kama vile tu Mungu alivyokuwa ameelekeza (Kum 31:7, 34:9). Musa ni kama mfano unaong'aa wa kiongozi mtumishi anayetafuta mazuri kwa ajili ya watu na kazi ya Bwana badala ya utukufu wake mwenyewe.

**B. Yesu**

Yesu alikuwa na mpango wa kueneza ujumbe ulimwenguni kote. Jinsi gani alifanya hilo? Alifundisha umati mkubwa katika matukio mengi, lakini mkazo wake ulikuwa kwenye maendeleo ya wafuasi wake wa karibu. Kundi hili dogo la wanaume wangeendeleza ujumbe wa wokovu hata kwa mguso mkubwa zaidi baada ya yeye kuondoka. Yesu mwenyewe alianza kuchagua watu hawa kabla ya kumalizia huduma yake kuu ya kuhubiri (Yn 1:35-51).

> Yesu alifundisha umati mkubwa katika matukio mengi, lakini mkazo wake ulikuwa kwenye maendeleo ya wafuasi wake wa karibu zaidi.

Yesu alitumia miaka miwili na nusu akionyesha nguvu ya ujumbe wake katika kuhubiri kwake na kuponya, na baadaye katika kifo cha kujitoa na kufufuka kimuujiza. Alikuwa kielelezo hai cha ujumbe wake kwa wanafunzi wake. Mwanzoni katika mda muafaka, Yesu aliwapa wafuasi wake nafasi ya kushiriki katika huduma kwa kuwatuma nje kama wamishenari (Mt 10). Wakati huduma yao ilipokuwa haina mafanikio, Yesu alitoa maelekezo ya mda kurekebisha tatizo (Mt 17:14-21). Mafunzo yao katika huduma yalikuwa ya kuonekana na muhimu zaidi kuliko kazi halisi walizokamilisha. Yesu aliwaandaa wanafunzi wake kuweza kuendeleza bila kuwepo kwake kimwili. Alikuwa na ujasiri mkubwa kwa wanafunzi wake kuwapa "funguo za ufalme" (Mt 16:19), na kuweka huduma ya mbele mikononi mwao (Mt 18:18-20).

Tunaona, kwa hiyo, kwamba Yesu aliongezeka mwenyewe kwenye maisha ya wengine ili kukamilisha kusudi lake. Alisema, "nifate na nitawafanya wavuvi wa watu" (Mt 4:19). Yesu yeye mwenyewe alikuwa mvuvi wa watu kwa hiyo kilazima alisema "nifate nitawafanya nilivyo!" Katika maendeleo ya uongozi, tunavutwa pia na kufunza badala tu ya kutafuta wasaidizi. Haja yetu inatakiwa kuona wafunzwa hatimaye wanafikia au kupita kiwango cha mafanikio ambayo tumekuwa nayo katika huduma.

**C. Paulo**

Tunaona kujitoa kwa Paulo kuendeleza viongozi zaidi wazi wazi katika maneno yake kwa 2Timotheo 2:2. " *Na mambo uliyosikia nikisema mbele ya mashahidi wengi, haya uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine*. Anarejesha kwenye "mashahidi wengi" waliopo kama alivyomfundisha Timotheo. Wote Yesu na Paulo walifuasa watu kwenye makundi madogo, badala ya "mmoja kwa mwingine." Tunahitaji kufata mfano wao kwa kuwaandaa viongozi "kwenye utekelezaji." Kwa njia hii, wengine wataona katika njia ya vitendo jinsi ya kuendeleza viongozi. Kumbuka, Kufuasa wengine ni kitu ambacho siyo tu kimefundishwa; kimekamatwa.

Paulo alikuwa na shauku kwa Timotheo kujifunza jinsi ya kuandaa wengine. Tambua marejeo haya katika 2 Timotheo 2"2 *kwa watu waaminifu.* Uchaguzi wa hao wanaotarajiwa kufundishwa ni sehemu muhimu ya utaratibu wa mafunzo. Hitaji kuu kwenye huduma ya kikristo ni uaminifu. Paulo hakuwa tu anapitisha *habari* kwa Timotheo, lakini pia njia ya kuandaa wengine. Kama Paulo alivyoshauri na kufuasa Timotheo, kwamba Timotheo ajifunze kuangalia na kufuasa wengine. Paulo alitakiwa kuwa na hakika na muundo wa mafunzo ambao ungerudiwa kwa kizazi cha tatu na hata cha nne.

Paulo alimfundisha Timotheo kwa ajili ya huduma kama vile alikuwa kijana wake mwenyewe. Lakini Timotheo kwa vyovyote hakuwa yeye tu aliyefunzwa na Paulo. Tunamsoma Sila, Yohana Mark, Barnabas, Akwila, Prisila, na Apolo—wote waliojifunza kutoka kwa Paulo kwa kiwango kadhaa. Safari ya mwisho ya kimishenari ya Paulo inaonekana kuwa safari ya kufundisha/kufuasa. Wakati wa safari hii tunasoma watu saba (Mdo 20:4) wakisafiri na Paulo, wengi wao wakijifunza kutoka kwake. Katika waraka wake mwenyewe, Paulo anamtaja Epafura, Dema, sapatro, Tito, Phoibe na wengine wengi. Kwa mfano, kwenye suluhu la waraka wake kwa Warumi, Paulo anawasalimia watu 27, wengi wao amefanya nao kazi na wanaweza wakawa wamefunzwa na Paulo.

> Lakini Timotheo kwa vyovyote hakuwa yeye tu aliyefunzwa na Paulo.

Unatakiwa utumie mtindo huu ulioelezewa katika 2 Timotheo 2:2 na kuelezewa na Paulo kwa kuwahusisha viongozi nyeti kila unachofanya wakati wa mda mnapokuwa pamoja. Endapo unapanga mikutano ya kikundi, kuwatembelea waliopotea, kuwashauri watu wanaoumia, kuomba kwa kondoo waliopotea, au kufundisha—yote inatakiwa iwe miradi ya pamoja.

## II. MAKUSUDIO YA KUFUNDISHA

Umeshatambulishwa kwenye "Z-Kufikiri" katika mandhali ya kupanda kanisa, hii ina maana kupanga ukiwa na matokeo kichwani. Mafunzo ya uongozi wenye ufanisi pia yanahitaji kwamba tunaangalia mbele kwenye mahitaji ya kanisa jipya tunapofunza. Maswali makuu tunayohitaji kuuliza ni: "Tunajaribu kuwasaidia watu kuwa nini?" "Ni aina gani ya viongozi wanaohitajika?" "Tunakusudia nini?" Namna gani bidhaa iliyokamilika inavyofanana?" Maswali haya ya kimsingi ni muhimu, kwa kuwa yanaelekeza utaratibu wa mafunzo.

Tunahitaji kuwa na picha wazi ya mahitaji ya uongozi, lakini pia tunatakiwa kuwa waangalifu tusimbane mtu asiyehusika kwenye matope hayo. Tunapopata watu "waaminifu" walio na uwezo wa uongozi, wanatakiwa wasifunzwe kwa kubanwa, kwa vipindi visivyo huru. Kila kiongozi nyeti ana hadhi yake, uwezo, kipawa cha kiroho, historia, na uzoefu ambao *lazima* uangaliwe. Kwa hiyo, tunapofundisha viongozi nyeti, fikiria vigezo vifuatavyo:

> Mafunzo ya uongozi wenye ufanisi pia yanahitaji kwamba tunaangalia mbele kwenye mahitaji ya kanisa jipya tunapofunza.

- *Vipawa vya kiroho* – Kumbuka kwamba Mungu amemjalia kipawa kila mjumbe wa mwili. Watu watavutwa na kutafuta utoshelevu katika huduma inayotumia vipawa vyao. Kwa mfano, mtu mwenye kipawa cha rehema na usimamizi anaweza kuwa mfanisi katika kuweka sawa mchuzi wa jikoni au kusaidia mzee, lakini siyo katika kufundisha shule ya jumapili. Weka viongozi wanaokua mahali wanapofaa zaidi, na siyo tu mahali palipo na hitaji la "mwili wenye uvuguvugu"


- *Uwezo* – Kila mmoja ana vipaji vya asili ambavyo wamejifunza kupitia juhudi na mazoezi, na ambavyo pia vinaweza kusaidia katika huduma. Kwa jinsi hiyo, uwezo huu wa kawaida hauwezi ukawa badala ya vipawa vya *kiroho*, kwa hiyo tunatakiwa kuwa waangarifu kutowalazimisha viongozi wanaokua kukazania katika huuduma ambazo wataweza kuzifanya, lakini ambazo hawana vipawa vyake vya kiroho. Hali ya maana, hakika ni kutafuta huduma inayofaa ambayo inatumia vipawa vya viongozi vile vile na uwezo wao.

- *Mahitaji ya Huduma* – Hitaji la huduma yako ya upandaji kanisa inatakiwa pia iguse utaratibu wa kufundisha. Kama kipawa cha mtu kwenye huduma maalumu inayoendelea, pengine wanatakiwa kufunzwa kwenye mpangilio mwingine. Kwa jinsi hiyo, kipawa cha kiongozi mpya kinaweza kisiwe wazi mara moja—kawaida vinagunduliwa kupitia huduma. Mungu anaweza akawa anataka mtu fulani kuendeleza kipawa ambacho mwanzoni hakuwa na uzoefu nacho au kujaliwa. Ni kweli kwamba pia kiongozi anatakiwa mara kwa mara kujifunza kutimiliza majukumu ambayo yanahitajika kusaidia kuendeleza mbele huduma ya upandaji kanisa. Wakati kiongozi wa kikristo anatakiwa kukazania kwenye kipawa chake, hakataliwi kuhusika katika maeneo mengine ya huduma. Kwa mfano, Timotheo alihitaji kujifunza kuwa mwinjilisti (2Ti 4:5).

- *Uzoefu* – Uzofu wa nyuma katika huduma unatakiwa utathiminiwe kwa uangalifu, kwa sababu unaweza kiubaya au kiuzuri kugusa maendeleo ya mbele ya mafanikio ya uongozi kwa mfunzwa. Unaweza kuwa uzoefu mzuri kwa sababu pengine mfunzwa ameshajifunza baadhi ya masomo magumu na ya thamani juu ya uongozi. Mahitaji haya hayatarudiwa, na kuokoa mda katika utaratibu wa mafunzo. Inaweza pia ikasaidia kuainisha kiharaka uwezo na udhaifu wa mfunzwa. Kwa jinsi hiyo, inaweza kuwa vibaya kama imefundishwa au kulazimishwa tena kimamlaka au mitindo mingine ya uongozi isiyo ya kibiblia. Inaweza pia kufanya uwezo wa maana vigumu kuutambua—muonyesho wa uwezo unaweza tu ukawa uzoefu, au kukosa uzoefu kunaweza kukafanya ikaonekana kwamba hakuna uwezo.
- *Hadhi*—Kuna vigezo vingi vya hadhi ambavyo hatuwezi kuvitaja mchanganyiko wote. Kwa jinsi hiyo, kiongozi nyeti anaweza au asiweze kuingiliana kirahisi na watu—ujuzi nyeti. Kiongozi mmoja anaweza kuwa anachanganyikiwa haraka na kuhitaji kutiwa moyo kwingi, wakati mwingine mchangamfu na bayana. Uwe na ufahamu wa haya na vigezo vingine unapokuwa unachagua na kufunza viongozi.

Kutafakari kimaombi kwenye vigezo hivi kunaweza kudhihirisha Mungu anachowaitia viongozi nyeti kuwa. Yafanyie marudio na yarekebishe kwenye hali halisi kwenye huduma yako na kwa wafunzwa wako. Hii ni rahisi kusemwa kuliko kufanywa. Inachukua hekima, kuwa macho kuendeleza kiongozi mpya kwenye unyeti wake, timiza mahitaji yaliyopo katika kanisa lililopandwa, na siyo taratibu. Kielelezo 10.1 kinaelezea ugumu na umuhimu wa kutafuta uwiano huu.

**Kielelzo 10.1 Kuweka Uwiano**




Mara nguvu hizi zinapoeleweka, mkufunzi anatakiwa kumtathimini mfunzwa na kuonyesha jinsi ya kuendeleza vema ujuzi wa uongozi na hadhi ya mfunzwa kwenye hali iliyopo ya upandaji kanisa. Kila hali ni tofauti, kama tu kila mtu alivyo tofauti.

Njia ambayo mara kwa mara ni ya ufanisi ni kuunda orodha ya uwezo na udhaifu wa mfunzwa, na andika chini maeneo maalumu ya ukuaji ambayo unataka kutia moyo. Unapokuwa unalinganisha viongozi nyeti na orodha hii ya makusudio, itakusadia kujua jinsi ya kukabili utaratibu wa kufundisha kwa kila moja yake. Kwa mfano, kama kiongozi anayefundisha anashindwa kusudi maalumu, kisha “shughuli ya kujifunza” inaweza kuandaliwa kumsaidia yeye kwenye eneo hilo. Tambua mifano ifuatayo:

**Jedwali 10.2 Makusudio Yanapelekea kwenye Shughuli za Kujifunza**


| KUSUDI LA KUJIFUNZA | SHUGHULI ZA KUJIFUNZA |
|---|---|
| Kukuza ujuzi wa kuhubiri. | Mwache aone jinsi unavyoandaa mahubiri yako. |
| Kuongeza ujuzi wa Biblia vya kutosha kuweza kuongoza kikundi kiini kiufanisi. | Mruhusu achukue kozi ya kuandika kuongeza kuelewa kwake kwa Biblia. |
| Kuimarisha uwezo (kichungaji) wa kulisha neno kidhaifu. | Mfanye asome nyaraka za kichungaji za kujifunza kwa kufata neno (1,2 Timotheo na Tito). |
| Muumini aliyekomaa ana shauku kuwa kiongozi wa kikundi kiini lakini haendani vema na watu wasiookoka. | Mfanye kiongozi nyeti kujaribu kufanya urafiki na mtu ambaye hajaokoka na kutunza kumbukumbu za uzoefu wake katika kukuza urafiki huu. |

## III. HATUA ZA UTARATIBU WA KUFUNZA VIONGOZI WAPYA

Utaratibu huu wa kufunza viongozi wapya umekwisha kuelezewa kwenye somo la kikundi kiini la 9, “Kufunza Viongozi Wapya wa Vikundi Kiini.” Vikundi kiini vinatoa uwanja wa ajabu wa kujifunzia katika kuendeleza viongozi wapya. Vinatoa nafasi ya kufunza viongozi wapya “kazini,”ukitambua kuwa **tunajifunza vizuri kwa kufanya**. Wakati wote kumbuka kwamba ni utaratibu wa kiutendaji. Usiweke msisistizo wote kwenye ufahamu na habari. Badala, tazama njia za ubunifu kupata kiongozi mwenye shauku ya kufanya mambo. Atajifunza zaidi kutokana na anayofanya.

Kielelezo 10.3 kinaonyesha ni kiasi gani kilichoonyeshwa kinachokumbukwa mwishoni mwa siku thelathini, katika hali ya kawaida. Uwezo wa kukumbuka unategemeana na aina gani ya kuhusika tumekuwa nako katika shughuli za kujifunzia. Ni wazi kwamba tunakumbuka zaidi tunapokuwa tumehusika katika *kufanya* shughuli.

**Kielelezo 10.3 Kiasi gani Tunakumbuka?**




Utaratibu wa hatua tano zifuatazo unaweza kutumika kumsaidia kiongozi nyeti kuendeleza ujuzi maalumu. Ni utaratibu unaotokana na shughulil.

### A. Hatua 1: “Ninaifanya”

Katika kuwafundisha viongozi, unatakiwa uongoze kwa kutoa mfano. Pengine sheria ya kwanza katika maendeleo ya uongozi ni kuwa aina ya kiongozi wengine watakayependa kumuiga. Mara kwa mara kufundisha kunashindwa kwa sababu kunakuwa hakuna kuhusisha utoaji kilelezo mzuri wa mawazo au ujuzi. Eleleza huduma kabla haijahitajiwa na mfunzwa kutoka kwako.

**B. Hatua 2: "Nitaifanya, Angalia"**

Wakati mfunzwa pia ʻakiwa ameangalia katika hatua 1, ilikuwa ni zaidi kutendewa, shughuli ya njia moja. Katika hatua hii, akilini tuna kujishughulisha, njia mbili za mwingiliano kati ya kiongozi na mfunzwa. Mfunzwa anajua kuwa ameandaliwa kuongoza, na anakamata kila kitu anachoweza kujifunza kwa kuangalia huduma yako. Kuelezea utekelezaji wako ni muhimu sana. Usichukulie jambo lolote kirahisi. Elezea kila unachofanya na kwa nini unafanya jinsi unavyofanya. Elezea kanuni za huduma ambazo zinaongoza matendo yako.

**C. Hatua 3: "Tunaifanya Pamoja"**

Uwe na hakika umefanya huduma ya ujuzi maalumu na viongozi wako wenye shauku kuwapa mkono kwenye uzoefu na kuwasaidia kuona na kujifunza makosa yao katika mazingira salama na mshauri wao. Hatua hii kidogo ni kama mtoto anayejifunza kupanda Baiskeli na mzazi akiishikilia inavyopaswa. Uwepo wako utawapa wafunzwa wako ujasili kwamba unaweza kusaidia kama wakiwa na tatizo, lakini pia wataweza kujaribi vitu wanavyojifunza kutoka kwako. Urefu wa mda ambao hatua hii inaendelea unategemeana kabisa na jinsi wewe na mfunzwa wako mnavyokubaliana kwamba mfunzwa yuko tayari kujaribu kuongoza mwenyewe.

**D. Hatua 3: "Unaifanya; Ninaaangalia"**

Mwangalie kiongozi wako akitumia ujuzi wa huduma. Usiingilie. Waruhusu kufaulu kushindwa wanavyoweza. Kisha, baada ya tukio na mahali pa siri, kimakusudi elezea uwezo na udhaifu uliochunguza. Fanya marudio ya makusudio katika kiwango hiki. Ni muhimu kuelezea yote, mazuri na mabaya, lakini kila inapowezekana, sisistizia mazuri. Toa shughuli za kujifunzia kuimarisha udhaifi kama ni lazima.

**E. Hatua ya 5: "Utaifanya"**

Mara unapofikiri viongozi wapya wako tayari, wakabidhi kazi. Usiiharakishe, lakini kawaida yetu ni kusubiri mda mrefu sana, na kumlemeza kiongozi mpya kwa kuendelea kwa uwepo wetu. Unatakiwa ubakie rafiki wa karibu, ukimfanya kiongozi mpya kana kwamba mko sawa. Utaratibu hauishii kwa kufundisha kiongozi mwingine mpya. Tunachojali ni kuzidisha viongozi wengi. Kwa hiyo mtie moyo kiongozi mpya mara moja kuanza kuzidi yeye mwenyewe kwenye maisha ya mwingine.

**Jedwali 10.4 Hatua Tano**

| Hatua | Kiongozi | Mfunzwa |
|---|---|---|
| **Hatua 1** | ***Fanya*** | - |
| **Hatua 2** | ***Fanya*** | ***Angalia*** |
| **Hatua 3** | ***Fanya*** | ***Fanya*** |
| **Hatua 4** | ***Angalia*** | ***Fanya*** |
| **Hatua 5** | - | ***Fanya*** |

Hatua hizi tano hazihitaji wakati wote kufatwa katika mtindo wa kukazia. Mara kwa mara, kwa jinsi hiyo, ufundishaji unashindwa kwa sababu sehemu ya utaratibu haikufatwa. Fikiria kiongozi mchanga mwenye shauku aliyekuwa ameombwa kutoa mahubiri, lakini hakuwa amefunzwa kwenye utaratibu huu. Mahubiri yake hayakuwa wazi sana na kila mmoja alifikia suluhu, akiwemo kijana, kwamba kuhubiri hakikuwa kipawa chake. Katika hali halisi, alihitaji tu kuona na kupata maelekezo kidogo juu ya jinsi ya kuandaa mahubiri.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini maendeleo ya uongozi ni muhimu?
- Jinsi gani ulivyofunzwa kama kiongozi? Elezea shughuli za kujenga zilizokusaidia kuendeleza uwezo wako wa uongozi.
- Ni vizazi vingapi vya uongozi vimeelezewa katika 2Timotheo 2:2?
- Ni jinsi gani Mathayo 4:19 inafanana na 2Timotheo 2:2?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Chukua kazi nzuri unayojua kuifanya vema kama vile kuendesha gari. Kupika chapati, au kujenga stuli ya mbao. Mfundishe mwingine kuifanya kwa kutumia hatua 5 zilizoelezewa katika somo hili. Elezea matokeo yako kwa mkufunzi au mshauri wako.
- Kwenye kikundi kidogho na wafunzwa wengine, au na timu yako ya upandaji kanisa, chukua makusudio matano kutoka Ziada 10A, “Sifa za Kutia Moyo kwa Kiongozi Mpya.” Elezea jinsi hatua hizi tano zinavyoweza kutumika kwa kila kusudio.

## VYANZO


- Allen, Roland. *Missionary Methods - St. Paul's or Ours?* Grand Rapids, MI: Wm. B. Eerdmans, 1962.
- Steffen, Tom A. “Leadership: Ten Implications for Cross-Cultural Church Planters.” N.p., n.d.

UONGOZI
*ZIADA*
10A

# Sifa za Kutia Moyo Ndani ya Kiongozi Mpya

## I. MAKUSUDIO YA KUFUNDISHA UONGOZI KWA UJUMLA

Makusudio yafuatayo ni muhimu kwa kila kiongozi katika ngazi yeyote

- Anajenga uhusiano wa karibu na Mungu.
- Anaonyesha matunda ya Roho.
- Anatumia vipawa vyake vya kiroho katika huduma.
- Ana upendo unaokua kwa Mungu na kwa wengine.
- Anaonyesha sifa njema.
- Amejitoa kwenye mamlaka ya kanisa la mtaa.
- Anaonyesha upendo na kujali kwa hao walio kwenye ushirika wake.
- Anahusiana na wengine kwenye mwili wa waumini.
- Anatumia kanuni za kibiblia kwenye uhusiano.
- Anaweza kutatua migogoro kati ya watu vyema.
- Anawasikiliza wengine na kujibu inavyostahili.
- Anashawishika kwamba Biblia ni neno la Mungu.
- Ana uwezo unaofanya kazi kwenye Agano la Kale na Jipya.
- Anajifunza na kuitumia Biblia.

## II. MAKUSUDIO YA KUFUNDISHA UONGOZI KWA VIONGOZI WA VIKUNDI VIDOGO

Viongozi wa vikundi vidogo pia wanatakiwa kuonyesha uwezo ufuatao na sura za tabia.

- Anaonyesha haja kwa ajili ya roho.
- Anafanya uinjilisti wa binafsi.
- Anahusiana vema na waliopotea.
- Anaweza kutoa injili wazi wazi.
- Anaweza kutoa ushuhuda wazi wa binafsi.
- Ameshafuashwa.
- Anaonyesha kujali wapya waliokata shauri.
- Anaonyesha upendo kwa anaofuasa.
- Anaunda wafuasi ambao watafuasa wengine.
- Anaweza kuendesha majadiliano ya kujifunza Biblia kwa kufata neno.
- Anaelewa hitaji la vikundi kiini kama msingi wa ukuaji wenye afya.
- Anaweza kuendesha kwa ufanisi mkutano wa kikundi kiini.

## III. MAKUSUDIO YA KUFUNDISHA VIONGOZI WA MTAAA

Viongozi wa mtaa pia wanahitaji kuwa na sura na tabia zifuatazo:

- Ni kielelezo cha kufaa kuanzisha ufuasishaji.
- Anaelewa kwamba kanisa ni chombo cha Mungu cha kuinjilisha ulimwengu.

- Anajua misingi ya kibiblia ya upandaji kanisa na misheni.
- Anaweza kutumia njia kadhaa na ujuzi wa uinjilisti.
- Anaweza kufanya utafiti wa kawaida katika utayarishaji wa ukuaji wa kanisa na upandaji.
- Anaweza kuendesha ibada ya hadharani.
- Anafundisha Biblia kiufanisi kwenye kundi au katika maandalizi ya mmoja kwa mwingine.
- Anaainisha na kuendeleza viongozi nyeti wa vikundi kiini.
- Anaweza kusimamia waumini katika kujiongoza wenyewe, kujilisha neno, na kusanyiko lenye mtazamo wa misheni.
- Anaelewa kuweka kazi za kibiblia katika mifumo inayoendana na utamaduni.
- Anajenga na kufanya kazi na timu vema.
- Anajua jinsi ya kugawa majukumu.
- Anaweka malengo, anaweka mipango na kuanzisha matarajio na kuyafikia.
- Anaendeleza vipawa na uwezo wa wengine.
- Ni mstari wa mbele wa utendaji.

## IV. MAKUSUDI YA KUFUNZA UONGOZI KWA KIENEO NA KITAIFA

Viongozi wa kieneo na kitaifa wanatakiwa kufikia kiwango sawa cha tabia na uwezo”

- Anaweza kuhubiri na kufundisha
- Ataweza kutoa uongozi wa kiroho na kutoa ushauri kwenye hali mbali mbali.
- Ana kiwango cha juu cha kuelewa Biblia na Theolojia.
- Anaweza kuwafundisha wafanya kazi wa kanisa uinjilisti, kufuasa, uongozi wa kikundi kiini, uwakili mwema, na kuabudu au maeneo mengine ya huduma kama yanavyohitajiwa.
- Anayejenga na kutumia vikundi kiini  kuenea kwenye jumuia na kuhamasisha mwili wa Kristo.
- Kufafanua tabia ya ukuaji. .
- Anaonyeasha kutafuta wepesi, anawaweka sawa wageni.
- Anaweza kufanya ubatizo na meza ya Bwana.
- Anawakilisha maono ambayo yanawavutia wengine
- Anaweza kuwaongoza wengine katika ugunduzi wa vipawa vyao na kuvitumia katika huduma.

# VIKUNDI KIINI

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 10

# Majadiliano ya Maswali na Matatizo ya Vikundi Kiini

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutoa mda wa majadiliano ya mwingiliano kati ya wafunzwa kuhusiana na matatizo na maswali waliyonayo kuhusu kikundi kiini.

☞ **Wazo Kuu**

- Majadiliano ya mwingiliano wa matatizo hasa ya kikundi kiini.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa baadhi ya maswali ya kawaida ambayo yanaibuka kwenye huduma ya kikundi kiini.
- Kutumia uzoefu wa binafsi kutoa majibu kwa baadhi ya maswali au matatizo ambayo yamejadiliwa.
- Tumia majibu na mapendekezo yaliyotolewa na wafunzwa wengine kusaidia kutatua matatizo au kujibu maswali kwenye vikundi kiini vyake.

☞ **Ushauri kwa wakufunzi**

Somo hili limeandaliwa kwa ajili ya kutoa mda wa majadiliano ya mwingiliano kati ya wafunzwa. Jukumu lako ni moja la mwezeshaji, au msuluhishi, kati ya wafunzwa. Utahitaji kuwauliza wafunzwa matatizo yao au maswali. Usitoe majibu au mapendekezo wewe mwenyewe—ruhusu majibu kutoka katikati ya kikundi, kama inawezekana. Katika tukio lisilotarajiwa kwamba hakuna mmoja wa wafunzwa aliye na maswali wala matatizo, kuna baadhi ya maswali yaliyoshauriwa ya kawaida yaliyotolewa katika somo. Jaribu kutumia uzoefu wa wafunzwa kujibu maswali na matatizo yaliyotolewa wakati wa mda wa somo hili.

Sisitizia kwamba wafunzwa wanahitaji kufikiri juu ya suluhu au mapendekezo ambayo yamejadiliwa na kuonyesha jinsi yanavyoweza kutumika kwenye makundi yao. Watie moyo kuandika njia maalumu za kuonekana ambazo watatumia kutatua baadhi ya matatizo kwenye makundi yao wenyewe.

## I. HALI HALISI YA HUDUMA YA KIKUNDI KIINI

*Max amekuwa akiongoza kikundi kiini kwa zaidi ya miezi mitatu. Ingawa watu sita wanakuja mara moja moja kwenye mikutano ya kikundi kiini, hawaonekani kukua sana katika imani yao, kikundi hakionyeshi haja yoyote ya kufikia watu wanaowazunguka. Wanaonekana wako tayari kukutana kila wiki, kuzungumuzia matatizo yao, na kujifunza Biblia kidogo. Max anaendelea kuchanganyikiwa zaidi na zaidi, na hajui nini la kufanya kitofauti ili kuwasaidia wajumbe wa kikundi chake kuwa wakomavu kiroho zaidi.*

Kama "Max" alivyogundua, huduma ya kikundi kiini inaweza kuwa yote kuleta manufaa au kukatisha tamaa. Wakati mambo yanapokuwa yanakwenda sawa katika kikundi kiini, inaweza kuwa inatosheleza kwa kiongozi wa kikundi kiini. Kwa jinsi hiyo, wakati matatizo yanapoibuka, inaweza kuwa vigumu sana kwa kiongozi kuyafanyia kazi kwa maombi.

Katika kikundi kiini chochote, matatizo yatatokea wakati mmoja au mwingine. Kusudi la somo hili ni kutoa mda wa majadiliano kwa matatizo mbalimbali au maswali ambayo wafunzwa wanaweza kuwa nayo kuhusiana na vikundi kiini vyao. Inatumainiwa kwamba baadhi ya wafunzwa watakuwa wamekutana na matatizo yanayofanana au ugumu na wanaweza kuwa na baadhi ya

mapendekezo kwenye kikundi. Kama maswali yanaibuka ambayo hayana majibu rahisi, kikundi kinaweza kutumia mda kadiri inavyotakiwa kujadili suluhu linalowezekana au majibu ya maswali hayo.

## II. MASWALI NA MATATIZO

Anza kujadili matatizo au maswali kwenye kikundi kiini chako. Mkufunzi atawajibika kuamua mda wa majadiliano. Kama kundi la wafunzwa wamekuwa na mafanikio mazuri kupita ya vikundi vyao na hawana matatizo, orodha ifuatayo inaweza kutumika kujadili maeneo hayo ya matatizo kwenye huduma ya kikundi kiini. Kumbuka, orodha hii iko tu kwenye tukio ambalo wafunzwa hawana maswali zaidi au matatizo ya kujadili:

- Kikundi kiini hakikui kiroho.
- Kiongozi hawezi kupata kiongozi mwanafunzi.
- Kikundi kiini hakiongezeki chenyewe.
- Kikundi kiini hakipati sehemu nzuri ya kukutana.
- Kikundi kiini hakikui kiidadi.
- Baadhi ya migogoro inakuwepo kati ya wawili au zaidi wa wajumbe wa kikundi, na kiongozi anaonekana hawezi kulitatua hilo.

## III. SULUHU

Kila kikundi kiini ni tofauti, na kila hali ya tatizo ina tabia ya kipekee. Hata hivyo, mara nyingi kuna kanuni za kawaida zinazoendana au sababu ya matatizo. Kila kiongozi wa kikundi kiini antakiwa kusikiliza kwa uangalifu kwenye mapendekezo au utatuzi uliotolewa wakati wa mda wa majadiliano wa somo hili. Kama inawezekana, anatakiwa afikirie jinsi ya kutumia kanuni za utatuzi uliotolewa kwenye kikundi kiini chake mwenyewe kama anakutana na tatizo lile lile.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni tatizo lipi ni kubwa au udhia kwenye kikundi kiini chako? Suluhu na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa mda huu wa darasa unaoweza kutumia kusaidia kutatua tatizo hili?
- Unafahamu viongozi wengine wa kikundi kiini ambao hawakuwa katika darasa hili lakini ambao wanaweza kufaidi kutoka kwenye mda huu wa majadiliano? Jinsi gani unaweza kuwatia moyo na kushirikishana baadhi ya vitu ulivyojifunza?
- Nani unayeweza kumzungumzia matatizo yanayoendela au yajayo katika vikundi kiini?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Andika matatizo makuu matatu unayokutana nayo kwenye kikundi kiini chako.
- Kutokana na majadiliano ya leo, andika angalau suluhu mbili zinazowezekana kwa kila moja ya matatizo.
- Omba kwa ajili ya hekima katika kuweka utatuzi ambao umemaliza kuandika. Panga kuyaweka mapema iwezekanavyo.

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 11

# Kuzidisha kwa Kikundi Kiini

**Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuandaa wafunzwa kwa ujuzi na ufahamu ambao ni wa lazima kuweza kuwezesha kuzidisha katika kikundi kiini.

**Wazo Kuu**

- Kuzidishwa katika vikundi kiini ni matazamio.
- Vishada vinawezesha utaratibu wa kawaida wa mgawanyo wa kiini na kuzidisha.

**Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa kwa nini ni lazima kwa kikundi kiini kuzaliana chenyewe.
- Kuelewa jinsi ya kutumia “vishada” kusaidia katika utaratibu wa kuzidisha.
- Kujifunza jinsi ya kushughulika hasa na vizuizi kadhaa, ambavyo vinaweza kufanya ugumu kwa kikundi kiini kuzidi.

## I. LENGO LA KUZIDISHA

Kundi lilikuwa linakutana pamoja kwa mara ya mwisho. Mambo yasingekuwa mabaya. Viongozi wao walikuwa wanaondoka, kiongozi mwanafunzi alikuwa si wa kutegemewa, wengine katika kikundi walikuwa wakizozana na kushindania nafasi iliyojitokeza, na mjumbe mmoja alikuwa karibu kujiweka kwenye kuiba fedha za amana, ufujaji, na kujitoa kwenye ufalme. Kushindwa na hofu kuligubika anga la chumba kiongozi aliposimama kuongea. Alisema,

"*Usiache moyo wako kusumbuliwa. Mtumaini Mungu . . .*"

Kiongozi alikuwa Yesu, kikundi kiini kilichokuwa hakijapangiliwa ilikuwa wafuasi kumi na wawili, na mkutano ulifanyika mara tu kabla ya masaa yake ya kukamatwa, kujaribiwa na kushitakiwa. Bila kujali uharibifu uliokidhi wa maadili ya kikundi hiki wakati wa hatua ya kuzidisha, kwa nguvu za Roho Mtakatifu, kilisalimika kuongezeka mara dufu tena. Kati kati ya kizazi, idadi yake ilikuwa imeongezeka kwa nguvu kujaza falme ya Urumi.

Kwa njia sawa, kila kikundi kiini kinachokaribia hatua ya kuzidi kinahitaji kufikiri maneno ya Yesu: “*Usiache moyo wako kusumbuliwa. Mtumaini Mungu...*" (Jn 14:1).

> Hatima ya lengo letu katika huduma ya kikundi kiini ni utimizaji wa Utume Mkuu.

Haijalishi ni kwa ugumu gani mpito huu unaweza kuonekana, Kuzidisha katika kikundi kiini ni kwa ajili ya ukuu wa ufalme wa Mungu. Hatima ya lengo letu katika huduma ya kikundi kiini ni utimizaji wa Utume Mkuu. Njia yetu ya kukabili lengo hilo ni kupitia vikundi kiini ambavyo vinainjilisha, kufuasa waumini, kuandaa viongozi, na kuzaliana. Bila kuzaliana, lengo hili kamwe halitafikiwa.

Imeelezewa kabla kwamba vikundi kiini vinaweza kutumika kama "matofali ya kujengea" kwa mkakati wa huduma kubwa. Vikundi kiini vinavyozaliana vyenyewe vinaweza kutumika kuimarisha makanisa yaliyopo na kuanzisha makanisa mapya. Kwa njia hii, vinaweza kutumika kama msingi kwa mkakati wa upandaji kanisa. Kwa njia sawa, kuzidisha vikundi kiini kunafanya uwezekano siyo tu kuona makanisa mapya yameanzishwa, lakini pia kusaidia kuanzisha na kuendeleza harakati za kueneza upandaji kanisa katika eneo na taifa. Kikundi kiini kiasili kinachangia "shughuli za msingi" za uinjilisti, kufuasa na maendeleo ya uongozi ambayo ni ya lazima ili kuona harakati za makanisa mapya zimeanza.


Kwa njia nyingi, kuzidisha ni ncha ya juu ya juhudi za miezi mingi kwenye kikundi kiini. Ni tukio muhimu kwa ajili ya kikundi, na moja ambayo inatakiwa kutiwa moyo na kusherehekewa. Ingawa kuna vitu vingi ambavyo kiongozi wa kikundi kiini anaweza na anatakiwa kufanya kuandaa kundi kwa ajili ya kuzidisha, pengine la muhimu zaidi kwa kifupi ni kumtumaini Mungu, kwamba ataongoza kundi moja kuwa mawili. Kwa nguvu zake na kwa uongozi wa Roho mtakatifu, Kuzidisha ni utaratibu ambao utatokea zaidi na zaidi tena kwenye vikundi kiini.

## II. UTARATIBU WA KUZIDISHA "KIASILI"

### A. Kuzidisha kwa Kibaolojia

Katika Bioloji, kiini kinazaliana kwa utaratibu wa kukua na kujitoa kopi chenyewe. Kila kiini kina kitovu (kinachoonyeshwa kama "N" katika Kielelezo 11.1), ambacho kinatawala shughuli za kiini. Kadiri kiini kinavyolishwa na kukua, kitovu kimoja kinaanza kukua na kuendelea kuwa sehemu mbili. Wakati kiasi cha ukuaji sahihi kinapotokea, kiini kimoja kinazaliana kuwa viwili, kila moja na kitovu chake. Utaratibu huu wa ukuaji na kujitoa kopi unaendelea zaidi na zaidi tena, kadiri kiini kinavyoendelea kulishwa na kinaweza kukua.

**Kielelezo 11.1. Kuzidi kwa Kiini Kibaolojia**




Kuzaliana katika vikundi kiini vile vile kunatokea katika njia sawa na ya kuzaliana kibaolojia. Kila kikundi kiini kina kiongozi, anayetoa "hali" inayofaa kwa kundi kukua na kulishwa. Kama kikundi kiini hakikulishwa neno na kuendelezwa (yaani ukuaji wa kiroho na kufikia nje kiunjilisti), kundi halitakua. Kiongozi anatoa mfano, mafundisho, na kichocheo kwa wajumbe wa kundi kufikia nje kwa watu wanaowazunguka. Kupitia utendaji wa Roho Mtakatifu, marafiki na watu hawa wa karibu wanaletwa kwenye kundi na kupata nafasi ya kujifunza kuhusu Yesu na kumpokea kama mwokozi wao.

Kadiri kikundi kiini kinavyokua katika ukomavu, kiongozi wa kikundi kiini vile vile anaanza kufanya kazi na kiongozi mwanafunzi. Kiongozi huyu mpya anajifunza kutoka katika maneno na matendo ya mshauri wake, na kwa njia nyingi anageuka kuwa mwigaji (1 Kor. 11:1) wa mshauri. Wakati kiongozi mwanafunzi anapokuwa ameandaliwa kiroho na kimwili kuongoza kundi lake mwenyewe, kikundi kiini cha kwanza kitazidi kuwa makundi mawili. Kila kundi linakuwa na kiongozi wake, kinaweza kuanza utaratibu wa kukua na kuzidi tena.


> Wakati kiongozi mwanafunzi anapokuwa ameandaliwa kiroho na kimwili kuongoza kundi lake mwenyewe, kikundi kiini cha kwanza kitazidi kuwa makundi mawili.

Mungu aliumba viini vya kibaolojia kwa kusudi na uwezo wa kujitoa kopi vyenyewe. Kwa jinsi hiyo, bila kuwa na hali inayofaa kwa ukuaji na maendeleo, hili halitaweza kutokea, na hatimaye viini vitakufa. Vikundi kiini vile vile vina umaarufu wa kukua, kuendelea na kujitoa kopo vyenyewe. Kwa njia sawa kama za kibaolojia, bila kuwa na hali inayofaa, hili halitatokea katika kikundi kiini.

### B. Vishada vya Asili

Fikiria kikundi kiini mahali ambapo kiongozi anashikilia machungwa mawili makubwa yaliyojaa maji mengi ya machungwa. Anawaomba watu wawili wa kujitolea kutoka kwenye kundi kwa kila mmoja kumenye moja ya machungwa na kisha kuligawa katika sehemu mbili. Kwa jinsi hiyo, kila mmoja atatumia njia tofauti kufanya hili. Mtu wa kwanza ataligawa chungwa lake kati kwa mapana, kwenye mstari wa ikweta. Mtu wa pili lazima aligawe chungwa lake kwa marefu kutokea kaskazini kuteleka kuelekea mstari wa kusini, kwenye alama ya kiasili ya chungwa.

**Figure 11.2 Gawanya Chungwa**




Unaweza ukafikiri nini kitatokea kwa kila chungwa. Mstari sambamba unaweza ukachorwa kwa kila kinachoweza kutokea kwenye vikundi kiini unapokuwa mda wa kuunda makundi mawili kutokana na moja. Kundi linameguka, bila kuangali kwa karibu kutokea kwa urafiki kiasili kati kati ya kundi, kunaweza kukafanya machafuko. Kama unaligawa kundi bila utaratibu, kwa idadi, kimipaka ya kijiografia, au kwa njia zingine mbali na uhusiano wa asili, unaweza kuishia na wajumbe wengi wa kundi waliojeruhika.

Kwa jinsi hiyo, kama unaainisha kutokea kwa urafiki wa vishada kiasili katikati ya kundi lako na kisha ukaligawa kundi kwa vishada hivi, matokeo yatakuwa yenye faida zaidi. Kutia moyo kutokea kwa vishada hivi, anza mapema katika maisha ya kundi kufanya uchunguzi wa mchanganyiko tofauti. Chunguza jinsi wajumbe wako kiasili wanavyogawanyika kwenye makundi madogo zaidi ya wajumbe watatu, wane, au watano. Tambua nani amezidi na kwa nani, na nani amechukua uongozi. Jaribu hili kwa mda wa wiki tatu au nne kuona kama vishada vyovyote maalumu vinaendelea kiasili.

> Ainisha kutokea kwa urafiki wa vishada kiasili katikati ya kundi lako na kisha ukaligawa kundi kwa vishada hivi.

Unaweza ukataka kupanga kwa ajili ya kutokea kwa makundi haya madogo zaidi kwa kuchora mchoro wa mahusiano haya. Ni kundi lipi la watatu, wane, au watano linafanana zaidi?. Nani wana watoto wenye umri sawa? Kazi zinazofanana? Mapendeleo sawa? Ambaye amewahi kuanzasha mahusiano nyuma au mtandao wa mahusiano? Unaweza ukaruhusu vikundi hivi vidogo zaidi kujiunda vyenyewe, au unaweza kuwatia moyo watu fulani katika kikundi kiini kuunda vijikundi kufuatana na kile unachojua kuhusu hadhi zao na mapendeleo yao. Vishada vitakuwa, kwa maana ya "viini vidogo." Utataka kukutana kama kundi kubwa kwa mikutano mingi ya kikundi kiini, lakini mnaweza kugawanyika kwenye vishada kwa ajili ya kujifunza Biblia, maombi au kushirikishana.

Kiongozi wako mwanafunzi anatakiwa ama kiasili, au kwa mapendekezo yako kuanza kufanya kazi na moja ya vishada. Kama kuna vishada kadhaa katika kikundi kiini chako, mfanye kiongozi wako mwanafunzi kufanya kazi na kishada kinachoonekana kuwa na umaarufu mkubwa wa kuwa "binti" mpya wa kikundi kiini. Kwa kuhusika, kiongozi mwanafunzi ataendeleza uhusiano wa karibu sana na wajumbe hawa na atakuwa ameandaliwa vyema kuwaongoza wakati utakapokuwa mda wa kuanzisha kundi mpya. Hili pia linachangia kwenye uangalizi mzuri wa kichungaji kati kati ya kundi lako. Watu wengi wataongea kwa uhuru zaidi katika makundi madogo zaidi ya watatu mpaka watano kuliko ambavyo wangefanya mbele ya kundi kubwa la watu kumi au zaidi. Kuwabadilisha watu katika vishada kunamaanisha kwamba kukosekana kwake kutagundulika kiharaka zaidi. Watatambua kuwa kuwepo kwao kunahitajika, na wataguswa na wengine kwa namna kwamba watajitoa zaidi kwenye kundi.

Vishada pia vinaweza kusaidia kutambua viongozi wanafunzi mashuhuri. Uzoefu umeonyesha kwamba katika kikundi kidogo cha watu, mtu mmoja kawaida atajitokeza kiasili kama kiongozi kunapokuwa hakuna mmoja wapo aliyekabidhiwa wajibu. Kiongozi wa kikundi kiini anapokuwa anafikiria nani anaweza kuwa kiongozi mwanafunzi kimaombi, anaweza kuchunguza vishada kuona ni wajumbe gani wanaoibuka kiasili kama "viongozi" wa vishada. Kuna watu ambao viongozi wanatakiwa kuwaombea na pengine kuwakabili kuhusu kuwa kiongozi mwanafunzi

### C. Hatua Kwenye Kuzidisha

Kuzidisha katika kikundi kiini kunatambulika—kiongozi na wajumbe wa kundi lazima watenge lengo hili mbele yao wenyewe, na kwa juhudi kulifanyia kazi kuelekea kulitimiza lengo hilo. Hii ni njia pekee ambayo kuzidisha kutaonekana kama sehemu ya asili ya mzunguko wa maisha ya kikundi kiini. Kama kiongozi wa kikundi kiini hafanyi kuzidisha kama kipaombele, wajumbe wa kundi hawatalifanya kuwa kupaombele, wala.

*1. Kuandaa Kabla kwa Ajili ya Kuzudisha kwa Kikundi Kiini*

Kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kuandaa kiini kwa ajili ya kuzudisha katika maisha yote ya kiini. Ili kuweza kutoa "hali" inayofaa kwa ukuaji na kuzidisha kwa kikundi kiini, kiongozi ana majukumu kadhaa:

- Kiongozi lazina atoe maono kwa <u>kuendelea</u> kwa wajumbe kwamba kikundi chao kimoja kitaendelea na kuwa viwili. Maono haya lazima yaanze kundi linapoanza, siyo wiki kadhaa kabla ya mda wa kuzidi. Anatakiwa aelezee kwa nini kuzidisha ni kuzuri na kwa lazima kusaidia kutimiza agizo ambalo Kristo alitupa la Utume Mkuu.
- Kiongozi lazima alitie moyo kundi kuwafikia nje wasioamini katika mitandao yao ya mawasiliano. Bila ukuaji wa kihesabu, hitaji la kuzidisha linaweza lisiwe wazi wazi.
- Kiongozi lazima atoe mazingira katika kundi mahali ambapo ufuasishaji unatokea kati kati ya waumini. Bila ukuaji wa kiroho, hitaji la kuongezeka linaweza lisieleweke wazi wazi.
- Kiongozi lazima amshauri kiongozi mwanafunzi atakayechukua jukumu la kuongoza moja ya makundi mawili. Mda wa kuzidisha unapokaribia, kiongozi mwanafunzi lazima aanzishe lengo la jumla la kundi lake mpya, vile vile na mpango wa angalau mikutano kadhaa ya kwanza. Kiongozi anatakiwa aliangalie hili pamoja na mwanafunzi na kutoa ushauri au mapendekezo.
- Lazima kuwe na tarehe iliyopangwa lini kuzidi kutatokea. Kiongozi lazima aliwajibishe kundi katika kukamilisha utaratibu wa kuzidisha kwenye au karibu na tarehe hiyo.

2. *Uwekaji wa Kuzidisha kwa Kikundi Kiiniu*

Kwa kudhani kuwa kiongozi wa kikundi kiini amefanya mambo yote haya, jinsi gani kikundi kiini hasa kitazidi?

- Jadili mabadiliko yanayokuja na kundi. Watu ambao hawajawahi kamwe kuwa kwenye kundi lililozidi watakuwa, katika kiwango kinachopishana, wenye kutazamia kuhusu kuzidisha. Kimakosa wanaamini kwamba uwezo wa kikundi kiini ni pamoja na nani anahusika kwenye kundi badala ya kwa nani kundi linahusika. Chukulia hofu zao bila mzaha na wasaidie katika hilo. Wakati wa utaratibu wa kuzidisha, SIKILIZA, OMBA, & TIA MOYO. Fanya kila uwezalo kuondoa kukatishwa tamaa au kuchukulia vibaya kusiwe nguvu inayotawala. Soma na tafakari Yohana 14-17 kupata utambuzi wa kiroho juu ya Jinsi Yesu alivyofanya kwenye hatua ya kuzidisha na kundi lake la wanafunzi.
- Onyesha kundi lipi litaongozwa na nani. Katika hali zingine, wakati kikundi kiini kinapozidi kiongozi mwanafunzi anakuwa kiongozi wa kikundi kiini “binti”. Kwa jinsi hiyo, kwa ujumla hili linategemeana na kundi lenyewe, na linakubalika tu na kiongozi wa kikundi kiini kilichopo kuanza kufanya kazi na kundi jipya, wakati kiongozi mwanafunzi anakuwa kiongozi wa kundi la awali. Hili wakati mwingine linafanya kazi vizuri wakati wajumbe wa kundi jipya wanapokuwa hawajakomaa kiroho kama walivyo wajumbe wanaoendelea kukaa na kundi la awali.

> Wakati mwingine, wakati kikundi kiini kinapozidi, kiongozi mwanafunzi anakuwa kiongozi wa kikundi kiini “binti”.

- Amua nani ataungana na kundi jipya na nani atabakia kwenye kundi la awali. Kiongozi wa kikundi kiini anahitaji kuwauliza wajumbe wa kundi kuomba na kuamua ni kundi lipi Mungu anawataka kuwa sehemu yake. Hawatakiwi kuuliza ni <u>kiongozi</u> yupi watampenda zaidi. Hili linaweza kuleta mashindano, kutokuwa na umoja, kuhangaika na hali isiyoridhisha kwa kila aliyehusika. Kiongozi anatakiwa asidhanie bila kuwa na uhakika au kuchagua ni wajumbe wapi waende na makundi yapi. Mapendekezo yoyote yanatakiwa yafanyike kwa uangalifu bila hata muonekano wa kulazimisha au uonevu. Mtegemee Roho Mtakatifu kuyapangilia makundi kwa njia anazotaka.
- Chagua sehemu ya kufanyia mkutano wa kikundi kipya. Kundi jipya linahitaji kuamua wapi litakutana. Hapa panaweza kuwa nyumbani kwa kiongozi mpya au nyumbani kwa mjumbe mmojawapo wa wajumbe wa kundi jipya. Ni muhimu kuamua juu ya mahali na kufanya mipangilio ya kupatumia. Wajumbe wa kundi jipya wanahitaji kujisikia hali ya uimara, usalama, na kuhusika kwenye sehemu ambayo watakutana pamoja.
- Panga kukutana na kiongozi mwanafunzi kuendelea kumshauri kwenye kundi jipya. Kiongozi wa kikundi kiini lazima apange kutumia mda pamoja na kiongozi wake mwanafunzi baada ya kuzidisha kutokea. Wiki kadhaa za kwanza na miezi ya kikundi kiini kipya itakuwa migumu zaidi kwa kiongozi mpya. Kuwa na mshauri karibu wa kuomba naye na kujadili naye matatizo utakuwa msaada mkubwa sana kwa kiongozi wa kikundi kiini kipya.
- Kama kundi, amua tarehe ya mwisho ya mkutano wa kundi la awali itakuwa lini, na panga kuisherehekea! Fanya marudio na toa shukurani kwa vitu vyote ambavyo Mungu amefanya kwenye na kupitia kikundi. Ombeaneni na ombea vikundi vyote kwa wakati ujao. Furahia kwamba kupitia vikundi, watu wengi wanaweza kufikiwa kwa upendo wa Kristo. Waonyeshe kundi umuhimu wa hatua hii katika kusaidia kutimiza Utume Mkuu. Uwe na “usimikaji” maalumu wa kiongozi mpya na wajumbe wa kundi—wakusanye kwa pamoja na omba kwa ajili yao, kwamba Mungu atawatumia kinguvu katika kundi lao mpya.

Kila wakati kikundi kiini kipya kinapoanzishwa, kiasili kunakuwa na mashaka fulani, hofu na kutokuwa na uhakika. Vipi kama kundi jipya siyo "zuri" kama kundi la awali? Nini kitabadirika? Jinsi gani mahusiano yatakuwa tofauti? Ni muhimu kukumbuka kwamba kundi jpya litakuwa na tofauti kubwa kutoka lile la zamani. Usitarajie kwamba kilakitu kitakuwa sawa kama kilivyokuwa kwenye kundi la awali, kwa sababu haitakuwa. Roho Mtakatifu anapenda kufanya kazi katika maisha ya waumini kwenye kundi jipya kwa njia tofauti na maalumu.

Pengine la muhimu zaidi kwa kifupi ni kutumaini kwamba Mungu anasimamia na kwamba ataongoza na kuaelekeza yote kundi la zamani na jipya. Yesu alisema katika Yohana 14:27, "Amani yangu nawaachia, amani yangu nawapa. Siwapi kama ulimwengu uwapavyo. Usiruhusu moyo wako kusumbuliwa na msiogope." Haya ni maneno ya kuishi kwa kuayafata, na hasa nyakati ambazo kikundi kiini kinapokuwa kimefikia ngazi ya kuzidisha.

## III. VIZUIZI KATIKA KUZIDISHA

Somo la kuzidisha vikundi kiini linafurahiwa zaidi miongoni mwa wajumbe wa kikundi kiini na viongozi. Aina mbili za nguvu katika vikundi kiini zinachochea vita dhidi ya kimoja kwa kingine. Ya kwanza ni ukweli kwamba kuzidisha kundi ni kwa afya kwa yote makundi na ufalme. La pili ni ukweli kwamba , kuachwa katika njia zake vyenyewe, vikundi kiini vichache kamwe vitaweza kuzidi. Kuzidisha kunaeleweka kama tukio mashuhuri la kuumiza, mgawanyiko ambao unaumiza mahusiano. Watu wanataka kuwa pamoja na kubakia pamoja. Mara chache wanatambua kuwa kundi linalokazania kwa wajumbe wake peke yake na mahitaji litachakaa au kufa kati kati ya mwaka mmoja au miwili.

Kuachwa katika njia zake vyenyewe, vikundi kiini vichache kamwe vitaweza kuzidi.. Watu wanataka kuwa pamoja.

Katika kikundi kiini chochote, kuna baadhi ya vizuizi vya kawaida ambavyo vinaweza kuzuia kuzidisha kutokutokea. Mchoro ufuatao unaelezea baadhi ya vizuizi hivi, na kutoa mapendekezo kwa kiongozi wa kikundi kiini ya jinsi gani anaweza kuvishinda. Hakika, kunaweza kukawa na baadhi ya vizuizi au vipingamizi ambavyo ni vya kipekee kwa utamaduni wako au mandhali. Kama ni hivyo, jaribu kufikiri kuhusu jinsi gani ungeweza kuvishinda vizuizi hivyo ili kwamba kuzidisha kuweze kutokea kwenye vikundi kiini vyako.

**Kielelezo 11.1 Vizuizi kwenye Kuzidisha kwa Viini**

| Tatizo | Mapendekezo |
|---|---|
| Kundi halielewi umuhimu wa kuzidisha. | • Kiongozi wa kikundi kiini lazima asitoe tu maono ya kuzidisha, lakini lazima pia aeleze kwa nini kuzidisha ni muhimu hivyo. Wajumbewa kikundi kiini lazima waelewe ni faida zipi zipo kwa ajili ya kundi na kwenye kuendeleza ufalme wa Mungu. |
| Kundi linaelewe hitaji la kuzidi, lakini wameridhika na mmoja kwa mwingine na hawataki kugawanyika. | • Omba kwamba Roho Mtakatifu atakupa hekima katika kulielewa kundi lako na hali yako ya kipekee.<br>• Kazia umuhimu wa kuzidisha na elezea kwamba ni hatua inayofata katika mwendelezo wa asili wa maisha ya kundi.<br>• Toa kielelezo cha jinsi gani kuzidisha kumekuwa utii kwenye amri ya Mungu ya "kwenda na kufanya wanafunzi" katika Mt. 28:19. Kupitia kuzidisha, kikundi chako kiini kina wajibu muhimu na bayana katika kusaidia kutimiza Utume Mkuu.<br>• Omba kwa ajili ya kugawa kundi katika mipaka ya asili, ukitumia sura ya vishada. |
| Hakuna kiongozi mwanafunzi. | • Kwanza, kiongozi wa kikundi kiini lazima atumie mda katika maombi, akimuonmba Roho Mtakatifu kumpa hekima juu ya nani wa kuchagua. Kisha, kimakusudi anatakiwa afanye uamzi huu na kuanza kufuasa na kushauri mwanafunzi.<br>• Tumia vishada katika kikundi kiini chako kuweza kuainisha kiasili viongozi wanaoibuka. Omba kwa ajili ya watu hawa kama viongozi mashuhuri wanafunzi kwa ajili ya kundi jipya.<br>• Katika mipaka ya kuchagua kiongozi mwanafunzi, fanya marudio ya Somo la Kikundi Kiini katika Mwongozi wa 3, "Kuwafunza Viongozi Wapya wa Kikundi Kiini" |
| Kuna kutokuelewana nani aenda na kundi lipi. | • Kama kundi lako lina vishada kadhaa, fikiria kutumia kishada kimoja au zaidi kuanza kundi jipya. Fikiria mipaka ya mahusiano ya asili kwenye kundi.<br>• Muombe kila mjumbe wa kundi kuomba na kumuomba Roho Mtakatifu kuliweka wazi kwake juu ya kundi lipi la kuweza kujiunga.<br>• Endesha majadiliano wazi ya kweli kwenye mkutano wa kikundi kiini kutafuta sababu ya kukosekana kwa umoja kwenye uamzi huo. |
| Wajumbe wa kikundi kiini wanajisikia kana kwamba mwanafunzi hajawa na sifa za kuwa kiongozi wa kikundi kiini. | • Subiri kuanzisha kundi mpaka kiongozi mwanafunzi anapokuwa tayari.<br>• Muhusishe mwanafunzi katika kila sura ZOTE za huduma pamoja nawe.<br>• Mfanye mwanafunzi kufanya zaidi na zaidi ya kazi za huduma katika kundi. Mfanye kiongozi kufanya huduma kidogo zaidi.<br>• Tenga tarehe mpya ya mwanafunzi kuwa kiongozi wa kikundi kiini na kazana kumwendeleza kiakili, kihisia, na kiroho kabla ya mda huo. |

Kunaweza kukawa na vizuizi kwenye uzidishaji katika kikundi kiini chochote, lakini kama kiongozi anafikiria uwezekano wa matatizo kabla na kuyafanyia kazi ya kukabili vizuizi hivyo kabla havijawa tatizo, vingi vya vizuizi hivyo vinaweza kuepukwa vyote kwa pamoja. Kitu kikubwa ambacho kiongozi anaweza kufanya kabla ni kuendelea kuweka maono na faida za kuzidisha mbele ya kundi tangu siku ya kwanza.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani kuzidisha katika vikundi kiini kunasaida kuendeleza kueneza harakati za upandaji wa kanisa?
- Nini ni "vishada vya asili" katika kikundi kiini? Jinsi gani vinaweza kutumika kusaida kundi kuhamia kwenye ngazi ya kuzidisha? Nini kinaweza kutokea kundi linapokuwa tayari kuzidi na wajumbe wa kundi lake wamegawanyika bila utaratibu, pasipo na kufikiria mahusiano katika kundi?
- Jinsi gani vishada vinaweza kutumia kusaidia kugundua viongozi mashuhuri wa vikundi kiini?
- Ni vizuizi vipi vya kawaida kwenye kuzidisha katika kikundi kiini? Jinsi gani vinaweza kushindwa?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Vishada katika kikundi kiini wakati mwingine vitaibuka kiasili tu, Kama vikundi vyako havina tayari vishada ndani yake, fikiria kuvitumia wakati wa sehemu tofauti za mkutano wa kikundi kiini. Unaona faida yoyote ya kutumia vishada katika makundi yako?
- Anza kufikira nini kinatakiwa kitokee katika kila moja ya makundi yako ili kufikia lengo la kuzidisha. Andika vitu vitano ambavyo utafanya katika miezi mitatu ijayo ili kuyasogeza makundi yako karibu na kwenye kuzidisha.
- Fikira juu ya vizuizi mashuhuri kwenye kuzidisha katika kila moja ya makundi yako. Nini unachoweza kufanya kabla ya mda kuvishinda na kuepuka matatizo unapokuwa mda wa kuzidisha?
- Anzisha mpango wa kuzidisha katika makundi yako. Hakikisha unawaweka viongozi wako wanafunzi kwenye utaratibu huu ili kwamba nao waweze kuandaliwa kupanga kwa ajili ya kuzidisha kwenye makundi yao. Omba kwa ajili ya kuzidisha na weka pamoja na tarehe ya kuzidisha katika mpango wako kwa kila kundi. Tafuta mtu fulani atakayekuwajibisha katika uwekaji wa mpango huu wa kuzidisha.

### VYANZO


- Portions of this lesson were quoted with permission from an article entitled, *Multiplication* by Dan Smith (Small Group Network, 1996. http://smallgroups.com).
- Logan, Robert. Multiplication of Cell Groups. Old Tappan, NJ: Fleming H. Revell Co., n.d.

# KUFUASA

UFUASISHAJI

SOMO 6

# Warsha ya Ufuasishaji

## MAJADILIANO YA MASWALA YA VITENDO YANAYOHUSIANA NA KUFUASA

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwaruhusu wapanda kanisa kuingiliana katika kila maagizo katika njia hii na maswala mengine ya kivitendo yanayohusiana na kufuasa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuwa na upana wa kuelewa kwa maswala ya kivitendo yanayohusiana na kufuasa.
- Kuwa na heshima kuu kwenye ubunifu ndani ya mwili wa Kristo katika kushughulikia yanayohusu kufuasa.
- Kuwa na mvuto wenye nguvu wa umuhimu wa ukaguzi na upangaji katika kuendelea kwa utaratibu wa ufuasishaji.
- Uwe na maandishi ya mpango ya kuanzia mkononi ya kufuasa waumini ambao anawahudumia.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Uwe na hakika kumpa ushauri mtu anayewajibika kuandaa kipindi cha mafunzo ya Mongozo wa Nne kwamba wafunzwa wote lazima walete mpango wao wa ufuasishaji uliokamilika kuweza kuingizwa kwenye mafunzo ya Mwongozo wa Nne. Zana hii itaunda msing wa majadiliano yaliyofanyika katika nusu ya kwanza ya somo hili.

Pia mpe ushauri mtu anayewajibika kwa ajili ya kuandaa vipindi vya mafunzo ya Mwongozo wa Nne kwamba wakufunzi wote wanatakiwa kuwa tayari kushiriki katika warsha ya kufanya ufuasishaji katika nusu ya pili ya saa. Warsha hii ya swali na jibu lazima ishughulikie maswali ya kiutendaji kutoka kwa wapanda kanisa. Katika tukio kwamba wapanda kanisa hawatakuwa na maswali, wakufunzi wanatakiwa wawe tayari kutoa maoni kwenye maswali yaliyomo kwenye somo hili.

Unda vibao vya matangazo au mashine ya kuonyeshea maandishi ubaoni tupu ya Mpango **wa Kufuasa** (kutoka Ziada 5A, Mwongozo wa Tatu) ya kukamilisha wakati wa majadiliano ya kundi kubwa. Hili linaweza kuhitajika kama majadiliano ya kundi dogo hayawezekani kwa sababu ya kumaliza vibaya kazi iliyokuwa imetolewa. Ni ya lazima kwamba wafunzwa wanafanyia kazi utaratibu na kufikiria maswala na mfuatano wa kufanya ufuasishaji. Ili kufanya matumizi mazuri ya mda uliotolewa kwa ajili ya kipindi hiki katika kufanya ufuasishaji, ni muhimu kwamba washiriki wanahamia kwa haraka kwenye makundi madogo ya watu 5 mpaka 8.

Kwa kusudi la kutolea kielelezo, wapanda kanisa wanatakiwa kuwa na mpango wao wa kufanyia ufuasishaji mkononi walioandaa wakati au baada ya Mafunzo ya Mwongozo wa Tatu.

### I. MAJADILIANO YA VIKUNDI VIDOGO (NUSU SAA)

Ruhusu nusu saa kwa ajili ya mwingiliano katika utaratibu na matokeo ya kuanzisha mpango wa ufuasishaji kwa ajili ya kila mmoja na ushirikiano. Chagua mmoja wa kuchemsha majadiliano, kwa kutumia maswali yafuatayo kama kiongozi. Jaribu kumuhusisha kila mmoja kwenye majadiliano.

1. Umekuta zoezi hili kivitendo likifaa kutumika katika huduma yako? Jinsi gani?
2. Jinsi gani umeonyesha utaratibu ambao ungetumia kugusia maswala?

3. Ni vitu gani vya ufatiliaji (ujuzi sura, au thamani) unavyoamini lazima viwemo katika miezi ya kwanza ya maisha ya mkristo? Kwa nini haya ni muhimu sana? Jinsi gani unaweza ______ (kuchukua kitu kimoja) ambacho kinaweza kuendelezwa zaidi katika maisha ya muumini au kanisa?
4. Jinsi gani wewe binafsi ulishawishiwa na umuhimu wa ______ (maswala/ukweli/ujuzi au sura)?
5. Ni mifumo ipi ambayo unaridhika nayo zaidi?
6. Umejaribu kuwianisha mifumo ili kwamba mmoja au miwili isitumike zaidi au kuachwa?
7. Unafanya nini kueneza kazi ya kufanya ufuasishaji mahali ulipo? Jinsi gani unaandaa “wafuasishaji”?
8. Nini utafanya wiki ijayo kuwasogeza wanafunzi mbele kwenye imani yao, tumaini na upendo?

## II. UONGOZI WA KITUMISHI

Tunaweza kwa ujumla kutarajia kwamba hali halisi ya mazoezi ya huduma, ikiunganishwa na msisimko wa mazingira ya mafunzo, yataanzisha ndani ya wapanda kanisa njaa ya kujifunza zaidi kuhusu jinsi ya kufanya wanafunzi. Kama wapanda kanisa wanasita kuuliza maswali, kwa jinsi hiyo, yafuatayo yanaweza kusaida kutamanisha hamu zao.

1. Elezea tukio, mkasa au shughuli ambayo ulikuwa umehusika mwanzoni mwa maisha yako ya ukristo ambayo bila mashaka ilikusaida kuendelea katika kutembea kwako na Kristo.
2. Ni kipande kipi cha ukweli unachoweza kurithisha kwa hao wanaoanza kufanya wanafunzi?

## III. SULUHU (DAKIKA 3)

Hili ni somo la mwisho katika njia ya ufuasishaji ya mafunzo ya wapanda kanisa. Katika njia hii, , tumefikiria kuleta kwenye utayari wako umuhimu wa kimkakati wa ufuasishaji katika utaratibu wa upandaji kanisa. Tumeangalia ufuasishaji kwa namna ya ufuatiliaji wa msingi na kumwandaa Bibi arusi wa Kristo wa milele. Tumeona shabaha ya ufuasishaji. Tumezungumzia hitaji la kuchunguza hali ya sasa ya kiroho ya mtu pekee au kanisa. Tumetambulisha zana ya kupanga kufikia mahitaji haya kiutendaji, na kuandaa nafasi kwa ajili yako kuanzisha na kujadili mpango wako mwenyewe.

Tunakutia moyo kuendelea kufikiria ufuasishaji kama njia ya kuzaliana mwenyewe katika maisha yako na ya wengine na kuzidisha wafanyakazi wanaoweza kwa ajili ya kufikia kijiji chako, miji, wilaya na kata kwa ajili ya Kristo.

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Katika mwanga wa majadiliano wakati wa warsha hii, fanya marudio na tathimini mpango wa ufuasishaji ulioandaa baada ya mafunzo ya Mwongozo wa Tatu kwa kila mtu unayemfuasa katika huduma yako ya upandaji kanisa. Fanya mabadiliko yoyote ya lazima kwenye mipango yako kufuatana na ulichojifunza wakati wa warsha hii. Kumbuka kwamba mipango uliyounda siyo ya kitakwimu—itabadilika na inatakiwa ibadilike kulingana na mda na ukuaji katika sehemu ya wanafunzi wako. Kwa vipindi fanya marudio ya na rekebisha mipango yako ya kufuasa uliyo nayo kwa kila mwanafunzi wako. ufuasishaji wako.

# UWAKILI

UWAKILI

SOMO LA 1

# Utangulizi Kwenye Uwakili

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea umaana wa uwakili wetu mbele za Mungu. Kila tulicho nacho ni cha Mungu. Kwa hiyo hatuhitajiki tu kumrudishia sehemu, lakini badala yake kutumia kila tulichonacho kwa ajili ya kazi yake na utukufu wake.

☞ **Wazo Kuu**

- Swala la ufunguo katika uwakili ni uaminifu wetu.
- Uwakili unapita zaidi ya fedha zetu ikiwemo na mali zetu, mda wetu, vipawa vyetu vya kiroho, n.k.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua kanuni ya kuwa wakili wa mali za Mungu kwa ajili yake.
- Kuelewa kwamba thamani ni msingi kwenye uwakili.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Anza kipindi kwa kuwauliza wafunzwa vitu gani Mungu amewapa. Orodhesha vitu hivi kwenye ubao wa chaki au kwenye ubao unaotumia mashine.

## I. UWAKILI NI NINI?

Uwakili ni neno linalotumika kuelezea shughuli za wakili. Wakili alikuwa yule aliyetawala mali za bwana yake. Jukumu lake lilikuwa la kuwajibika, na ilikuwa nyeti kwamba anakuwa mtu mwaminifu wa tabia. Uwezekano wa wizi na matumizi mabaya ya mali za bwana wake ulikuwa mkubwa.

Tunapokuwa tunaangalia kanuni zinazohusiana na wakili tutaona kwamba uwakili wa kweli unahusisha jinsi tunavyoshughulikia rasilimali Mungu alizotuamini nazo kutumia. Hizi zinahusish:

- Pesa zetu
- Mda wetu
- Mali zetu
- Miili yetu
- Familia zetu
- Huduma zetu

## II. KWA NINI KUZUNGUMZIA KUHUSU UWAKILI? MASWALA MAWILI

### A. Swala la Uaminifu

Uwakili ni kuwa muwajibikaji kwa kile Mungu alichotupa. Kutoka siku ya kwanza ya mwanadamu kwenye uso wa dunia, tumekuwa mawakili wa Mungu. Mtu alikuwa ameumbwa kutawala juu ya uumbaji (Mwa 1:28). Bwana alimuweka Adamu kwenye bustani kuilima na kuitunza kwa ajili yake (Mwa 2:15). Ingawa mtu kawaida haelewi kwamba kwa kifupi ni wakili wa uumbaji wa Bwana, maandiko wazi wazi yanaeleza kwamba dunia na kila kilichomo ni vya

Mungu (1Kor 10:26). Chochote tulichonacho kilitolewa kwetu na mungu kuvitumia kwa ajili ya utukufu wake. Anaangalia uaminifu wetu, na atatulipa kufuatana nao.

### B. Swala la Thamani

Jinsi watu wanavyojihusisha kwa vitu vilivyoorodheshwa kabla (katika wazo la kwanza) inaonyesha mioyo yao ilipo. Kama Yesu alivyosema “Palipo na utajiri wako ndipo moyo wako utakapokuwa pia.” Kwa maneno mengine unaweza ukaelezea mengi kuhusu moyo wa mtu kwa namna anavyozichulia fedha zake au vitu vyake vya thamani.


> Thamani yetu ndiyo inayomaanisha au vitu tunavyofikiria ni muhimu katika maisha.

Thamani yetu ndiyo inayomaanisha au vitu tunavyofikiria ni muhimu katika maisha. Baadhi ya watu wanathamini mali au faraja. Wengine wanathamini familia au huduma kwa jumuia. Kwa jinsi halisi tunatumia maisha yetu na mda kwa vitu hivyo vinavyoonekana kuwa vya lazima na nyeti kwetu binafsi. Katika Mathayo 22:37-39 tunapata kitu fulani kinachoitwa ‘Utume Mkuu’ ambapo Yesu anaweka kwa kifupi thamani yote ya Biblia katika sehemu mbili za maelezo.

1. *Thamani Yetu ya Juu Inahusiana na Uhusiano na Mungu—“mpende Bwana Mungu wako.”*

   Kusema kwa marefu, tunatakiwa kumtumikia Mungu. Kumpenda na kujihusisha kwa Mungu ni thamani yetu ya juu zaidi. Kwa kuwa ni kitu cha asili kwetu kutumia mda na hao tunaowapenda, kila muumini anatakiwa atumie mda wake wa pekee katika kujifunza neno la Mungu na maombi. Tunapokosa ukaribu wa kipekee na Mungu, tunakosa baraka za Mungu na kukosa nguvu katika huduma.

   **Kielelezo 1.1**

   Kumtumikia Mungu kwa uwezo wetu wote siyo kitu tu cha hisia kwa mda, lakini uamzi wa kila siku ambao unahusisha rasilimali zetu zote. Kadiri muumini anavyotumia mda wake, mali n.k. kiufanisi, ndivyo anavyomtumikia Mungu wake kiufanisi. Mda binafsi wa kuwa na Bwana ni kitu kinachohitaji kupangwa katika ratiba ya mpanda kanisa yenye mambo mengi vinginevyo hauwezi ukatokea tu. Uhusiano wenye afya na Mungu ni kitu muhimu kinachohitajika kwanza kabla ya kuendelea katika kuwatumikia wengine.

2. *Thamani Yetu Nyingine Inahusu Uhusiano Wetu na Wengine—“Mpende Jirani Yako Kama Unavyojipenda.”*

   Kiulalo, tunatakiwa kuwatumikia wengine. Uhusiano wa upendo tulionao na Mungu unatakiwa utapakae kwenye upendo kwa watu wengine. ‘Wengine’ ni pamoja na familia zetu, wafanya kazi wenzetu, wajumbe wa kanisa tunakotoka, na waliopotea ambao tunawashirikisha Kristo. Kama mawakili tunatakiwa kutumia rasilimali ili kwamba mahitaji ya hawa ‘wengine’, ambao Mungu amewaweka katika uangalizi wetu, yanatimizwa.

   Wapanda kanisa ni watu walio na kazi nyingi zaidi katika jumuia. Kutumia mda vizuri, fedha na rasilimali zingine kutamsaidia mpanda kanisa kuwa mtumishi mzuri kwa wengine, kwa kuwezesha huduma yenye kusudi badala ya kuruhusu misukosuko kutawala maendeleo.

Kabla hatujaanza kujadili uwakili kwa undani zaidi, lazima tuangalie thamani zetu. Amri Kuu inatakiwa iwe ndiyo kiongozi wetu kuhusiana na thamani zetu na vipaombe. Wewe ni mtu unayempenda Mungu kwa moyo wako wote na vile vile kuwapenda wengine kama unavyojipenda? Kama hili ni hivyo, uwakili wako unatakiwa udhihirishe hilo.

## III. KANUNI ZA UWAKILI KATIKA BIBLIA

Kuna mifano mingi ya uwakili katika Biblia. Wengi wa watu matajiri walikuwa na mawakili. Kuliko tu kujijali wenyewe binafsi na kuendesha haki zao za kila siku, wangeweza kumwajili mtu wa kutegemeka, mtu mwenye uwezo. Wakili hakuwa na mali zake mwenyewe. Badala, alikuwa ameruhusiwa kuishi katika nyumba ya tajiri yake, kula katika meza ya bwana wake, na kuvaa kutokana na mali ya bwana yake. Kuliko tu kuwa na mali yake, wakili alikuwa anaweza kufikia mali zote za bwana yake.

## A. Maana ya Uwakili

Maneno kadhaa yametumika katika Biblia kwa sura ya uwakili. Tafasiri zinaachana, lakini maana ya jumla ni wazi. Baadhi ya maneno yaliyotumika ni kama ifuatavyo:

1. *Wakili (oikonomos[5])*

   Hili ni neno maalumu kwa yule aliyefanya kama wakili. Alikuwa anawajibika kwenye uangalizi wa utajiri wa Bwana yake. Alikuwa na mamlaka makubwa kwenye vitu vya nyumba. Mzizi wa neno 'wakili' ni sawa na mzizi wa "vitu vya nyumba.' Mtu huyu kikawaida alikuwa mtumwa, lakini alikuwa anafikiriwa wa kutumainiwa vya kutosha kuweza kuchaguliwa kwa kazi muhimu. Neno hili linatumika katika Luke 12:42, Luka 16:1-3, na 1 Wakorintho 4:1.

2. *Mwangalizi (epitropos[6])*

   Neno hili linaonekana kutumika wakati mtu anapokuwa katika nafasi ya mamlaka kwa watu wengine. Katika Wagalatia 4:2 inamaanisha kwa yule aliyekuwa anawajibika kumfundisha mtoto kufikia ukomavu.

3. *Mtumwa (doulos[7])*

   Mtumwa alikuwa mali ya mtu mwingine. Wakili kawaida alikuwa mtumwa, lakini si watumwa wote waliitwa mawakili. Mtumwa haikuwa lazima awe na mamlaka yoyote kwa mtumwa mwingine au juu ya utajili wa bwana yake. Kama alikuwa na mamlaka haya, kisha neno 'wakili' lilikuwa linafaa. Mfano wa mtumwa alifanya kama mawakili unapatikana katika Mathayo 24:45 na Mathayo 25:14.

4. *Mtumishi (doulos)*

   Katika tafsiri nyingi neno hilo hilo limetolewa kama yote 'mtumwa' na 'mtumishi.' Linaweza kuchukua maana zote. Nyakati za Biblia, kulikuwa na watumwa waliokuwepo katika umasikini wa unyonge na shida, na kulikuwa na watumishi pia walioendesha maisha mazuri zaidi. Kwa jinsi hiyo, wote wlikuwa mali ya mtu mwingine, na kwa hiyo neno moja lilitumika.

5. *Uwakili (oikonomia[8])*

   Uwakili ni ofisi au kazi ya wakili, badala ya mtu. Tunapoongelea uwakili wetu, tunarejesha kwenye wajibu wetu kuendesha kitu fulani. Mifano ya neno hili inapatikana kutoka katika Luka 16:2, 1 Wakorintho 9:17 na Waefeso 3:2.

Kutokana na matumizi ya maneno haya, tunaweza tukaunda picha inayoleta maana ya nini uwakili unachomaanisha. Wakili kikawaida alikuwa mtumwa aliyekuwa anmeaminiwa kupewa mamlaka kusimamia na kuangalia utajili wa bwana wake, vitu vya nyumba, mashamba, biashara, watumishi wengine, au hata kufundisha kijana wake.

> Wakili alikuwa mtumwa aliyekuwa ameaminiwa kupewa mamlaka kusimamia na kuangalia utajili wa bwana yake.

## B. Yusufu—Mfano wa Uwakili

Yusufu anaweza kuwa mfano wa wakili mzuri. Kwanza alisimamia vitu vya nyumba ya Potifa, Mumisri wa kiofisi aliyemununua kama mtumwa (Mwa 39). Ingawa Potifa hakuwa mtu anayeamini, mara moja aliona kwamba Mungu alikuwa pamoja na Yusufu na alifaniskisha kila alichofanya. Kwa hiyo Potifa alitoa kila alichokuwa nacho mikononi mwa Yusufu isipokuwa mke wake tu (Mwa 39:9).

Kama wakili wa Potifa, Yusufu aliweza kujilisha na kuvaa mwenyewe kutokana na vitu vya bwana yake. Aliishi katika nyumba ya Potifa na kusimamia yote vitu vya nyumba ya Potifa na mashamba yake. Lakini masimulizi ya majaribu kutoka kwa mke wa Potifa yanaonyesha wazi kwamba Yusufu hakusahau kamwe kuwa vitu vyote hivyo vilikuwa mali ya bwana yake na

[5] οικονομος
[6] επιτροπος
[7] δουλος
[8] οικονομια

kwamba kulikuwa na mipaka kwa kile ambacho angeweza kufanya. Angeweza kufurahia matunda ya jasho lake kadiri bwana wake alivyokuwa anafurahishwa na uwakili wake, na kadiri ambavyo hangemfanyia dhambi Potifa.

Baadaye, Yusufu tena alifanywa wakili, kwanza alikuwa wakili wa gereza na kisha wa Farao mwenyewe. Kama wakili wa Farao, alikuwa tajiri kupita huko Misiri kufuatia Farao. Kwa jinsi hiyo nafasi yake ilitegemeana na uaminifu wake kusimamia haki za Farao katika namna iliyomridhisha Farao.

### C. Uwakili katika Mifano

Kwa sababu wakili ilikuwa kitu cha kawaida nyakati za Biblia, Yesu alitumia mifano kuhusu mawakili kuwakilisha ukweli kuhusu uhusiano wa waumini kwa Mungu. Ni ukweli upi Yesu anataka kuwakilisha kwetu kupitia kivuli cha wakili?

1. *Wakili Mzuri ni Mwaminifu*

Katika Luka 12:42-48 Yesu anafundisha kwamba wakili lazima awe mwaminifu hata bwana wake anapokuwa hayupo. Kama bwana wake anarudi ghafla na kumkuta anashughulika na biashara yake, atazawadiwa. Lakini kama hajajiandaa kwa ajili ya kurudi kwa Bwana wake, atashughulikiwa vikali. Hii inakwenda sambamba na hali ya muumini. Bwana wetu ameondoka, na atarudi ghafla. Tunahitaji kuwa waaminifu katika kutokuwepo kwake.

2. *Wakili Mwelevu Anatumia Nafasi yake Kuandaa Kwa Ajili ya Wakati Ujao*

Yesu alisimulia mfano mwingine wa uwakili katika Luka 16:1-12. Mfano huu unashangaza kidogo, kwa kuwa wakili anasifiwa kwa ajili ya kumdanganya bwana yake. Mfano kwa hakika haukusudiwi kuchochea kutokuwa mkweli. Badala, unafundisha ujumbe wazi juu ya hekima ya kutumia vitu tulivyonavyo sasa kwa ajili ya wakati wa mbele. Wakili mbaya anatambua kuwa nafasi yake ni ya mda, kama maisha yetu yalivyo duniani. Anaamua kutumia kila kitu kwa nguvu zake kuandaa mapokezi mazuri kwa ajili yake kazi yake inapomalizika. Yesu anasema kwamba alitenda kihekima zaidi kuliko ambavyo tunafanya mara nyingi. Tunatakiwa tuwe tunatumia kila tulichonacho duniani kuandaa utajiri mbinguni.

3. *Mawakili Watatathiminiwa Kufuatana na Uwezo wao*

Mfano wa talanta katika Mathayo 25:14-30 unaeleweka kwetu. Kila mtumishi anaaminiwa kwa fedha wakati bwana wake anapokuwa ameondoka. Wanakuwa mawakili kwa hiyo wa talanta hizo. Kwa jinsi hiyo, hawapewi kiasi sawa. Badala, kila mmoja anapokea kufuatana na tathimini ya bwana yake ya uwezo wake. Wakati bwana aliporudi, alimzawadia kila mmoja kufuatana na uaminifu wake. Yule aliyekuwa amepewa talanta mbili alipokea sifa sawa na na yule aliyepata tano. Isipokuwa yule tu aliyeichimbia talanta yake alihukumiwa. Swala la ufunguo lilikuwa ni uaminifu wa wakili na siyo kiasi cha vitu alivyokuwa amepewa.

### D. Mahesabu

Mtume Paulo wazi wazi alifundisha kuwa tu mawakili wa Kristo. Wapanda kanisa na viongozi wanawajibika hasa hasa kuhudumu maajabu ya Mungu (1Kor 4:1-2; Efe 3:2; Tit 1:7). Pia alifundisha kwamba Bwana wetu anarudi ten ghafla, katika wakati ambao hatumtarajii (1The 5:2). Yesu atakaporudi kwa ajili ya kanisa lake, atatuhukumu endapo kama tulikuwa waaminifu katika huduma zetu kwake (Rum 14:4-12; 2Kor 5:10). Kila moja ya vifungu hivi, vinaelekezwa hasa hasa kwa wakristo. Ukweli kwamba Yesu atawahukumu waumini hata ni wazi katika 1Wakorintho 3:10-15. Kwenye aya hiyo, Paulo anaelezea jinsi moto utakavyozijaribu kazi zetu, na ama tutapokea zawadi ama kupata hasara, kutegemeana na jinsi tulivyotumika. Hili ni wazi linarejea kwa waumini, kwa kuwa hata yule asiyekuwa na kitu anayestahili zawadi ataokoka (v. 15).

## IV. UWAKILI WETU

### A. Pesa Zetu

Waumini wengi wanajua kuwa wanatakiwa watoe sehemu ya fedha zao kwa Bwana. Kwa jinsi hyo, kuelewa kwa kweli kwenye uwakili kunapelekea tabia tofauti. Siyo tu lazima tutoe,

> Hatuna pesa zozote, Isipokuwa tuna pesa za Mungu tu alizotuamini nazo.

lakini hatutakiwi kupoteza pesa wala kuzitumia kwa vitu ambavyo havimpendezi Mungu. Baada ya yote, ni pesa zake. Hatuna pesa zozote, Isipokuwa tuna pesa za Mungu tu alizotuamini nazo. Ama kwa kuzitoa kwa kanisa au kwa kuzitumia kwa vitu ambavyo vitamfurahisha, nasi kwa moyo tunavirudisha kwa Mungu.

### B. Mda Wetu

Mda wetu pengine ndiyo mali yetu ya ajabu zaidi kwa sababu hakuna njia tunazoweza kuuongeza. Sisi sote tuna idadi ya siku fulani zilizotolewa kwetu na Mungu (Zab 139:16). Anatutarajia kuzitumia kwa utukufu wake. Yesu alipokuwa amechukuliwa kwenda juu, malaika waliwakemea wanafunzi kwa kusimama kuzunguka kuangalia angani (Mdo 1:11). Walitakiwa wawe na bidii kutunza amri zake wakimusubiri Roho Mtakatifu na kisha kuichukua injili kwa mataifa yote. Paulo anatukumbusha kuwa wenye bidii kuishi maisha ya kimungu, kwa kuwa siku ya wokovu wetu inakaribia (Rum 13:11-14). Pia anatuambia kutumia kila nafasi tuliyonayo katika siku hizi mbaya (Efe 5:15-17). Mungu amegawa kazi kwa kila mmoja wetu za kufanya, na kutupa mda mfupi wa kuzikamilisha (Efe 2:10). Lazima tutathimini kwa uangalifu jinsi tunavyotumia mda wetu kuhakikisha tunafanya yote anayopenda tuyafanye.

### C. Mali Zetu

> Sehemu kubwa ya riziki ya waumini wa Agano Jipya ingekuwa pia katika mfumo kuliko tasilimu.

Hata waumini waamifu mara nyingi wanaliacha eneo hili. Wanaweza wakafikiri kwamba Mungu anataka sehemu ya fedha zao, lakini ni hivyo tu. Kama wana kipato kidogo cha pesa, wanaweza wakajisikia kuwa hawahitaji kutoa. Katika hali halisi, Biblia haipunguzi utoaji wetu kuwa wa pesa. Zaka ya Agano la Kale kawaida inatolewa kutokana na ongezeko la mifugo au mazao. Sehemu kubwa ya riziki ya waumini wa Agano Jipya ingekuwa pia katika mfumo kuliko tasilimu. Mungu anatukata kutoa sehemu ya chochote tunachopata. Inaweza ikawa mshahara, viazi kutoka katika bustani zetu, maziwa kutoka kwa ng'ombe wetu, au aina nyingine ya kipato. Chanzo siyo muhimu. Mungu ndiye chanzo na mwisho wa vyote tulivyonavyo, na anatutarajia kukumbuka kwamba na kumuheshimu kutokana navyo.

Uko tayari kutumia mali Mungu alizokuamini nazo kumpendeza yeye na kuhudumu kwa wengine? Wajumbe wa kanisa la Yerusalemu waliuza vitu walivyokuwa navyo ili kuweza kutoa kwa wahitaji (Mdo 2:44). Kwanza tunatambulishwa kwa Barnabas katika maandiko wakati anapouza aridhi yake kutoa thamani yake kwa kanisa (Mdo 4:36-37). Mungu kiutajiri alimbariki na kumchagua kuwa msaidizi wa mtume Paulo.

### D. Miili Yetu

Wakristo wachache wanafikiria juu ya wajibu huu, lakini ni muhimu. Miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu (1Kor 6:19), na ni kwa utukufu wa Mungu. Ingawa Biblia haizuii unywaji wa vileo, uvutaji sigara, au kutumia madawa ya kulevya, vitu hivi vinaweza kuharibu hekalu hilo na kuzuia uwezo wetu wa kumtumikia Bwana. Uwakili wa hekalu unahitaji kwamba tunakuwa wangalifu kuepuka kile kinachoonekana kuwa cha madhara kwa afya zetu. Hii inaweza kuwa pamoja na ukosefu wa mazoezi au usingizi, mlo hafifu au chochote chenye madhara.

### E. Familia Zetu

Familia zetu ni zawadi kubwa kutoka kwa Mungu. Kama hatuwezi kutunza familia zetu vyema, kisha hatufai kuendesha kanisa (1Tim 3:4-5). Familia zetu hazikatizi huduma zetu. Zinatakiwa kuwa sehemu yake, na maisha yetu ya familia yanatakiwa yatuandae kuhudumu kiufanisi. Tunapokua katika uwezo wetu kuziangalia familia zetu na kwa upendo kuziongoza kwenye neno, tunajifunza kuangalia na kuongoza makaka na madada katika Kristo kiufanisi zaidi.

### F. Huduma Zetu

1 Petro 4:10 inatuambia kwamba waumini wote wanatakiwa wawe mawakili waaminifu wa neema ya Mungu kwa kutumia vipawa vyao kuhudumu kwa wengine. Mtazamo sahihi wa huduma utainua mzigo kutoka mabegani mwa viongozi wengi wa kanisa. Huduma ni ya Mungu. Ni kazi yake na siyo kazi yetu. Tu watumishi wake tu, tukitumia rasilimali zake kukamilisha kazi. Kama tunakosa rasilimali, atatupatia. Kama tu waaminifu, tutakamilisha kila Mungu anachotaka. Tunahitaji kujisikia mzigo unaokandamiza kama mambo ni mazito. Badala, tunahitaji kusubiri juu ya Bwana kwa uongozi wake na nguvu zake.

Ni sharti kwamba tunatumia mda na Mungu kila siku. Tunapokuwa waangalifu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, tutafanya maamzi mazuri, na huduma itakuwa yenye ufanisi zaidi. Hata Yesu alijisikia hitaji la kufanya shauri na Baba kwa ajili ya hekima. Hili hasa ni dhahiri alipokuwa na hitaji la kufanya uamzi mkuu, kama vile mahali pa kufanya kazi (Lk 4:42-44) au nani wa kuchagua kama mwanafunzi (Lk 6:12-16). Tunahitaji hekima sawa. Kama hatusahau kamwe kwamba tu watumishi tunaofanya mapenzi ya Mungu, tutamsikiliza kila mara.

## V. UWAKILI NA MPANDA KANISA

Uwakili mzuri ni wa muhimu zaidi kwa wapanda kanisa. Watahitaji kutumia vipawa vyao vyote, mali, mda na pesa vema ili kupanda kanisa jipya. Watahitaji pia kujua majukumu yao ya kutunza miili yao na familia wanapoviwianisha na huduma. Lazima watumie kanuni za uwakili kwao wenyewe na kuzifundisha kwa wengine.

### A. Kuzitumia Kwao Wenyewe

> Mfano wako na kufundisha bila kukoma kutawasaida waumini wapya kuelewa jinsi ya kuwa mawakili wema.

Wapanda kanisa wanakutana na kazi ngumu. Lazima waokoe wafungwa kutoka mikononi mwa adui mwenye nguvu asiyeonekana na kuanzisha ngome mpya kwa ajili ya Bwana. Hawana uwezo wa vitu hivyo kwa nguvu zao wenyewe. Lakini ni watumishi wa Mungu wanaotumia rasilimali zake alizotoa kwa ajili yao kukamilisha kazi yake. Atatoa kila kinachohitajika. Jukumu lao ni kuvitumia kwa uangalifu. Kila wanachofanya, kutoka utoaji mpka utumiaji wa mda, vinatakiwa wipimwe na haja zao za kuhitaji baraka zake na wajibu wao kama mawakili wake.

Kama unaona ugumu kwenye uwakili inaweza ikawa inaletwa na ukosefu wa mkazo. Kutazama thamani kunaweza kusaidia kuleta mkazo kwenye maisha katika huduma. Una tabia kama za mtu anayempenda Mungu na wengine? (Mt 22:37-39). Njia unazotumia mda wako, mali, mwili, familia, huduma n.k. zinaendana na hili?

### B. Alifundisha Wengine

Upandaji kanisa wenye ufanisi unahitaji kuhusisha kila mjumbe. Kutoka mda wa kukata shauri kwao, tunahitaji kumfundisha kila mkristo mpya kuhusu wajibu wake kama wakili mbele za Mungu. Usidhani kuwa wengine watajifunza kuwa mawakili wema wenyewe. **Mfano wetu** na kufundisha **bila kukoma** kutawasaida waumini wapya kuelewa jinsi ya kuwa mawakili wema.

Hasa hasa, waumini wapya wanatakiwa wafundishwe:

- Kutoa kwa ukarimu kutoka kwenye pesa zao na mali nyingine.
- Kutafuta na kutumia vipawa vyao vya kiroho katika huduma kulijenga kanisa.
- Kutoa mda wao kwa ajili ya huduma kwa waumini sawa na wasioamini.
- Kuangalia familia zao ili kuweza kujua jinsi ya kutunza waumini wengine.

## SULUHU

Mkristo ni wakili awe anajua au la. Kila tulichonacho ni cha Bwana na tunatarajiwa kukitumia kwa utukufu wake. Kanuni hii inawahusu waumini wote—siyo tu wapanda kanisa. Lakini wapanda kanisa wana jukumu maalumu kwa sababu ndio sisi ambao lazima tuonyeshe kanuni hii katika maisha yetu na kuifundisha kwa wengine. Kwa yule aliyepewa vingi, vingi vitatakiwa kutoka kwake.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni rasilimali zipi Mungu ametoa kwa ajili yako? Ziorodheshe
- Ni eneo lilpi lililoelezewa katika wazo IV ni gumu zaidi kulifanya? Kwa nini?
- Mtu masikini anaweza kumtolea Mungu hasa? Anaweza? Kwa kiasi gani?
- Nini mkristo mpya anatakiwa afundishwe kuhusiana na uwakili?
- Jinsi gani thamani ni muhimu kwenye majadiliano ya uwakili?

UWAKILI

SOMO LA 2

# Uwakili Kifedha

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha utoaji wa kujitoa na makanisa yanayojisaidia yanaweza kuzidisha mafanikio ya upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Mungu anapenda tuwe na imani kutoa kwa kujitoa kwa kazi yake.
- Makanisa yanayojisaidia yanakua kwa haraka kuliko mengine.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa…

- Kuelewa jinsi ya kujisaidia kunavyosaidia kanisa kukua na kukomaa.
- Kushiriki katika kutoa kwa kiwango kikubwa, na kuwafundisha wengine kufanya hivyo.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Jaribu kuepuka mjadala uliochemshwa kwenye swala la utoaji zaka. Wazo kuu la somo hili ni kwamba tunawajibika kutumia pesa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kazania katika swala hilo, ambalo linaendana bila kujali anachoamini mtu mwingine kuhusu utoaji wa zaka.

Uwe macho wakati wa tukio kwamba baadhi kwenye mafunzo wana uzoefu katika kupanga bajeti na wanaweza kuwashirikisha wengine.

## I. KUIPELELEZA BIBLIA

Biblia ina mengi ya kusema kuhusu pesa. Tumechagua vifungu vifuatavyo kutusaidia kuelewa akili ya Mungu kuhusiana na utoaji wetu wa pesa.

### A. Utoaji Zaka katika Sheria ya Agano la Kale

Watu wa Israeli walikuwa wanatakiwa kutoa zaka, au asilimia kumi ya mazao yao, kwa Bwana na kwa kazi yake (Law 27:30-32; Hes 18:23-24). Kwa nyongeza na kuhitajika kwa zaka hizi, kulikuwa na matoleo mengi pia na kodi iliyoitwa zaka. Muumini wa Agano la Kale asiye na mzaha aliyejaribu kutunza sheria inawezekana alitoa karibia asilimia 28 ya mapato yake kwa Mungu. Hii ilikuwa zaidi mifugo na mazao kutoka shambani mwake.

Sura ya kiufundi ya utengaji wa zaka katika Agano la Kale, zaka ilikuwa ni malezi ya kiroho kwa mtu binafsi ambayo Mungu aliahidi kuyajibu. Kushindwa kutoa zaka kulikuwa kunachukuliwa na Mungu kama wizi, kwa kuwa ilikuwa ni yake. Mungu aliwatia changamoto Waisraeli kumjaribu katika hilo, akiahidi kumwaga baraka zake nje kwa hao walioleta zaka yote kwake (Mal 3:8-12).

### B. Sadaka Huru kwa Ajili ya Hema ya Kuabudia

Zaka ilikuwa ndiyo njia pekee ya kukusanyia hazina kwenye Agano la Kale. Wakati wa kutanga tanga jangwani, Mungu alimwamuru Musa kukusanya sadaka huru kutoka kwa watu kujenga hema (Kut 25:1-8). Watu walitoa mifugo yao, vitu vyao binafsi, na hata nguvu zao katika kuitikia wito huu (Kut 35:4-29). Walikuwa hawakulazimishwa kutoa lakini walitoa kwa kupenda. Kwa hakika, walitoa zaidi sana kupita vilivyohitajika, mpaka Musa akawaomba watu kuacha kutoa! (Kut 36:4-7).

**C. Daudi Anatoa Kielelezo cha Utoaji kwa Ajili ya Kujenge Hekalu**

Daudi alielewa utoaji wa kujitoa, ndiyo maana alikataa kumtolea Mungu kile ambacho hakikuwa na "gharama" (1Nya 21:24). Mfalme Daudi kwa kujitoa alitoa utajiri wake ili kwamba hekalu la Mungu baadaye lijengwe na mtoto wake Solomoni (1Nya 29:1-5). Utoaji wa Daudi ulikuwa mfano wa kuvutia kwa wengine, na baada yake viongozi wa Israeli walitoa (1Nya 29:6-9). Maombi ya Daudi yakifuatia utoaji huu yanaonyesha tabia yake kuhusu utoaji (1Nya 29:10-20). Tunasoma kwamba Daudi alitoa kwa moyo wa sifa na shukurani kwa Mungu. Daudi pia anaonyesha kwamba mali na utajiri—kila kitu ni cha Mungu (1Nya 29:16). Utoaji kwa kifupi ni nafasi ya kumrudishia Mungu sehemu ndogo ya kile alichotoa. Hata hivyo Daudi anashangaa kwa sauti jinsi ambavyo Mungu angemruhusu nafasi kama hiyo ya utoaji. (1Nya 29:14).

**D. Kutoa Nje ya Umasikini**

Yesu alimsifu mjane aliyetoa kiasi kidogo (Lk 21:1-4). Alifanya hivi kwa sababu sarafu zake mbili zilikuwa na kiasi cha asilimia mia ya utajili wake. Tukio hili lilitokea kabla kanisa halijaanzishwa wakati wa Pentekosti. Kwa hiyo hata kabla ya umri wa kanisa, kulipokuwa hakuna swali kwamba Mungu alihitaji zaka, Mungu alipendezwa wakati waumini kwa uhuru walipotoa zaidi ya kiasi hicho. Ni wazi pia kwamba anapendezwa na anaangalia kuona ni kiasi gani tunatoa.

Kuna kanuni nyingine wazi katika fungu hili. Hekalu lilikuwa jengo la gharama lililofunikwa kwa dhahabu (Mk 13:1; Mt 23:16). Kwa hakika hekalu halikuhitaji pesa za mjane masikini. Lakini Yesu alipendezwa kwamba alitoa hata hivyo kwa sababu alilifikiria kana kwamba ametoa kwa Mungu badala ya kwenye hekalu. Haikujarisha kwamba viongozi wa dini walikuwa wanafiki. Au alijua kwamba Warumi wangeharibi hekalu kwa miaka michache ijayo. Tunamtolea Mungu badala ya mwanadamu. Lakini tunamtolea Mungu kupitia kanisa.

**E. Usaidizi wa Fedha kwa Viongozi wa Kanisa wa Agano Jipya**

Viongozi wa kiroho katika Agano Jipya walikuwa wanasaidiwa kwa njia nyingi. Yesu na wanafunzi wake walisaidiwa, angalau kwa sehemu, na mwanamke aliyesafiri pamoja nao (Lk 8:1-3). Wakati Yesu alipowatuma wanafunzi wake kwenda kuhubiri injili Galilaya aliwaamuru kutarajia kupewa na hao ambao wangewahudumia (Mt 10:10; Lk 10:5-8). Kama mtumishi wa Mungu, mtume Paulo alikuwa na haki ya kusaidiwa kifedha na hao ambao miongoni mwao aliwahudumia kama vile ambavyo wahudumu wa Agano la Kale walivyosaidiwa (1Kor 9:4-14). Hapa ni mahali pengine (1Tim 5:18). Paulo anayatia moyo makanisa kuwasaidia hao wanaowahudumia. Kwa sababu zake mwenyewe, Paulo wakati wote hakutumia haki yake ya kupata msaada wa kifedha kutoka kwa hao aliowahudumia. Kwa mfano, Paulo hakupokea msaada wa kifedha kutoka kwa Wakorintho, hata kama angeweza kuwauliza juu yake (1Kor 9:12). Badala yake, Paulo zaidi alijisaidia mwenyewe katika kutengeneza mahema ili kutokuwa mzigo kwa kanisa (Mdo 8:2,3; 1Kor 4:12).

Vile vile tunasoma kwamba Wafilipi walitoa kwenye huduma ya Paulo' (Flp 4:15-20). Inafurahisha kuona kwamba kifungu kidogo kilichorudiwa zaidi *"Mungu wangu atatimiza mahitaji yako yote"* kinapatikana katika mandhali ya Paulo akiwapongeza Wafilipi kwa utoaji wao. Paulo alijua kwamba Mungu atatoa mahitaji yote ya Wafilipi kwa sababu walitoa kwa ukarimu kwenye huduma yake. Kwa maneno mengine, Mungu anatoa tunapokuwa tumetoa kwa uaminifu.

**F. Makusanyo kwa Ajili ya Watakatifu wa Yerusalemu**

Paulo aliandaa kukusanya matoleo ya pekee kwa watakatifu waliokuwa wahitaji Yerusalemu waliokuwa wanakabiliana na njaa. Katika barua yake ya kwanza kwa Wakorintho waumini alielezea sawa sawa jinsi makusanyo yangekusanywa (1Kor 16:1-2). Alitarajia kila muumini kutoa kwa kupenda kwa siku ya kwanza ya kila juma (jumapili). Hakuna kiasi maalumu kilichokuwa kimeelezwa. Badala yake Paulo aliomba kiasi "kinachoendana na vipato vyao."

Katika barua ya pili ya Paulo kwa Wakorintho tena alifundisha juu ya utoaji huu. 2 Wakorintho 8:1-6 na 9:6-11 zina pengine kanuni zinazotia changamoto zaidi juu ya utoaji katika Agano Jipya. Paulo anaanza kwa kutumia mfano wa utoaji wa makanisa ya Masedonia (2Kor 8:1-6). Walitoa kwa ukarimu kutoka kwenye umasikini wao, hata zaidi ya kile ambacho kibinadamu wangetoa (kwa kumtumaini Mungu). Wamasedonia walikuwa wamevutiwa na ukweli kwamba wao wenyewe kwanza wamejitoa kwa Mungu.

Hao wanaotoa jinsi hii wanafurahia ahadi ya ajabu kutoka kwa Mungu kwamnba atawalipa kulingana na utoaji wao. Kwa hakika, Mungu kwa ukarimu atatoa kwa ajili ya mahitaji yetu kama tuna imani ya kumtolea kwa ukarimu (2Kor 9:6-11; Lk 6:38).

## II. UTOAJI WA BINAFSI

> Katika uchumi wa Mungu uwezo wa kutoa na kupokea hauzuiliwi kwenye rasilimali zilizopo.

Kuna kanuni muhimu ya kiroho ambayo iko kwenye Biblia yote ambayo kila mkristo anatakiwa kujifunza. Kanuni ni rahisi sana. Katika uchumi wa Mungu uwezo wa kutoa na kupokea hauzuiliwi kwenye rasilimali zilizopo. Katika maneno mengine kila muumini, haijalishi ni kiasi gani ni masikini, anatakiwa atoe. Kama ilivyoelezewa kwenye matumizi ya mafungu mengi hapo juu, umasikini siyo udhuru. Kila mmoja anatakiwa amtolee Mungu. Zaidi sana, wakati watu wa Mungu wanapotoa kila wanachoweza kwa imani, Mungu anatumia zawadi hizi kimuujiza akizizidisha mara kadhaa zaidi. Hili linaelezewa kwenye hadithi ya mjane wa Serapta (1Fal 17:7-16) na katika kulisha 5,000 (Mk 6:30-44). Katika hali zote, kilichokuwa kimetolewa hakikuwa cha kutosha lakini ndicho kilichokuwepo—na hicho kilitosha kilipokuwa mikononi mwa Mungu.

Utoaji kwenye kazi ya Mungu unatakiwa uwe zoezi la mara kwa mara kwa maisha ya kila muumini. Wakati wakristo wengi wakiwa wanafahamu wajibu huu, maoni yanapishana ya kiasi gani kinatakiwa kitolewe. Bado zaka inahitajika katika umri wa kanisa? Kama siyo, kiasi gani tunatakiwa tutoe? Wengi wanaamini kwamba zaka ilikuwa ni zoezi la sheria ya sanamu ambayo, kama sheria ya lishe, haikuchukuliwa kwenye Agano Jipya (Rum 10:4; Gal 3:25). Wengine wanaamini kwamba kwa kuwa zaka ilikuwa wakati wa sheria ya sanamu (Ge 14:19-20) na Yesu aliithibitisha matumizi, ingawa alionyesha kuhusu mvuto (Mt 23:23), kwamba Mungu anatutarajia kutunza matumizi leo.

Waumini wote waliojifunza vifungu vya Agano Jipya juu ya utoaji pengine wanaweza wakakubaliana kwamba asilimia kumi, zaka, kinaweza kuwa kiwango cha chini cha utoaji wetu kwa Bwana. Ingeweza kuonekana kwamba kama asilimia ilikuwa inatakiwa kwenye Agano la Kale, waumini wa Agano Jipya wenye kuelewa zaidi wokovu wangetaka kutoa zaidi.

Bila kujali asilimia ya kipato ambacho muumini anaamua kutoa, ni muhimu kutambua kuwa kipato siyo tu tasilimu inayopokelewa kama mshahara au malipo. Kama vyote tulivyonavyo ni mali ya Bwana, kisha zaka inatakiwa itolewe kutoka kwenye aina nyingine ya kipato kama vile mazao, mifugo, n.k. kama mtu anapokea kidogo au hana kipato cha tasilimu, hii haimanishi kwamba kwa namna fulani anaachiliwa kutokutoa zaka. Ana njia zingine zinazomuwezesha kuishi, na rasilimali hizi pia zinatakiwa zifikiriwe anapokuwa analeta zaka zake kwa Bwana.

Kanuni zifuatazo zinalinda utoaji kwa waumini:

- Kila muumini anatakiwa atoe.
- Utoaji wetu unatakiwa uwe unaendana na kipato chetu, zote tasilimu na zisizo tasilimu. Fikiria kama Mungu amefanya kipato chako kulingana na utoaji wako!
- Tunatakiwa kutoa hata katika umasikini wetu.
- Tunatakiwa tutoe kwa ukarimu na kwa sababu tunapenda kufanya hivyo—siyo kwa sababu mtu anatulazimisha. Utoaji lazima utokane na utayari wa moyo ili kumpendeza Mungu.
- Tunatakiwa tutoe zaidi ya tunavyoweza (tukimutumaini Mungu).
- Utoaji wetu wa fedha unatakiwa ufate kujitoa kwetu wenyewe kwa Mungu. Utoaji ni kuonyesha kujitoa kwetu kwa Mungu.
- Mungu anatuzawadia kulingana na utoaji wetu. Mungu ameahidi kutoa kwa ukarimu kwenye mahitaji yetu kama tuna imani ya kutoa kwa ukarimu kwake.

Katika Malaki, Mungu aliwaahidi Waisraeli kwamba angefungua ghala za mbinguni na kumwaga baraka zake kama wangetoa. Leo tuna aina hiyo hiyo ya ahadi. Uwakili una maana kwamba rasilimali zote ambazo Mungu ametuamini nazo ni za Mungu. Kama tu waminifu kumurudishia, kisha atatubariki zaidi ya mahitaji yetu. Kama tunasahau ni za nani, na tunakuwa wanyimifu kwake, tutakosa baraka kutoka kwa Mungu. Hatuhakikishiwi kwamba baraka kutoka kwa Mungvu ni fedha. Mungu anaweza akamubariki mtoaji kiroho.

## III. FEDHA ZA KANISA LA MTAA

Moja ya majukumu ya kanisa ni kushughulika na zaka na sadaka za watu wa Mungu kwa uangalifu na uaminifu.

### A. Makanisa Yanayojisaidia

Zaka katika Agano la Kale ziliwezesha hekalu, na baadaye masinagogi, kujisaidia yenyewe kifedha. Wakati wote wa nyumbani wanapotoa asilimia 10 kisha, hata familia chache kama kumi, nyumba mpya, nyumba ya Mungu, inaweza kuanzishwa. Ukiwa na hili akilini, Imekuwa ni mila za Wayahudi kujenga sinagogi kwa kila mji ulio na familia 10 au zaidi za Wayahudi.

Chochote mtu anachoamini kuhusu utoaji wa zaka kwenye Agano Jipya, kanuni nyuma ya utoaji zaka, kwamba kanisa linaweza na linatakiwa lijisaidie lenyewe, inabakia kuwa kweli. Kusoro tu utoaji wa Yerusalemu kutokana na njaa, ilikuwa ni kawaida kwenye Agano Jipya kwa kila kanisa kutunza mahitaji yao ya kifedha. Kwa mfano Paulo aliwaambia Wagalatia kuwasaidia walimu wao wenyewe (Gal 6:6). Alimwambia Timotheo kufundisha makanisa kuwaangalia masikini wao na wajane (1Tim 5:3-10), na kuwalipa walimu wao wa neno la Mungu (1Tim 5:18).

Utafiti utaonyesha kwamba makanisa yanayochukua jukumu la kujisaidia yenyewe yanakua na kuzidi kwa haraka kuliko yale yasiyofanya hivyo. Kuna faida kadhaa za kujisaidia:

> Makanisa yanayochukua jukumu la kujisaidia yenyewe yanakuwa na kuzidi kwa haraka.

1. *Kujisaidia Kunaendeleza Ukomavu*

   Utegemezi kwa wengine nje ya kanisa la mtaa kunaweza kupelekea kwenye hisia duni za heshima na kukosa nafasi ya kuendelea. Kwa jinsi hiyo, Wakati kanisa linaposaidia huduma yake na kusimamia fedha zake, linaendela kukomaa kupitia maamuzi yanayotokana na kuwajibika kama huko.

2. *Kujisaidia Kunajenga Kuwajibika*

   Ni kitu cha kawaida kwa mfanya kazi anayepokea fungu kutoka kanisa jingine au wakala kujisikia kuwajibika zaidi kwa hao wanaomlipa mshahara kuliko kwa kanisa analohudumu. Katika hali kama hiyo, mahitaji yanaweza kupita bila kutimizwa kwa kuwa kiongozi anakazania kwenye mahitaji ya "'wajiliwa"' kuliko mahitaji ya kundi. Kinyume chake kinaonekana kuwa kweli pia. Wajumbe wa kanisa wanaweza wasijisikie kuwajibika kwenye mahitaji ya viongozi wao na kuwachukulia viongozi bila kujali. Kwa sababu iwayo yoyote, watoaji wanajisikia hisia ya umilikaji kwa vitu wanavyotoa kwa ajili yake. (Mt 6:19-21). Kwa maneno mengine, watu wanathamini kile ambacho wanawekeza. Ni muhimu kwamba watu wa mtaa wanamiliki huduma ya kanisa ili kuweza kushamili kwenye jumuia yao.

3. *Kujisaida Kunafanyia Mazoezi Imani*

   Kujisaidia kunaweza kukaleta majaribu mengi na magumu. Kwa jinsi hiyo, majaribu ni nafasi ya kukua katika imani (1Pet 1:6-7, Yak 1:3-4). Kujisaida kwa hakika ni swala la imani. Kukosekana kwa kujisaidia mara nyingi hakutokani na umasikini, lakini ni ukosefu wa imani. Kuna mifano ya wote watu masikini wanaoweza kusaidia makanisa yao wenyewe, vile vile na watu matajiri wanaotegemea kutoka nje kusaidia kanisa lao. Swali ni "Mungu ataweza kutoa kwa ajili ya watu wake au hataweza? Watu wa imani watajibu hilo kwa kuliunga mkono. Ni busara kuomba kwa ajili ya utoaji wa Mungu na kutokuwa tayari kuwa jibu la ombi hilo? Kiuwazi siyo busara. Kufanya hivyo inaweza kuwa "imani bila matendo." Kwa jinsi hiyo, wakati watu wa Mungu wanapotoa kwa kujitoa na kwa imani, wakiamini kwamba Mungu ni mwaminifu, Mungu anarudisha kwa njia ambazo wasingeweza kudhani.

4. *Kujisaidia Kunaongeza Ushuhuda kwa Waliopotea*

   Wakati kanisa likiwa limesaidiwa na fungu la nje kisha uchukuliaji ni kwamba imani iliyotangazwa na kanisa ni imani ya nje. Hili mara nyingi linarudisha nyuma ushuhuda wa jumuia. Hili hasa ni kweli kwenye mishahara. Wakati watu wanapopokea mishahara kutoka chanzo cha nje wanaweza kufikiriwa kama wauzaji walioajiriwa badala ya waumini wa kweli wenye imani thabiti. Kwa upande mwingine, wakati wajumbe wa kanisa wanaposaidia huduma kwa kujitoa kunaweza kukawa na mashaka kidogo kuhusu uaminifu wao.

Kama kanisa linatarajia wa nje kulipia madeni yao, watawatarajia pia wa nje kuinjilisha jumuia yao?

5. *Kujisaidia Kunaruhusu Ukuaji usio na Kikomo*

Wakati fungu linapotoka kwenye chanzo cha nje kwa hiyo kuna kawaida karibu kikomo cha kulifikia fungu. Kawaida mfumo unahitaji kuwekeza rasilimali kuamsha huduma kwenye wasaidizi maarufu. Kwa maneno mengine, inagharimu pesa kupata pesa. Kuna hofu pia kwamba fungu linaweza kusimamishwa wakati wowote. Matokeo yake ni kwamba kunakuwa na kikomo cha kiasi gani cha pesa kinachoweza kupokelewa, na kanisa halikui. Kwa upande mwingine, katika kanisa linalojisaidia mahali ambapo watu wamefundishwa kutoa, fungu litaongezeka watu wapya wanapoletwa kwa Kristo na kushirikishwa kwenye kanisa. Kanisa linapokua na utoaji unaongezeka kiasi kwamba kunakuwa hakuna kikomo cha nini kinachoweza kufanyika.

Wakati kipepeo anapokuwa amezaliwa lazima asitahimili mahangaiko makubwa kutoka kifukoni. Mchunguzi mzuri mwenye maana anaweza kutaka kumsaidia kipepeo kutoka kwenye kifuko. Lakini kama akifanya hivyo, hasa hasa anarudisha nyuma maendeleo ya kipepeo na kwa hiyo kipepeo atakufa mara tu anapotoka kwenye kifuko. Kufuatana na mpangilio wa Mungu, zoezi la kupanda kutoka kwenye kifuko ndilo zoezi linalotakiwa kuendeleza nguvu muhimu kwa kipepeo.

Hilo linaweza kuwa sawa kwa kanisa mpya. Kama halijifunzi kujisaidia mwanzoni kabisa, linaweza kubakia kufanya kazi bila utaratibu milele, kamwe kutojifunza furaha na uwezo wa kujisaidia. Kila kanisa mpya linatakiwa kuwa na nafasi ya kukomaa katika imani yake lenyewe na kufata mpango wa Mungu wa usaidizi na ukuaji.

## B. Usimamizi wa Fedha za Kanisa

Usimamizi wa fedha katika kanisa lazima uonekane siyo kama biashara ya kawaidia au utawala, lakini huduma ya kiroho.

1. *Fundisha Utoji wa Kiutaratibu*

Chochote unachoamini kuhusu utoaji, sisitiza furaha ya utoaji, siyo sheria ya utoaji zaka! Utoaji wa kibiblia, iwe ni zaka au la, ni tendo la imani, alama kwamba wote ni wa Mungu. Watu wanapotoa kwa kupenda mara nyingi wanatoa zaidi na kupokea baraka kuu.

Viongozi wanatakiwa watoe kama mfano kwa wengine. Fikiria jinsi utoaji wa mfalme Daudi ulivyokuwa mfano kwa viongozi wengine na kwa taifa zima la Israeli (1 Nya l9:1-20). Mchungaji au mpanda kanisa ambaye hasisistizi utoaji ili kutoonekana mwenye tamaa hawafanyii wengine mema yoyote. Anawanyima watu wake nafasi ya kushiriki kwenye huduma, na kanisa linapoteza rasilimali ambazo Mungu kwa hekima yake ametoa.

> Mchungaji au mpanda kanisa ambaye hasisistizi utoaji ili kutoonekana mwenye tamaa hawafanyii wengine mema yoyote.

Kukosekana kwa uwakili pia kunaweza kurudisha nyuma upandaji wa makanisa mengine. Makundi madogo hata ya familia kumi wanaotoa asilimia kumi au zaidi ya kipato chao wanaweza kwa urahisi kisaidia mchungaji katika ngazi sawa na wanayoishi. Kwa jinsi hiyo, kama hawaelewi jukumu lao la kutoa, mpanda kanisa atahitaji kutafuta rasilimali sehemu nyingine ambazio zinaweza kutumika kupanda kanisa lingine jipya. Inatakiwa ieleweke kwamba hili halimfurahishi Bwana, anayetutaka tueneze nchi zetu kwa makanisa na wanafunzi na kwa hiyo kutimiza Utume Mkuu.

2. *Kuanzisha Mfumo Unaokubalika kwa Matumizi*

Wakristo ulimwenguni wana njia tofauti za kusimamia fedha za kanisa. Bila kujali njia, ni muhimu kwamba viongozi wa kanisa wanakadiria gharama (Lk 14:28-30) katika kupanga kwa ajili ya huduma. Makanisa mengi, wakichukulia jukumu hili bila mzaha, wanaandika bajeti ambayo kwa kifupi ni makadirio ya kiasi gani cha fedha kitahitajika kwa kipindio fulani cha mda. Bajeti inaweza ikawa ni pamoja na matumizi yanayotarajiwa kwa yafuatayo:

- Utawala/Upangaji
- Huduma za Hisani

- Huduma za Ufuasishaji/mafunzo
- Uinjilisti
- Majengo/Vifaa
- Misheni
- Mishahara
- Ibada

Bajeti inaweza ikaandikwa (pengine kwa mwaka) na hao wanaoshikilia fedha (baraza la fedha) lakini inatakiwa ipitishwe na viongozi wa kiroho wa kanisa wa ushirika. Bajeti lazima iandikwe kimaombi ikilenga mkazo wa shabaha za huduma.

3. *Funza na Toa Wahasibu wa Kanisa*

Watu watasita kutoa kama wanajisikia kwamba pesa hazitaangaliwa vema. Mipaka katika (kielelezo 2.1) ni mapendekezo ya utunzaji wa fedha katika mtindo wa kuwajibika, na ukweli.

Katika huduma yako unaweza kuchagua au usichague kuandika bajeti. Unaweza usichague kutumia mipaka iliyopendekezwa. Kitu cha muhimu siyo mfumo, lakini ni kazi. Mfumo wa kukusanya na kusambaza fungu unatakiwa uwe na: watu kadhaa, kupanga kimaombi, uwajibikaji, kukusanya kwa mara kwa mara, kutunza maandishi kiuangalifu, na kutoa taarifa mara kwa mara.

## IV. UTOAJI FEDHA NA HARAKATI ZA UPANDAJI KANISA

Harakati za upandaji kanisa kawaida zinahitaji fedha za kusaidia huduma katika ngazi mbali mbali, kutoka kwenye uhamasishaji wa mtaa mpaka kwenye yanayohitajika kwenye ngazi ya juu. Watu lazima wafunzwe na kuhamasishwa, vitu lazima vizalishwe na kutawanywa, viongozi lazima wakutane kuomba na kunoa maono, utafiti lazima ufanyike, makanisa lazima yapandwe. Vyote hivi vinahitaji fedha. Fedha hizi zinatoka wapi?

Kwa kuwa kuenea kwa injili kunahitaji kufadhiriwa, utoaji ni kipengele muhimu cha harakati za upandaji kanisa. Harakati zinachochewa na imani, na watu wa imani wanatoa vinginevyo imani yao imekufa. Yesu alielezea muujiza wa kiroho unaohusiana na utoaji wa fedha aliposema, "*Kwa kuwa palipo na mali zako, ndipo moyo wako utakapokuwa*" (Mt 6:21). Mtu anapotoa kifedha na kiuhakika *kufuatana na mtu anavyojiweza,* mtu anageuka kujitoa moyoni kwenye uwekezaji wao. Kama mtu mwingine anatunza pesa na kuzimwaga ndani ya nyumba, au ya gari, au kwenye elimu—iwe wamezilipia—hili ndilo watakalolinda na kupenda. Kama hilo litatokea kama mtu anatoa kuendeleza injili kutoka moyo wa upendo kwa Yesu. Utoaji kwa kazi ya Mungu unaongeza nia ya mtu kutoka moyoni, kuwabadilisha kwa ndani na kwa nje.

Hao wanaohusika katika harakati lazima wawe wako tayari kutoa kwa kujitoa kwenye harakati, au vinginevyo harakati hazina wafuasi wenye moyo. Kitu fulani cha nguvu sana kinatokea watu wanapoamua kwamba huduma au vipindi ni vyao na kwamba mafanikio yake au kushindwa kunategemeana na kazi ya Mungu kupitia kwao peke yake. Misaada ya nje ya fedha inaweza kusaidia harakati za upandaji kanisa, lakini kwa mda mrefu kusaidia kunamaanisha ajenda inapangwa na wa nje. Kwa maana hiyo inakuwa ya mtu mwingine tu. Hili linaweza kuua harakati.

**Kielelezo 2.1 Mipaka ya Kusimamia Zaka na Matoleo**

- Matoleo yanatakiwa yapokelewe na kuhesabiwa na angalau wajumbe wawili wa kanisa.
- Kumbu kumbu sahihi zinatakiwa zitunzwe zikionyesha kiasi kilichotolewa kwenye matoleo yote.
- Watu wote wanaohesabu matoleo wanatakiwa waandike majina yao, wakionyesha kuwa kiasi ni sahihi.
- Bodi ya Fedha ya angalau wajumbe watatu wanatakiwa wawajibike kwenye uangalizi wa mawakilisho ya matoleo kufuatana na mipaka iliyowekwa na viongozi wa kiofisi wa kanisa.
- Mhasibu anatakiwa ateuliwe kutoka kwa washiriki kutunza kumbu kumbu makini za mafungu yote ya kanisa. Mhasibu anatakiwa kutunza pesa za kanisa kwenye sehemu salama kwa matumizi ya mbeleni.
- Matoleo yanayotolewa kwa makusudi maalumu yanatakiwa yatumike kwa kusudi hilo.
- Taarifa ya mwisho wa mwaka inayoonyesha kilichokuwa kimepokelewa na jinsi gani kilitumika inatakiwa ifanywe kuonwa na wajumbe wote.

Inawezekana kwa harakati kutegemezwa kwa msaada wa fedha wa mtaa? Jibu, kama unavyoweza kutarajia, ni "*Ndiyo, inawezekana.*" Mahali ambapo wana maono yanayounguza na imani inayovuta kwenye harakati za upandaji kanisa, Mungu anatoa rasilimali, kama inavyoweza kushuhudiwa na waumini ulimwenguni, India, moja ya nchi masikini sana ulimwenguni kwa viwango zaidi vya kiuchumi ina mifano kadhaa. Kikosi cha Umishenari wa Kirafiki wa Maombi ni harakati za wenyeji ambazo zinasaidia Wahindi wamishenari 1,000 na kina wasaidizi wa maombi 30,000. Huduma inafanya kazi bila ufadhili wa nje. Badala yake, wajumbe kumi wa kikosi wanasaidia wainjilisti wao.

## SULUHU

Katika mpango wa Mungu, watu binafsi vile vile na makanisa yanatakiwa yaendelee katika ukomavu na uaminifu mbele za Mungu. Kubakia katika hali ya utegemezi hakusisimui ukomavu na imani ambayo ni ya lazima kwa misheni Mungu aliyotupatia. Waumini wengi wanakuta ni vigumu kumtumaini Mungu kwa maswala ya fedha. Lakini Mungu anatualika kumuweka kwenye jaribu kwenye eneo hili. Kama unaona ugumu kutoa kwenye kazi ya Mungu kisha leta hizo mbele za Bwana. Atajidhirisha kuwa mwaminifu.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Uko tayari kutoa kupita kipimo chako, kama Wamasedonia?
- Nini wakristo wapya wanatakiwa wafundishwe kuhusiana na utoaji?
- Unaonyesha kiasi chako cha zaka kufuatana na kipato chako tasilimu tu, au vile vile na vyanzo vingine ambavyo Mungu amekubariki navyo?
- Jinsi gani unaweza kuelezea utoaji kwa asiye mkristo anayefikiri kwamba makanisa yanaomba pesa tu?
- Ni matokeo yapi mafungu ya nje yaliyo nayo kwa kanisa la mtaa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Ordhesha mapato yako kutoka katika vyanzo vyote (yakiwemo na yasiyo tasilimu) na utoaji wako kwa wiki au mwezi. Hili ni kati yako na Mungu. Piga hesabu ni asilimia ngapi umempa. Unapendezwa na hili? Anapendezwa?
- Gawanya jumla ya matoleo ya kanisa lako kwa mwezi kwa idadi ya watu wazima waliowakilishwa kupata wastani wa utoaji kila mwezi kwa watu wazima. Zidisha tarakimu hizo kwa kumi kuona ni kiasi gani kila mtu mzima atakuwa nacho kuishi kila mwezi kama kweli matoleo yao yamewakilisha zaka. Unafikiri kanisa lako linaendeleaje? Wanahitaji maelekezo zaidi kwenye eneo hili? Kama ni hivyo, anzisha mpango wa kuwafundisha. Kumbuka kwamba kusudi la hili ni kuwasaidia waelewe uwakili, na siyo kutaka kutunga sheria ya kutaka utoaji ambayo italazimisha. Mungu anawapenda hao wanaotoa kwa uhuru.

**VYANZO**


- Pate, Larry. *Starting New Churches.* International Correspondence Institute. Irving, TX: 1984.
- Swartz, Glenn. *Dependency Among Mission Established Institutions; Exploring the Issues.* Lancaster, PA: World Missions Associates, 1996.

UWAKILI

SOMO LA 3

# Usimamizi wa Mda

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha umuhimu na matumizi ya busara ya mda kutoka katika msimamo wa Biblia na kuwapasha habari wapanda kanisa kwa kanuni za msingi za matumizi ya mda wao kiufanisi.

☞ **Wazo Kuu**

- Kuweka kitabu kidogo cha matumizi ya mda kunaweza kumsaidia mpanda kanisa kwa busara kutathimini matumizi ya kitu cha thamani—mda wake.
- Kuandika ratiba ni msaada mwingine wa ufundi wa matumizi ya mda.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa

- Kuelewa kanuni za kibiblia kuhusiana na matumizi ya mda.
- Kujua kanuni ya umuhimu wa mda na hitaji la kuchukua hatua za kutumia mda kwa busara katika maeneo yote ya maisha yako.
- Kushiriki katika kutumia zana ambayo inaweza kusaidia mpanda kanisa kufanya matumizi mazuri ya mda.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Inapendekezwa sana kwamba mkufunzi anaanza kujiandaa kwa ajili ya somo hili vya kutosha kabla ili kuipitia sehemu ya "Uwekaji wa Kimazoezi' mwenyewe. Kwa kifupi somo hili litachukua zaidi kwenye maana kama mkufunzi ana uzoefu binafsi wa kimazoezi na zoezi hili. Chukua mda kushirikisha uzoefu wako wa mafanikio/kushindwa katika kuweka muhutasari na kuainisha ratiba, vile vile na upangaji wa malengo yako, kujumlisha ratiba mpya ya kila siku ambayo inatokana na kufanyia kazi zoezi hili. Kadiri utakavyolifanya zaidi somo hili kuwa la binafsi ndivyo litakavyokuwa na mguso zaidi kwa hao unaowafunza.

## UTANGULIZI

Hapaonekani kuwa na mda wa kutosha kwa siku kukamilisha kila kinachotakiwa. Mwenzi wako anasema unahitaji kutumia mda mwingi nyumbani na watoto. Waumini wapya wanahitaji mda wa kutosha kuweza kufuaswa. Kiongozi ajaye wa kikundi kiini anahitaji kukuona. Kuna hao ambao kawaida wanaumwa na wanahitaji kutembelewa. Na usisahau kuhusu mda wa kujiandaa kwa ajili ya kujifunza Biblia na mahubiri ya jumapili. Orodha ya kazi, hayo yanayokula mda, yanaendelea na kuendelea. Na usisahau mda kwa ajili ya Mungu. Na vipi mda kwa ajili yako mwenyewe? Unahitaji mda kufikiri kutembea kwako na Mungu, malengo yako katika maisha, huduma yako na wapi inaelekea. Pia unahitaji mda wa kupumzika.

> Matumizi sahihi ya mda yanaweza yakakusaidia kutawala mda wako kuliko mda ukutawale.

**MDA:** Zawadi ambayo Mungu amempa kila mmoja wetu. Ni rasilimali yenye thamani; mara unapotumika hauwezi kurudi. Kama rasilimali, mda unahitaji kutumiwa kwa busara na mtazamo wa kila mara mpaka milele. Matumizi sahihi ya mda yanaweza yakakusaidia (kwa msaada wa Bwana) kutawala mda wako kuliko mda ukutawale. Tunatambua kuwa utafiti mwingi juu ya matumizi ya mda unafanywa kutoka katika mtazamo wa Matumizi yote yanaweza yasitumike katika utamaduni wako. Lakini kwa kiwango kwamba unaweza ukayatumia,

tunaamini utakuta yanasaidia. Somo hili litatoa mipaka ya wapi unatakiwa kutumia mda wako na kutoa njia za vitendo za kutumia mda wako kwa njia zinazomletea heshima Mungu.

## I. KUWEKA VIPAO MBELE—KUJIFUNZA JINSI YA KUTUMIA MDA

Matumizi ya mda kwa ukubwa ni swala la thamani au, hasa hasa zaidi, *vipao mbele.* Vipao mbele vinavyoeleweka wazi wazi vinatakiwa viwe msingi wa kupanga mda. *Vipao mbele vinawezesha maisha na huduma kuwa na kusudi badala ya kuwa hali ambayo misuko suko inatawala maendeleo*. Kwa maana, somo hili hasa linahusu kuweka vipao mbele katika maisha na huduma.

### A. Kanuni za Kibiblia za Kutunza Mda

- Maisha yako ni ya Mungu; mfanye kuwa Bwana wa mda wako (Zab 24:1; Yak 24:15).
- Mda ni rasilimali adimu—utumie kwa busara (Efe 5:15-17). Tumika ukiwa na hisia za uharaka na ufahamu kwamba maisha yako yanaweza yakakoma wakati wowote (Zab 39:4-5).
- Weka vipao mbele na jitoe kwenye mda kufuatana na vipaji na vipawa alivyokupa Mungu (1Pet 4:10; Mit 16:3). Mda unatakiwa utumike ipasavyo (Omb 3:1-8).
- Uwakili wa kweli wa mda unaletea baraka nyingi sana kutoka kwa Bwana (Mt 6:20; zab 37:23-24).
- Matumizi ya mda yanawakilisha ujumbe wazi kuhusu kiwango cha thamani yako (Efe 5:15-17).

### B. Vipao mbele Kwa Mpanda kanisa

Matumizi ya mda ni, kwa sehemu, swala la kujitoa. Jinsi mtu anavyofanya mda wake kunaonyesha nini alichojitoa kwa ajili yake—hata anachopenda. Kama ratiba yako iko kiasi kwamba huwezi ukatumia mda na watu wanaokuhitaji, kisha inaweza ikaonyesha kukosekana kwa kujitoa kwao. Kujitoa kwa wengine kunatakiwa kuonekane kwa namna tunavyotumia mda.

Upendo wetu kwa Mungu na wengine (Mt 22:37-39) unatakiwa uguse matumizi yetu ya mda. Hasa hasa vipaombele vifuatavyo vinaweza kutumika kuongoza matumizi yetu ya mda.

1. *Mda wa Kila Siku wa Sala na Maombi kwa Mungu*

   Ushirika na Mungu inatakiwa iwe kipao mbele chako cha kwanza. Kuwatumikia wengine kwa njia sahiihi haiwezekani bila uwepo wa Mungu na nguvu zinazotokana na mda wa binafsi na Yeye.

2. *Mda na Familia (1Tim 3:4-5; Tit 1:6)*

   Mda unaotumiwa na familia ni mda wa thamani. Hadhi ya familia ya mpanda kanisa moja kwa moja inaendana na kufaa kwake kwenye huduma kwenye mandhali ya kanisa. Fanya mda wa familia kama kipao mbele.

3. *Shughuli za Huduma Zinazohusiana na Huduma ya Upandaji Kanisa (Efe 4:11-13)*

   Una jukumu la kuinjilisha, kufuasa, kufundisha na kuwatoa wengine. Ufunguo kwa shughuli zote hizi ni kuanzisha mahusiano, ambako kunahitaji mda. Utahitaji pia kuweka kipao mbele cha mda wa kujifunza Biblia, maandilizi ya mahubiri, usimamizi wa ofisi, kutoa ushauri n.k.

4. *Huduma kwa Jumuia au Kuifikia Jumuia (Mt 28:19-20, Mdo 1:8)*

   Upandaji kanisa ni shughuli ya kiuinjilisti. Ni lazima uwe nje kwenye jumuia miongoni mwa hao unaowainjilisha.

## II. UWEKAJI KIVITENDO

### A. Weka Kitabu cha Matumizi ya Mda Uliopo

Njia zaidi ya vitendo za kuweka ratiba ya mda wako kwanza ni kuandika jinsi unavyotumia mda wako kila siku kwa mda wa kipindi cha wiki moja. Unafanya nini na mda wako? Tumia mchoro (Kielelezo 3.1) ufuatao kuandika, saa kwa saa, kila kitu unachofanya kila siku. Hii itakusaidia kuonyesha vipao mbele vyako. Hili siyo zoezi la kufanya kila siku ya maisha yako,

lakini badala yake ni zana ya kuonyesha endapo kama matumizi yako halisi ya mda yanaoana na vipao mbele vyako.

**Kielelezo 3.1 Kitabu cha Mda**

## KITABU CHA MDA

**MAELEKEZO:** *Kitabu hiki kinakusaida kutathimini jinsi unavyotumia mda wako kila siku. Kaa na kitabu hiki na andika kila namna unavyotumia kila saa kwa wiki nzima. Hii itakupa picha halisi ya jinsi hasa unavyotumia mda wako kinyume na jinsi ambavyo ungependa kuutumia mda wako kwa makusudi ya Mungu kwako.*

| | Jum | Jm | Jn | Jt | Alh | Ij | Jms |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | | | | | | | |
| 1:00 | | | | | | | |
| 2:00 | | | | | | | |
| 3:00 | | | | | | | |
| 4:00 | | | | | | | |
| 5:00 | | | | | | | |
| 6:00 | | | | | | | |
| 7:00 | | | | | | | |
| 8:00 | | | | | | | |
| 9:00 | | | | | | | |
| 10:00 | | | | | | | |
| 11:00 | | | | | | | |
| 12:00 | | | | | | | |
| 1:00 | | | | | | | |
| 2:00 | | | | | | | |
| 3:00 | | | | | | | |
| 4:00 | | | | | | | |
| 5:00 | | | | | | | |
| 6:00 | | | | | | | |

Baada ya kujaza kitabu cha mda kwenye kielelezo 3.1, tenga shughuli zako. Tumia mchoro kwenye kielelezo 3.2 kama kiongozi. Tambua kwamba orodha kwenye mchoro huu siyo ya kuchosha. Unaweza ukataka kuandaa aina yako ambayo inafaa kwa mtindo wa maisha yako mwenyewe.

### Kielelezo 3.2 Mchanganuo wa Matumizi ya Mda

**MCHANGANUO WA MATUMIZI YA MDA**

**Maelekezo:** Kufuatana na habari ulizoandika kwenye kitabu cha mda, tenga matumizi ya mda wako kwenye makundi kadhaa makubwa. Andika jumla ya idadi ya masaa kwa kila kitengo.

| | Kitengo | Jumla ya Saa |
|---|---|---|
| **1.** | *Kawaida ya kila asubuhi. Tambua inachukua mda kiasi gani kuvaa,* kula n.k. | |
| **2.** | *Sala ya kila siku. Tambua lini na mda kiasi gani unatumia katika sala ya kila siku.* | |
| **3.** | *Mwenzi. Ni mda kiasi gani unatumia na mwenzako? (kwa mfano: mda wa pamoja, mda wa mmoja kwa mwingine mkisoma pamoja, kuomba pamoja, etc.)* | |
| **4.** | *Familia. Ni mda kiasi gani unatumia pamoja na familia yako (sala ya familia, kusaidia watoto kwa kazi za shule, kucheza mchezo, kutembea, n.k.).* | |
| **5.** | *Huduma. Jinsi unavyotumia mda wako ofisini au kanisa (kuandaa mahubiri, kupiga na kupokea simu, mikutano, nyumbani, kutembelea hospitalini n.k.)* | |
| **6.** | *Mlo. Lini na wapi unapata mlo wako na unakuwa na akina nani.* | |
| **7.** | *Kawaida ya kila jioni. Unachofanya kila jioni (kujifunza Biblia, kampeni za uinjilisti, mapendeleo n.k.)* | |
| **8.** | *Kulala. Unapokwenda kupumzika kitandani. Unapata usingizi wa kutosha kila usiku?* | |
| **9.** | *Mengine.* | |

### B. Changanua Matumizi ya Mda Wako

Sasa kwamba unaweza kuona wazi wazi jinsi unavyotumia mda wako, vipao mbele vyako vitadhihirika. Hakuna kadiri ya moja kwa moja kati ya kipimo cha vipao mbele na mda uliotumika, lakini kuna hali ya kukubaliana. Kwa mfano, kama mwenzi wako ni kipao mbele na hutumii mda wowote maalumu pamoja naye, kisha mda unatakiwa kurekebishwa kuwa na hakika kwamba uhusiano wako ni wa kujitoa hasa.

Njia za kukuza matumizi ya mda wako zinatakiwa sasa ziwe wazi. Angalia katika kitabu chako cha mda (kielelezo 3.1) na mchanganuo wa matumizi ya mda wako (kielelezo 3.2) na jibu maswali yafuatayo kugundua vipande:

- Ni shughuli zipi unafanya kwa kurudia rudia?
- Unatoa kipao mbele kwenye maeneo muhimu zaidi ya maisha yako?
- Kuna kuingilia kunakoendelea kwa mda uliopotea?
- Ni mabadiliko yapi maalumu unayotaka kufanya kwenye ratiba yako?

Unatakiwa uwezo kutambua vipao mbele vyako vya wakati huo: wajibu mkuu na majukumu katika maisha yako. Orodhesha vitu ambavyo ni muhimu zaidi kwako kwenye nafasi ifuatayo:

Mchanganuo wako wa matumizi ya mda unaonyesha vipao mbele hivi? Ni marekebisho yapi ungependa kufanya?

**C. Andika Ratiba Inayowezekana**

Kwa kutumia kitabu cha mda (kielelezo 3.1) panga ratiba yako tena kwa wiki ijayo, kufuatana na vipao mbele vyako vile vile na kile ulichojifunza kwenye uchunguzi wa wiki iliyopita. Kama unajisikia kana kwamba kulikuwa na vitu fulani vilivyokosekana kutoka kwenye shughuli zako, kisha weka mda kwa ajili yake. Inaweza ikawa vema kufanya mabadiliko kwenye ratiba yako ya kawaida kwa nyongeza kidogo.

1. *Chagua angalau kipao mbele kimoja na panga mda maalumu kufikia kipao mbele hicho. Tambua mifano hii.*

**Mfano #1**

KIPAOMBELE: *Uhusiano wangu na Bwana.*

LENGO: *Amka saa moja mapema kwa asubuhi tatu kila wiki kuomba. Hii inaweza ikamaanisha kwenda mapema saa moja kabla kulala kuhakikisha kuwa na kiasi cha usingizi wa kutosha.*

**Mfano #2**

KIPAOMBELE: *Uhusiano na mwenzi wangu.*

LENGO: *Panga mda maalumu kila wiki kujitoa kipekee kwa mmoja kwa mwingine.*

2. *Ondoa vitu hivyo ambavyo siyo vya kufaa kutumia mda au kipao mbele.*

   Unafanya vitu hivyo ambavyo watu wengine kanisani wana ujuzi navyo wote zaidi na wako tayari kuvifanya? Jifunze kufuasa watu na kugawa majukumu kwao. Saidia wengine kugundua na kutumia vipawa vyao vya kiroho na kujaliwa kwa kawaida. Waongoze katika maendeleo yao yanayoendelea kama viongozi. Gawa kazi kwa hao walio chini ya uongozi wako haitasaidia kuokoa mda tu, lakini itawasaida kukomaa katika maisha yao ya kikristo.

3 *Panga mda wa familia*

   Mda unaotumiwa na familia yako ni wa thamani sana. Hadhi ya mpanda kanisa moja kwa moja inaendana na sifa zake za huduma katika mandhali ya kanisa (1Tim 3:4-5).

4. *Weka ratiba ya shughuli za huduma*

   Hii ni pamoja na mda wa kujifunza, kufikia nje kiuinjilisti, uongozi wa kanisa, ufuasishaji, mafunzo ya uongozi, matukio ya maombi, na kutembelea, n.k.

5. *Weka ratiba ya mda wa kupumzika*

   Weka akilini kwamba unapopumzika hauko unapoteza mda. Kupumzika kutahakikisha afya nzuri na huduma yenye nguvu zaidi kwa siku nzima. Unaweza ukahitaji kusinzia kidogo kati kati ya siku kuwa na nguvu kwa ajili ya huduma ambayo mara nyingi inaisha jioni sana. Unahitaji kufikiria kwa maombi na kwa uangalifu amri ya maandiko ya kupumzika. Kama mpanda kanisa jumapili yako (siku "halisi ya kupumzika") itakuwa siku ngumu kwako. Wachungaji wengi wanaokutana na msahangao wa uchaguzi huo huo wanachagua siku nyingine, kama vile jumatatu, kama "siku yao ya kupumzika."

6. *kazania uwiano katika wiki yako.*

   Kama una ratiba nzito siku moja, fanya ratiba nyepesi kwa siku inayofata

**D. Chunguza Maendeleo Yako**

Ujuzi wako katika kufanya matumizi mazuri ya mda utaongezeka unapofanyia kazi hatua zifuatazo. Unaweza ukataka kuwajibika kwa mtu fulani kufuatana na malengo uliyoweka. Kama kweli unataka kujifunza kuweza mda wako ili kuwa wakili mwema, kisha utachukua hatua zozote ambazo ni za lazima kuweza kuleta mabadiliko yanayotakiwa. Fikiria kuweka katika ratiba yako mda mchache kukutana na mtu fulani unayemuheshimu na ambaye amekubali kuwepo kwa ajili yako. Kuwajibika kwa wote na ushirika kutakuwa kwa thamani kwa maisha yako yote.

**SULUHU**

Siyo dhambi kupanga, kuweza mda wako, kuweka ratiba ya siku yako, wiki, mwaka na hata maisha yako. Kwa hakika, ni kinyume chake. Utumiaji mzuri wa mda unaweza kukaongeza ufanisi wa huduma na kumletea heshima Bwana. Uwezekano wa dhambi upo pale kama tunapunguza umuhimu wa uhusiano katika utumiaji wetu wa mda. Mda ni rasilimali lakini kuweka mkazo usiofaa kwenye mda kunaweza kuharibu uhusiano badala ya kuujenga. Uwe mwangalifu katika upitilizaji. Tafuta kuwa na uwiano katika eneo hili.

> Kama tunashindwa kupanga, tunapanga kushindwa!

Unafahamu vizuri kwamba wapanda kanisa, kwa asili yao halisi ya kazi yao, ni watu wenye kazi nyingi. Matumizi ya mda yatakusaidia, kama mpanda kanisa, kuwa mfanisi zaidi. Kuna mithali ya zamani ambayo inaweza ikaweka kwa kifupi somo la matumizi ya mda: KAMA TUNASHINDWA KUPANGA, TUNAPANGA KUSHINDWA!" Kutathimini matumizi ya mda wako kwa vipindi, kwa kutumia mazoezi katika somo hili, kunaweza kukusaidia kuhakikisha kwamba unatumia mda kwa busara.

Sote tunataka siku moja kusikia kutoka kwa Bwana wetu, "kazi njema, mtumishi mwema na mwaminifu." Ni matumaini yetu kwamba somo hili litakusaidia kupata"kazi njema" katika maisha yako na huduma.

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Soma Luka 10:38-42. Tambua vipao mbela vya Mary na Martha. Jinsi gani mistari hii inaendana na somo hili? Ni yupi kati ya watu hawa unafanana naye zaidi?
- Soma Luka 4,6,9,11. Tambua jinsi Yesu alivyotenga mda wa kuomba. Unafanya hili vile vile? Unaomba pamoja na mwenzi wako mara moja moja kuhusiana na maisha yako na huduma?
- Kusoma kwa uangalifu kwa Luka 9:51-62 kunaonyesha kwamba Yesu alikuwa na kazi fulani ambazo alitakiwa kuzikamilisha kwa mda wa kipindi fulani. Nini ilikuwa kazi hiyo? Umuhimu wa kazi hii ulikuwa na matokeo yoyote juu ya uhusiano wake na watu? Unafikiri kwamba kimakusudi alipanga kwa ajili ya mda wa ziada kwenye kazi hii ili kwamba aweze kuendelea kukazania kwenye mahusiano?
- Soma Kutoka 18 na tambua jinsi Musa alivyotatua tatizo la matumizi ya mda wake.
- Soma mfano wa talanta unaopatikana katika Mathayo 25:14-30. Badilisha neno "talanta" kwa neno "miaka" na jina lako kwa jina la mtumishi wa kwanza aliyepokea talanta tano. Umepata miaka mitano kutoka kwa Bwana. Shirikisha ambavyo umewekeza katika mda wa Mungu ambao anakusifu na hatimaye kumuletea utukufu.

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Soma kitabu cha Nehemia na angalia matukio ambapo Nehemia alionyesha hali yoyote ya matumizi ya mda ambayo yamezungumziwa katika somo hili.
- Anza kuratibu shughuli zako za kila siku kwa wiki moja. Changanua matokeo na kisha weka lengo kuweka mabadiliko katika utumiaji wa mda. Mwambie ama mwenzi wako au rafiki wa caribú lengo lako ni lipi na mjulishe mtu huyo kila wakati maendeleo katika kulifikia lengo.
- Anzisha mpango wa kupunguza mda wako wa kuhusika katika badhi ya matukio ya huduma yako kwa kuitoa kwa wengine. Shirikisha lengo hili kwa mtu fulani na wajulishe maendeleo yako.

UWAKILI

SOMO LA 4

# Utaratibu wa Upangaji Kimkakati

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwatambulisha wafunzwa kwenye njia za vitendo za upangaji kimkakati ambazo zinaweza kutumika katika ngazi yoyote ya huduma na kuwaruhusu kuweka vipao mbele na kuunga shughuli za huduma kwenye makusudi ya huduma.

☞ **Wazo Kuu**

- Upangaji kimkakati ni utaratibu.
- Upangaji kimkakati ni zana ya kukusaidia kuendelea kukazia kwenye kusudi la huduma yako.
- Kama unashindwa kupanga, unapanga kushindwa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa

- Kuelewa jinsi ya kuanzisha mpango wa kimkakati wa huduma ya upandaji kanisa.
- Kujua jinsi ya kutafsiri makusudio na kuweka malengo yanayopimika.
- Kushiriki katika utaratibu wa uandaaji wa mpango wa kimkakati kwa ajili ya huduma ya upandaji kanisa.

## I. NI NINI UPANGAJI WA KIMKAKATI?

Upangaji kimkakati ni njia ya kusaidia timu ya upandaji kanisa kuwa ya ufanisi zaidi na mafanikio katika kazi zao za upandaji kanisa. Ni utaratibu ambapo wajumbe wa timu ya upandaji kanisa wanajiunga wenyewe, familia zao, huduma zao—kila kitu—kwenye mkakati wa “Z” ambao wameugundua kwa ajili ya huduma yao ya upandaji kanisa. Baada ya kufanyia kazi mpango wa kimkakati, timu ya upandaji kanisa wanatakiwa waweze kuelewa na kutofautisha kati ya shughuli “bora”—hizo ambazo zitachukua kueneza upandaji wa kanisa kufanya kazi zaidi, haraka—na shughuli “njema—shughuli hizo zolizo na nafasi katika maisha ya kanisa lakini hazileti kwa haraka eneo lote kwenye ufahamu wa Yesu Kristo. Upangaji kimkakati unasaidia timu kutafsiri mwelekeo wake, chama chao na rasilimali zao za kukamilisha kazi maalumu kuelekea kufikia “Z.” Upangaji kimkakati siyo kuhusu mpangilio mzuri; ni kuishi kimakusudi, ukikazia katika mda na nguvu Kwenye shughulu “bora” za kile Mungu anachotuita kufanya: kuoma maeneo yetu yakijazwa na makanisa hai.

**Mifano ya Kibiblia ya Upangaji Kimkakati**


Katika zote Agano la Kale na Agano Jipya, upangaji kimkakati ni dhahiri.

- Yusufu, kwa hekima aliyopewa na Mungu, alianzisha na kuweka mpango wa kuwaokoa wamisri na maeneo ya mataifa yanayozunguka kutokana na janga wakati wa miaka saba ya njaa (Mwa 41).
- Nehemia alichunguza maangamizi ya mji wa Yerusalemu na akaanzisha na kuweka mpango wa kuujenga upya ukuta wa mji bila kujali vikwazo vingi na hatari.
- Maisha ya Yesu na huduma yanaonyesha kwamba alikuwa na mpango halisi na njia halisi za kutimiza kusudi hilo. Kwa mfano, Yesu kwa ujasiri alielekeza hatua zake kuelekea msalabani (Mt 16:21-23). Alikazia huduma yake kwa wanafunzi 12 na miongoni mwa Wayahudi.

## II. UTARATIBU WA UPANGAJI KIMKAKATI

Upangaji kimkakati ni utaratibu wenye hatua nyingi na una vipengele vikuu vitano: thamani ya kati kati, utofauti, makusudio na malengo. Kwa pamoja vinaunda mpango wa kimkakati. Mpango huu unaanzishwa na kuwekwa kuendana na wakati mara kwa mara kufuatana na utaratibu ulioonyeshwa hapo chini. Upangaji unatakiwa usifanyike bila maombi ya kutosha kabla na wakati wa utaratibu wa upangaji. Kazi ya upandaji kanisa ni kazi ya kiroho na kwa hiyo inahitaji utegemezi kwa Mungu kwa ajili ya hekima na kuwa na akili ya Kristo (Yak 1:5-7; 1Co 2:16). Utaratibu wa upangaji kimkakati unafanyika vema angalau na watu wawili.

**Kielelezo 4.1 Utaratibu wa Upangaji Kimkakati**




Ni muhimu kukumbuka kwamba matokeo ya mipango ya kimkakati siyo yasiyobadilika. Badala yake, ni mipango ya kufanyia kazi ya kile wewe na timu yako mnachoona kuwa ni shughuli bora za kufanya, katika wakati huu, ili kuendelea kuelekea kwenye "Z." Mnapoanza kuweka shughuli zilizogunduliwa kwenye mpango wenu, mnaweza kutambua maswala mengine au fikira ambazo zinaweza kusababisha marekebisho kwenye mpango wako. Hii ndiyo maana ya kufanya marudio ya mpango wako wa kimkakati mara kwa mara. Mpango unatumika tu kama unakusaidia kuishi zaidi kimakusudi na kutunza huduma yako ikikazia kwenye shughuli muhimu zaidi.

### A. Hatua 1: Omba

Pamoja na timu yako ya upandaji kanisa, omba kwa ajili ya hekima na uwazi wa maono kutoka kwa Mungu. Muombe Mungu kuongoza na kuelekeza mda wako wa upangaji, kuwasaidia kusikilizana, na kuwa na "akili ya Kristo" katika upangaji wako. Kwa nyongeza, pata msaada wa marafiki kadhaa wa kuombea timu yako mnapokuwa mnafanyia kazi utaratibu.

### B. Hatua 2: Andika au Tazama Upya Marudio ya Maelezo Yako ya Kusudi

Maelezo ya kusudi ni msingi wa upangaji wako. Tazama upya eneo ulilolenga kwa ajili ya huduma yako, endapo ni ujirani, kijiji, mji, tarafa au nchi. Tazama upya tena pia aina ya huduma ambayo Mungu amekuitia kufanya—upandaji kanisa, kuhamasisha maombi, usambaji wa maandishi—kufuatana na eneo linalolengwa na huduma yako.

Tazama upya maelezo ya kusudi uliyoandaa mapema kwa ajili ya huduma yako. Kama hujafanya hili bado, kisha andika maelezo yako ya kusudi. Maelezo yako ya kusudi yanatakiwa yawe sentensi moja au mbili na yanatakiwa yajibu swali, “kwa nini timu yetu (au kundi) lipo?” na yanatakiwa yaonyeshe yote eneo lako linalolengwa na huduma yako.

Baadhi ya mifano ya maelezo ya kusudi ni:

- Timu hii ipo kuwezesha wana injili kujaza Urumi kwa makusanyiko yanayozaliana. (Timu ya uwezeshaji wa upandaji kanisa kitaifa).
- Timu hii ipo kujaza nchi hii kwa makanisa yanayozaliana. (Timu ya upandaji kanisa).
- Timu hii ipo kusaida huduma ya maombi ya mtaa kwenye mji huu kuomba pamoja na kwa maombi zaidi kusaidia kazi ya upandaji kanisa kwenye mji. (Timu ya maombi).

Katibu aandike maelezo ya kusudi kwenye ubao (au karatasi) ili kwamba muweze kuiangalia kwa pamoja. Pamoja na timu yako chukua mda wa kuangalia upya maelezo haya ya kusudi na mjiulize maswali yafuatayo:

- Bado maelezo haya yanaonyesha kusudi letu, au limebadilika?
- Maelezo haya yanakubaliana na thamani yetu ya kati na utofauti? Kama siyo, nini tunahitaji kubadilisha kuyafanya kukubaliana?
- Maelezo ya kusudi ni wazi na mafupi?
- Je maelezo ya kusudi yanatafsiri “Z” yetu—eneo linalolengwa au kundi la watu tunaojaribu kuwafikia na aina ya huduma tuliyoitiwa kufanya?

Kama ni lazima, fanya mabadiliko kwenye maelezo ya kusudi lenu kwa kujibu maswali yafuatayo. Weka maelezo ya kusudi yaliyofikiwa mbele ya timu kurejea wakati wa utaratibu uliobaki wa upangaji.

### C. Hatua 3: Onyesha kwenye Thamani ya Kati na Utofauti

**Thamani ya kati** ni misingi, kibiblia sura zinazohusiana ambazo umejitoa kwake na kwa heshima kubwa. Wewe na timu yako mnapoonyesha nini ni thamani yenu ya kati, njia pekee ya kuwa kwenye eneo salama ni kufuatisha kila thamani kwenye maandiko. Thamani hizi zitawasaidia kutambua kile unachofanya na kile usichofanya. Mkakati wowote unaoanzisha ambao hauendani na thamani yako ya kati pengine unaonekana kushindwa au kuwa wa uharibifu.

*Badhi ya mifano ya thamani ya kati:*

- *Kanisa la Mtaa:* Tunaamini kwamba kanisa la mtaa ni chombo cha msingi cha Mungu cha uinjilisti na kulisha neno, yaani njia kuu anayotumia kufanya kazi yake.
- *Kuzidisha:* Mtindo wa kuzidisha, badala ya mtindo wa kuongeza, ndio mtindo pekee wa kanisa unaozaliana ambao kamwe unaweza kufikia lengo la kufuasa taifa zima.
- *Uongozi wa kitumishi:* Tunaamini uongozi wa kitumishi unatakiwa kuanzishwa kwa uwezeshaji na utoaji watu waliojaliwa vipawa.
- *Kuwajibika:* Kama timu tunaamini ni lazima tuwajibike kwa mmoja kwa mwingine, kwenye kanisa la mtaa, na kwa viongozi wetu. Tunaamini kuwa kupitia kuwajibika kwetu kwenye makundi haya, tunawezaa kutunza uhusiano wa karibu na Bwana wetu na Mwokozi, Yesu Kristo.
- *Uaminifu:* Tumejitoa kwenye thamani za kikabila tunapojiendesha wenyewe kwenye kazi hizi: Ubora, ukweli, uaminifu katika fedha…

***Utofautu*** ni vitu vinavyokufanya tofauti. Vinasaida kutafsiri ulivyo. Vinadhihirisha unayojulikana na jinsi unavyojihusisha kwa wengine. Vinaweza kutoa mipaka ambayo inadhuru ushirika na wengine, picha nzuri au mbaya. Vinatakiwa kukusaidia kutokwenda nje ya mwelekeo kutoka kwenye kusudi lako.

Baadhi ya mifano ya utofauti ni:

- Tunafanya kazi miongoni mwa waislamu tu.
- Tunakazia juhudi zetu kwenye kufunza wakufunzi wa wapanda kanisa.
- Tunatafuta kushirikiana na madhehebu yote ya kiinjili na mashirika yanayofanya kazi katika eneo letu linalolengwa.

***Tambua thamani ya kati na utofauti wa huduma yako ya timu.*** Hii ni shughuli nzuri ya kuchangia mawazo. Wafanye wajumbe wa timu kusema wanachofikiri kuwa thamani na utofauti wa timu. Mwandishi anatakiwa kuandika kila mawazo yanayochangiwa. Kinachofata, iangalie orodha. Tathimini thamani na utofauti ambao ulitajwa wakati wa shughuli ya kuchangia mawazo. Zinaonyesha thamani ya kibiblia? Timu inakubaliana kwamba hizi ni thamani na hizi ni utofauti wa timu yako? Weka alama ya x au fanyia kazi tena thamani yoyote au utofauti ambao hauwakilishi timu yako. Mwandishi aandike orodha iliyofikiwa mwishoni ya thamani ya kati na utofauti kwenye karatasi kubwa ili kwamba iweze kutunzwa akilini wakati uliobaki wa utaratibu wa upangaji kimkakati.

### D. Hatua 4: Tambua Makusudi Yako

Mara unapotambua kusudi lako, thamani yako ya kati na utofauti, hatua inayofata ni kutambua makusudi yako. Makusudi yanajibu swali ya jumla, “Mtafanya nini?” Nini ni msukumo mkuu wa huduma yenu? Nini mwelekeo wa jumla ambapo timu yako itaelekeza juhudi zake? Makusudi ni kitengo cha jumla cha shughuli utakazohusika munapokuwa mnafanya kazi kuelekea kutimiza kusudi lenu. Baadhi ya mifano ya makusudi ya huduma ya upandaji kanisa ni:

- Kutafiti eneo linalolengwa na watu
- Hamasisha maombi kwa ajili ya upandaji kanisa
- Injilisha
- Funza na shauri viongozi kwa makanisa yanayoibuka
- Funza na shauri wapanda kanisa
- Endeleza vikundi kiini vinavyozaliana
- Hamasisha makanisa mengine kwenye eneo kwa ajili ya upandaji kanisa

Hii ni shughuli nzuri ya kuchangia kama ifuatavyo:

- Uliza timu, “Ni eneo lipi tutaendelea kukazania nguvu zetu kwa miaka mingine mitatu ijayo?”
- Wafanye wajumbe waseme kile wanachofikiri makusudi ya timu ni nini. Mwandishi anatakiwa kuandika kila wazo linalotolewa.
- Inayofata, iangalieni orodha. Tathimini makusudi yaliyotajwa wakati wa shughuli ya kuchangia mawazo. Yanakubaliana na maelezo ya kusudi lenu, thamani ya kati na utofauti? Weka alama ya mkato au fanyia kazi upya makusudi yoyote ambayo hayawasaidii kutimiza maelezo ya kusudi lenu au hayaonyeshi thamani na utofauti wenu.
- Weka kipao mbele orodha hii na igawanye isizidi makusudi saba. Timu nyingi au watu binafsi kawaida hawawezi kufanyia zaidi ya makusudi saba tofauti kwa mda.
- Mwandishi aandike orodha iliyofikiwa ya makusudi kwenye karatasi kubwa yenye nafasi ili kwamba malengo yaweze kuongezwa.

### E. Hatua 5: Weka Malengo

Katika kuweka malengo, hasa hasa unatoa tafsiri ya hatua maalumu utakazochukua katika kipindi maalumu cha mda (miezi mitatu, sita, mwaka mmoja…) kufikia makusudi yako. Wakati makusudi yakiwa situ cha kawaida kiasili, malengo ni maalumu kiasili. Kuweka malengo kunawasaidia kusogea kutoka kuzima moto kwenda kwenye kuzuia moto—kutoka kuitikia kwa kifupi kwenye uharaka kwenda utumiaji wa kilicho muhimu. Kutafsiri malengo maalumu, wazi, yanayopimika itakufanya kuzifikia hatua, A, B, C… ambazo hatimaye zinafikia "Z" kusudi lenu. Lengo lililoandikwa vema linaweza likachukuliwa na mtu yeyote na kuelezewa kikamilifu kwa mwingine, hata kama mtu huyo hajui chochote kuhusu kuandikwa kwa lengo hilo. Malengo mazuri yana tabia zifuatazo:

- **Kiwango cha mda**. Lengo zuri linahitaji kuwa na kiwango cha mda maalumu katika kumalizika kwake. Kiasi cha mda kitategemeana na unachodhani kuwa cha lazima katika kumaliza kazi. Kama unafanya upangaji wa kimkakati mwisho wa mwaka, mda wa juu wa kukamilisha malengo yenu unatakiwa uwe kati kati ya mwaka ujao. MFANO: Kufikia MWISHONI MWA MWEZA WA SITA...
- **Kuweza kumalizika**. Lengo zuri litamfanya mtu "kukujua" ili kumaliza kazi. Mda huo huo haitaweka kazi nje ya mahali mtu anapoweza kufika. Kama malengo hayawezekani kukamilisha, kawaida kutakuwa na kusita hata kujaribu kukamilisha lengo. MFANO: ANDAA MASOMO MATATU YA KUJIFUNZA KWA KUFATA NENO...
- **Kupimika**. Lengo zuri litakuwa na njia za kupima kama au la lengo limefikiwa. Kuna njia nyingi za kupima: kwa kuandika, kwa kuongea, kwa kufanya baadhi ya kazi, kwa kuchunguza baadhi ya vitu…kama huna kipimo cha kupimia, kisha kunakuwa hakuna njia ya kujua kama au lini linafikiwa. KWA MFANO: KUONGOZA MAFUNZO YALIYOANDALIWA KATIKA KIKUNDI KIINI CHANGU...
- **Lugha Inayoeleweka**. Lengo zuri litatumia lugha inayoeleweka wazi kuwakilisha ni kazi ipi iliyo wazi ya kukamilisha. Mara nyingi maneno kama "jua" na "elewa" yanatumika katika kuandika malengo, lakini maneno haya yako kwenye tafsiri nyingi. Kwa mfano, ni njia ngapi ziko pale za "kujua" kitu fulani? Tunajua vitu kwa kuhisi kwetu, kwa hiyo kuna angalau njia tano za "kujua." Kama "kujua" unawezeshwa na "jinsi gani"," kisha inaweza ikaruhusiwa kutumika. Tena, jinsi gani unaweza kupima "kuelewa"? Maneno yanahitaji kuchaguliwa kwa uangalifu kuhakikisha yanawakilisha kilichokusudiwa.

> **Mfano Lengo**
>
> Mwishoni mwa mwezi wa sita nitaanda na kuongoza mfuatano wa masomo matatu ya kujifunza kwa kufuata neno kwenye kikundi kiini changu juu ya kisa cha "Utume Mkuu na Upandaji kanisa katika mji wetu."

Ni kawaida hasa kuwepo na malengo maalumu kadhaa kwa kila kusudi. Wakati timu yako inaweza kuamua juu ya makundi manne au matano, mnaweza kuishia kwenye malengo kumi au zaidi maalumu ambayo yatawasaidia kufikia makudio yenu. Utahitaji kuona ni malengo mangapi yanahitaji kupangwa kwa kila moja ya makusudio yenu kuweza kufikiwa kiufanisi. Unatakiwa kujibu maswali yafuatayo unapokuwa unafanyia kazi malengo yako:

- Ni vitu gani vya kupimika tutakavyofanya mwaka huu kuelekea ukamilishaji wa kusudio hili?
- Jinsi gani tutakamilisha vitu hivi?
- Jinsi gani tutapima mafanikio yetu?
- Nini kitatokea kama lengo hili halikufikiwa? (Hili litakusaidia kutathimini kipao mbele cha lengo.)
- Ni ushauri upi, rasilimali, au mafunzo tunayohitaji kukamilisha lengo hili?
- Ni vipingamizi au matatizo yapi yanayohitaji kushindwa kufikia lengo hili? (Hili litawasaidia kutathimini jinsi gani lengo lenu linawezekana.)

- Nani atafanyia kazi lengo hili? Lini linatakiwa limalizike? Jinsi gani utajua kuwa umekamilisha lengo hili? (isipokuwa mpaka mtu awajibike kwenye lengo, halitaweza kuwekwa.)
- Nani anaweza kutusaidia kuwajibika kwa malengo yetu?

Mwandishi anatakiwa aandike malengo ya timu kwa kila kusudio pamoja na tarehe iliyowekwa ya kukamilisha na sehemu inayowajibika.

Unapokuwa umemaliza zoezi hapo juu, utakuwa umemaliza utaratibu wa upangaji wa kimkakati. Sasa utakuwa na maelezo ya kusudi ya huduma mikononi mwako, orodha ya thamani yako ya kati na utofauti, makusudio yako ya jumla, na malengo yako maalumu. Tumia "hati" hii kama sehemu ya kuanzia kwa kipindi cha upangaji kimkakati ujao pamoja na timu yako (kundi).

### SULUHU

- Mpango wa kimkakati unatumika tu kama unaonekana kama hati inayotumika na kuangaliwa upya kwa mda wa vipindi. Kama una malengo ambayo yana mda mfupi wa kumalizika, unaweza ukataka kuangalia upya mpango wako wa kimkakati kila robo mwaka, lakini hasa hasa nusu mwaka au kwa mwaka. Kawaida maelezo ya kusudi lako, thamani ya kati, na utofauti hayabadiliki. Ni msingi wa kile Mungu alichokuitia na timu yako kufanya. Mpaka hapo kusudi hilo linapotimizwa, linabakiwa kuwa lile lile. Kwa jinsi hiyo, unapoendelea kufanya kazi kuelekea kwenye kusudi lako, na kuelewa kwako kunakua, unaweza ukajikuta ukilainisha kusudi lako.
- Makusudio na malengo ni zana za kukusaida kuendelea kukazia katika kufikia kusudi lako. Vinakusaida kuweka kipao mbele cha kazi yako, kukazania kwenye shughuli muhimu ambazo Mungu amekuitia kufanya, na kuzifikiria kivitendo nini lazima kifanyike ili kufikia kusudi lako.
- Mwisho, lazima ukumbuke kwamba hakuna mpango ulio kamili. Ni kiongozi cha kukufanya kubakia kwenye njia. Mpango uliowekwa vyema si kitu kama Bwana hayuko kwenye kazi yako. Kama mwandishi wa Mithali anavyotukumbusha, "Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe. Katika njia zako mkiri yeye, naye atanyoosha mapito yako" (Mit 3:5-6).

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Nini tofauti kati ya upangaji kimkakati na kupangilia vema?
- Unaweza kufikiri maeneo mengine ya maisha ambapo upangaji kimkakati unaweza kutumika?
- Ni mifano ipi mingine ya maandiko, au kutoka katika maisha yako mwenyewe, ambapo umeona upangaji kiufanisi ukipelekea kwenye matokeo yenye ufanisi?
- Jinsi gani unaweza kuitikia kwenye maelezo, "Mazao ya malengo yasiyo dhahiri, kwa hali ya juu, yana matokeo yasiyo dhahiri"?
- Ni kwa njia zipi watu katika utamaduni wako wanachangia mawazo kutatua matatizo?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Fanya upangaji wa kimkakati pamoja na timu yako au uongozi wa kanisa lako linaloibuka. Uwe tayari kushirikisha mpango wako wa kimkakati kwenye kipindi kijacho cha mafunzo.

UWAKILI

SOMO LA 5

# Warsha ya Utaratibu wa Upangaji Kimkakati

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutoa zoezi kwa wafunzwa katika kuendesha kipindi cha upangaji kimkakati katika mkao wa timu.

☞ **Wazo Kuu**

- Upangaji kimkakati ni kwa lazima kwenye huduma ya upandaji kanisa.
- Upangaji kimkakati siyo kazi ngumu.

☞ **Matokeo yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua jinsi ya kuendesha kipindi cha upangaji kimkakati katika mandhali ya timu.
- Kuwa na ujasiri zaidi kuhusu jinsi ya kufanya upangaji kimkakati.
- Kujitoa kwenye kufanya upangaji kimkakati na timu ya upandaji kanisa.

Wakati wa saa hii tutaweka katika mazoezi mawazo tuliyojifunza kwenye masomo ya nyuma kuhusu upangaji kimkakati. Mtajitenga katika makundi ya watu wanne au watano kila moja na mtafanya kazi kana kwamba mu wapanda kanisa. Kwa sababu ya mda finyu, tunatwaa kuwa “timu” yako imeshaanzisha maelezo ya kusudi ya huduma yake na kuamua juu ya thamani yake ya kati na utofauti.

Kama timu mumeandaa makusudio ya huduma kuwa na **kwenda kufundisha vijana kambini siku ya mapumuziko.** Kazi sasa ni kuanzisha aina zifuatazo za malengo mkiyatumia kama kielezo cha tabia zilizofundishwa katika masomo yaliyopita.

- Anzisha lengo la jumla kwa ajili ya mafunzo ya kambi ya situ ya mapumuziko.
- Anzisha lengo kwa ajili ya shughuli maalumu wakati wa mafunzo.

Uwe na uhakika kuyaangalia malengo yako dhidi ya tabia zilizotolewa kwenye somo la mwisho kuhakikisha zinafikia sifa za malengo mazuri.

Una dakika thelathini za kufanyia kazi shughuli hii. Mwishoni mwa mda huu tutaruhusu kila kundi kushirikisha malengo yake kwa ajili ya kutazama upya na kutathiminiwa na darasa.

# FAMILIA

FAMILIA

SOMO LA 1

# Wajibu wa Kibiblia Katika Familia

**Kusudi la Somo**

Kusudi la somo ni kutoa mafundisho wazi na ya msingi kwa ndoa na nafasi ya mwanaume, mwanamke na watoto katika familia.

**Wazo Kuu**

- Katika ndoa, Mungu anaweza kuoanisha uwezo na udhaifu wa mwanaume na mwanamke kuwafanya kamili, ambako kunawawezesha kumtumikia Mungu vema.
- Huduma ya mpanda kanisa ni pamoja na familia yake, kwa kuwa familia ni kitu kinachoonekana na kimuli cha kibiblia cha uwezo wa uongozi na ufanisi wa ufuasishaji.

**Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa kusudi la ndoa kutoka kwenye mtazamo wa yule aliyeiamuru.
- Kuwa na kuelewa kuzuri kwa mafundisho ya kibiblia kuhusu nafasi ya mwanaume na mwanamke katika uhusiano wa ndoa.
- Kuelewa uhusiano wa familia kama mfano wa kanisa.

**UTANGULIZI**

Kanisa limekuwa kitovu cha amani cha ufalme wa Mungu duniani. Kati kati ya jumuia ya waumini, Mungu amewaita watoto wake wote kwenye uhusiano wa kupendana na yeye mwenyewe na mmoja kwa mwingine. Baadhi wameitwa kumtumikia Bwana na kanisa katika hali ya ubachela na wengine katika hali ya ndoa. Lakini endapo uwe umeoana au bachela, kila mmoja amewekwa katika familia.

> Kama mtu hajui kuangalia nyumba yake mweneyewe vema, jinsi gani anaweza kuangalia kanisa la Mungu?" (1Tim 3:5).

Familia ni mfano mmoja uliotumika kuelezea kanisa. Kuelewa kwako kwa uhusiano katika familia zinazoonekana kutagusa namna unavyoangalia familia ya Mungu. Ni muhimu, kwa hiyo, kwamba wewe kama mpanda kanisa unaelewa wajibu wa kibiblia katikati ya familia kwa maisha yako mwenyewe na huduma. Zaidi ya hayo, Paulo, akimwandikia kiongozi wake mchanga Timotheo, anamkumbusha Timotheo majukumu ya kiongozi kati kati ya kanisa. Paulo anauliza, “Kama mtu hajui kuangalia nyumba yake mweneyewe vema, jinsi gani anaweza kuangalia kanisa la Mungu?" (1Tim 3:5). Wazo hili la swali linaloamsha linawatia changamoto viongozi wote, hasa mpanda kanisa, kutathimini huduma yake mwenyewe kwenye familia yake. Jinsi gani kulivyo kuangalia kwake familia yake kama familia yake inatoa msingi wa uwezo wa uongozi wake kanisani?

Kwa kuwa uko na kazi nyingi za majukumu ya kufanya uinjilisti, kufuasa, na kufunza viongozi, ikitafuta kwamba kanisa jipya litakua vema, ni lazima pia ukumbuke kwamba familia yako mwenye inabakia kuwa kimuli wazi kabisa cha uwezo wa uongozi na ufuasishaji wa ufanisi. Kama mpanda kanisa anaanzisha tabia ambayo inaangusha huduma yake kwa familia, hili linaweza kupelekwa kwenye kanisa mpya vile vile. Mpanda kanisa lazima atoe usikivu kwa familia yake kama sehemu ya kazi kwa ujumla ya huduma.

## I. WENZI WALIOOANA

Muungano wa msingi wa familia ni wenzi waliooana. Kwa kusoma historia ya uumbaji katika Mwanzo, tunaona kwamba Mungu alipoumba mtu katika kufanana naye aliumba mwanaume na mwanamke. Watu hawa wawili wanaishi pamoja kama mmoja (Mwa 2:24) Ilikuwa kionyesho cha kivuli cha Mungu wa utatu anayeishi katika umoja kamili katika mapana. Kama mmoja, walitakiwa kuishi katika upendano wa kirafiki ambao ungepelekea katika kuzaa watoto. Walikuwa wamepewa kazi ya kufanya: Kutawala samaki, ndege, na wanayama wa duniani. Walipofanya dhambi, kutokuwa umoja kuliingilia uhusiano wa kupendana, kuzaa kukawa kwa maumivu, na badaa ya kutawala dunia walijaribu kutawalana mmoja kwa mwingine.

Sehemu ya kazi ya ukombozi ya Kristo ni kurejeshwa kwa kivuli cha Mungu kati kati ya uhusiano wa ndoa. Kuna kanuni tatu zitakazotumika kama msingi kwenye majadiliao ya nafasi katikati ya ndoa.

**Kanuni Tatu Zinazoongoza**

1. *Mume na mke wana thamani sawa*

   Kutoka Wagalatia 3:28 tunagundua kuwa Mungu ameumba *waume na wake wakiwa na thamani sawa*. Thamani ya mtu haitokani na kazi, au nafasi, lakini kwenye ukweli kwamba ameumbwa kwa sura ya Mungu.

   > Thamani ya mtu inatokana na… ukweli kwamba ameumbwa kwa sura ya Mungu.

2. *Mme na mke wanatakiwa wategemeane.*

   Katika Wakorintho 11:11, tunaona kwamba Mungu ameumba *mme na mke kuwa wa kutegemeana.* Kanisa linaundwa na wanawake na wanaume wa aina zote za hadhi. Moja ya kigezo kinachotofautisha cha kanisa ni kwamba wajumbe wake wanakuwepo katika umoja bila kujali tofauti zao. Kuna tofauti za undani katika mahusiano haya, lakini uhusiano wa kijinsia unaweza ukawa ndio wenye utata. Katika ndoa iliyojawa na Roho, kutegemeana kutaelelezwa vizuri. Na kwa hiyo ushuhuda huu kutegemeana ambako kupo kwenye uungu wa Mungu.

3. *Kuna utaratibu wa wajibu katika familia.*

   Kutoka 1Wakorintho 11:3, tunaelewa kwamba Mungu ameumba *utaratibu wa wajibu katika familia.* Kama tu ulivyo utaratibu wa kazi kwenyeUungu, kuna utaratibu mzuri wa kikazi katika ndoa. *Mungu* ni kichwa cha Kristo, ambaye ni kichwa cha kilamtu, aliye kichwa cha mke wake.

## II. WAJIBU WA MME

### A. Kuwa Kichwa cha Mke: Waefeso 5:23

Paulo anaeleza kwamba mme ni kichwa cha mke kama Kristo alivyo kichwa cha kanisa. Uongozi unahusisha wajibu na kuwajibika mbele ya Mungu kwa ajili ya familia. Kwa kuwa msisitizo wa fungu ni juu ya upendo wa mme kwa mke wake, hii ndiyo sehemu muhimu zaidi ya wajibu wake.

Waume wanatakiwa watafute mazuri kwa ajili ya wake zao, hata kwa gharama zao wenyewe. Ukichwa unaotafsiriwa namna hii ni wito wa juu na wa kitakatifu. Kama mpanda kanisa, hali ya mbele ya ndoa yako na/au\ya hao watakaokuwa sehemu ya huduma yako inategemneana na uwazi halisi wa wajibu huu. Ukichwa ni wito wa kumwezesha mtu mwingine kuwa; siyo kibari cha mtu kujipendele. Moja hasa la kiutendaji wa wazo hili liko katika eneo la kujaliwa vipawa vya kiroho. Mme anatakiwa ajihusishe kwa bidii

Kwa jinsi hiyo, baadhi ya watu wanabisha kwamba kufuatana na Mwanzo 3, mtu anapashwa kutawala mke wake. Mandhali halisi ya Mwanzo 3:16 inaeleza: "…haja yako itakuwa kwa mme wako, na <u>atatawala</u> juu yako. Neno la Kiebrania lilitafsiri "tawala" maana yake kuwa na nguvu, kuweka karibu, kutwala juu yake kama mwenzi hasa. Neno linatumiwa na wafalme na ofisi za umma kwenye Agano la Kale lote. Lakini weka akilini kwamba Mwanzo 3:16 ni maelezo ya laana, siyo ya ufalme. Yanatangulia kueleza jinsi wanaume walioanguka watakuwa juu ya wanamke na kuwatishia kuwa kwenye nafasi ya hali ya chini. Hili limekuwa neno kwenye maelefu ya tamaduni kwa maelfu ya miaka.

Kutawala kwa ukali siyo namna ya Kristo. Kwa hiyo Paulo anaposema kwamba mwanaume ni kichwa cha mke wake kama Kristo alivyo kichwa cha kanisa, haungi mkono laana—anaivunja! Anaonyesha jinsi wanaume wanavyoweza kuvunja mzunguko wa hali mbaya na akili ya "mimi kwanza" ambayo anguko lilisimika.

Kwa hiyo mtindo wa uongozi wa Kristo ulikuwaje?

> Uongozi wa mme kwa mke wake unatakiwa kuelelezwa kufuatana na uoongozi wa Cristo kwa Bibi Arusi wake, kanisa.

Mtindo huu unaelezwa katika Luka 22:25-27 na unaelezewa kama "uongozi wa kitumishi" "mtumishi" na "kiongozi" siyo maneno yanayoungana kiasili. Yanaonekana kuwa katika kupingana. Hata hivyo, kwenye ufalme wa Mungu kuwa "kichwa" ni kuwa mchanganyiko huu wa kipekee wa kiongozi na mtumishi. Ni kweli kwamba wanaume wamepewa mamlaka kuongoza wake zao, lakini mtindo unatakiwa kuwa wa kitumishi, siyo kama bwana. Dhumini, kwa hiyo, ni kuwa chanzo cha maisha kwao. Uongozi wa mme kwa mke wake unatakiwa kuelelezwa kufuatana na uoongozi wa Kristo kwa Bibi Arusi wake, kanisa. Kristo hanyonyi kanisa. Halikandamizi, au kulazimisha uongozi wake juu yake. Kinyume chake, alipata haki ya uongozi kwa kujitoa mwenyewe kwa Bibi Arusi, na hatimaye kwa kufa kwa ajili yake. Kufuatana na kielelezo cha Kirsto, uongozi wa mme juu ya mke wake una tabia za:

- Kuwajibika, siyo cheo
- Kujitoa, siyo ubinafsi
- Kazi, siyo kukandamiza

## B. Kutunza Mahitaji ya Kati ya Mke Wake

Fikiria marudi ya Petro katika 1 Petro 3:7, "kadhalika ninyi wanaume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima kama chombo kisicho na nguvu na kama warithi pamoja nanyi wa neema ya uzima."

Wanawake wanahitaji waume zao kuishi nao pamoja kwa njia ya kuelewa. Hii ina maana kwamba waume wanahitaji kujihusisha kwa wake zao kiufahamu, wakifahamu ukweli kwamba wako tofauti na wanaume. Mbali na tofauti wazi ya kimwili, kuna tofauti pana ya kisaikolojia na kihisia. Waume kwa hiyo wanatakiwa watoe umakini kwa yafuatayo yanayowahangaisha.

1. *Umwandani*

   Cha kwanza ni kwamba wake wanahitaji mwandani. Mungu amewaumba wanawake kuhitaji uhusiano wa ndani unaoendelea na wanawatarajia waume zao kutimiza hitaji hilo. Wanataka na kuhitaji umwandani, uwepo na haja ya waume zao.

2. *Usalama*

   Hitaji la pili ni usalama. Wanawake wanahitaji usalama wa mwanaume. Anahitaji kujua kuwa ana weza kumlinda na kumpa mahitaji. Anahitaji kuweza kumuamini. Kibiblia, vitu hivi ni wajibu wa mme (1Tim 5:8).

3. *Umaana*

   Hitaji la tatu ni umaana, ambalo ni hitaji linalochangiwa na wote mke na mme. Mme mara nyingi anapokea kumaanisha kutokana na kazi yake, nafasi yake kanisani, au shughuli nje ya nyumbani. Lakini mengi ya yale mke anayofanya yamefichika na kutokuonwa. Mtu pekee anayeweza kutambua michango yake wa pekee, ambaye anaweza akamshukuru kufuatana, ni mme wake. Ni rafiki, mlishaji wa neno, rafiki wa roho. Sehemu ya wajibu wa uongozi ni kumfanya kujisikia kuheshimiwa na bila kuchukuliwa kirahisi.

## C. Kufanya Kazi za Baba

Jukumu kubwa la baba ni kuwaweka watoto wake katika mafundisho na maelekezo ya Bwana (Efe 6:4). Hii ni pamoja na kuwafundisha njia za Bwana (Kum 6:7), na kuwarudi iwezekanavyo (Mit 19:18, 22:6, 23:13,14, 29:17).

## III. WAJIBU WA MKE

Mithali 31:10 inauliza swali linalolazimisha, “Mke mwema, ni nani awezaye kumwona?" kwa mwanamke kuwa mke “mwema” ni kwa yeye kuelewa uumbaji wa Mungu kwa mke na, kwa neema yake, kudhihirishwa na yeye kwenye uumbaji huo.

### A. Mwenzi Msaidizi

> Kwa pamoja, wakifungwa na kujaliwa na Roho Mtakatifu , mke na mme wanakuwa wakamili na kuweza kumtumikia vyema.

Mungu aliwaumba wanawake kuwa wenzi wasaidizi (Mwa 2:18). Ni mkamilishaji wa kihisia na kimwili kunakomfanya mwanaume kufaa kwenye kusudi lake zaidi na huduma mbele za Mungu. Hamfanyi kuwa mkamili katika hali ya kiroho, kihisia, na kimwili. Kwa jinsi hiyo, anamfanya kuwa mkamili zaidi kuliko alivyokuwa mwenyewe bila yeye. Analeta kwake mtazamo, hisia, vipawa na udhaifu ambao yeye mwenyewe hana. Kwa pamoja, wakifungwa na kujaliwa na Roho Mtakatifu, mke na mme wanakuwa wakamili na kuweza kumtumikia Bwana vyema.

### B. Anayeunga Mkono

Kama alivyo mtimizaji kwa mme, mke pia ni msaada kwake. Msaada wake ni sehemu yake, “mwendo safi na wa hofu" (1Pe 3:2) kwake. Anajua uwezo wake na udhaifu, na anamjenga kwa ajili ya kazi yake. Mithali 14:1 inaonyesha kwamba mwanamke anaweza kujenga au kubomoa nyumba yake. Anaweza kujenga uwezo wa kihisia na kumpatanisha mme wake, au anaweza kusaidia kumwangamiza, akimwaibisha na kuwa kama “kuoza mifupani mwake" (Mit 12:4b).

### C. Mtiifu

Mke pia ana wajibu wa kuwa mtiifu kwa mme wake. Hakuna amri iliyorudiwa zaidi kwa mke kuwa mtiifu kwa mme (Efe 5:22, Col 3:18, 1Pet 3:1), tabia ya mwanamke wa kimungu kama mke wa Ibrahimu, Sara (1Pet 3:6). Hata hivyo, mkao wake wa utiifu ni wa nguvu. Kwa imani anamtii mme wake na kukata rufaa kwa baba yake wa mbinguni. Kama moyo wa mfalme (Mit 21:1), moyo wa mme uko mikononi mwa Mungu. Anapomuheshimu mme wake, anamuheshimu Mungu na kuruhusu mkono wake kujongea kwenye maisha ya mme wake. Kwa matendo yake ya utiifu, anamruhusu Mungu kumleta mme wake kwenye utii mkubwa kwake mwenyewe (1Pet 3:1). Hajaamuliwa kuasi kupinga mchango wa mme wake. Ameamriwa kutii kwa imani ili kutoa mkono wa Mungu kwenye maisha ya mme wake na yeye mwenyewe.

### D. Msimamizi

Maandiko yanatoa kielelezo cha mwanamke wa kiwandani anamuhudumia mme wake na kuleta faida kwa nyumba (Mit 31:10-31, hasa hasa mstari 11). Siyo kama mwanamke wa Samaria ambaye, katika siku za Amosi, alimkandamiza masikini na muhitaji na kufanya matakwa ya kutotosheka juu ya waume zao (Am 4:1), mwanamke wa Mithali 31anamuogopa Bwana (v. 30), anamuhudumia mme wake (v. 12), anajenga nyumba yake (v. 27), anasababisha heshima ya mme wake kuongezeka (v. 23) na kumfanya kumuamini (v.11). Siri yake ni kwamba anaweza kumsaidia mme wake, anatunza na kusimamia nyumba yake, akiifanya kuwa mahali pa amani na sehemu yenye faida ambayo inaleta mema zaidi kwa mme. Anamuhudumia, akimshika kwa heshima, huku akisimaia nyumba yake kwa kuweza kuliko ambavyo angweza. Mume anaweza tu kumshukuru Mungu kwa wema wake katika kumpa huyo (Mit 19:14).

### E. Mama: Tito 2:4

Wajibu wa kati wa mwanamke hauishii kumpenda mme wake, Tito 2:4 inaendelea kumtia moyo kuwa “anayependa watoto.” Watoto, hasa wadogo, wanahitaji dozi ya ajaba kutoka kwenye kujali kwa mtu, msaada, na upendo mkuu. Watoto wanahitaji nguvu ya ajabu ya kuwepo kwa mama zao. Kutokana na wataalamu wengi wa watoto, maendeleo ya mtoto mwenye afya, wa kawaida anahitaji, kupendwa kwa karibu, na uhusiano ulioimarishwa na angalau na mtu mmoja wakati wa kiwango cha chini cha miaka miwili ya maisha. Tito anaonyesha kwamba mama anatakiwa atoe uangalizi, lakini tamaduni zinazotawala za siku zetu ni, kwa sehemu kubwa, zinaondoa kanuni hizi za kimaandiko na badala yake kutafuta mapendeleleo yao ya binafsi.

## IV. WAJIBU WA WATOTO

### A. Kuwatii wazazi wao katika Bwana

Waefeso 6:1 inasema "watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, kwa kuwa hili ni haki." Maelekezo haya kutoka kwa Paulo kwa kanisa la Waefeso yanaibua maswali kadhaa ambayo mpanda kanisa anatakiwa ayagusie:

- Anamaanisha kwa watu wa chini tu?
- Watu wazima wanatakiwa waendelee kuwatii wazazi wao, hata kama hawaishi tena nyumbani kwa wazazi wao?
- Kama mtu mzima anaendelea kuwa katika nyumba ya wazazi wake, hili linamuhusu?
- Je "katika Bwana " kuna maana kwamba kama mzazi siyo mkristo, mtoto hahitaji kumtii?

### B. Kuwaheshimu Baba Zao na Mama Zao

Maelekezo ya Paulo yananukuru kutoka Agano la Kale na kuwakumbusha Waefeso kwamba hii ni amri ya kwanza pamoja na ahadi: "kwamba utakuwa na heri na kuishi miaka mingi duniani" (Efe 6:2-3, Kum 5:16).

## SULUHU

Somo hili ni la thamani kwako endapo ni mpanda kanisa bachela au aliyeoa. Unaelewa wajibu wa kibiblia kwa familia, maisha yako mwenyewe yataimarishwa, kusanyiko lako lote litasaidwa na jumuia unamoishi inaona umoja na upendo wa Mungu ukielelezwa kupitia kwenu binafsi na kupitia nafasi za mafundisho na ushauri ambazo Mungu atatoa.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kama ni mtu bachela, jinsi gani somo hili linaweza kuwa la faida kwako na huduma yako?
- Kama umeoa, unaweza kusema kwamba ndoa yako inaonyesha kioo cha sura ya Mungu kwa kuonyesha umoja?
- Unapata umwandani katika ndoa yako? Inaonekana je?
- Ni vigezo vipi katika jamii na katika ndoa vinafanya ugumu leo wa kuwa mwenzi mfanisi? Ni mahangaiko yapi makubwa katika kuwa wenzi wazuri?
- Ni vigezo vipi katika jamii na katika kanisa vinavyofanya vigumu kuishi kama bachela leo? Ni mahangaiko yapi katika kuwa bachela?

## UTEKALAZAJI WA AZIMIO

- Soma 1 Petro 3:8-12. Tabia ya ubinafsi inaharibu umojao. Kwa kulifikiria hili, soma kwa mara nyingine kifungu hapo juu na kisha orodhesha vitu unavyotakiwa kufanya wakati mwenzi wako anapokuwa mbinafsi.
- Uongozi wa kitumishi wa mme ndiyo kitu pekee kinachomfanya mke kuweza kutii. Mme wa kutendewa anafanya utiifu kutowezekana na mwanaume anayetawala anafanya utiifu kutovumilika. Uongozi wa kitumishi, kwa upande mwingine, unafanya kutii kuwa furaha. Kwa mwanga wa mawazo haya, jibu maswali yafuatayo:
  - Jinsi gani kuwa kwako kiongozi mtumishi kutagusa uwezo wa mke wako kuwa mtiifu?
  - Jinsi gani anaitikia katika maeneo mengine kama ungekuwa zaidi kiongozi mtumishi?
  - Je Biblia inafundisha kitu chochote kuhusu kwa nani wanawake bachela wanatakiwa watii? Ni mipaka ipi unayoweza kupata?
- Katika barua yake kwa kanisa la Filipi, Paulo aligusia swala la umoja miongoni mwa wakristo. Soma Wafilipi 2:1-4 na kisha fikiria jinsi mstari 2 unavyoelezea kupata umoja kwenye mahusiano. Jinsi gani unaweza kutumia kanuni hizi katika maisha yako ya familia, iwe katika ndoa au kwenye mahusiano mengine ya familia?

- Kama wapanda kanisa mtakuwa na nafasi nyingi kutoa ushauri wa kibiblia kwa wasioamini na wanaoamini waliopata shida kutokana na ndoa zilizoshindwa au ambao kwa wakati huo wanakutana na kutokuwa na umoja katika ndoa zao. Vile vile, utakuwa na nafasi ya kutoa ushauri kwa wanaume na wanawake wanaotaka kuoana. Anzisha majadiliano ya kundi dogo na wanaume wasiooa na wanawake wa umri wako wanaotaka kuoana mbeleni. Waongoze katika kugundua vipande vya kibiblia vilivyojadiliwa katika somo hili na kumalizia kivitendo kwa vipande hivi.

**VYANZO**

Lewis, Robert and Hendricks, William. *Rocking the Roles.* Colorado Springs, CO: NavPress, 1991.

FAMILIA

SOMO LA 2

# Uleaji

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwasaida wapanda kanisa kuelewa na kutumia kanuni za kibiblia kwenye uleaji wa watoto

☞ **Wazo Kuu**

- Kulea watoto kunahitaji kutembea kwa imani
- Neno la Mungu linatupa baadhi ya kanuni ambazo zinatakiwa katika kulea watoto

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua nini Biblia inafundisha kuhusu kulea watoto.
- Kuweza kutathimini malezi yake ya watoto kwa kiwango cha kibiblia.
- Kuanzisha njia za kukuza uleaji wake wa watoto.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Tumia zana hii kuwapa wafunza kanuni za msingi za kibiblia. Pinga mabishano ya "kuwaambia jinsi ya kufanya." Acha mda wa kujadili maswali mwishoni, au katika vikundi vidogo au kwa pamoja.

## UTANGULIZI

Makitaba za kikristo zimejaa vitabu vyenye maelekezo ya wazazi wa kikristo. Vitabu hivi vina vielelezo vingi vyenye mifano, kila kimoja kikidai KUWA njia ya kibiblia. Lakini ingawa Biblia inatupatia maelekezo fulani, ambacho haitoi ni maelekezo ya hatua kwa hatua ya kulea watoto. Katika somo hili tutaangalia baadhi ya kanuni za kibiblia ambazo zinaweza kutumiwa katika hali ya malezi ya watoto. Kwa sababu kila mtoto ni wa kipekee na mwenye mahitaji ya kipekee, jinsi wazazi wanavyotumia kanuni ni swala la kutafuta hekima kimaombi kutoka kwa Bwana. Kama ilivyo maisha mengine ya kikristo, kulea watoto ni mwendo wa imani.

Katika Utume Mkuu, Yesu aliwaelekeza wafuasi wake kufanya wanafunzi wa kila taifa... wakiwafundisha kutii yote aliyosema. Wajibu wa mzazi ni kama huo wa mpanda kanisa: kufanya wanafunzi na kuwafundisha utii kwa Mungu: Ni kwa maana kwa wajumbe wa familia wenyewe, ni muhimu kwa ushuhuda wao kwa ulimwengu, na ni muhimu kwa kanisa. Namna wazazi wanavyohusiana na watoto wao inaonyeshwa kwa namna wanavyojihusisha kwa kanisa (1Ti 3:4,5). Kwa wapanda kanisa ambao si wazazi, somo hili bado ni muhimu kwa sababu kanuni sawa inatumika kuwasaidia watoto wa kiroho kati kati ya huduma zao.

## I. BAADHI YA UCHUNGUZI WA MWANZONI

### A. Hakuna Hakika

Kinyume na ambacho kimefundishwa, Biblia haifanyi uhakika wowote kwamba kama mzazi anafanya kila kitu sawa, watoto watampenda Bwana na kumtumikia. Mstari ambao mara nyingi unanukuriwa kama ahadi kutoka kwa Mungu ni Mithali 22:6, "Mlee mtoto katika njia impasayo, na anapokuwa mkubwa hataiacha njia hiyo." Kama watoto wao wanakua na kumkataa Bwana, wanajisikia kana kwamba Bwana amewasaliti.

Tafadhali tambua kuwa mstari huu unaelezea kanuni ya sababu na matokeo: kama unafanya "X" kisha "Y" itatokea. Kitabu cha Mithali, ambacho kiliandikwa kusaidia kuongoza vijana kwenye kuishi utakatifu, kina vitu vingi vinavyofanana. Kuwafundisha watoto wanapokuwa wadogo kunawaanzishia njia kwenye utakatifu. Badala ya ahadi iliyo ya kweli kwenye hali zote, msitari huu unaelezea kanuni ya jumla kwamba kama wazaze wanafundisha watoto wao kumtii Bwana wanapokuwa wadogo, watakapokuwa wazima wataendelea katika njia yake. Ukweli kwamba wakati mwingine wanamwacha Bwana bila njia yoyote inayoipunguza kanuni au jukumu la wazazi la kuwafundisha watoto wao katika njia za Bwana. Watoto wengi wanaopata mafunzo hayo wakiwa wadogo wanaendelea nayo.

### B. Hakuna Watoto Walio Kamili

Kwa nini watoto walioanza kwa kutembea katia njia ya utakatifu kisha "wanaiacha"? Kila mtu ni mwenye dhambi aliye na uchaguzi wa kufanya. Mithali 1: 29 inazungumzia hao ambao "...waliokataa maarifa na kutokumuogopa Bwana." Hatimaye, kila mtu lazima achague yeye mwenyewe kama endapo au la atamfuata Bwana. Hata watoto walio na mafundisho mazuri wanaweza kufanya uchaguzi mbaya.

### C. Hakuna Wazazi walio Kamili

Mungu ni mzazi pekee mkamilifu; wazazi wa dunia siyo kamili. Haijalishi ni kwa kiasi gani wanampenda Bwana na watoto wao, wakati mwingine watashindwa (1JY 1: 8-10). Hakuna aliye na majibu yote. Wazazi wanahitaji kuendelea na kwa maombi kutafuta hekima ya Bwana ya kuwafundisha watoto namna wanavyotakiwa kwenda.

## II. BAADHI YA KANUNI ZA KIBIBLIA

Ingawa hakuna hakika kwa sababu ya asili ya dhambi ya wote watoto na wazazi, Mungu ametupatia kanuni fulani za kutuongoza katika kufundisha watoto.

### A. Onyesha Upendo na Utii wa Bwana (Kumb 6:4-9, 17)

Katika Agano la Kale, Mungu aliwaamuru Waisraeli "Kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa nguvu zako zote…sisitiza (amri zake) kwa watoto wako…Uwe na hakika kutunza amri za Bwana." Watatakiwa kufanya hili nyumbani, wakitembea katika mstari, wanapolala na wanapoamka. Kumpenda Mungu na kutunza amri zake ulitakiwa uwe mtindo ambao wazazi wanatakiwa wauanzishe na kuurithisha kwa watoto wao.

### B. Waelekeze Watoto Wako Kutunza Njia ya Bwana (Mwa 18: 19)

Kuzungumzia kuhusu jukumu la wazazi kuwaelekeza watoto wao, Biblia mara nyingi inalinganisha hili na malezi. Mistari kama Mithali 3:11,12 na Waebrania 12:5-11 inatukumbusha kwamba malezi ni ya lazima. Lakini sababu yake ni kwa sababu baba (wote wa mbinguni na wa duniani) wanawapenda watoto. Wakati wowote malezi yanapotumika, yanatakiwa yafanyike kwa upendo ambao unalenga katika akili ya mtoto. Mtoto lazima aweze kutambua upendo huo kati kati ya malezi. Matokeo yanayotakiwa ni kwamba mtoto anajifunza kutunza njia za Bwana.

### C. Usigadhibishe Watoto Wako (Efe 6:4)

Wazazi wengi wanang'ang'ania sehemu ya pili ya Waefeso 6:4, kuwalea katika adabu na maonyo ya Bwana, na kusahau sehemu ya kwanza, msiwachokoze watoto wenu. Masimulizi ya wafanya kazi wakristo ambao watoto wao wamekuwa na uchungu na kumwacha Bwana hayahesabiki. Watoto hawa mara nyingi wanaelezea habari za wazazi ambao wazi walikuwa wagumu, wasio wa haki, wakiwataka na walazimishaji: wazazi waliogadhibisha watoto wao kwa jitihada za kuwafundisha kumpenda Bwana. Hata hivyo, sala nyingi za familia zinaonekana kama mda wa nyakati wazazi wanapoweza kuhubiri matokeo yake ni watoto wenye uchungu na wapinzani kwa wazazi wao na kwa Mungu.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni baadhi ya njia zipi za kivitendo unazoweza kufanya upendo na utii mtindo wa maisha kwa Bwana nyumbani kwako?
- Ni baadhi ya njia zipi za kivitendo unazoweza kuona kama malezi yako yanafanyika nje ya upendo? Nini unachofikiria kizuizi kikuu kwa aina hiyo ya malezi?
- Ni vitu vipi vya kivitendo unavyoweza kufanya mda was sala kwa familia kuwa wa kufurahiwa na watoto?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Orodhesha baadhi ya tabia unazopenda watoto wako kuwa nazo kiroho, kijamii, kiakili na kimwili wanapofikia umri wa miaka 18. Kisha andika jina la kila mtoto kwenye karatasi tofauti. Andika unachofanya au unachotaka kufanya kumsaidia mtoto kupata kila moja ya tabia hizi.

### VYANZO

- Kimmel, Tim. *Raising Kids Who Turn Out Right*. Sisters, OR: Multnomah, 1993.
- Phillips, Mike. *Building Respect, Responsibility & Spiritual Values in Your Child*. Minneapolis, MN: Bethany House, 1981.
- Stanley, Charles. *How to Keep Your Kids on Your Team.* Nashville, TN: Oliver Nelson, 1986.